# 1

"Kama ambavyo nilipata kusema hapo awali tunahitaji kushirikiana kwa ari na mali ili jambo hili liweze kufanikiwa. Hamna namna nyingine itakayokuwa muafaka zaidi kwetu na kutuwezesha kufanya shughuli zetu kwa amani!" Alitulia kidogo kiasi cha kupepesa macho yake huku na kule na alipohakikisha anasikilizwa,aliendelea:
"Hakuna asiyejuwa ni namna gani ushindani wa kibiashara ulivyo mkubwa hivi sasa Afrika na duniani kwa ujumla. Lazima tufahamu kwamba, katika hali kama hii, hatuna budi kufanya lolote lililo ndani ya uwezo wetu ili tuweze kujenga mazingira muafaka kwa ustawi wetu. Jambo hili ni muhimu katika kukabiliana na mazingira yanayoelekea kuibuka ndani ya nchi hii ambayo yanaweza kuzalisha *Niger Delta* nyingine ndani ya ardhi ya Afrika. Sauti zinazoanza kusikika hivi sasa toka kwa wanaharakati mbalimbali ni ishara mbaya kwetu inayopaswa kuzimwa kwa gharama yoyote ile. Nazani wenyewe mnaweza kushuhudia jinsi wapuuzi wachache wanavyojifanya wana uchungu na nchi hii wakati ni wanafiki watupu! Hatuna budi kufanya jambo la maana kuwafykelea mbali wanafiki hawa na wengine wote wenye mawazo kama hayo. Hatutawafyeka kwa silaha bali kwa hadaa! Hivyo basi, ni wajibu wetu kujipanga upya ili kukabiliana na hali hii. Ni lazima tufanye jambo la maana kabla ya uchaguzi mkuu ujao. Ni lazima tuwe na watu wa kutosha watakaotetea ustawi wetu na kuzima hujuma zozote dhidi yetu kwenye nchi hii na ukanda mzima wa Afrika ya Mashariki. Na

kama ambavyo niliwaeleza kwenye kikao kilichotangulia, Kamati Kuu (*Central Strategic Commitee-CSC*) iliketi kikao chake juma lililopita ambapo limeandaa mikakati mbalimbali ambayo tukiitekeleza basi hapana shaka yoyote kwamba kila siku sisi tutakuwa ndio washindi." Alipofika hapa, kiongozi wa kikao hicho, Fredrick De Souza, alitoa makarabrasha mbalimbali na kisha kuyagawanya kwa wajumbe waliohudhuria. Kilikuwa ni kikao cha siri kilichofanyika chini ya ulinzi mkali ili kuzuia yeyote asiyehusika. Wajumbe walianza kuzama kwenye makarabrasha haya na kuanza kuyapitia kwa makini.

"Kama mlivyoona kwenye hizo kalabrasha, huo ndio mpango wenyewe tunaotakiwa kuujenga, kuusimamia na kuuratibu kwa nguvu zetu zote." Hatimae Fredrick De Souza alianza tena baada ya wajumbe waliopo kuyapitia makarabrasha ambayo aliyagawa kwao kabla, kisha akaendelea: "Hivyo basi, ili mpango huu uweze kufanikiwa, ni lazima kwanza ziundwe na kuziimarisha taasisi zilizotajwa. Hata hivyo, kampuni zetu zitajihusisha na taasisi hizo kwa usiri mkubwa kwavile hatutakiwi kwa namna yoyote kuonesha kwamba sisi na taasisi hizo ni wamoja. Na kama mlivyoona, mkakati wetu utaanza kwa kuanzisha kampuni ya ulinzi itakayojulikana kama Intercontinental Security, Legal & Investigation Bureau (ISLIB). Aidha, tutaanzisha taasisi zingine mbili ambazo ni School of Democratic Thoughts & Political Economy (SDTPE) na nyingine itajulikana kama Purpossive Strategies for Socio-Economic Support (PSSES)."

“Hapa ningependa kusisitiza kwamba hatutakiwi kwa namna yoyote ile kuonesha kwa uwazi kwamba tuna uhusiano na ISLIB au SDTPE. Na endapo atatokea mtu yeyote mbali na sisi akafahamu uhusiano huu basi stahiki pekee ya mtu huyo ni kifo na si vinginevyo! Kwa upande mwingine, tutajihusisha moja kwa moja na taasisi ya PSSES. Siku ya uanzishwaji wake itabidi ijulikane na kila mtu nchini. Vyombo mbalimbali vya habari vitatumika kutangaza uzinduzi rasmi wa taasisi hiyo ambayo kimsingi itaonekana ni mkakati wa makusudi uliobuniwa na makampuni ya kimataifa yaliyowekeza hapa nchini ili kusaidia wananchi katika huduma za kijamii na uchumi.”

“Ndugu wajumbe, ningependa tuelezane ni namna gani taasisi za ISLIB na SDTPE zitakavyoendesha shughuli zake. Tukianza na ISLIB, hii itajihusisha na mambo ya usalama, sheria na uchunguzi ambapo itafanya kazi zake kwa kukodiwa na wakati mwingine kwa utashi wa kampuni yenyewe. Kwavile sheria za nchi zinamruhusu Mkurugenzi wa Mashitaka, yaani DPP kuteua mtu au kampuni binafsi kuendesha mashitaka kwa niaba yake, basi ISLIB itajitahidi kutafuta nafasi hiyo ya kufanya uchunguzi wa masuala mbalimbali na kuendesha mashitaka. Lengo la kufanya hivyo ni kuifanya ISLIB ikubalike kwa wananchi na hivyo kuficha lengo kusudiwa. Hapa tayari kuna watu wetu serikalini ambao watafanikisha mpango wa ISLIB kuingia mkataba na Idara ya Mwendesha Mashitaka ya Taifa ili kuweza kuendesha kesi hizo. Kama mjuavyo, nchi hii hivi sasa inasumbuliwa na masuala ya ubadhirifu kwenye sekta mbalimbali, na kila mwananchi anajifanya anachukia hali hii! Huu kwetu ni mtaji mkubwa hivyo tutaanza na kufanya uchunguzi kwenye masuala haya ili tujenge imani na uungwaji mkono kutoka kwa wananchi!

Ikibidi, tutapandikiza hata kesi ambazo hazipo hususani kwa viongozi na wanaharakati wanaojifanya vimbelembele. Aidha, pamoja na yote hayo, ndani ya ISLIB kwenyewe kutakuwa na kitengo kingine ambacho ni cha siri sana na ni watu wachache sana watakaokijua. Kitengo hiki kitajulikana kama *Intercontinental Blackmail Unit*, kwa kifupi IBU. IBU itakuwa ni kitengo muhimu sana kwa shughuli zetu kwavile kitajihusisha katika kuwapata watu wenye ushawishi serikalini ambao ni vigumu kuwapata kwa njia za kawaida. Watu kama hao tutawatengenezea aina mbalimbali za kashfa na kuwalazimisha kutufanyia kazi zetu endapo watataka kashfa hizo zisitoke nje. Hakika nawaambia, yeyote atakayeingia kwenye mtego wa IBU, basi atakuwa mtumwa wetu hadi siku anaingia kaburini! Kutokana na hilo, mtaona kwamba IBU ni kitengo kinachohitaji watu makini na wenye akili za ziada!

“Kwa upande wa SDTPE, vilevile hatutajihusisha nayo kwa namna yoyote ile kwavile ni taasisi ya kisiasa, nasi sio wanasiasa. Katika hili, itabidi kuwepo na chama cha siasa ambacho ni mkono wetu na ambacho kitafanya kazi kwa maslahi yetu. Hatuna haja ya kuanzisha chama kingine, tutakitumia kimoja kati ya vingi vilivyopo hususani kile kitakachoonekana kinatishia maslahi yetu. Katika kufanikisha hili, maafisa wa juu wa SDTPE watakutana kwa siri na viongozi wa juu wa chama husika ambapo wataeleza nia ya kutaka kukisaidia chama hicho kwa mlango wa nyuma ili kiweze kuingia madarakani. SDTPE itaahidi kukisaidia chama husika kwa misaada ya wazi na ya siri ambayo itasaidia kukijenga chama na kuwa imara. Kwavile vyama vyenyewe vina matatizo ya kifedha, basi hatuna shaka yoyote kwamba mpango huu utafanikiwa kuwatia mtegoni. Jambo la msingi hapa ni

kwamba SDTPE itakuwa inakutana na uongozi wa chama husika kwa siri huku kukiwa na idadi yote ya viongozi wenye ushawishi kwenye chama. Aidha, tutalazimika kuwa na wanasiasa binafsi kutoka pande zote mbili, yaani kutoka chama tawala na upinzani. Wanasiasa hawa ni wale tutakaoona wana ushawishi mkubwa miongoni mwa jamii na hata kwenye vyama vyao . Wakati wa kufanya vikao na watu hawa, kutakuwa na kamera za siri ambazo zitakuwa zinachukuwa matukio yote ikiwa na pamoja na yale ya kukabidhiwa misaada kwa siri. Na endapo itatokea kiongozi yeyote kuhama chama husika kwa namna yoyote basi hapana adhabu itakayomstahili zaidi ya kifo."

"Ndugu wajumbe, wakati kazi ya SDTPE itakuwa ni kuwarubuni viongozi wa vyama husika na kuwaingiza mtegoni, IBU itatumia nafasi hiyo kuwataka viongozi hao wafanye kazi zao kwa maslahi yetu. Na kama mjuavyo, hamna mwanasiasa duniani ambae angependa kuonekana kuwa ni msaliti kwa wananchi wake. Hivyo, kwavile hawatapenda kuumbuliwa kwa picha tutakazokuwa tumepiga kwa siri, basi sina shaka kwamba matakwa yetu yatatekelezwa tu! Labda jambo la msingi hapa ni kwamba yote haya yatafanyika bila hata ya wao kufahamu kwamba kuna uhusiano kati ya SDTPE, ISLIB, IBU, PSSES na sisi."

"Hivyo basi, huo ndio mkakati mzima ambao hatimae utatufanya tuendeshe biashara zetu kwa amani na hivyo kufanikisha malengo yetu. Jambo la msingi la kukumbuka ni kwamba mpango huu ni siri kubwa. Kama ambavyo mliingia bila kitu chochote, vilevile mtatoka bila kitu chochote; na hii ni kwa sababu za kiusalama." Baada ya kufika hapa alitulia kidogo kisha akamalizia, "Nawatakia kazi njema na tutakutana tena hapa kila itakapoonekana ni muhimu."Alimalizia hotuba yake na

baada ya muda kila mmoja wa wajumbe wale alianza kuondoka.

Kama ilivyosemwa hapo awali, kikao hiki kiliitishwa na Mr. Fredrick De Souza ambae ni mmoja wa viongozi wa kampuni moja kubwa kabisa hapa nchini. Kikao kilihudhuriwa pia na baadhi ya wawekazaji wenye biashara zao hapa nchini. Wawekezaji hawa ni wale wenye hofu kwamba malengo yao kibiashara yapo hatarini kutokana na mwamko wa wananchi wanaotaka uwekezaji wenye maslahi zaidi kwa taifa kuliko vinginevyo. Ili kukabiliana na changamoto hiyo toka kwa wananchi, wakaamua kuchukua hatua za taadhari ili kuhakikisha maslahi yao yanalindwa! Aidha, katika kufanikisha malengo hayo, viongozi wa juu toka kwenye makampuni mama ya haya yaliyopo nchini walikuwa wamekutana jijini London Uingereza juma moja kabla ya kikao hiki ili kupanga mikakati mbalimbali chini ya umoja wao haramu unaojulikana kama Central Startegic Committee au CSC kwa kifupi. CSC ni kamati ya siri ya baadhi ya kampuni kubwa za Ulaya na Amerika ya Kaskazini zenye vitega uchumi vyao barani Afrika, Asia na Amerika ya Kusini. Nyingi ya kampuni hizi zinaendesha biashara zake isivyo halali pasipo kujulikana, na hata pale inapojulikana wanafumbiwa macho kutokana mtindo wao wa kuwahonga watendaji wakuu wa serikali na wanasiasa. Na hata wanaofanya biashara halali, unakuta wengi wao ni wale waliowekeza kwenye biashara halali kupitia mitaji iliyotokana na pesa haramu kama vile zinazotokana na biashara za madawa ya kulevya, silaha za kivita na biashara ya madini toka kwenye maeneo ya vita kama vile Congo, Siela Leone na Liberia. Hivyo basi, kutokana na sababu walizoziona wenyewe, CSC walikutana kwenye

kikao cha siri jijini London na kupanga mikakati itakayowawezesha kufanya biashara katika ardhi ya Tanzania kwa namna ile wanayotaka wao na kwa manufaa yao zaidi!

☙❧☙❧

Miezi sita ilishapukutika tangu kifanyike kikao cha siri kilichowakutanisha baadhi ya wawekezaji wakubwa nchini. George Kamau, raia wa Kenya na mwenzake Michael Mchupi, raia wa Tanzania walikuwa wamejifungia kwenye nyumba moja jijini Nairobi. Wote walikuwa wamezamisha akili yao kwenye mtandao wa kompyuta unaowakutanisha watu wanaosaka marafiki kutoka sehemu mbalimbali duniani; yaani *Face Book*. Walichokuwa wanafanya ni kutafuta wasichana wenye sura za mvuto kutoka Tanzania. Wakati watu wengine waliokuwa wanatembelea mtandao huu walikuwa na lengo la dhati la kupata marafiki, George Kamau na Michael Mchupi walikuwa na lengo tofauti kabisa. Akiwa kama wakala wa IBU, na Michael Mchupi kama rafiki yake, George Kamau alipewa jukumu la kutafuta warembo kutoka Tanzania ambao wangetumika kwenye kazi zao. Kutokana na hilo, hivi sasa George Kamau alikuwa anapitia taarifa (*profile)* za msichana aliyejitambulisha kama Glory Mushy, Mtanzania anayeishi jijini Dar es salaaam. Alipitia taarifa zake mbalimbali ikiwa ni pamoja na mambo anayopendelea kuyafanya. Dada mwingine mwenye taarifa zilizofanana na Glory Mushy alikuwa ni Wendy Michael. Tofauti na Glory Mushy, Wendy Michael alijitambulisha ni Mtanzania anayeishi mjini Arusha, Tanzania. Hata hivyo, wote hawa

walikuwa na kitu kimoja kinachofana, nacho ni urembo uliotukuka!

Fredrick De Souza alionekana ni mwenye pilikapilika mno huku kila wakati akiwa anaitupia macho saa yake ya mkononi. Taratibu, alijivuta kwenye kiti chake na kukaa kisha akaanza kutupa macho kwenye luninga ndogo inayoratibu usalama wa eneo zima la hapo!

Alitulia kwa muda, na mara wageni aliowatarajia walianza kuwasili mmoja baada mwingine. Dakika chache baadae wote waliwasili na bila kupoteza muda, Fredrick alianzisha maongezi:

"Ndugu wajumbe tunakutana tena leo hii ili kupeana taarifa ya maendeleo ya mkakati wetu tangu ulipoanza. Kama mjuavyo, uanzishwaji wa CDTPE, PSSES, ISLIB pamoja na IBU umefanikiwa kwa kiasi kikubwa na tayari taasisi hizi zimeshaanza kufanya kazi. Hata hivyo, Central Strategic Committee (CSC) ilikutana tena na kufikia muafaka wa kuanzishwa kampuni nyingine itakayongozwa na Meneja wa IBU ukanda wa Afrika ya Mashariki aitwae George Kamau. Kampuni hiyo itahusika na ushauri juu ya masuala ya uwekezaji ambayo itaitwa East Africa Opportunities & Consultancy, kwa kifupi EA-O&C. Kimsingi, EA-O&C itakuwa inatoa ushauri wa kitaalamu kwa wawekezaji waliopo na wale wanaofikiria kufanya biashara hapa nchini. Aidha, jambo muhimu zaidi ni kwamba, wawekezaji watakaoonekana ni muhimu kwetu watakuwa wanapenyezewa taarifa za siri za namna gani EA-O&C inavyoweza kuwasaidia kurahisisha mambo yao kupitia mlango wa nyuma! Ushauri wa aina hii, utajulikana kama *Undercover Consultations Package,* kwa

kifupi UCP ambao utakuwa maalumu kwa makampuni maalumu na kwa sababu maalumu. Ni matumaini yetu kwamba, ndani ya UCP tutafanikiwa kuwapata watendaji mbalimbali watakaoingizwa kwenye orodha ya IBU. Watendaji hawa ni wale watakaokuwa wamezisaidia kampuni hizo maalumu tutakazoziona ni muhimu kwetu. Hata hivyo, wakati George Kamau atakuwa anajificha kwenye mwamvuli wa EA-O&C, atakuwa ndie Kiongozi Mtendaji wa IBU.

Kama ilivyo desturi yake pale anapoamua kupumzika, Glory Mushy, msichana wa makamo anayejishughulisha na mambo ya mitindo alikuwa kwenye mtandao wa Face Book akijaribu kupitia wadau kadhaa waliokuwa wamevutiwa na maelezo mafupi kuhusu yeye, yaani *profile* yake. Alishazoea kukutana na wasifu wa watu mbambali, hususani wanaume waliokuwa wamevutiwa naye kiasi cha kuomba urafiki nae. Hata hivyo, alijitahidi kuwapuuza wote hawa kwani aliona wengi wao hawakuwa na lengo la urafiki wa dhati bali walivutiwa na urafiki wa ngono! Huku akiwa anavutiwa sana na fani ya uanamitindo, Glory alikuwa anajaribu kutafuta rafiki kutoka ng'ambo ambae angemsaidia kwa namna moja au nyingine katika kujiimarisha katika nyanja hiyo. Katika kupitia marafiki kadhaa, ndipo akakutana na wasifu wa mtu ambae alimgusa vilivyo. Rafiki huyu alijitambulisha kama Aesha Suleiman, Mtanzania mwenye uraia wa Scotland ambae anafanya kazi za uanamitindo barani Ulaya. Kutokana na maelezo yake mafupi kwenye mtandao huo, Aesha alikuwa na mpango wa kuanzisha shule kubwa

ya uanamitindo ukanda wa Afrika wa Mashariki. Kwavile alikuwa hajafika nchini kwa muda mrefu, alikuwa anatafuta mtu ambae angempatia taswira ya tasnia hiyo kwenye ukanda huu. Aidha, maelezo hayo yaliendelea kwamba, katika hangaika hiyo ya kutafuta mtu kutoka ukanda huu, ndipo akakutana na maelezo mafupi ya Glory ambayo yalimvutia baada ya kuona nae ni mdau katika tasnia hiyo!

# 2

Hii ilikuwa ni moja ya siku zenye pilikapilika nyingi hususani jijini Dar es salaam. Miongoni mwa watu walioonekana kuwa na pilikapilika zaidi ni Bwana Bwana Hassan Muki, Mwenyekiti wa chama cha siasa kinachoitwa *Democracy and Resources For All*, kwa kifupi DRFA! Bwana Bwana Hassan Muki alionekana ni mtu mwenye haraka ya kuwahi aendako! Alikuwa anawahi nyumbani kwake maeneo ya Kijitonyama kukutana na wenzake ifikapo saa tatu usiku!

Glory Mushy, msichana wa Kitanzania mwenye ndoto kubwa za kujiendeleza kwenye fani ya uanamitindo alikuwa anakaribia kutua kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Bangkok, nchini Thailand. Safari yake ya Bangkok ilianzia London Uingereza akitokea Dar es salaam baada ya kupata mwaliko kutoka kwa rafiki yake mpya, Aesha Suleiman. Baada ya mawasiliano ya mara kwa mara, hatimae Aesha alimtumia Glory tiketi ya ndege kwa kile alichodai akashuhudie maonesho makubwa ya mitindo yaliyotarajiwa kufanyika jijini Bangkok!

Glory aliondoka Dar es salaam wakati akiwa juu ya kilele cha mafanikio! Hakuna mtu ambae ungemwuliza kuhusu Glory Mushy akashindwa kumfahamu! Si uzuri na urembo wa kuzaliwa nao pekee ndio ulimfanya afahamike na kupendwa na wengi jijini humo, bali pia ni tabia njema

aliyokuwa anaionesha kwa kila mtu. Glory alikuwa ni miongoni mwa wasichana wachache sana wenye majina makubwa ambae alikuwa hajawahi kukumbwa na kashfa yoyote ile! Hakika, yeye alikuwa ni mfano wa kuigwa kwa msichana yeyote yule, awe mwanamitindo au vinginevyo. Kutokana na hilo, alikuwa ni mtu mwenye kuheshimiwa mno jijini Dar es salaam kiasi cha wakati fulani kupewa heshima ya kwenda kuonana na kiongozi mkuu wa nchi!

Siku yake ya kwanza kufika jijini London, Glory alipokewa na dada wa makamo ambae alishajulishwa kabla na *rafiki* yake Aesha kwamba ni dada mkubwa wa rafiki yake huyo! Alikaa hapo London kwa siku tatu kisha akaandaliwa safari ya kwenda Bangkok.

Tofauti na matarajio yake, ndoto za Glory ziliyeyuka juma moja tu tangu aingie jijini Bangkok! Siku zilipoyeyuka ndoto zake ilikuwa ni siku tatu kabla ya kuanza kwa maenesho ya mitindo aliyoahidiwa na rafiki yake kwamba akayashuhudie. Siku hiyo ambayo ilibadilisha kabisa historia ya maisha yake, aliagwa na Aesha kwamba anaenda mazoezini na angerejea jioni. Hata hivyo, jioni hiyo Aesha hakurejea na siku ya pili mchana aliletewa taarifa kwamba kuna msichana mmoja mwenye asili ya Afrika amekutwa ameuawa na mwili wake kutupwa kwenye viunga vya jiji la Bangkok!!

Huo ukawa ndio mwanzo wa kuharibika maisha ya mrembo huyu! Muda wa kukaa hoteli aliyofikia ulikuwa unaisha siku hiyo na pale alipoenda mitaani ili akajaribu kutafuta makazi ya bei nafuu, ghafla alivamiwa na vijana wa kihuni na kumpora kila kitu ikiwa ni pamoja na hati ya kusafiria! Kabla hajafahamu cha kufanya, alitokea msichana mmoja mwenye asili ya Kisomali aliyejitambulisha kwake kwa jina la Nuraiyah. Kukutana

kwake na Nuraiyah ulikuwa ndio mwanzo wa maisha ya kihalifu kwenye ya nchi ya kigeni akijihusisha zaidi na uuzaji wa mihadarati na ukahaba! Hata hivyo, pesa zilizopatikana kwenye shughuli yake hiyo mpya zilikuwa zinaenda kwa tajiri yake na yeye kuachiwa kiasi kidogo tu cha kumwezesha kuishi!

"Ndugu zangu nimewaita hapa ili tujadili jambo nyeti sana, lakini lenye umuhimu mkubwa kwa mustakabali wa chama chetu." Hatimae Bwana Hassan Muki alianza kuwaeleza wenzake baada ya wote kuwa wameshawasili: "Kwa kifupi ni kwamba juma lililopita nilikutana na mmoja wa viongozi waandamizi wa CDTPE; Bwana George Malilo na kunieleza nia ya taasisi yake ya kutaka kukisaidia chama chetu. Aidha, leo nilikutana nae tena akiwa na mwenzake mmoja ambapo kimsingi wameahidi kutupatia fedha za kukiimarisha chama. Hata hivyo, ili wasijiingize matatani na serikali, wanataka kusaidia harakati zetu kwa siri! Kutokana na hilo, ndio maana nimeamua kuwaita ili tuweze kujadili suala hilo kwavile nisingeweza kutoa maamuzi peke yangu kwa jambo linalohusu chama."

Pamoja na Bwana Bwana Hassan Muki, kikao hiki pia kilihudhuriwa na Katibu Mkuu wa DRFA, Bwana Anatory Saibaba, Makamu Mwenyekiti Bi. Theresia Mwaipopo, Kiongozi wa Umoja wa Vijana Bwana Dunstan Mkundi na Mweka Hazina Bi. Fatma Mosha. Minong'ono ikaanza kuibuka miongoni mwao kabla Bwana Dunstan Mkundi hajanyoosha kidole na kuhoji:

"Binafsi ningependa kufahamu vigezo walivyotumia kuchagua chama chetu badala ya chama kingine!"

"Sababu ya msingi ya kutuchagua sisi ni kwavile tayari tumeuthibitishia umma kwamba DRFA kinalenga kujenga demokrasia ya kweli na kuwaondelea wananchi umaskini. Na huo ndio mtazamo wa CDTPE."

"Je, kuna masharti yoyote yanayoambatana na msaada huo?" Aliuliza Bwana Saibaba.

"Bila shaka!, hawewezi kusaidia bila masharti yoyote. Hata hivyo masharti yenyewe ni ya kawaida kabisa. Mathalani, wametaka tuandikishiane mkataba wa siri ambapo siku ya kuandikishiana inabidi sote tuliopo hapa tuwepo. Aidha, wametaka pesa zitakazopatikana zitumike zaidi kukiimarisha chama kwenye maeneo yaliyosahaulika kimaendeleo pamoja na vijijini. Kwa mtizamo wao, sehemu kama hizo ni rahisi zaidi kupata ufuasi kwavile mazingira ya huko peke yake yanatosha kuihukumu serikali."

Baada ya maelezo hayo, wajumbe walianza kuyatafakari yote yaliyoelezwa na wakati ikionekana kama hamna mwenye swali zaidi mara Bi. Fatma Mosha aliinua kidole juu kuonesha kwamba ana swali.

"Chama chetu hakina chanzo cha mapato kitakachoweza kuthibitisha uhalali wa fedha tutakazokuwa tunapewa; je tumejiandaa vipi kwa hilo?"

"Swali zuri sana, jambo hilo tumelijadili kwa mapana na marefu na ndio mjadala ambao nilitaka kwa sasa tuujadili vilevile. Hata hivyo, wao wametoa pendekezo lao ambalo tutalijadili tuone kama linafaa, vinginevyo tunaweza kutoa pendekezo la kwetu. Pendekezo lililopo ni kwamba kwavile mimi ni mfanyabiashara basi nitaingia ubia na kampuni moja ya uvuvi ambayo inatafuta mbia

hapa nchini. Wafadhili wakuu wa CDTPE wana uhusiano wa karibu na hiyo kampuni, yenye makao yake makuu nchini Denmark. Tutafungua akaunti kwenye benki moja hapa nchini nami nitakuwa mmoja wa watia sahihi waandamizi wa akaunti husika. Hivyo basi, CDTPE watakuwa wanapitishia pesa zetu huko kutokea nchi za Ulaya nami nitakuwa nazichukua kwa matumizi ya chama ingawaje zitaingia kule kama pesa za kampuni." Alimalizia na kutoa nafasi ya kujadili suala zima kwa urefu.

Glory alibakiwa na muda mfupi tu ili aende danguroni! Alifanya maandalizi yake ya mwisho lakini kabla hajatoka, mlango wa chumba chake uligongwa!

Akashangaa!

Hakutarajia kupata mgeni yeyote muda huo! Kutokana na yeye kuishi Thailand kinyume cha sheria na kufanya biashara haramu, basi wakati wote alikuwa ni mtu mwenye kuchukua tahadhali ili asije kutumbukia kwenye mikono ya sheria. Huku akiwa mwenye hofu, alienda kufungua mlango na hapohapo mtu aliyevalia sare za jeshi la polisi wa Thailand aliingia na bastola mkononi!

*"Glory, siku utakayoingia mikononi mwa polisi, fahamu itakuwa ndio mwisho wako kwavile hii nchi ina sheria kali sana dhidi ya wahamiaji haramu,biashara ya ukahaba na madawa ya kulevya!"* Glory alikumbuka maonyo ya Nuraiyah aliyokuwa anayatowa kwake mara kwa mara! Baada ya kukumbuka onyo hilo, Glory alijikuta akipata nguvu za ziada za kupambana kwa kuokota kiti kilichokuwa humo chumbani na kumtwanga nacho huyo mtu! Hapohapo, huyo mtu aliyevalia sare za jeshi la polisi alisita na ghafla akala

mwereka hadi chini huku mboni za macho yake zikiwa zimejipinduwa kwa juu!

Akaonesha dalili zote za mtu mfu!

Kabla hajajua nini cha kufanya, ghafla mlango wa chumba ulifunguliwa na Nuraiyah akaingia!

"*My god* (mungu wangu)! Umeua Glory! Tutakimbilia wapi kwenye nchi hii ya kigeni wakati hatuna hata hati za kusafiria!" Nuraiyah alilalamika mara baada ya kuingia humo chumbani!

"Tena umeua polisi!!" Nuraiyah alizidi kulalamika!

"Nilitaka kujiokoa Nuraiyah kwavile ulishawahi kunitahadharisha nisiangukie mikononi mwa polis!" Glory alijitetea huku mwili wote ukiwa unatetemeka kwa hofu!

"Ndio nilikutahadhalisha lakini sikukutuma kuua!" Nuraiyah alizidi kulalamika kisha akamshika mkono na kuondoka nae hadi kitongoji kingine cha mbali kabisa na hapo!

Baada ya kuwa mafichoni, Siku iliyofuata Nuraiyah alimuaga Glory kwamba anaenda kuangalia hali ya hewa ya kule walikotoroka huku akimuonya kutotoka nje. Aliporudi mchana, alikuwa na gazeti mkononi ambalo kabla hajaongea lolote alimtupia Glory!

"Angalia *kisanga* ulichoanzisha Glory!"

Huku akionekana kutawaliwa na hofu, Glory alichukuwa gazeti hilo na kama alivyotarajia alikuta likiwa limepambwa na picha zake kadhaa zikiambatana na maelezo kwamba anatafutwa kwa udi na uvumba!

George Kamau alikua anafurahia ushindi wao katika kumnasa Glory! Alikuwa na kila sababu ya kufurahia

kwavile haikuwa kazi rahisi! Kamau aliamini umaarufu na tabia njema aliyokuwa nayo Glory vingekuwa kikwazo katika kumwingiza kwenye shughuli zao haramu hivyo ikamlazimu kutumia mbinu mbalimbali katika kufanikisha azma hiyo!

Mbinu za Kamau katika kumnasa Glory zilianzia kwenye mtandao wa *Face Book* pale Glory alipokutana na Aesha kwenye mtandao huo. Jambo ambalo halikufahamika kwa Glory ni kwamba, mawasiliano kati yake na Aesha yalikuwa yanaratibiwa na Kamau! Aidha ni Kamau huyo huyo ndie aliyekuwa amegharamia safari ya Glory toka Dar es salaam hadi Bangkok!

Baada ya Glory kuwasili Bangkok, mbinu za Kamau nazo zikahamia huko! Mbinu hizi zilianzia kwenye kifo cha uongo cha Aesha hadi kifo cha uongo cha kijana aliyejifanya polisi, wakati ni kijana wa kihuni anayepatikana kwenye viunga vya Bangkok! Hata gazeti lililobeba picha za Glory kwamba anatafutwa na kuletwa kwake na Nuraiyah, lilikuwa ni kipeperushi tu kilichofanana na gazeti ambacho Kamau alikuwa ameshakiandaa siku chache zilizopita!

Aesha, ambae jina lake halisi ni Nurait pamoja na Nuraiyah, ni mawakala wa George ambao aliwaajiri kwa muda kwa ajili ya kumnasa Glory tu! Wote hao wana asili ya Somalia huku wakiwa wamekulia Mombasa! Katika kufanikisha jambo hilo, wasichana hao wa Kisomali kwa kutumia maelekezo ya George Kamau, walifanikiwa kutegesha kamera za siri kwenye chumba cha Glory pamoja na kule alikokua anafanyia biashara ya ukahaba na mihadarati! Katika hili wakafanikiwa kupiga picha zilizoonesha matendo yote machafu ya Glory! Aidha, Kamau nae akazitumia picha hizi chafu pamoja na matatizo

ya Glory kuwa nchi ya kigeni katika kumshinikiza kuingia kwenye shughuli zao!

Aidha, kwa kutumia mbinu nyingine sawa na hizi, Michael Mchupi; mshirika wa Kamau alifanikiwa kumnasa msichana mwingine mrembo aliyeitwa Wendy!

# 3

Jonas Siyame aliteremka kaunta ya chini ya hoteli aliyofikia iliyopo kwenye pwani ya Cancun, nchini Mexico. Alikuwa amefika jijini hapa kwa ajili ya mapumziko mafupi ya mwisho wa mwaka!

Cancun ni miongoni mwa sehemu ambazo kila wakati Jonas aliziota kuwa angejitahidi angalau mara moja katika maisha yake aweze kufika na kujionea mwenyewe. Hivyo basi, akiwa ni kiongozi mwandamizi wa TAKUKURU mwenye mshahara wa kutosha, aliweza kujiwekea akiba na kutimiza ndoto yake hiyo.

Umaarufu wa Jonas Siyame ulitokana na jitihada zake za kupambana na rushwa nchini bila kumuogopa wala kumuonea aibu mtu yeyote. Hili alilimudu kutokana na utaratibu aliojiwekea wa kutotaka kujichanganya ovyo na watu, hivyo kutoa nafasi finyu ya kuzoeleka! Tofauti na wakubwa wenzake, kwa upande wake alijizuia kuzoeana na wafanyabiashara wakubwa na hata wanasiasa; kwavile aliamini hao ndio maadui namba moja kwenye vita dhidi ya rushwa. Si wanasiasa na wafanyabiashara wakubwa pekee ambao alijiepusha nao; bali hata viongozi wengine wa taasisi nyeti kama vile jeshi la polisi na taasisi za dini. Hawa wote aliwakwepa na kukutana nao pale tu ilipobidi. Wengi wao walimchukia kutokana na tabia yake hii; na wapo waliomwita ana majivuno!Mbaya zaidi, alichukiwa hata na baadhi ya wakubwa wenzake ndani ya TAKUKURU yenyewe!

Bila mwenyewe kujua, mawakala wa IBU walikuwa Cancun kwa ajili yake! Baada ya  majaribio kadhaa ya kumnasa akiwa Tanzania kugonga mwamba, IBU waliamini kwamba Jonas nae ananunulika, jambo la msingi ni kutafuta eneo muafaka la *kufanya nae biashara*! Hivyo basi, baada ya kupata fununu kwamba angekuja Cancun, walikata shauri la kufunga nae safari hadi huku bila Siyame mwenyewe kujua!

Jonas alifika sehemu aliyoihitaji na kuvuta kiti na kuketi. Aliangaza macho yake huku na huko na kushuhudia ukumbi ukiwa na watu wengi wa mataifa mbalimbali. Hata hivyo, watu weusi kama yeye walikua ni wachache sana ambao aliamini wengi wao kama sio wote wangekua ni kutoka bara la Amerika.

Baada ya kuagiza alichohitaji, aliyarudisha mawazo yake nyumbani na kuufikiria mustakabali wa nchi yake. Alirejesha akili yake kazini, kazi ambayo aliipenda kwa moyo wake wote na kuitumikia kwa uwezo wake wote. Alishangazwa kwa jinsi ambavyo wakubwa wenzake walivyokua wakimchukia pale kazini ingawaje chuki yao hawakuionesha wazi! Kuna wakati alifikiria kuacha kazi baada ya kugundua mizengwe iliyokua imeandaliwa dhidi yake; hata hivyo baadae alifuta wazo hilo. Baada ya kufuta wazo la kutaka kuacha kazi alijikuta ni kama mtu aliyezaliwa upya! Akaapa kupambana na wala rushwa hadi tone la mwisho la damu yake! Kwavile alishajua kwamba adui wa kiapo chake ni binadamu wenzake tena pengine wale walio karibu kabisa na yeye basi akakata shauri la kujitenga na watu kwa kadri alivyoweza!

Jonas hakua mtu wa baa, wala mtu wa kwenye kumbi za starehe! Pale alipojisikia kukata kiu kwa bia, basi angeweza kuzinunua na kwenda kunywea nyumbani!

Ajabu zaidi, alijitenga hata na wanawake kwavile aliamini hao ndio sumu zaidi kwavile wangeweza kutumiwa katika kumwangamiza! Jonas alikua na uhakika kwamba kutokana na msimamo aliokua nao basi kwa vyovyote vile alikua na maadui wengi sana.

"Hapana, mie Dar es salaam sio mwenyeji sana. Nimezaliwa, kukulia na kusomea Arusha!" Ghafla sauti nyororo ilijipenyeza masikioni mwa Jonas na kumzindua toka kwenye lindi zito la mawazo! Bila kutarajia alijikuta akigeuka na kutafuta ni wapi ilikotokea sauti hiyo! Kwa kifupi, ni kama alipatwa na mshituko! Hakutarajia kabisa kwamba sehemu ile angekuwapo mtu toka Afrika ya Mashariki; achilia mbali Tanzania!

Aliangaza macho huku na huko lakini hapakuonesha dalili ya mtu aliyeongea kiswahili kile fasaha! Alijaribu kuwaibia mmoja baada ya mwingine lakini hakuambua kitu! Alitamani sana kufahamiana na huyo mtu. Alitamani angetokea mswahili yeyote akampigia simu muda huo ili aongee nae kwa sauti ambayo aliamini ingeweza kusikika na hao aliokua akiwatafuta ambao bila shaka wangevutiwa nae tu! Watanzania tulivyo, tukikutana ugenini tunakua marafiki hata kama huko tulikotoka tulikua maadui! Ndio, Jonas hakua mtu wa kuzoeana na watu ovyo ovyo, lakini si ughaibuni kama huku. Isitoshe, alichokua anajizuia yeye ni kuzoeana na watu ambao baadae wangekuja kumchafulia kazi yake!

Baada ya kutoonekana kwa dalili ya mtu aliyekua akimtafuta, aliamua kuendelea na kinywaji chake.

Akiwa tena amezama ndani ya fikra nzito mara akaona wasichana wawili wakija upande wake. Hata hivyo, hakufahamu ni kwanini alielekea kuvutika nao; labda ni

kwavile mmoja alikua msichana mzungu na mwingine alikua mwenye asili ya Afrika.

Wasichana wale waliendelea kumkaribia huku ikionekana kwamba yule mwafrika alikua anamsindikiza tu yule msichana wa kizungu. Hata hivyo, hakuna hata mmoja miongoni mwao aliyeonekana kuvutika na kuwapo kwa Jonas mahali pale! Wasichana hao walisogea mbele kidogo kisha wakasimama na kuagana.

"*Take care* Wendy, tutaonana!" Yule dada wa kizungu aliongea wakati akiagana na mwenzake!

"*Thanks* Babara, nenda salama!"

Jonas akafurahi!

Akafurahi kugundua kumbe yule mtu aliyekua kwa muda mrefu akipepesa macho kumtafuta hatimae kamfahamu, tena hadi kwa jina! Alifurahi zaidi alipogundua yeye hakuweza kufahamu kwamba pale kuna Mtanzania mwenzake; hivyo akaamua kwenda kumfanyia *suprise (*kumshitukiza)! Aliamini kwa vyovyote iwavyo, Wendy angefurahi kufahamiana nae huku ughaibuni!

Jonas alifanya haraka kumaliza kinywaji chake kisha akainuka na kwenda alipokaa Wendy!

"Samahani Wendy, sijui kama naweza kukaa?!" Hatimae Jonas alimweleza huyo msichana huku akitabasamu. Mshangao uliokuwapo machoni kwa Wendy ungeweza kugundulika hata na mtu aliye umbali wa meta kadhaa kutoka hapo!

"Karibu kaka yangu, ingawaje unanitisha kidogo!"

"Ondoa hofu Wendy, mie ni rafiki yako wa siku nyingi, labda tu umenisahau!" Jonas alijitia uchakaramu huku akivuta kiti na kukaa jirani na msichana huyo; huku Wendy nae akiendelea kuwa ndani ya mshangao wa kuigiza!

Waliendelea kuongea mambo mbalimbali huku wakila na kunywa. Kadri muda ulivyoenda ndivyo walivyozidi kuzoeana na kuonekana ni kama watu waliofahamiana kwa muda mrefu! Kitu kimoja kilimtia Jonas hamasa ya kuendelea kufahamiana na msichana huyo mrembo. Jambo lenyewe ni ile kugundua kwamba Wendy hakua hapo kwa ajili ya kumsubiri mwanaume, bali mwanafunzi mwenzake ambae ni raia wa Mexico.

"Kwahiyo Wendy umesema unaishi Miami sio?! Je, unashughulika na nini Marekani?"Hatimae Jonas aliuliza.

"Nipo Marekani kimasomo, nachukua shahada ya pili ya Menejementi ya Utalii. Hata hivyo, kwa sasa nipo likizo na wiki ijayo naenda Tanzania!" Wendy alijibu kwa sauti yake nyororo iliyojaa ushawishi. Kadri sekunde zilivyoenda, ndivyo Jonas alivyozidi kuchanganyikiwa zaidi. Kwa kifupi tayari alishadondoka penzini, tena si kidogo! Aliamini kwamba Wendy alikua na sifa zote za kuwa mke wa bosi kama yeye!

"Samahani Jonas, unaonaje tukienda kukaa kwa kule?" Wendy alitoa wazo huku akinyoosha kidole chake. Wazo ambalo lilifurahiwa zaidi na Jonas kwavile sehemu ambayo ilipendekezwa ilikuwa imejificha kidogo, hivyo Jonas aliamini angekua huru zaidi kuliko hapa!

Bila kupoteza muda walimaliza sehemu ndogo ya vinywaji vyao kisha wakaenda kutafuta sehemu ambayo haikua na watu wengi.

Msururu mrefu wa magari ulionekana barabara ya Chang'ombe karibu na makutano na Barabara ya Nyerere. Mmoja wa watu waliokuwamo katikati ya rabsha hii ni

kijana Bon Mtambo aliyekua akiendesha kuelekea nyumbani kwake Chang'ombe. Ingawa alikuwa amebakiza umbali mfupi tu, lakini ufupi wa safari yake ulimezwa kabisa na urefu wa msururu huu wa magari.

Msururu ulianza kutembea lakini alipokaribia TAMECO, mara gari moja iliyotokea maeneo ya Chang'ombe iliingia kwa kasi barabarani na kutaka kushika barabara ya Taifa. Kufumba na kufumbua, Bon Mtambo alijikuta akiivaa gari hii ambayo iliserereka na kwenda kugota kwenye nguzo ya umeme iliyokua jirani na hapo. Kwa kasi ya umeme, Bon Mtambo aliegesha gari yake pembeni na kuifuata gari aliyoigonga!

Hamadi!

Kwenye gari kulikuwa na mtu mmoja tu aliyekuwa upande wa dereva! Alikuwa ni msichana wa makamo aliyeelekea kuwa na umri usiozidi miaka ishirini na tano. Msichana huyu alionekana kupotewa na fahamu pengine kutokana na msukosuko alioupata. Bon Mtambo alibaki ameduwaa kutokana na uzuri wa msichana huyu! Pamoja na kwamba alikuwa amepoteza fahamu lakini bado nuru ya uzuri wake iliendelea kuonekana waziwazi pasipo na kizuizi chochote!

Hakika alikuwa ameumbika hasa!

"Mbona mnashangaa shangaa badala ya kumsaidia?!" Ghafla mama mmoja alipiga kelele na kumzindua Bon Mtambo! Bila kujiuliza mara mbili, alifungua mlango wa gari na kumbeba huyo msichana tayari kwa kumwaisha hospitali moja kubwa inayomilikiwa na mmoja wa marafiki zake wakubwa.

"Shamte, mchunguze huyu dada nami nitarejea muda si mrefu." Bon Mtambo alitoa maelekezo kwa Dk. Shamte mara baada ya kumfikisha mgonjwa wake

hospitali. Alimuacha na kurudi eneo la ajali ambako alikuta askari wa usalama barabarani wameshakamilisha kazi yao na kuondoka na gari hadi kituo cha polisi cha Chang'ombe. Kikubwa kilichomfanya arudi ni ukweli kwamba alijua gari ya yule msichana ingepelekwa kulazwa kituo cha polisi jambo ambalo yeye kama Bon Mtambo hakutaka litokee. Si kwamba hakutaka kumtia matatizoni yule msichana, la hasha! Alichotaka ni kwamba gari ikakae nyumbani kwake ili yule msichana akishatoka hospitali aifuate gari nyumbani kwake yeye na sio polisi. Kwa kifupi ni kwamba tayari Bon Mtambo alishampenda mtoto wa watu!

Baada ya kufika eneo la ajali na kukuta gari imechukuliwa, Bon Mtambo alienda moja kwa moja kituo cha polisi Chang'ombe ambapo baada ya kujitambulisha kwa mkuu wa kituo kwamba yeye ni nani aliruhusiwa kuondoka na gari.

*"Ama kweli mungu ana mambo yake. Kama si hii ajali ningepata wapi nafasi ya kukutana na mrembo kama huyu!"* Bon Mtambo alijisemea mwenyewe wakati akipiga honi kwenye lango la kuingilia nyumbani kwake alikoiacha gari ya mgonjwa wake na kurejea hospitali!

ᏇᏅᏍᏔᏇ

"Hebu niambie Wendy, unazani sekta ya utalii inaweza kuinua uchumi wa nchi yetu?" Hatimae Jonas aliuliza mara baada ya kuketi sehemu waliyohamia. Wendy alijihisi kijasho chembamba kufuatia swali hilo! Si kwamba hakua na jibu la swali aliloulizwa, la hasha! Kwake Wendy, hii ilikua ni kama bahati ya mtende kuota jangwani! Alikusudia kuitumia nafasi hiyo kujionesha ni namna gani

anavyochukizwa na rushwa, jambo aliloamini litamsaidia kumweka jirani zaidi na Jonas!

"Bila shaka Jonas, hii sekta ingekuwa na mchango mkubwa kiuchumi lakini ubadhirifu, rushwa na kutozingatia vipaumbele ndiko kunakokwaza ukuaji wa sekta hii!" Wendy aliongea huku *uchungu* ukionekana dhahiri machoni mwake, kisha akaendelea, "Endapo sekta ya utalii itawekezwa kwa kuzingatia maslahi ya taifa basi sina shaka kwamba uchumi wetu utapaa. Jambo la msingi tunalotakiwa kutosahau ni kwamba sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta chache duniani ambazo zina ushindani mkubwa kibiashara miongoni mwa nchi tajiri na maskini!"

"Aidha, suala la soko la namna gani vilevile ni muhimu sana kwetu kwavile kama nilivyoeleza hapo awali, nchi maskini na tajiri duniani tunagombea soko la utalii. Kama uonavyo hapa, asilimia kubwa ni watalii watokao sehemu mbalimbali duniani na kuja hapa kwa mapumziko. Ukifika Marekani ni biashara ya utalii. Ukienda Amerika ya Kusini hadi Asia, huko nako wanajiimarisha katika biashara za utalii. Australia, New Zealand, hadi visiwa vya Karibeani; huko kote wapo kwenye jitihada za kujiimarisha kwenye sekta hii! Ulaya nako, kuanzia kusini hadi kaskazini; mashariki hadi magharibi, ni utalii! Hadi nchi za kiarabu ambazo awali usingezifikiria kufanya biashara ya utalii wa kimataifa, leo hii zinafanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta hiyo!"

"Jonas, nimekupa mnyambuliko huo ili kukuonesha ni namna gani soko katika biashara ya utalii lilivyo la ushindani duniani! Hivyo basi, kama ilivyo kwa biashara nyingine yoyote ile, ni lazima nchi yetu ijue ni soko gani hasa tunalotafuta! Kujitapa tu kwamba kuna Mlima

Kilimanjaro, mbuga za wanyama za Serengeti na nyingine kama hizo bado haitoshi. Tatizo letu tunazani watu wengi duniani wanafahamu na wana hamu sana ya kuuona Mlima Kilimanjaro, Mbuga za Serengeti, Manyara na vivutio vingine kama hivyo, isipokuwa wasichofahamu ni nchi gani vilipo vivutio husika! Tuna vivutio vingi sana, lakini biashara ya utalii bado ni ndogo! Hapo ndipo tunapopaswa kuanza kujiuliza tatizo hasa ni nini!"

"Kwa mtizamo wangu, nchi yetu bado haifahamiki; hali kadhalika vivutio vyetu navyo bado havifahamiki vizuri, hususani kwa watu wa kawaida, ambao ndio watalii wenyewe! Hivyo basi, pale tunapofikiria kuutangaza utalii wetu basi hatuna budi kujiuliza tunataka kutangaza nini na ni nani mlengwa wetu! Hii ni lazima iende sawia na kuitangaza nchi yetu na kumfanya mlengwa avutiwe kwanza na nchi yenyewe. Si hivyo tu, lazima tujiulize ni kwanini tunataka kutangaza hicho tulichokusudia kutangaza. Ndio, tunataka kuutangaza mlima Kilimanjaro. Lakini bado tunalazimika kumshawishi mlengwa wetu ni kwanini aje kuupanda Mlima Kilimanjaro na si mlima mwingine wowote ule duniani. Hebu fikiria, Msweden wa kawaida, asubuhi akichungulia nje ya dirisha la nyumbani kwake anakuta mabarafu yameganda barabarani! Pamoja na hilo, unaamua kumshawishi aje kuona Mlima Kilimanjaro eti tu kwavile una barafu kwenye kilele chake wakati mlima wenyewe upo kwenye ukanda wa tropiki! Unazani hapo unaweza kumshawishi wakati kwake barafu ni kitu cha kawaida? Kwani yeye ni mtafiti wa mambo ya jiografia? Na ni mtafiti gani huyo ambae hadi leo hii hajafahamu maajabu haya ya Mlima Kilimanjaro?! Jonas, tunatakiwa kujiuliza maswali sawa na hayo wakati tunapotarajia kutangaza aina kwa aina ya vivutio vyetu."

"Nionavyo mimi, wakati umefika wa kuviongezea thamani vivutio vyetu na kuachana na mazoea. Mathalani, ndani ya mbuga za wanyama kwenyewe, tunaweza kuweka bustani za wanyama zitakazowapa nafasi watalii kuwaona wanyama mbalimbali waliopo, kwa nafasi na ukaribu zaidi kiasi cha hata kupiga nao picha katika msimu wote wa mwaka. Ni bahati mbaya sana sijawahi kufika Mlima Kilimanjaro, lakini naamini kabisa mlima huo unaweza kuufanya uwe na vitu tofauti na vile vilivyozoeleka! Mathalani, kutoka usawa fulani wa bahari, tunaweza kuchonga barabara kuzunguka mlima ambapo watalii watapata nafasi ya kuendesha magari, baiskeli, pikipiki au hata farasi kuuzunguka mlima na hivyo kuwapa nafasi ya kujionea nini kinapatikana upande mwingine wa mlima! Hata kama hatutakamilisha mzingo wote wa mlima, lakini angalau tukifikia sehemu iliyo nje ya upeo wa macho yetu. Barabara hizi zinaweza kuchongwa kupitia umbali tofauti tofauti kutokea usawa wa bahari na hivyo kutoa nafasi ya kujionea sura ya dunia ya mlima huu. Asikuambie mtu Jonas, kila mmoja angependa kuona nini kilichopo nje ya upeo wa macho yake! Aidha, kwa kushirikiana na makampuni makubwa duniani, tunaweza kuanzisha mashindano ya mbio za kuzunguka mlima kwa magari, pikipiki na hata hata mbio za farasi!Vilevile si ajabu hiyo ikatusaidia kugundua urithi mwingine uliofichika!"

"Lakini huoni aina hiyo ya utalii itasababisha uharibifu wa mazingira?"Hatimae Jonas aliuliza.

"Sizani kama inaweza kusababisha uharibifu wa mazingira. Sana sana itapunguza uharibifu kwavile tatizo kubwa lililopo Mlima Kilimanjaro ni uchomaji hovyo wa misitu. Hivyo basi, utalii wa aina hiyo utawanyima

wachomaji moto nafasi ya kutenda uhalifu wao kwavile ukimya uliopo kuzunguka mlima utakuwa umetoweka."

"Endelea Wendy na maelezo yako kwavile inaonesha nilikuwa nimekukatisha."

"Ni kweli Jonas, ulikuwa umenikatisha. Hata hivyo, wakati mimi naendelea unaweza wakati wowote kuuliza jambo ambalo utahisi hujalielewa."

"Sawa Wendy."

"Hata hivyo Jonas, maelezo yangu yaliyotangulia yanalenga uongezaji wa thamani ya bidhaa kwenye vivutio vyetu. Lakini hata kama tutaongeza thamani hiyo kwa maradufu bado haitakuwa na maana endapo tutakosa mbinu za kushawishi soko hilo la utalii kuja kushuhudia vivutio vilivyopo. Hapa namaanisha mikakati ya kutangaza vivutio vyenyewe. Ni bahati kwamba serikali yetu imelipa kipaumbele suala la utangazaji wa vivutio vyetu kupitia vituo ya televesheni kama vile CNN. Hata hivyo, pamoja na nia nzuri ya serikali sizani kama mbinu hii inaweza kuleta tija inayotarajiwa. Ni bahati mbaya sana nchini kwetu hatuna utamaduni wa kufuatilia matokeo ya mikakati mbalimbali ambayo tunaifanya. Lakini naamini endapo leo hii angetokea mtu akafanya utafiti wa kuangalia ni namna gani mbinu hii imesaidia katika kuongeza idadi ya watalii basi si ajabu angeshauri vinginevyo."

"Wasiwasi nilionao ni kwamba matangazo kwa kutumia vituo vikubwa vya televisheni ni gharama sana kiasi kwamba itatuwea vigumu kuyaweka matangazo yetu hewani kwa muda mrefu. Hapa lazima ikumbukwe kwamba, tunavyotangaza utalii kwa nchi kama Tanzania ni tofauti kabisa na utakavyoutangaza utalii wa nchi kama Afrika Kusini. Tangazo la nusu, au hata robo dakika linatosha kabisa kutangaza vivutio vya Afrika Kusini au

Nigeria kwavile tayari nchi hizo zinafahamika duniani hivyo wanachohitaji kufahamu ni nini watakikuta watakapoamua kutembelea nchi hizo. Hii ni tofauti kabisa na nchi yetu ambayo si maarufu duniani. Hivyo basi, kama nilivyosema hapo awali matangazo ya vivutio vyetu hayana budi kwenda sawia na kuitangaza nchi vilevile. Kutokana na ukweli huo utaona ni namna gani matangazo yetu yanavyohitaji kuhusisha mambo mengi ili yaweze kuwavuta wahusika. Na endapo mambo yote ya msingi tutayahitaji kwenye matangazo yetu basi bila shaka yatahitaji muda wa kutosha kuwa hewani ambao ni gharama sana."

"Lakini Wizara ya Utalii na Mali Asili ina tovuti yake, huzani huko kunafaa zaidi kwavile kila kitu kuhusu Tanzania na vivutio vyake kitapatikana kwenye tovuti husika kwa gharama nafuu!?" Hatimae Jonas alihoji.

"Unayosema ni kweli kabisa, lakini ni watu wangapi wanaifahamu hiyo tovuti? Ikiwa nchi yenyewe haifahamiki, unatarajia tovuti yake itafahamika vipi?! Hata hivyo, hiyo ni changamoto kwetu kwamba ikiwa kuna vitu tunavyotakiwa kuvitangaza duniani basi tovuti hii iwe ni kitu cha kupewa kipaumbele. Kosa kubwa linalofanyika Tanzania na duniani kwa ujumla ni ile kuzani kwamba ukishakuwa na tovuti tayari umeshamaliza kazi! Tovuti nayo ni bidhaa ambayo nayo inapaswa kutangazwa ili watumiaji wa intaneti wapate kuifahamu na kushawishika kuitembelea. Hivyo basi endapo tungeweza kuitangaza tovuti yetu ambayo itahusisha masuala ya utalii peke yake basi bila shaka tunaweza kupata matokeo mazuri."

"Pamoja na matumizi ya intaneti, matumizi ya *intraneti* nayo bila shaka yanaweza kuwa na msaada mkubwa sana kwetu. Kama ujuavyo, makampuni na taasisi

mbalimbali duniani hivi sasa yana njia za mawasiliano ya mtandao wa ndani kwa ndani yanayojulikana kitaalamu kama *intraneti*. Njia ya *intraneti* inaweza kusaidia sana kutangaza vivutio vyetu duniani tena kwa ufanisi mkubwa. Tunachotakiwa kufanya hapa ni kuchagua angalau nchi moja ya majaribio (*pilot country*) kwa kigezo kwamba nchi yenyewe iwe ni yenye taasisi na makampuni makubwa yenye wafanyakazi wengi wanaokaa ofisini. Baada ya kupata taasisi hizo hapo tunaweza kufanya nao mazungumzo ya kibiashara yatakayotuwezesha kutuma matangazo na taarifa mbalimbali zinazohusiana na utalii kupitia kwenye mitandao yao ya intraneti. Hapo ikumbukwe kwamba, kwa kawaida mitandao ya intraneti inatumika na taasisi husika kama mbao zao za matangazo kwa matukio mbalimbali yanayotokea kwenye taasisi zao. Hivyo basi, uzoefu unaonesha kwamba wafanyakazi wanapoingia ofisini asubuhi ni lazima waangalie kuna taarifa gani mpya iliyoingia kupitia mtandao wao. Na kama ujuavyo, kila ofisi inafikia wakati wafanyakazi wanakua wamechoka huku wakisubiria muda tu waondoke. Inapofikia muda kama huo, wengi wao watapata nafasi ya kutosha ya kupitia matangazo yetu yaliyotumwa kwenye mtandao wao wa ofisi."

"Kwa upande mwingine, tunaweza kuvitumia vyuo vya elimu ya juu vilivyo nchi mbalimbali duniani kutangaza utalii wetu. Mathalani, tunaweza kuanzisha kitu kama *Tanzania Tourism Scholarship Award*; maalumu kwa wanafunzi wa kigeni wa shahada ya pili waliopo nga'mbo. Tunaweza kuweka viwango vya tuzo hizo kulingana na uwezo wetu, lakini jambo la msingi ni kwamba washindi wapatikane kutokana na uandishi wa insha juu ya utalii na vivutio vyake vilivyopo nchini. Hii itasaidia kuwafanya

wanafunzi hao kutafuta taarifa za kutosha kuhusu Tanzania na utalii kwa ujumla ili waweze kuandika insha zenye ushindani. Hivyo basi, hata wale ambao hawatafanikiwa tayari watakua wameshapata ufahamu mkubwa kuhusu Tanzania na vivutio vyake na bila shaka wanaweza kuja kuwa watalii kwa siku za usoni. Aidha, miongoni mwa tuzo tutakazoweka zinaweza kuwa za kuja kutembelea vivutio vyetu kwa gharama zetu wenyewe. Ni matumaini yangu kuwa wale watakaofanikiwa kupata tuzo hizo bila shaka watakuja na wenza wao."

"Hata hivyo, sina shaka kwamba kutakuwa na watu watakaoshangaa na hata kupinga kama sio kubeza kuona nchi maskini inatoa tuzo kwa wanafunzi kutoka nchi zilizoendelea! Lakini sisi lengo letu hapo sio kutoa msaada bali ni kutangaza biashara yetu! "

"Pamoja na hayo vilevile wakati umefika sasa wa kuzitumia ofisi zetu za ubalozi zilizopo sehemu mbalimbali duniani. Kwa maoni yangu nazani ingekuwa busara zaidi endapo baadhi ya balozi zetu zingekua na idara za utalii zenye maofisa watundu(*aggressive*) katika suala zima la masoko. Iwe ni wageni au watanzania, maofisa hao itabidi wawe wanafanyiwa tathmini ya utendaji wao kwa kuangalia ongezeko la idadi ya watalii. Jambo la msingi hapa ni kwamba, kabla ya mtu kuajiriwa ni lazima kwanza aeleze mikakati yake ili kuepuka kuajiri watu wenye vyeti vizuri lakini waliokosa ubunifu!"

"Pamoja na hayo......!"

"Samahani Wendy, hebu tufikirie kwamba kampeni hizo zimeweza kuongeza watalii wanaokuja nchini kwa maradufu, je unazani tuna miundo mbinu ya kutosha ikiwa pamoja na hoteli za kulaza wageni hao?"

“Upo sahihi Jonas kuhusu wasiwasi wako! Ni kweli wapo wanaoamini kwamba tatizo lingine linalokwaza kukua kwa utalii hapa nchini ni uhaba wa mahoteli yenye hadhi! Inawezekana, lakini sizani kama hilo nalo ni moja ya matatizo ya msingi yanayokwaza sekta hii!! Sizani kama wawekezaji wachache waliopo kwenye sekta ya mahoteli nchini wangeshindwa kujenga hoteli zingine endapo kungekuwa na soko la uhakika, kwa maana ya wateja au watalii wa kutosha. Katika hili, wapo vilevile wanaolalamika kwamba gharama za hoteli zipo juu sana. Ndio! Lazima ziwe juu kwavile wateja ni wachache hivyo hawana budi kutawanyisha gharama za uwekezaji kwa wateja wachache wanaokuja! Kwa kuangalia hilo, utagundua kwamba tatizo la msingi ni uhaba wa watalii na sio mahoteli. Watalii wakiongezeka, na mahoteli yataongezeka tu tena watakaoyaongeza ni wawekezaji hawahawa waliopo labda kama si wawekezaji makini! Leo hii, ukienda ng’ambo kutafuta wawekezaji kwenye mahoteli, watakuja tu! Hata hivyo, kabla hawajafanya chochote lazima kwanza watachunguza takwimu za watalii na wageni wengine wanaokuja nchini kabla hawajawekeza! Jambo moja tunajifanya hatulifahamu! Katika mazingira yaliyopo, inahitajika kazi ya ziada kuwavutia watalii kuja nchini mwetu! Wakati Afrika ya Kusini au Nigeria wangehitaji tangazo la robo dakika kusema wana Mlima Kilimanjaro, Tanzania ingehitaji angalau dakika moja kwavile ingelazimika kutangaza vitu viwili, kivutio na nchi!! Gharama hizi za kuitangaza nchi ndio kubwa zaidi kuliko kuvitangaza vivutio vyenyewe!! Ni gharama hizi za kuitangaza nchi ndizo wanazozikwepa wawekezaji wa sekta ya utalii!! Wajibu wa mfanyabiashara ni kuitangaza biashara yake, na sio kuitangaza nchi! Mwekezaji

angependa yule mtu wa kawaida awe kwanza anaifahamu Tanzania. Hii ni kwavile hata akija kuwekeza wakati watalii bado ni wachache, bado hatatumia gharama kubwa kuitangaza biashara yake. Gharama kwake hazitakuwa kubwa kwavile tayari soko litakuwa linafahamu kuna nchi inaitwa Tanzania lakini wasichofahamu ni nini wanaweza kukipata endapo wataamua kutembelea!! Pamoja na hayo, vilevile ni kweli kwamba endapo watalii wataongezeka kwa ghafla, bado tunaweza kupata tatizo la maeneo bora ya ujengaji wa hoteli za kisasa! Lakini tukumbuke kwamba kuna maeneo kadhaa yenye mvuto ambako hoteli kubwa za kitalii zinaweza kujengwa. Ni bahati mbaya sana maeneo hayo yamefanywa kuwa ni makazi ya watu wazito nchini! Endapo serikali inaweza kubomoa makazi ya watu maskini sehemu mbalimbali nchini kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, basi wakati umefika vilevile wa kubadilisha matumizi ya maeneo ya Oysterbay hadi Msasani hususani yale yaliyo kandokando ya bahari na kufanya uwekezaji kwenye sekta ya utalii! Kwavile eneo hili ni zuri kwa ujenzi wa mahoteli, basi sina shaka yoyote ile kwamba wawekezaji wakubwa wanaweza kujitokeza kujenga mahoteli kwenye eneo hilo. Siamini endapo wakoloni wangefanya eneo hilo ni makazi ya watu endapo biashara ya utalii ingekuwa imekomaa enzi za ukoloni! Aidha, kubadilisha matumizi ya ukanda huo kutachochea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa utalii wa ufukweni, yaani *beach tourism* na hivyo kufanya eneo hilo kuwa ni Ukanda Maalumu wa Utalii, yaani Special Tourism Belt. Wawekezaji kwenye ukanda huo wanaweza kupewa upendeleo maalumu kama ilivyo pale *Benjamini Mkapa Special Exporting Zone*!" Amini usiamini Jonas, utalii wa

aina hii ni bora kuliko utalii mwingine wowote ule unaoufahamu!”

“Nina imani bado una mengi ya kueleza kuhusu sekta ya utalii, lakini bado hujasema lolote kuhusu utalii wa ndani.”Jonas alihoji.

“Bila shaka Jonas, huko nako ningekuja kwavile suala la utalii wa ndani nalo ni muhimu sana. Kama ujuavyo, soko pekee la uhakika kwa nchi yoyote ile duniani ni soko lake la ndani. Hivyo basi, mkakati wowote usiozingatia soko la ndani utakuwa ni mkakati usio endelevu! Hivyo basi, tukija suala la utalii wa ......!”Mara Wendy alikatiza ghafla hicho alichotaka kuongea. Aliingiza mkono wake kwenye kibegi kidogo na kutoa simu ya mkononi.

Simu yake ilikuwa inaita!

Aliipokea na kuanza kuongea, lakini ghafla alianza kubadilika. Akabaki ametulia tulii, ameganda mithili ya mtu aliyepigwa shoti ya umeme! Ghafla kiti alichokalia kikaanza kutoa dalili zote za kuelemewa na uzito wake; na bila kutarajia, alijibwaga chini puu!

Kizaazaa kikazuka huku kila mtu akitaka kujua kulikoni. Kwa kuhofia kujaza watu katika eneo hilo, Jonas alimbeba Wendy na kumpeleka chumbani kwake! Alisikiliza mapigo ya moyo wake, akakuta yanafanya kazi kama kawaida! Akahisi labda simu aliyopigiwa ilihusu taarifa mbaya iliyomletea mshituko wa moyo. Kwavile aliona ni hali ya kawaida, alikata shauri la kumwacha apumzike tu humo chumbani hadi atakapopata fahamu.

Laiti angejua, asingediriki hata kupoteza nguvu zake!

"Inakuwaje Shamte, mgonjwa wangu amezinduka?"Bon Mtambo alimuuliza Dk. Shamte mara baada ya kufika hospitali.

"Hadi natoka wodini alikua bado labda azinduke sasa."

"Vipi naweza kwenda kumwangalia?"

"Unaweza kwenda, lakini endapo utakuta hajazinduka naomba usijaribu kumwamsha!" Dk. Shamte alionya.

Bon Mtambo alienda na kukuta hajazinduka! Alivuta kiti na kukaa jirani kabisa na msichana huyu mrembo ambae mwanga wa taa ya bluu nyepesi uliokua unawaka ulizidisha uzuri wake. Alianza kuvuta hisia vile atakavyokua anaangaliwa na wanaume wakwale atakapokua ameambatana na binti huyu kwenye kumbi mbali mbali za starehe! Mawazo yake akayaamishia siku atakayoenda kumtambulisha kwa wazazi wake ambao mara kwa mara amekuwa akimpigia kelele za kuoa!

"Hapa ni wapi?"Ghafla Bon Mtambo alizinduliwa toka kwenye kichaka cha mawazo. Sauti tamu na laini mithili ya kinanda ilijipenyeza moja kwa moja kwenye ngoma za masikio yake! Huku akionekana kubabaika, Bon Mtambo aliinua macho yake na kuyatupa kule kitandani.

"Pole bibie!"

Zilipita takribani dakika mbili kabla ya kurejewa na fahamu sawasawa!

"Wewe ni nani?"

"Naitwa Bon Mtambo. Je, unajisikiaje hivi sasa?"

"Najisikia vizuri kakangu; sijui ni nani aliyenifikisha hapa hospitali!"

“Ni mimi dadangu na ajali ambayo ilitokea ilikuwa ni kati ya gari yako na yangu kwahiyo utaona ni namna gani nilikua na jukumu la kuhakikisha unapona ma.....”

“Samahani sana kakangu kwa kukusababishia ajali. Najua ilikuwa ni kosa langu hivyo ahsante sana kaka.”

Baada ya kuomba msamaha huo, alipepesa macho yake humo wodini na kisha kuyatuliza kwenye saa ya ukutani ambapo ilikua inakaribia kabisa kutimu saa tatu usiku!

“Ehee! Ina maana nilipoteza fahamu kwa karibu masaa manne?”

“Ndo hivyo dadangu, pole sana!”

“Ahsante kaka.”

“Usijali, sijui unaitwa nani dadangu?”

“Naitwa Glory!”

“Pole sana Glory!”

“Vipi mgonjwa, unajisikiaje hivi sasa?” Dk. Shamte aliuliza mara alipoingia na kuwakuta Glory na Bon Mtambo wakiongea.

“Najisikia vizuri Dokta, tena unaweza kuniruhusu niondoke kwavile nipo safi kabisa.”

“Haina shaka, subiri kwanza nichukue baadhi ya vipimo kabla sijachukua uamuzi wa kukuruhusu ama kutokukuruhusu.”

“Nipo wapi?” Hatimae Wendy aliuliza mara baada ya kuzinduka! Msichana huyu alikuwa amepatiwa taarifa zote kuhusu vile Jonas alivyo mgumu kuingilika, hivyo ilimpasa kutumia kila hila ili awe karibu nae.

"Pole sana Wendy!"

"Ahsante, wewe ni nani na hapa nipo wapi?!"

"Ni Jonas hapa Wendy!"

Wendy alijifanya kutuliza akili na kuanza kuvuta kumbukumbu ya nini hasa kilichotoeka. Ilimchukuwa takribani dakika moja na ushee kuweza kuonesha kwamba kesharejewa na kumbukumbu. Ghafla alianza kudondosha kilio humo ndani na kumpa wakati mgumu Jonas aliyeanza kumbembeleza!

"Pole sana Wendy, kwani ni nini kimetokea?"

"Ni historia ndefu Jonas, naomba unisindikize hotelini nilikofikia."

"Unaweza kulala hapa hapa Wendy, kwani sizani kama ni busara kwa hali uliyonayo kuwa peke yako!"

Wendy aliinua kichwa na kumwangalia Jonas kwa jicho la mshangao kiasi cha kumfanya Jonas ajisikie aibu!

*"Unatakiwa kuwa karibu na Jonas kwa gharama zozote, lakini hutakiwi kujirahisisha! Ni lazima umjengee hamu zaidi ya kutaka kuendelea kuwa na wewe!"* Wendy alikumbuka maagizo aliyopewa!

"Nisindikize tu Jonas, sitakuwa peke yangu. Najuwa una hamu ya kuendelea kuwa na mimi, nakuahidi kesho nitakuja kwako."

*"Promise!"*

*"I promise Jonas!"*

Baada ya vijana hawa kufungiana ahadi, hatimae walitoka humo chumbani na kuanza kusindikizana!

Kiasi cha robo saa baadae Bon Mtambo na Glory walikuwa kwenye gari pamoja! Kwa upande wa Mtambo,

alijihisi ni kama anaepaa hewani ile tu kuwa karibu na msichana huyu mrembo!

"Kaka Bon, sasa mimi itabidi unifikishe nyumbani endapo hutajali!"

"Kwanini tusiongozane kwangu kwavile bado unahitaji uangalizi wa karibu?"

"Ondoa shaka kaka, nyumbani kuna watu ambao wataniangalia bila matatizo."

Ili asionekane kuwa ni king'ang'anizi, Bon Mtambo alikubali japo ni kwa shingo upande. Alikanyaga mafuta hadi Mwenge alikokua anaishi Glory.

Mlio wa simu ndio uliomgutusha Jonas toka usingizini. Ilikuwa ni simu ambayo ilimlazimisha kuondoka siku hiyo hiyo na kuahirisha likizo yake!

Baada ya kujiandaa kwa haraka na kufanya mawasiliano na kampuni ya ndege aliyotarajia kusafiri nayo, aliteremka chini na kupata kifungua kinywa kisha bila kupoteza muda alienda kuonana na Wendy.

"Mnh! Mbona mapema hivi Jonas!?" Wendy alimuuliza Jonas mara baada ya kuingia chumbani kwake.

"Nimeletewa simu kwamba mama ni mgonjwa taabani, na yupo hospitali Muhimbili!" Hatimae Jonas alimweleza Wendy huku akionekana kukosa raha kabisa.

Pamoja na kukosa raha kutokana na taarifa za kuumwa kwa mama yake, lakini vile vile aliingiwa na huzuni zaidi kuona anaondoka kabla hajapiga hatua mzuri ya mahusiano kati yake na Wendy!

"Pole sana Jonas, nami naondoka kesho kwavile ile jana nililetewa taarifa kwamba mchumba wangu anatarajia

kufunga ndoa na rafiki yangu! Nataka nikahakikishe kwavile siamini kama kweli wanaweza kunisaliti!”

“Unaonaje nikikusubiri ili tuondoke wote hiyo kesho?!”Jonas alitoa wazo huku akionekana kutaka kupuuza simu iliyomwambia arudi haraka!

“Hapana Jonas, wewe tangulia. Nikifika tu nitakutafuta!”

“Tafadhali Wendy, usikose kunitafuta mara utakapowasili Dar es salaaam!”

“Usihofu Jonas. Nipatie basi namba yako ya simu unapokuwa dar es salaam.”

Baada ya maongezi ya hapa na pale, Wendy alimsindikiza Jonas uwanja wa ndege tayari kwa kurejea Dar es salaam.

# 4

“Ah! Bon, karibu kakangu!” Alikuwa ni Glory akimkaribisha Bon Mtambo mara alipoingia kwenye ofisi za NasDesign, ofisi geresha ya Glory Mushy! Ilikuwa inakaribia kutimia saa kumi na moja jioni, muda ambao walikubaliana amfuate.

“Nimekaribia bibie.” Bon Mtambo aliitikia na kuketi.

Baada ya kukaa na kuogea mambo mawili matatu waliondoka kuelekea Chang’ombe; nyumbani kwa Bon Mtambo.

“Hapa ndio nyumbani Glory, karibu sana!” Bon Mtambo alikaribisha mara walipoingia ndani.

“Ahsante kaka Bon!”

Glory aliitikia na kuketi kwenye sofa lililokuwa karibu na alipoketi Bon Mtambo. Baada ya kuletwa vinywaji, walianza kuongea mambo mbalimbali kuhusu maisha yao binafsi. Kama angekuja mtu, basi angehisi vijana hawa wamefahamiana muda mrefu kwa jinsi walivyoonesha kuzoeana kwa haraka! Jambo hili lilimfurahisha sana Bon Mtambo ambae tayari nafsi yake ilishatokea kuzama kwa msichana huyu mrembo! Wakiwa katikati ya maongezi mara mlango uligongwa!

“Shenzi taipu, kumbe nyinyi!” Bon Mtambo aliongea kwa utani alipokuta rafiki zake wamesimama mlangoni! Alishasahau kwamba waliahidi wangekuja jioni hiyo. Bila

shaka endapo angekumbuka kwamba Glory nae aliahidi kuja basi si ajabu asingeukubali ugeni wa rafiki zake hao!

“Glory,“ Hatimae Bon Mtambo alianza kuwatambulisha rafiki zake mara walipoketi, “Huyo jirani yako anaitwa Hamidu, ni mfanyakazi wa banda langu la mifugo, anayefuata anaitwa Khalifa, ni mfanyakazi wa ndani, na huyo hapo ni Tony, yeye ni mpishi wangu na mwisho pale anaitwa Ayoub, yeye ni mwangalizi wa mbwa na paka wangu!” Alimaliza utambulisho wake, ambao kimsingi ulikuwa ni utani mtupu!

“Sisi ni wafanyakazi wako, na huyo ni nani wako bosi?” Tony aliingilia kati baada ya kuona Bon Mtambo keshamaliza kutambulisha bila ya kutaja Glory ni nani hasa kwake!

“Shemeji, hebu tujuze. Bosi Mtambo alitudokeza kwamba anataka kufungua kampuni ya mitindo, bila shaka wewe ndie mkurugenzi wake sio?” Khalifa alimchokoza Glory baada ya kumuona muda mrefu akiwa anacheka tu kwa yale wanayoongea bila ya yeye kuchangia chochote!

“*Stop* Khalifa, Glory sio mpenzi wangu; ni rafiki tu!” Bon Mtambo aliingilia kati baada ya kuona Glory anajing’atang’ata, bila shaka hakuutarajia ule utundu wa Khalifa!

“Hata kama ni rafiki yako lakini bado mna haki ya kuwa na urafiki zaidi ya huo kwavile sio ndugu!”

“Hata kama!” Bon Mtambo alijihami. Si kwamba maongezi haya hakuyafurahia, la hasha. Tena alitamani sana waendelee nayo ili na yeye apate nafasi ya kuchombeza katikati ya maongezi. Ingawaje ni kweli kwamba tayari Bon Mtambo alishampenda Glory, lakini alijikuta anakuwa mzito kumtamkia wazi; jambo ambalo hata yeye mwenyewe alilishangaa!

“Ingawaje Bon Mtambo anaonekana kukanusha lakini macho yake yanaongea lugha tofauti!”Ayoub, aliyekuwa kimya kwa muda mrefu alichangia na kuwafanya wote waangue kicheko.

Waliongea mambo mengi sana kiasi kwamba muda ulienda bila ya wao kujua!

“Hamidu hebu tuambie, umefikia wapi lile suala la uchumba na Maria?” Hatimae Bon Mtambo alibadilisha maongezi na kumtupia swali mwenzake.

“Imeshindikana.”Alijibu kwa kifupi huku simanzi ikiwa inasindikiza jibu lake!

“Kwanini?”

“Dini!”

“Dini imefanya nini?”

“Wazazi wake wamekataa binti yao kuolewa na mtu mwenye imani tofauti na yao!”

“Dini! Dini! Dini!” Alikuwa ni Glory aliyekua kama anayeongea peke yake huku uso wake ukiwa umebeba simanzi na kumfanya kila mmoja amtupie jicho la mshangao!

“Vipi Glory, na wewe umeshawahi kukutwa na mkasa kama huo?!” Hatimae Tony aliuliza huku Bon Mtambo akisubiri jibu lake kwa shauku!

“Hapana Tony, lakini hata ikitokea sitaacha kufunga ndoa na mtu nimpendae eti kwavile tu dini au kabila zetu ni tofauti!” Glory alijibu kwa kujiamini kabisa hali iliyomfanya Bon Mtambo ashushe pumzi kwa nguvu na kusababisha wote waliopo hapo waangue kicheko! Kila mmoja; isipokuwa Glory alishajua ni kwanini Bon Mtambo alikua katika hali ile! Kwa mtu asiyemfahamu vizuri, angezani Bon Mtambo ni Mkristo kutokana na jina lake, lakini haikuwa hivyo! Inasemekana hapo zamani, alikuwa

anaitwa jina la Kiislamu lakini akabadilisha jina kwa kiapo cha mahakama ingawaje dini yake ilibaki ileile! Hata hivyo, hakuna anaefahamu kwa yakini ni kwanini aliamua kubadilisha jina!

“Nachukia sana watu wanaoyapa nafasi mambo ya udini na ukabila wakati wenyewe si wafuasi wazuri!” Huku akionekana kukereka, Glory alianza tena kuongea kisha akaendelea “Inakuwaje mzazi mwenye mapenzi ya dhati kwa mtoto wake halafu tena aidhulumu nafsi ya mtoto huyo!? Kinachokera zaidi ni kwamba ingawaje mara nyingi wazazi hao wameonekana kuwa ni vikwazo kwa jambo hili lakini nao si waumini wazuri wa dini zao! Ni jambo lisiloingia akilini kwa mzazi wa kiislamu kumkataza mtoto wake kufunga ndoa na mkiristo wakati hata msikiti wenyewe unafananaje kwa ndani hajui! Hata kwa wazazi wa Kikristo nao ambao angalau wanaonekana kuwa ni wahudhuriaji wazuri kwenye nyumba za ibada unakuta wengi wao inatokana na mazoea zaidi kuliko kusukumwa na imani!”

“Watu kama hawa wananikera kwa sababu mara nyingi utakuta upuuzi wao huu wanaupeleka hata sehemu zao za kazi; hususani endapo ni watu wenye mamlaka fulani huko kazini kwao. Bado namkumbuka kaka wa rafiki yangu mmoja aliyekuwa anafanya kazi kwenye taasisi moja iliyopo hapa Dar es salaam. Bosi wake aliyekuwa anaitwa Magdalena alikuwa ni mtu aliyekuwa anajinadi kwamba anaishi kwa damu ya Yesu! Lakini pamoja na kujinadi alikuwa anaishi kwa damu ya Yesu, bado matendo yake hayakuwiana kabisa na vile alivyokuwa akiishi Yesu Kristo mwenye upendo kwa wote! Basi nasikia siku moja mama huyu alipewa agizo na wakubwa wake kwamba amuhamishe mhasibu mmoja

kwavile ofisi yake ilikuwa wahasibu wengi! Wakati kila mmoja akitarajia kwamba bosi yule angemwamisha mhasibu ambae ufanisi wake ulikuwa mdogo; kwa mshangao wa wengi akamuhamisha kijana ambae alikuwa ni mchapa kazi kwelikweli! Aidha, wiki chache baadae wakahamishwa wafanyakazi wengine wawili! Baada ya hapo, likatokea tatizo lingine la kipuuzi kabisa lililomuhusu huyo kaka. Amini msiamini, huyo bosi akala njama na bosi mwingine aliyekuwa anaitwa Bwana Oleander, kisha wakamwachisha kazi huyo kaka! Sasa.....!"

"Samahani Glory, nikukatize mara moja!"

"Bila samahani Hamidu, uliza tu!"

"Kutokana na maelezo yako ni kwamba huyo bosi alikuwa anafanya maamuzi yake kwa kusukumwa na chuki za kidini, sasa huyo kaka yako alijuaje juu ya jambo hilo? Aidha, huyo bosi alikuwa anasukumwa na chuki za kidini, je huyo bosi mwingine ambae alishirikiana nae kumwachisha kaka yako kazi alikuwa anasukumwa na nini?" Hamidu alihoji na kutoa nafasi kwa Glory kuendelea na maelezo yake!

"Kutokana na maelezo ya huyo kaka ni kwamba ingawaje hana ushahidi lakini ushahidi wa mazingira unathibitisha hilo. Kwa mfano haiingii akilini kwa mtu asiyesukumwa na jambo fulani kumwamisha mfanyakazi mwenye ufanisi kwenye kazi na kumwacha mzembe! Kwahiyo, endapo bosi huyo hakusukumwa na jambo lolote basi itakuwa uwezo wake kimaamuzi ni mdogo! Lakini jambo la msingi hapo ni kwamba, walipokuja kuhamishwa wafanyakazi wengine wawili, bosi huyo wa kike alisikika akisema kwamba humo ofisini wangebaki wakristo watupu! Ikumbukwe kwamba, wote waliokuwa

wamehamishwa walikuwa na imani tofauti na huyo mama! Sasa kama si upumbavu tuite nini?”

“Na je, kuhusu huyo bosi mwingine? Yeye alisukumwa na nini?” Hatimae Hamidu akakumbushia swali lake la pili!

“Ahsante kwa kunikumbusha Hamidu! Kuhusu huyo bosi mwingine ilikuwa ni kama alitaka kumkomoa huyo kaka ! Chanzo chake ni kwamba huyo kaka alikuwa amefanya kazi kwenye hiyo taasisi kwa zaidi ya miaka minne. Aidha, inasemekana kwamba huyo kaka alikuwa ni mchapa kazi kwelikweli na kila mmoja alilifahamu hilo. Na si kuchapa kazi tu, bali pia alikuwa kazi anazijua kwa kiasi kikubwa tu pengine kuliko wafanyakazi wengi tu. Hata hivyo, likatokea zoezi la kuajiri wafanyakazi wengine wasio na uzoefu ambao kimsingi wangekuwa kwenye nafasi za juu kuliko yeye ingawaje sifa zao kielimu ni sawa! Baada ya kuona hivyo, huyo kaka akamwandikia huyo bosi mwingine na kumuuliza vigezo vilivyotumika kuona watu wasio na uzoefu ni bora kwa nafasi za juu kuliko wao ambao tayari wapo kwenye ajira kwa miaka kadhaa! Vilevile akahoji ni kwanini hawakutaka kwanza kuwapa nafasi wafanyakazi ambao tayari wapo nao kabla ya kuanza kuajiri kutoka nje!”

“Hata hivyo, badala ya kujibu hoja bosi huyo akakanusha kabisa suala la kuajiri hao maofisa! Lakini kama mjuavyo, huwezi kuficha mimba muda wote! Na kwavile huyo bosi hakupendezwa na suala hilo la kuulizwa, akaanza kumtafutia sababu kama njia ya kumshikisha adabu na kuwanyamazisha wengine wenye tabia ya kuhoji! Hivyo, kabla hawajaletwa hao maofisa hapo ofisini akahakikisha kwamba huyu aliyekuwa kimbelembele anaondolewa kwanza! Na ikumbukwe

kwamba, viongozi wenye upumbavu kama huu ni wengi sana nchini! Hawapendi kuhojiwa!"

"Sasa tukirudi kwa yule bosi wa kwanza ambae alifanya maamuzi yake kwa kusukumwa na itikadi za kidini, mnafikiri kuna viongozi wangapi ambao wameweza kutoa upendeleo wa aina fulani kwa watu fulani kwavile tu ni waislamu wenzao, au ni wakristo wenzao au kwavile tu ni watu wa kabila lao?! Ni viongozi wangapi wamepata kufukuzisha kazi wafanyakazi walio chini yao tena kwa sababu za kipuuzi kabisa na hata bila ya kuwapa fursa ya kujitetea! Hali kadhalika, ni viongozi wangapi wamepata kupendekeza kuhamishwa kwa wafanyakazi wao bila sababu zozote za msingi zaidi ya hisia na chuki za kidini au ukabila? Hata tukija kwa yule bosi wa pili, unafikiri kuna viongozi wangapi wanaofanya maamuzi yao kwa lengo tu la kuwakomoa watu walio chini yao kwavile ni watu wa kuhoji? Bila shaka, jibu lake ni kwamba viongozi wa aina hii ni wengi sana, hususani kwenye taasisi zilizo chini ya sekta binafsi! Amini msiamini, nchi haiwezi kusonga mbele hata chembe unapokuwa na viongozi wabovu kama hao!"

Binafsi nawaona hawa watu wanaosukumwa na udini ama ukabila ni watu ambao wamefilisika sana kiakili pengine kuliko wendawazimu wenyewe! Si ajabu bosi wangu yule amesahau kabisa kwamba hamna lolote alilofanya hadi yeye kuwa mkristo zaidi ya ukweli tu kwamba yeye ni mwenyeji wa mkoa wa Mara ambako Wamisionari wa Kikristo ndiko walieneza dini yao. Hivi utaithaminisha vipi akili ya mtu aliye na majivuno kwavile tu yeye ni Mchaga au Mhaya wakati ni kudra za mwenyezi mungu tu ndizo zilizomfanya yeye awe ni mwenye asili ya huko?! Hivi utaithaminisha vipi akili ya mtu anayemdharau mwenzake kwavile tu mwenzake huyo ni

Mgogo, Mmakonde au Mzaramo wakati nae hamna lolote alilofanya hata asiwe ni mwenye chimbuko la makabila hayo! Hivi utaithaminisha vipi akili ya mtu anayewadharau wanawake kwavile tu yeye ni mwanaume huku akijua wazi kwamba hajalipa japo punje ya mchanga ili yeye awe mwanaume?! Amini msiamini, hawa wote wamefilisika sana kiakili kwahiyo ni hatari sana wanapopewa madaraka ya aina yoyote!" Glory alimalizia kwa kuhoji na kuwafanya vijana hawa wa kiume wabaki wakiwa wamepigwa na butwaa. Bila shaka hawakutarajia kwamba angekuwa na mawazo kama hayo kutokana na wajihi wake!

Viongozi wa DRFA walikuwa kwenye nyumba ya mmoja wa vigogo wa CDTPE iliyopo maeneo ya Mbezi Beach jijini Dar es salaam. Aidha, kulikuwa pia na watu watatu kutoka CDTPE ambao hata hivyo, wawili walipandikizwa tu, na wala hawakuwa wakazi wa Tanzania! Hapa walikutana ili kuwekeana saini mkataba wa CDTPE kukisaidia kwa siri chama cha DRFA!

Pamoja na hayo, kuna jambo halikufahamika kwa viongozi wa DRFA! Jambo hilo ni kamera za siri zilizokua zimetegeshwa kwa sababu maalumu! Punde si punde, Bwana George Malilo akasimama na kutoa nasaha zake:

"Ndugu wapiganaji, hatimae ile siku iliyokuwa inasubiriwa kwa hamu leo imewadia. Kama mjuavyo, lengo kuu la CDTPE ni kuchochea ukuaji wa demokrasia kwa nchi changa za Afrika na dunia nzima kwa ujumla. Katika hali ya kawaida, taasisi yetu inafanya shughuli zake

kwa uwazi na usawa lakini pale inapobidi tunalazimika kufanya kama hivi ili kukuza vuguvugu chini kwa chini!"

"Kwa kawaida CDTPE hutoa misaada kwa asasi zinazojihusisha na ukuzaji na uendelezaji wa demokrasia. Katika hili, CDTPE huendesha warsha, semina na makongamano. Vilevile huwa tuinaitisha mchanganuo kuhusiana na eneo fulani la demokrasia na ile inayoshinda huzawadiwa."

"Pamoja na hayo, ilionekana kwamba mazingira yaliyopo hapa nyumbani hayatoi fursa sawa kwavile vyama vilivyopo, hususani vya upinzani havina uwezo wa kifedha. Baada ya kuliona hili, CDTPE Tanzania ilitoa taarifa CDTPE makao makuu nchini Norway na wao wakatoa wazo kwamba tuteue chama cha mfano, yaani *pilot party* chenye mwelekeo ili kiweze kusaidiwa. Hata hivyo, wao walitupa uhuru wa ama kusaidia kwa uwazi au kwa siri, lakini kutokana na mazingira ya siasa ya hapa nchini tuliona tukiwasaidia kwa uwazi basi itatuletea migogoro na serikali. Kwakweli tusingependa kuingia kwenye mgogoro na serikali kiasi cha kuwapa sababu za kufuta taasisi yetu kabla malengo hayajafikiwa. Hivyo basi, ni matumaini yetu kwamba mtaitumia nafasi hii adimu ili kuweza kufikia malengo yenu kisiasa." Alimalizia na kutoa nafasi kwa viongozi wa DRFA kuupitia mkataba kwa mara ya mwisho kabla ya kuwekeana saini rasmi. Hata hivyo, ulikuwa ni mkataba wenye masharti ya kawaida tu!

# 4

Hiki kilikuwa ni kikao kingine kilichoitishwa na CDTPE kwa kushirikiana kwa siri na IBU! Wakati kikao cha awali kiliikutanisha CDTPE na DRFA, kikao hiki kiliikutanisha CDTPE na baadhi ya vyama huru vya wafanyakazi, vyama visivyo vya kiserikali pamoja na baadhi ya asasi za kiraia! Kwa kutumia ghiliba ya hali ya juu kabisa, mawakala wa CDTPE walianza kwa kukutana na kiongozi mmoja mmoja wa taasisi hizi na kuwaeleza juu ya kuwapo kwa mkutano utakaowakutanisha viongozi wa asasi kama zao kutoka nchi za Afrika Mashariki. CDTPE walikata shauri la kujipenyeza kwenye taasisi hizi kwavile waliamini nazo zina ushawishi mkubwa kwa jamii!

“Ndugu wapiganaji, awali ya yote ningependa kuwashukuru kwa kujitolea kuacha shughuli zenu na kuhudhuria kikao hiki muhimu kwa mustakabali wa nchi zetu.” Mwenyekiti wa kikao alianza hotuba yake kisha akaendelea: “Hii inaonesha ni jinsi gani mlivyo na nia ya dhati ya kupigania maslahi ya wanyonge walio wengi ambao hawana sauti ya kweli ya kuwasemea! Inasikitisha sana kuona hata wale wanaojigamba kupigania maslahi ya wanyonge wanaonekana hivyo mbele ya macho ya jamii tu lakini ndani ya nafsi zao kilichojaa ni ulafi, uchoyo na ubinafsi huku wakiwa na nia ya kutumia taasisi zao kwa manufaa binafsi! Hili si jambo jema hata kidogo kwa ustawi wa jamii zetu. Ni jambo lisilotakiwa kuachwa liote mizizi

ndani ya jamii yoyote iliyostaarabika! Na kwa hakika, jambo hili si jema zaidi hususani katika kipindi hiki ambacho ubeberu unaelekea kurudi barani kwetu kwa kasi ya kutisha! Ubeberu unaokuja katika taswira ya uwekezaji!" Alitulia kidogo kisha akaongea kwa hamasa ya hali ya juu huku akipunga ngumi hewani!

"Mshikamano!"

"Daima!" Wajumbe wote waliitikia kwa pamoja huku nao wakipunga ngumi hewani!

"Mshikamano!"

"Daima!"

*"An injury to one* (Maumivu ya mmoja)!

*"An injury to all* (Ni maumivu ya wote)!"

Alichukua bilauri ya maji na kupiga funda moja kisha akairudisha mezani na kuendelea:

"Ndugu wapiganaji, lazima nikiri kwamba sijawahi kukutana na wapiganaji wenye ari, hamasa na ujasiri kama nyinyi! Hakika naanza kuiona taswira ya ushindi huku nikiwaona wanyonge nao wakiwa wanapunga mikono yao hewani kama ishara ya kusherehekea ushindi huo! Ni ushindi dhidi ya ubeberu! Ushindi dhidi ya unyanyasaji! Ni Ushindi dhidi ya dhuluma!"

"Mshikamano!"

"Daima!"

"Ndugu wapiganaji, amini amini nawaambia, nafsi yangu inaninong'oneza kwamba ushindi upo njiani, milimita chache tu toka kwenye pua za wanyonge! Pua za ndugu zetu; pua za baba na mama zetu! Ni ushindi dhidi ya mabeberu, uonevu, ukandamizaji na unyanyaji kwenye jamii yetu. Hivyo basi, hatuna budi kuzidi kusonga mbele na kamwe tusifikirie kurudi nyuma katika hili kwani kufanya hivyo itakuwa ni sawa na kula nyama za ndugu

zetu wanaotegemea msaada wetu. Rafiki zenu toka nchi za Ulaya Mashariki na nchi za Scandinavia wameamua kuwaongezea nguvu ili muwe na uwezo wa kushindana na nguvu hizi za kibeberu! Hamtashindana na mabeberu hawa kwa kuingia barabarani na kuwarushia mawe, bali mtashindana nao kisayansi! Na hakika lazima mkumbuke kwamba, katu hamtaweza kushindana na nguvu hizi za kibeberu wakati taasisi zenu zipo hoehae zikitegemea michango ya wanachama na wafadhili wasio na nia njema! Kwa kuliona hili, rafiki zenu wamechukua jukumu la kuwasaidia ili muweze kuwa na vyama vyenye nguvu! Marafiki zenu wanataka muwe na vitega uchumi ili kuziimarisha taasisi zenu badala ya kutegemea michango na hisani za wafadhili. Wengi ni wafadhili wanaojifanya kuwafadhili ili wapate tu kuwadhibiti! Hakika nawaambia, kamwe hatutaweza kufika kwa mtindo huu!"

"Ndugu wapiganaji, kuwaleta nyinyi pamoja haikuwa kazi ndogo kwani ni kazi ambayo ilikumbana na upinzani tangu awali! Sisi wenyewe, tulikataa katakata kujihusisha na vuguvugu hili kwa sababu ambayo kila mmoja wenu wenu anaifahamu! Taasisi yetu haina uhusiano wowote na vyama kama vyenu; na ndio maana tulikataa! Hata hivyo, walivyotupasha wazi kwamba hakuna demokrasia kwenye nchi ambayo raia wake wanadhurumiwa, tulijikuta ni kama tumevuliwa nguo! Ikawa ni kama tumebakishwa uchi wa mnyama mchana kweupe kwenye halaiki ya watu! Hapo, tukajiona kweli sisi ni wajinga! Unafikiri ni nini mtu wa kawaida anachokihitaji zaidi, kati ya demokrasia ya kisiasa na demokrasia itakayoamua mustakabali wa tumbo lake! Tukakuta ni kweli, pasipo na shibe hapana demokrasia! Njaa ndio inawafanya watu wauze haki zao za kumchagua

wamtakae! Kwa maana hiyo, njaa ni adui mkubwa demokrasia! Baada ya kubaini ukweli huu, ndipo nasi tulipokubali kuingia katika vuguvugu hili la kuvisaidia vyama vya wafanyakazi pamoja na asasi za kiraia. Hata hivyo, kwavile jambo hili ni kinyume na sheria iliyotumika kuisajili CDTPE, basi hatuna budi kulianza vuguvugu hili kwa usiri mkubwa hadi pale CDTPE itakavyoongezewa malengo yake kisheria. Kwa sasa taratibu zinaendelea ili CDTPE isiwe tu inalenga vyama vya kisiasa, bali hata taasisi kama zenu! Tuna hakika kwamba ndani ya mwezi mmoja tutakuwa tumeshakamilisha taratibu na kuanzia hapo tutakuwa huru kuendesha shughuli zetu kwa uwazi kwa kushirikiana nanyi moja kwa moja. Hivyo basi, kwavile huu ni mwanzo tu, CDTPE na marafiki zetu wataipatia kila taasisi shilingi milioni hamsini. Jambo la msingi ni nidhamu bora ya matumizi ya fedha hizo. Nidhamu ya matumizi ndiyo itakayowafanya wafadhili waendelee kuvisaidia vyama vyenu!"

"Pamoja na hilo, marafiki zetu wamegundua kwamba kamwe bunge letu halitaweza kukabiliana na ubeberu huu kwavile limejaa wabunge wasio na hisia za kimapinduzi! Bunge imara ni lile lenye idadi kubwa ya wabunge wenye hisia za kimapinduzi au wanaharakati kama ninyi. Duniani kote ni wanaharakati na wanamapinduzi ndio wanaoleta mabadiliko, ikiwa pamoja na yale ya kisiasa. Kwa kawaida, wanaharakati si waoga. Hivyo basi, CDTPE inatumia nafasi hii kuwapa changamoto ya kushiriki kwenye siasa na itakuwa nanyi bega kwa bega katika kutimiza malengo hayo. Tunajua yeyote miongoni mwenu akishaingia bungeni ataiacha nafasi yake ya sasa na kutoa nafasi ya kuivisha wanaharakati wengine." Mwenyekiti huyu ambae awali

alijitambulisha kama Samson Kaijage alimalizia maelezo yake. Alijitambulisha kama Samson Kaijage na kwamba alikuwa hapa kumwakilisha George Malilo, Mkurugenzi wa CDTPE aliyekuwa nje ya nchi kwa shughuli za kikazi!

Ni kengele ya mlangoni ndiyo iliyomgutusha Bon Mtambo toka usingizini. Alitupa macho kwenye saa ya ukutani na kukuta inakaribia kabisa kutimia saa tatu asubuhi! Hakuwa na mazoea ya kulala hadi muda huo, lakini kwa leo alikua na kila sababu!

Aliyaondosha macho yake toka kwenye saa na kuyarudisha kitandani. Hapo yalilakiwa na utundu ambao muumba amepata kuufanya katika shuguli zake za uumbaji! Glory; msichana mrembo alikuwa amelala kitandani huku akionesha bado yu ndani ya usingizi mzito!

Bon Mtambo aliyarudisha mawazo yake tangu siku ya kwanza alipokutana na Glory baada ya kutokea ajali pale maeneo ya Keko! Alikumbuka jinsi alivyotokea kumpenda ghafla huku Glory akiwa haoneshi dalili yoyote ya kuvutiwa nae! Mbaya zaidi, ilimchukua muda kabla ya kukata shauri la kumpasulia ukweli! Si kwamba alikuwa mwoga kwa wanawake; hususani warembo kama alivyo Glory. Hofu iliyokuwa imetanda kwenye fikra zake ilikuwa ni kumpoteza kwenye himaya yake endapo Glory asingekuwa tayari. Hakutaka kumfanya Glory aishi kwa tahadhari dhidi yake. Alikuwa tayari kubaki nae katika urafiki wa kawaida kuliko kufanya jambo ambalo lingesababisha msichana huyu kuwa mbali nae. Hata hivyo, siku ya siku ilifika na Bon Mtambo alikata shauri la kupasua ukweli uliokua unachonyota kwa kipindi kirefu

ndani ya moyo wake. Haifahamiki angekuwa na shauku nae kiasi gani endapo angefahamu historia ya nyuma ya mrembo huyu!

Alijizoazoa hapo hapo kitandani kisha akaenda nje alikorudi na baadhi ya magazeti ya hiyo siku.

***"Kituo cha Fikra za Kidemokrasia na Siasa-Uchumi (CDTPE) kutoa tuzo"***

Hicho kilikua ni moja ya vichwa vya habari kilichomvutia Bon Mtambo. Alipitia kurasa zingine za hilo gazeti kisha akaanza kuisoma habari hiyo ya siasa.

*Taasisi inayojihusisha na masuala ya siasa na demokrasia, CDTPE tawi la Tanzania imeandaa tuzo ya mamilioni ya shilingi kwa vyama ambavyo vitafanya vizuri kwenye shindano lililoandaliwa na taasisi hiyo. Akizungumza kwenye mkutano na waandishi wa habari jana,mkurugenzi wa CDTPE alisema vigezo vitakavyotumika katika kumpata mshindi ni andiko zuri litakaloonesha mpango mzima wa chama husika katika maendeleo ya demokrasia na uchumi nchini. Akifafanua zaidi alisema, "lengo la CDTPE hivi sasa ni kuona vyama vya kisiasa vinaondokana na dhana ya kwamba ni lazima kwanza viingie madarakani ndipo vifanye shughuli za maendeleo kwa wananchi. Kuanzia sasa tungependa kuona kwamba serikali ya upinzani inayoundwa bungeni isiishie kufanya kazi bungeni peke yake bali kazi hiyo ifanyike kivitendo uraiani kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo. Tunaamini hata wapinzani nao wana mipango bora kabisa ya kuwaletea wananchi maendeleo, sasa hatuwezi kusubiria hadi waingie madarakani ndipo mipango hiyo waweze kuitekeleza!"*

*Alipoulizwa endapo lengo la CDTPE ni kuupigia upatu upinzani; Bwana George Malilo Mkurugenzi wa CDTPE alifafanua "Tuzo hii si kwa ajili ya vyama vya upinzani peke yake, bali hata kwa chama tawala. Kwa jinsi ilivyo, hata chama*

*tawala chenyewe hakina tofauti na vyama vya upinzani. CDTPE inaamini kwamba vyama vya siasa nchini vina nafasi kubwa sana ya kuwaletea wananchi maendeleo badala ya kutumia muda mwingi kwa ajili ya kuimarisha vyama vyao peke yake. Huwezi kuimarisha chama katika sehemu ambayo watu wake wanaishi chini ya dola moja kwa siku huku mkiisubiria serikali ilete maendeleo. Tungependa kuona vyama vya siasa vikiibua miradi mbalimbali ya maendeleo kwa ajili ya wananchi bila ya kujali itikadi zao za kisiasa.Hivyo basi, tuzo hii itaangalia kwa undani kabisa nini malengo ya chama husika katika ujenzi wa demokrasia na shughuli za maendeleo kwa wananchi bila kujali kama chama hicho ni cha upinzani au chama tawala." Alisema.*

Bon Mtambo aliendelea kuisoma habari hii ambayo ilikuwa ni ndefu huku ikiwa imeelezea sifa mbalimbali zitakazotumika kumpata mshindi!

Baada ya kupitia kwa haraka haraka magazeti ya hiyo siku, Bon Mtambo alielekea uani ambako alianza kufanya mazoezi mepesi. Hata hivyo, kadri mwili ulivyozidi kupata moto ndivyo alivyozidi kupandisha mzuka wa mazoezi! Ilifikia wakati Glory akaja kujiunga nae bila ya yeye Bon Mtambo kufahamu! Na hata pale alipogundua kwamba yupo na Glory bado hakuonesha kushituka na ujio wa msichana huyo!

Ni kama hapakuwa na mtu yeyote aliyejiunga nae!

Glory nae hakuonesha kujali! Alianza kufuata kila hatua iliyofanywa na Bon Mtambo!

Baada ya mazoezi ya muda mrefu wote walienda maliwatoni kuoga kisha wakarudi mezani na kuanza kupata chai. Jambo moja lilizoeleka kila wanapokuwa

wamekaa pamoja katika mazingira ambayo si ya kimapenzi. Nalo ni kuzungumzia masuala mbalimbali ya kiuchumi, kisiasa na kijamii! Wakati Bon Mtambo alikuwa ni mkereketwa zaidi katika masuala ya biashara na uchumi, Glory alikuwa mkereketwa katika masuala ya kijamii!

"Glory, hivi umesikia kwamba serikali imefunga vyuo vikuu vya umma ambavyo vilikuwa kwenye mgomo?" Bon Mtambo alimchokoza Glory mara baada ya kumaliza chai! Akilini mwa Glory, Bon Mtambo ni mpenda siasa! Hivyo, kana kwamba hajasikia swali la Bon Mtambo Glory alianza kushughulika na vyombo vilivyokuwa mezani! Alianza kuviondoa ili aanze usafi!

"Ina maana hujaguswa na hili jambo?"Bon Mtambo aliendelea na uchokozi wake.

"Hata nikiguswa sasa nitafanya nini?!"

"Huna cha kufanya, lakini ningependa kusikia maoni yako!"

"Maoni yangu ni kwamba nimesikitishwa sana!"

"Umemaliza?!"

"Ndiyo!"

"Bado"

"Bado nini?!"

"Nataka maoni yako ya nini kifanyike kumaliza hali hii ambayo ishaonekana ni mazoea kwa sasa! Kusema kweli hii ni hali ambayo inanisikitisha sana mpenzi!" Bon Mtambo aliongea kwa hisia kali hali iliyomshitua hata Glory na kumfanya ainue kichwa na kumwangalia usoni. Katika hali ya kushangaza, Glory aliinuka hapo kitini na kwenda kusimama dirishani na kuangalia nje kana kwamba alitarajia ujio wa mtu au watu fulani!

"Suluhisho ni mabadiliko ya kifikra Bon!" Baada ya kupita takribani dakika mbili hivi, hatimae Glory aliongea

akiwa bado hapohapo dirishani. Aliongea kana kwamba anaongea peke yake!

Bon Mtambo aliielewa hali hiyo!

"Bon, hakika kuna mengi yanatakiwa kufanyika kuhusiana na hali hii lakini binafsi nasikitishwa zaidi na vile ambavyo viongozi wa vyuo wanavyotatua migogoro hii! Na kama kuna watu wanaopaswa kubadilika kifikra basi ni viongozi wakuu wa taasisi za elimu ya juu nchini. Sio siri Bon, wakati umefika kwa wakuu hawa kuchukulia vyuo vikuu kama taasisi za kibiashara na hivyo maamuzi yao yawe na mtizamo wa kibiashara. Wanapaswa kuchukulia kwamba, serikali ambayo ndio mmiliki wa vyuo hivyo kama ndio wamiliki wa biashara na wao wakuu wa vyuo kama maafisa watendaji wakuu, yaani CEOs wa biashara hizo! Wasiishie hapo, vilevile wanapaswa kuwachukulia wanafunzi wa vyuo hivyo sawa na wateja wao badala ya wanafunzi kama ilivyozoeleka. Nazani kila kitu hapo kipo wazi kwamba pasipo na wanafunzi, wao hawana ajira, angalau hiyo ya uhadhiri. Hivyo basi, wakishakuwa na mtizamo kama huo nazani wataacha mara moja tabia yao ya kukimbilia kufunga vyuo pindi inapotokea migogoro ambayo inatatuirika. Wataacha mara moja kwavile wanafunzi ni wateja wao na kufunga, kisha kufukuza wanafunzi itakuwa ni sawa na kuwafukuza wateja kwenye biashara yako! Sizani kama kuna CEO duniani ambae anaweza kufanya maamuzi ya kudhalilisha wateja wake! Sizani kama kuna CEO ambae anaweza kuitia polisi wateja wake ambao wala hawaoneshi dalili za kuvuruga amani! Na hilo likifanyika, hata heshima kati ya wanafunzi na uongozi wa vyuo itaongezeka! Heshima itaongezeka kwavile uhusiano utakaokuwepo baina yao si tena kati ya wanafunzi na uongozi bali kati ya mteja na

mtoa huduma! Hii itaongeza wigo wa maelewano kati yao kiasi cha kutoa fursa ya kufanya majadiliano ya kirafiki zaidi pale panapotokea matatizo mbalimbali!”

“Bon, serikali nayo ina nafasi yake katika kumaliza tatizo hili. Endapo serikali nayo itajichukilia kama mmiliki wa biashara hiyo basi sina shaka kwamba haitakuwa tayari kuona wateja wake wakidhalilishwa kirahisi hivyo! Ni matumaini yangu kwamba, wote wakishakuwa na mtizamo kama huo basi hata namna ya uendeshaji wa vyuo hivyo unaweza kubadilika. CEO yeyote anajua moja ya majukumu yake ni kuifanya biashara istawi na kuvutia wateja wengi zaidi kadri inavyowezekana! CEO anayeijua kazi yake hawezi kurudi tena kwa mmiliki na kulalamika kwamba biashara yao inazidiwa na wateja badala ya kutafuta mbinu za kutosheleza mahitaji ya wateja hao. Karibu vyuo vikuu vikubwa vyote nchini vina ardhi ya kutosha, tena sehemu kubwa ya ardhi hiyo ikiwa haitumiki! Pamoja na hayo, bado unakuta wakuu wa vyuo wanalalamika kwamba madarasa hayatoshi wakati kuna ardhi kibao haitumiki! Wakuu wa vyuo wakijiona sawa na ma-CEO, basi sina shaka yoyote kwamba wataacha tabia ya kuilalamikia serikali kwamba madarasa hayatoshi, na badala yake wataongea na taasisi za fedha ili kuangalia uwezekano wa kujenga madarasa mengi iwezekanavyo ikiwa pamoja na miundo mbinu mingine. Elimu ya juu ni miongoni mwa fursa ambazo bado hazijazitosheleza soko! Aidha ni miongoni mwa fursa chache zenye uwezo wa kuchomoa wateja kila pande ya dunia! Wakuu wa vyuo vyetu wakijiona sawa ma-CEO basi wataviwezesha vyuo vya umma kuwa na madarasa na miuondombinu ya kutosha itakayowavutia wanafunzi toka kila pande ya dunia. Wakuu wa vyuo wakijiona sawa na ma-CEO basi

hawatasita kuvitangaza vyuo vyetu nje ya mipaka ya Tanzania na hivyo kuvutia fedha za kigeni. Mathalani, chukulia Chuo Kikuu cha Dar es salaam, kina hadhi kubwa sana barani Afrika, lakini wanashindwa kabisa kuitumia nafasi hiyo kujiimarisha! Kwa vile kinavyotambulika kitaaluma, basi ungetarajia chuo kama kile kingekuwa na maelfu kwa maelfu ya wanafunzi kutoka nje ya Tanzania na hivyo kukiingizia chuo na serikali kwa ujumla fedha za kigeni! Uwezekano huo upo kabisa endapo Mkuu wa chuo pale atajiona sawa na Afisa Mtendaji Mkuu wa chuo na hivyo kufanya maamuzi yake kibiashara zaidi! Uwezekano upo kwavile uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya kuongeza miundombinu upo, na wateja kwa maana ya wanafunzi wanaotaka kusoma wapo toka kila kona ya afrika hii kama sio duniani kwa ujumla. Taasisi za fedha hazitaogopa kukopesha vyuo vyetu kwavile watakuwa wanazikopesha taasisi za kibiashara. Magazeti yetu kila siku yanajaa matangazo ya vyuo vya nje ya nchi; hii inaonesha kwamba kumbe hata hapa Tanzania peke yake bado kuna maelfu kwa maelfu ya watu wanaotaka huduma hiyo. Wakati magazeti yetu yanajaa matangazo ya vyuo vya nje, sijui ni magazeti mangapi ya nje yanayotangaza vyuo vyetu ili kuvutia wanafunzi kutoka huko!"

"Bon, hiyo ni kwa upande mmoja, sasa turudi kwenye suala zima la migomo! Binafsi sina shaka yoyote kwamba tukiwa na mtizamo huo hapo juu basi migomo nayo itakufa kifo cha kawaida. Migomo itapungua kwavile Wakuu wa vyuo watawaona wanafunzi kama wateja wao. Na kwavile watakuwa tayari wameshachukuwa mikopo kwenye taasisi za fedha, basi inapotokea chokochoko za migomo kwa vyovyote wataishughulikia mapema. Lazima waishughukie mapema kwavile kufukuza wanafunzi

itamaanisha kufukuza mapato na hivyo kufukuza uwezo wa kurudisha mikopo waliyokopa. Aidha, kwavile watakuwa na mtazamo wa utendaji wa kibiashara, basi sina shaka yoyote kwamba vyuo vyenyewe vitakuwa mstari wa mbele kuyafanyia kazi mambo ambayo yana asili ya kusababisha migomo ya mara kwa mara. Hivyo basi, ni changamoto vilevile kwa serikali kufahamu kwamba matatizo mengi ya vyuoni yanakuwa ndani ya uwezo wa uongozi wa vyuo. Kwa kufahamu hilo, serikali wawaagize viongozi wa vyuo kwamba wasingependa kuona biashara zao zinayumba kwa matatizo yanayoweza kutatulika. Hivyo basi, kwa maoni yangu naamini yakifanyika hayo basi migogoro itapungua kama sio kwisha kabisa kwenye vyuo vyetu!" Glory alimalizia na kumtupia swali Bon Mtambo ili kutaka kujua mtazamo wake yeye.

"Nakubaliana na wewe Glory! Kwa sasa taasisi za fedha zinaweza kusita kuvikopesha vyuo vyetu lakini endapo wakibadilika na kuwa na mtizamo wa kibiashara basi sina shaka kwamba jambo hilo litawezekana! Mathalani, wakiweza kudahiri wanafunzi wapya elfu kumi zaidi, kwa ada ya shilingi milioni moja kila mmoja basi kwa mwaka chuo kitakuwa kimeengiza shilingi bilioni kumi zaidi! Kama wakidahili awamu mbili kwa mwaka ina maana watakuwa wameingiza bilioni ishirinii, kiasi ambacho naamini wataweza kulipia mikopo yao kwenye taasisi za fedha!" Bon Mtambo aliunga mkono kisha wakaanza kuongea mambo kadhaa kwenye suala hilo!

Simu ya Jonas iliita wakati ndio kwanza akiingia ndani kwake akitokea ofisini. Aliitazama namba ya mtu

aliyepiga, lakini hakuifahamu. Alijiuliza endapo aipokee, au aiache. Baada ya kufikiri kwa muda, aliamua kuipokea!

“Mbona ulikuwa unasita kupokea Jonas!?” sauti nyororo ilijipenyeza masikioni mwa Jonas Siyame!

“Siamini masikio yangu, Wendy ni wewe?” Jonas aliuliza kwa bashasha! Alishakata tamaa ya kuonana na mrembo huyu kwani zilishapita kama siku tatu tangu siku aliyoahidi angemtafuta!

“Ni mimi Jonas, je tunaweza kuonana?!”

“Bila shaka, nipo hapa nakusubiri. Ni matumaini yangu kwamba bado unakumbuka maelekezo ya ninapoishi.” Jonas alijibu

“Nakumbuka Jonas!” Wendy aliongea huku akiendelea kukanyaga mafuta. Kiasi cha dakika ishirini baadae alikuwa sebuleni kwa Jonas.

“Mama anaendeleaje Jonas?!”

“Bado hali yake si nzuri sana!”

“Pole sana, ukienda kumwangalia naomba ukamsalimie!”

“Salamu zimefika Wendy.”

Waliongea na kufurahi pamoja hadi majira ya saa mbili usiku pale Wendy alipoaga kwa miadi ya kuja rasmi kesho yake!

# 5

Kama ilivyo kawaida yake, baada ya kupata kifungua kinywa Bon Mtambo alianza kuyapitia magazeti ya hiyo siku. Haikumchukuwa muda kuvutiwa na kichwa kimojawapo cha habari kutoka kwenye moja ya magazeti!

***DRFA Chaibuka Kidedea!***

- *Chama tawala chaambulia nafasi ya pili!*
- *Modern Ujamaa Part (MUP) nao wamo,*
- *Wananchi wabashiri mizozo ya ruzuku kuibuka tena nchini.*

Baada ya kuridhika kwamba hakukuwa na habari nyingine yenye msisimko kwake hatimae alianza kuisoma habari ambayo alivutiwa nayo:

*Chama cha Demokrasia na Raslimali kwa Wote, (DRFA) jana kimetangazwa mshindi kwenye shindano lililoshirikisha vyama mbalimbali vya siasa nchini na kuratibiwa na kituo cha demokrasia nchini, yaani Centre for Democratic Thoughts and Political economy.*

*Akikabidhi zawadi kwa washindi, Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, aliviasa vyama vilivyoshida kutumia pesa walizopata katika kuviendeleza vyama vyao na hivyo kukuza demokrasia nchini.*

*Pamoja na DRFA kilichoibuka mshindi na kujinyakulia donge nono la shilingi nusu bilioni, chama tawala kiliibuka mshindi wa pili na kujinyakulia kitita cha shilingi milioni mia mbili na chama cha Modern Ujamaa kiliibuka mshindi wa tatu na kujinyakulia shilingi milioni mia moja.......!"*

Habari hii ilikuwa ndefu, lakini hata hivyo Bon Mtambo aliisoma yote bila kusaza!

Ilikuwa inakaribia saa kumi jioni wakati Wendy alipokuwa anaparamia ngazi za ofisi ya IBU ili kwenda kutoa taarifa kuhusu Jonas Siyame. Alifika na kugonga mlango kisha akaingia kabla hata hajaitikiwa!

"Karibu Wendy, nilikuwa nakusubiria kwa hamu sana."

"Ahsante bosi, nimekaribia!" Wendy aliitikia na kuvuta kiti kisha akaketi.

"Bila kupoteza muda, hebu tupatie taarifa zozote unazohisi zinaweza kusaidia kumpata Jonas Siyame!"Michael Mchupi alimuuliza Wendy mara baada ya kuvuta kiti na kukaa!

"Sina hakika endapo taarifa nilizonazo zitakuwa na msaada." Hatimae Wendy alianza kuongea kisha akaendelea "Kwa kifupi, jitihada za makusudi zinahitajika katika kumnasa Jonas kutokana na mtindo wake wa maisha! Amekuwa ni msiri mno kiasi kwamba inakuwa vigumu kidogo kupata taarifa zake. Ikumbukwe kwamba, hata pale kwake anaishi peke yake! Aidha, ushahidi mwingine kwamba Jonas ni msiri mno unaweza kuelezeka kutokana na suala la mama yake mzazi. Tulipokuwa nje ya nchi, Jonas alipigiwa simu kwamba mama yake amelazwa Muhimbili na ndio maana alikatiza likizo yake. Na tangu tumerudi hapa nchini, mara zote amekuwa akinificha mama yake amelazwa wapi hasa, kwani nimegundua hajalazwa Muhimbili. Mara kwa mara nimekuwa nikimfuatilia bila mafanikio. Usisahau kwamba Jonas ni

kachero hivyo michezo ya kukwepa mitego ya kufuatiliwa bila shaka kwake ni jambo dogo sana."

"Pamoja na hayo, kuna jambo moja nimegundua kuhusu Jonas. Anaonesha ni mfuasi mzuri sana wa mambo ya kishirikina. Kutokana na hofu yangu hii, nina wasiwasi huenda hata mama yake yupo kwa waganga wa jadi na hivyo anaona aibu kusema ukweli. Hofu yangu kuhusu ufuasi wake na mambo ya kishirikina ilinijia siku niliyolala kwake. Usiku wa manane tukiwa tumelala, ghafla tulisikia paka wakilia dirishani kutokea nje. Mimi nikiwa nimejifanya kutopewa na usingizi, nilimshudia Jonas akihangaika sana hapo kitandani na wakati mwingine alikuwa akichungulia nje na kuwafukuza hao paka. Alipoona paka hao hawatii vitisho vyake, alitoka kitandani na kuvaa kisha akajaribu kunitingisha ili aone endapo nimelala au hapana. Alipohakikisha nimelala, aliinuka polepole na kutoka nje, na ghafla nikasikia akiliondoa gari kwa kasi. Alirudi kiasi cha saa moja baadae!"

"Awali alipoondoka, nilihisi ameenda kumwangalia mama yake kwavile watu wengi wanaamini paka wakilia dirishani basi ni uchuro! Hata hivyo, wazo hilo lilifutika baada ya yeye kurudi kwani alikuja moja kwa moja chumbani kuangalia endapo nimeamka au hapana! Alipojiridhisha kwamba bado nimelala, alienda moja kwa moja jikoni ambako bila shaka alikuwa anachemsha dawa. Baada ya dakika chache alirudi chumbani na kuanza kunyunyunyiza maji fulani kwenye pembe zote za chumba kabla hajalala!"Alimalizia Wendy.

"Kazi nzuri Wendy, hiyo ishara ya ushirikina ni mtaji mkubwa sana kwetu! Hebu jaribu kufuatilia kwa karibu juu ya suala hili kisha ukishathibitisha kwamba kuna mahali huwa anaenda usiku basi itakuwa ni wajibu

wetu kujuwa ni wapi." Michael Mchupi alieleza kisha wakaagana.

"Unajua Bon unanichanganya sana mpenzi wangu?" Hatimae Glory alimweleza Bon Mtambo mara waliporejea nyumbani wakitoka matembezini.

"Nakuchanganya nini mpenzi?! Nimeletwa duniani kwa ajili yako, na bila shaka nawe umeletwa duniani kwa ajili yangu! Hivyo, sioni sababu ni kwanini kuwe na utata kati yetu! Una haki ya kufahamu chochote kuhusu mimi, hali kadhalika nami bila shaka nina haki ya kufahamu chochote kuhusu wewe! Nakujali, nakuheshimu, pia nakuthamini! Mbali ya yote, wewe ni kama mwalimu wangu, na ndio maana mara kwa mara nimekuwa nikiibua mijadala ninayokusudia kujua hisia zako juu ya masuala hayo! Na hata sasa.....!"

"Tafadhali Bon, usitake kupoteza lengo! Huna lolote, unatoa maelezo yote hayo ili kufifisha hoja yangu!"

"Toa basi dukuduku lako mpenzi!" Bon Mtambo alieleza.

"Tupo pamoja kwa karibu mwezi sasa, lakini bado hutaki kuniambia kazi yako hasa ni ipi hapa mjini!"

"Lakini si nilishakuambia kwamba mimi ni mkimbizi wa kisiasa kutoka Burundi? Hata hivyo mimi ni kipusa kwa serikali ya Burundi hivyo usipende kufahamu mengi zaidi kwani itakuwa ni hatari kwako!"

"Una hakika na unachoongea Bon?"

"Kwa asilimia mia moja!"Bon Mtambo alijibu kwa kujiamini, kisha katika hali iliyoonesha ni kutaka kubadili mada, hatimae aliendelea "Samahani Glory, endapo wewe

leo hii unachaguliwa kuwa kiongozi wa nchi, unazani utafanya nini kukabiliana na tatizo la rushwa?"

"Kiongozi wa nchi gani?" Glory aliuliza huku akiwa ameyatuliza macho yake kwa Bon Mtambo.

"Tanzania!"

"Mambo ya Tanzania yetu hayakuhusu Bon! Uliza namna ya kutatua migogoro kwavile ndio matatizo makubwa zaidi nchini kwenu Burundi!" Glory aliongea kwa kejeli huku akibetua midomo yake juu!

"Nina maana yangu Glory!"

*"It's none of your business (*Hayakuhusu*)!"*

"Sikiliza Glory, ingawaje mimi ni raia wa Burundi lakini ukumbuke kwamba Afrika ni moja na ndio maana hata matatizo yetu yanafanana! Ikipatikana tiba ya rushwa Tanzania itakuwa ndio ya Burundi vilevile! Napendwa sana nchini kwetu, na nina hakika siku moja nitakuja kuwa mtu mzito sana kule! Hivyo basi, ndio maana ningependa kufahamu namna nitakavyoweza kukabiliana na changamoto za rushwa pale nitakuporejea nyumbani Burundi!" Bon Mtambo aliendelea kuongopa na kumfanya Glory aendelee kumwangalia kwa jicho la kejeli kwavile alijua anaongopa! Kimsingi, ni kweli Glory alikuwa na shauku ya kumfahamu Bon Mtambo kiundani kwani licha ya kupewa jukumu la kutoa taarifa juu yake, lakini hakujua msingi wa maagizo hayo ni nini!

"Tafadhali Glory, nijibu swali langu!"Bon Mtambo alikumbushia. Glory aliyatuliza macho yake kwake kabla hajaangua kicheko cha masikitiko, na kuanza kuongea:

"Asikuambie mtu Bon, kabla hujaanzisha vita ya aina yoyote ile, ni lazima kwanza ujue ukubwa na mbinu za jeshi la adui yako. Kwa upande wa rushwa nchini kwetu, tatizo ni kubwa pengine kuliko vile watu

wanavyofikiria. Hapa nchini, na Afrika kwa ujumla kumekuwa na rushwa ya kutisha kwenye sekta ya manunuzi, zabuni, hadi kwenye huduma za kila siku. Mara nyingi miradi inayopewa kipaumbele ni ile itakayoweza kutoa ulaji wa kutosha kwa wakubwa kuliko kuangalia manufaa kwa wananchi. Amini usiamini, miradi mingi mikubwa inakuwa imefunikwa na rushwa, tena za kutisha! Ukiona waziri mwenye dhamana anatoa msamaha wa kodi bila sababu za msingi basi ujue kuna jambo. Ni bahati mbaya sana kwamba hata akipelekwa mahakamani, tuhuma dhidi yake zitakuwa ni za matumizi mabaya ya ofisi badala ya rushwa! Ukiona mahali kuna mradi umesimama kwa muda mrefu lazima ujue napo kuna jambo! Tatizo ni kwamba, wafuasi wa rushwa wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali kufanikisha uovu wao. Mathalani, utakuta wakati mwingine mtu ameshinda kandarasi kwa njia zilizo halali kabisa! Lakini kwavile anafahamu hana uwezo wa kuifanya kazi hiyo, au kuimaliza kwa muda alioahidi anaamua kutoa ahsante kwa waliompa kandarasi hiyo! Wale waliotoa kandarasi, wakati mwingine wanachukulia ahsante hiyo ni ya kawaida kwavile kandarasi ilifuata taratibu zote! Mkandarasi yule akishaona ameshawapa pesa ya kutosha anaweza kazi hiyo akaifanya ama katika kiwango cha chini kabisa au asiifanye kabisa! Na hata kama ataifanya, basi huenda asiimalize na kwavile alishatoa *ahsante*, wahusika watashindwa kumchukulia hatua za kisheria! Si hivyo tu, kuna wengine wanaweka vigezo ambavyo wakati mwingine si vya msingi sana lakini wana hakika hamna atakayevifikia zaidi ya watu wao waliopanga kuwapa kandarasi husika! Katika mazingira hayo, unaweza kukuta taratibu zote zilifuatwa lakini nyuma ya taratibu hizo ziliratibiwa na vitendo vya

rushwa. Hivyo basi, huo ni mfano mdogo tu wa namna watu wanavyoweza kuhalalisha hujuma zao. Aidha, ukishafahamu mbinu wanazozitumia basi bila shaka hutapata taabu kufuatilia na kukomesha vitendo hivi! Kwa kuangalia mfano huo, kama umepewa jukumu hilo basi lazima uwe tayari kufuatilia miradi unayoona kwa mfano utekelezaji wake unasuasua. Ukifuatilia na kukuta watendaji wakuu waliohusika na utoaji wa kandarasi husika wana mapato yasiyoendana na kazi yao basi lazima utafute chanzo cha mapato hayo. Ukiona mtu anatoa kandarasi ya kujenga uwanja wa ndege mkubwa kabisa bila sababu za msingi basi jaribu kufuatilia kwa siri na hapo utakuta kilichosabaisha kutolewa kwa kandarasi hiyo ni rushwa ama ubadhirifu wa mali ya umma!

“Sasa unazani nini kifanyike kukabiliana na hii hali Glory? Maelezo yako yanaonesha zaidi kutibu tatizo badala ya kuzuia!”

“Njia pekee ni kumfanya kila mmoja asimwamini jirani yake. Kuna simulizi moja ya mitaani kwamba ukiwalaza *mabasha* wawili kitanda kimoja basi hakuna hata mmoja kati yao atakayepata japo lepe la usingizi! Watakesha macho usiku kucha, kwavile kila mmoja hamwamini mwenzake! Ninachomaanisha ni kwamba, lazima ijengeke hali ambayo kila mmoja atakuwa anamuhisi jirani yake kuwa ni askari kanzu katika vita dhidi ya rushwa. Leo hii, endapo ningekuwa ni kiongozi wa juu wa nchi hii, ningeunda kikosi cha siri cha kupambana na rushwa. Hii haimaanishi kuivunja TAKUKURU, la hasha. Kikosi hiki kingekuwa cha siri, tena cha siri kwelikweli! Hata hivyo, kila mtu angefahamu kuwapo wa kikosi hiki. Kitu ambacho kisingefahamika ni nani watumishi wa kikosi hicho! Ni kikosi ambacho

watumishi wake wasingefahamika hata na maofisa na watendaji wakuu serikalini, wakiwamo mawaziri. Kufahamika kwa askari kanzu yeyote kwenye kikosi hiki, ingekuwa ni sababu tosha ya kuachishwa kazi na yeye kueleza kiundani mazingira yaliyopelekea kufahamika kwake! Kikosi hiki kingekuwa na kazi maalumu, na kubwa zaidi ni kujua ni nani hasa anaweza kuaminika hadi kupewa dhamana ya kuongoza taasisi nyeti za serikali. Wapo mawaziri na watendaji kadhaa serikalini ambao tangu kuwa kwao madarakani hawajahi kuomba wala kupokea rushwa. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba wote hao ni maadui wa rushwa. Inawezekana kabisa kwamba wapo kwenye wizara au idara zilizokosa mianya ya rushwa. Na endapo watakuwa kwenye wizara au idara zenye mianya ya rushwa si ajabu wakageuka ni wala rushwa wa kutisha! Hivyo basi, kikosi hiki cha siri kitawezesha kufahamu ni nani hasa asiye mla rushwa kwavile tu hajapata mwanya huo, na nani asiye mla rushwa kwavile anaichukia rushwa! Haidhuru hata kama kikosi hiki kitaitwa *The Devil Army*, kwavile ni kweli kingefanya kazi yake mithili ya shetani, au ibilisi ukipenda! Wakati mwingine Mungu humtuma ibilisi kwa binadamu ili ajue ni namna gani binadamu yule alivyo na imani juu yake. Ningekuwa ni rais, ningewatuma ibilisi wa kikosi changu ili kujua ni nani hasa asiye mfuasi wa rushwa kwa maana ya kuichukia na si kwavile tu hajapata nafasi hiyo. Ibilisi wangu hawa wangekuwa wanafanya kazi kila inapoonekana ni muhimu kufanya hivyo. Nina hakika, ingefikia mahali hadi wenye mamlaka nchini wangeshindwa kujua ni nani mtoa rushwa wa kweli na ni nani mtoa rushwa ibilisi! Ibilisi hawa wangefanya kazi kwa kiapo, na kiapo chao kikubwa ni wao kutojitambulisha kwa

yeyote na kwa namna yoyote kuwa wao ni nani hasa! Wangekuwa na taswira zote za muonekano ambao usingekuwa ni wa kutia shaka! Kama ambavyo ibilisi wa mungu anavyokuja kwako katika sura mbalimbali, ibilisi wangu hawa nao wasingekuwa na sura maalumu! Upo wakati wangekuja kwako wakiwa kama wafanyabiashara wakubwa, mawakala wa makampuni ya nje, wasichana warembo wenye kuvutia na wakati mwingine wangekuja wakiwa ni kama watu wa *misheni town*! Vilevile, ibilisi wangu hawa nao wasingekuwa salama kwavile usipokua makini unaweza kukuta ibilisi nao wanajisahau na kuyeyushwa kwa tamaa! Kutokana na hilo, vilevile ibilisi wangu hawa wangepeana mitihami wenyewe kwa wanyewe bila kujua!"

"Si hivyo tu, ningehakikisha sheria nazo zinaangaliwa upya. Tatizo kubwa lililopo kwenye suala zima la rushwa ni ushahidi. Si Tanzania au Afrika pekee, bali hata Ulaya na Amerika nako wanakabiliwa na tatizo la kuthibitisha madai ya rushwa. Na kwavile suala la kutuhumiwa peke yake halitoshi kumuhukumu mtu kwamba ni mla rushwa lakini tuhuma peke yake zinatosha kabisa kumtilia mtu shaka katika utendaji wake kwa ujumla. Endapo mtu anatuhumiwa kuomba ama kupokea rushwa wakati mwenyewe anadai si kweli, hapo ni lazima tujiulize kuna mazingira gani yaliyosababisha shaka hiyo. Kutuhumiwa peke yake ni sababu tosha kabisa ya kumfanya kiongozi wa serikali kukaa pembeni. Dhana ya kujiuzuru si lazima uwe umefanya kosa husika kwa namna moja au nyingine, bali hata pale unaowahudumia wanapokosa imani kwako. Hata hivyo, kama nilivyosema hapo awali, jambo muhimu ni kuangalia mazingira yaliyosababisha tuhuma husika. Aidha, kwenye suala hilo

hilo la sheria, ningehakikisha madaraka ya Waziri wa Fedha katika kusamehe kodi yanapunguzwa. Hapa ningehakikisha kwamba misamaha yote ya kodi inayofikia kiasi fulani cha pesa basi lazima ijadiliwe na bunge. Pale inapobidi, hata kikao cha dharura cha bunge kitakuwa kinaitishwa kujadili misamaha husika. Hivyo basi, hiyo ingekuwa ni moja ya mbinu ambazo ningetumia kukabiliana na tatizo hili! Je, wewe unasemaje?" Glory alimalizia na kumtupia swali Bon Mtambo. Bon Mtambo nae alitoa mawazo yake ambayo kimsingi ilikuwa ni ya kuunga mkono yale yaliyosemwa na Glory.

# 6

Bwana Hassan Muki alikuwa anajiandaa kuingia ndani ya gari yake wakati simu yake ya mkononi ilipoita. Bila kupoteza muda, aliipokea akiwa tayari ameshaingia garini.

"Bwana Hassan Muki kwenye simu, nani mwenzangu?"

"Naitwa Mohamed Salehe, au Senti Kumi!" Sauti upande wa pili ilijipenyeza masikioni mwa Bwana Hassan Muki.

"Unasema!?" Bwana Hassan Muki aliuliza kwa hamaki. Si kwamba hakusikia, la hasha! Bila shaka pasingekuwa na tatizo lolote endapo mpigaji angejitambulisha kwa jina la Mohamed Salehe pekee!

Lakini Senti kumi!?

Hapana!

Hii si miongoni mwa simu alizozizowea!

"Nini hakijaeleweka Bwana Bwana Hassan Muki!?" Huyo mtu aliyejitambulisha kama Senti Kumi aliuliza!

"Wewe ni nani?!" Bwana Hassan Muki alijikuta akiuliza swali ambalo tayari jibu lake alishakuwa nalo!

"Nikuambie mara ngapi kwamba naitwa Mohamed Salehe, au Senti Kumi ukipenda?!"

"Shida yako nini?"Bwana Hassan Muki aliuliza kwa ukali.

"Nahitaji kuwa mwanachama wa DRFA!"

"Kama hiyo ndio shida yako, basi tuonane kesho asubuhi ofisini."

“Hapana Bwana Mushi, nataka tukutane leo tena sasa hivi!”

“Eti?!”

“Nimekuambia tukutane sasa hivi!”

“Wewe ni nani hata uwe na jeuri ya kunipa amri!?” Bwana Hassan Muki aliuliza hivi sasa akiwa ameghadhibika zaidi! Aliangaza macho huku na huko kama angeweza kumuona mtu aliyekuwa na shauku na yeye lakini kila mmoja alikuwa na hamsini zake!

“Nimekuambia naitwa Senti Kumi, wakala wa siri wa TAKUKURU. Wewe na chama chako mnatuhumiwa kupokea kwa siri mamilioni ya pesa kutoka CDTPE! Mmefanya hivyo huku mkifahamu fika kwamba hiyo ni kinyume cha sheria na taratibu za nchi hii!”

“Umesema unaitwa nani?!” Bwana Hassan Muki aliuliza tena swali lilelile huku ikionesha wazi kwamba amechanganywa na taarifa hizi!

“Tusipotezeane muda Bwana Muki, sema kama upo tayari kuonana na mimi au hutaki! Lazima ujue kwamba nina ushahidi wote wa tukio lile ambalo mliwekeana saini kwa siri!”

“Tukutane wapi?” Hatimae Bwana Hassan Muki aliuliza akiwa amelowana!

“Angalia kushoto kwako utaona gari aina ya Toyota Surf 4 yenye rangi ya majani makavu. Gari yako iache hapo hapo, utaifuata baada ya mkutano wetu!” Baada ya kupewa maelezo haya, Bwana Hassan Muki aligeuka kushoto na kugongana macho na mtu aliyekuwa kwenye gari aliyoelekezwa! Huyo mtu akatoa ishara ya kumuita Bwana Muki!

“Unapokuwa humu Bwana Muki unatakiwa kufuata malelekezo utakayopewa bila kuleta ukaidi wowote.”

Bwana Hassan Muki alielezwa mara alipoingia kwenye gari. Katika hali ambayo hakuitarajia, alijikuta akifungwa kitambaa cheusi usoni, kisha gari ikaondolewa kwa mwendo wa kasi!

Bon Mtambo alifanya haraka kuwahi ofisi za chama cha siasa cha Modern Ujamaa Part, kwa kifupi MUP ili kufanya mahojiano na mwenyekiti wa chama hicho; Bwana Najum Mchunda. Pamoja na kazi yake maalumu, Bon Mtambo vilevile ni mwandishi wa kujitegemea wa makala kwenye magazeti mbalimbali nchini na nje ya nchi. Alipendelea zaidi kuandika makala za uchumi, siasa na kijamii. Kilichomsukuma kwenda MUP ni malalamiko ya wananchi kuhusu tuzo zilizokipa ushindi chama cha DRFA. Alikusudia kuandika makala mara baada ya mahojiano hayo.

"Karibu kijana!" Bwana Najum Mchunda alikaribisha mara baada ya Bon Mtambo kuingia.

"Ahsante Bwana Mchunda, kabla hatujazungumzia tuzo ya CDTPE, ningependa kufahamu ni mambo gani hasa chama chako inatarajia kuyafanya pindi kitakapopata ridhaa ya wananchi ya kuingia madarakani! Zaidi, ningependa kufahamu mawazo ambayo unaamini ni mapya !" Bon Mtambo alianzisha mjadala.

"Ahsante sana Bwana Mwandishi. Awali ya yote, sizani kama hapa tulipofikia unaweza kuanzisha mawazo mapya, lakini naamini kuna baadhi ya mambo yakiboreshwa basi bila shaka tunaweza kupiga hatua." Bwana Najum Mchunda alianza kueleza, kisha akaendelea "Kwa kifupi ningependa kuzungumza machache kuhusu

sera zetu za kiuchumi ambazo kimsingi zinalenga kufanya mabadiliko makubwa ya kimuundo na utawala. Mpango wa MUP ni kutenganisha shughuli za kiuchumi na uongozi wa kisiasa. Ili kufanikisha hili, wizara zinazoshughulika na maendeleo ya kiuchumi zitavunjwa na badala yake kuundwa idara za serikali. Aidha, lengo letu ni kuufanya mfumo huo ufanye kazi kupitia kanda maalumu za kiuchumi zitakazoongozwa na Waziri Mkuu wa Kanda. Waziri Mkuu wa Kanda atakuwa ndie msimamizi mkuu wa shughuli zote za kiuchumi na maendeleo kwenye kanda husika, akiwa pia ndie mwakilishi wa serikali. Pamoja nae, kila kanda itakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kanda, yaani *Zonal Executive Director* (ZED) atakayekuwa ni mtaalamu hususani katika nyanja za uchumi na uwekezaji. Vilevile chini ya ZED, kutakuwa na Wakurugenzi wa idara mbalimbali kutegemeana na fursa za kiuchumi zilizopo ndani ya kanda husika. Idara hizi ndizo zitakazochukua nafasi ya wizara mbalimbali zinazohusika na shughuli za kiuchumi hivi sasa. Chini ya Wakurugenzi wa idara hizi kutakuwa na mameneja wa sekta ndogondogo zinazounda sekta kuu ya idara husika. Mathalani, tukichukua wizara ya kilimo, tutakuwa na Idara ya Maendeleo ya Kilimo itakayoongozwa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Kilimo, kwa kifupi ZADD, yaani *Zone Agriculture Development Director*. Chini ya ZADD kutakuwa na mameneja wa maendeleo ya uvuvi, maendeleo ya mazao, maendeleo ya mifugo, pamoja na maendeleo ya umwagiliaji."

“Pamoja na hayo, kutakuwa na programu maalumu za kuchochea ukuaji wa baadhi ya sekta kwenye baadhi ya idara hizo. Kwa sasa, tayari tumeandaa programu kubwa mbili ambazo ni programu ya uzalishaji wa mazao maalumu, yaani *Agriculture Enterprises Specialization*

*Program*, kwa kifupi AESP pamoja na programu ya kuchochea ukuaji wa viwanda, kwa kifupi IDSP, yaani *Industrial Development Stimulation Program*. Hata hivyo, AESP itakuwa chini ya Idara ya Maendeleo ya Kilimo ya kila kanda wakati IDSP itakuwa ni programu ya kitaifa."

"Chini ya AESP, nchi itagawanywa katika kanda maalumu za uzalishaji wa aina moja ya zao lenye kutoa tija kubwa zaidi kuliko zao lingine lolote kwenye kanda husika. Jambo hili ni muhimu sana kwani mara nyingi wananchi wamekuwa wakitumia nguvu nyingi kulima mazao yasiyo na tija ya kutosha kwenye maeneo yao. Hivyo basi, wananchi watakaojiunga na mpango huu watanufaika na misaada mbalimbali kutoka serikalini. Wajibu wao itakuwa ni kuunda vikundi vidogo vidogo vya ukulima wa mazao yaliyoteuliwa kwenye maeneo yao. Baada ya hapo, serikali itakuwa inawapatia pembejeo zote muhimu ikiwa ni pamoja na kuwalimia mashamba yao kwa trekta huku wao wakiwa na wajibu wa kuyatunza mashamba hayo pamoja na kufanya shughuli zingine zinazohitaji nguvu kazi watu. Na pale inapobidi, watalazimika kuchangia kiasi kidogo cha fedha ili kufanikisha mradi huo."

"Kama nilivyosema awali, mpango huu utaenda sawia na uundaji wa kanda maalumu ingawaje kanda hizo hazitagawanywa kwa kuangalia mipaka iliyopo, na badala yake zitatokana na sura ya nchi ya eneo husika. Mathalani, chini ya mpango huu Mbinga, Moshi na Karagwe zinaweza kuwa kanda moja ya uzalishaji wa kahawa, wakati Kyela, Kilombero na Ruvu zinaweza kuwa kanda moja ya uzalishaji wa mpunga! Aidha, chini ya mpango huu, MUP inakusudia kuanza na mazao ya nafaka na mikundekunde yanayotumika sana hapa nchini na nchi za jirani kwa

chakula. Kwa maana hiyo, tutaanza na mahindi, mtama, ngano, mpunga, maharage na kunde. Kwa siku za usoni, mpango huu utaenda sawia na mazao kama korosho, ufuta, kahawa, chai, tumbaku na pamba."

"Ndugu Mwandishi, ili kufanikisha mkakati huu tunarajia kuufanya mfumo wa usimamizi na uongozi uwe ni wa kikampuni zaidi, ambapo kutakuwa na Meneja Uzalishaji wa Mahindi, Meneja Uzalishaji wa Maharage na kadhalika. Hawa wote, watakuwa na wajibu wa kuhakikisha sekta zao zinafikia malengo yatakayowekwa."

"Aidha, kwa upande wa IDSP, ni programu itakayofanya kazi chini ya programu nyingine inayojulikana kama Kuweka Akiba Kabla ya Kubajeti, kwa kifupi SBBS yaani *Saving Before Budget Scheme.* Chini ya SBBS, asilimia kumi ya mapato yote ya serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, yatakuwa yanaenda kwenye mfuko maalumu wa IDSP. Mapato ghafi ya TRA ya kila mwezi yatakuwa kwanza yanakatwa asilimia kumi na kiasi kinachobaki ndicho kitakachoenda kwenye mzunguko wake wa kawaida."

"Chini ya IDSP kutakuwa na vivutio mbalimbali vitakavyolenga kuvutia wawekezaji kutoka nje kuja kuwekeza kwenye sekta ya viwanda nchini. Hapa tunalenga kupata wawekezaji wenye mitaji na teknolojia muafaka itakayowezesha kuongeza uzalishaji kwenye sekta ya viwanda. Moja ya vivutio hivyo vipo chini ya mpango wa Wekeza Tanzania kwa Mikopo ya Uwekezaji Isiyo na Riba, yaani *Invest in Tanzania with Free Interest Capital Investment Loans*, kwa kifupi IT with FICIL. Chini ya mpango huu, mwekezaji mwenye sifa zinazokubalika atadhaminiwa na serikali katika uchukuaji wa mikopo ambapo riba ya mkopo husika itakuwa inalipwa na serikali.

Aidha, hata kwa kampuni zisizo na mtaji wa kutosha, tutapenda kufanya nazo kazi ili mradi turidhike kwamba zina teknolojia muafaka, ujuzi na uzoefu kwenye sekta husika. Kwa upande huu, serikali itakuwa tayari kuchangia gharama zote za uwekezaji na uendeshaji wa viwanda husika kwa makubaliano maalumu. Mathalani, serikali itaweza kumiliki hisa si pungufu ya asilimia sabini ya kiwanda husika na asilimia itakayobaki kumilikiwa na wawekezaji kwa mkopo. Mkopo huu utakuwa unalipwa kila mwaka kupitia gawio la hisa za wawekezaji hao ambao kimsingi watakuwa wamewekeza ujuzi na teknolojia."

"Ndugu Mtangazaji, naomba hapa nifafanunue kidogo kuhusu aina hii ya wawekezaji. Tuseme serikali imeonelea kuwekeza kwenye kiwanda cha elekroniki. Hapa tutaziagiza balozi zetu zilizopo kwenye nchi zilizoendelea kwenye masuala ya elektroniki ili kutafuta vijana na hata wastaafu wabunifu na wenye uzoefu katika sekta hiyo. Tukimpata mmoja, tutamweleza lengo la kuanzisha kiwanda cha aina hiyo nchini Tanzania. Aidha, tutamweleza nia yetu ya kushirikiana na yeye ili kufanikisha lengo hilo. Tutachomuomba ni yeye kutafuta watu wengine wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha na kuwaahidi kuwamilikisha kwa mkopo kiasi fulani cha hisa za kiwanda husika. Ni matumaini ya MUP kwamba wengi miongoni mwa watu wa aina hiyo wangependa kukifanyia kazi kiwanda ambacho nao wanakimiliki kuliko vinginevyo. Na moja ya vyanzo vya mapato ya kufanikisha mradi huo ni fedha kutoka SBBS. Serikali ya UMP itakuwa tayari kupunguza ama kukata kabisa matumizi kwenye maeneo fulani fulani ili kufanikisha mpango huu. Ni matumaini yetu kwamba wawekezaji wa aina hii watatoa mchango mkubwa sana katika kufikia azma yetu ya

maendeleo ya viwanda nchini kwavile watafanya kazi kwa kushirikiana na Watanzania."

"Mkakati wetu hauishii hapo. Kama ujuavyo ndugu, tatizo kubwa linaloikabili sekta ya uzalishaji nchini, hususani kilimo ambayo ndio sekta kuu, ni masoko. Tatizo la masoko tunatarajia kulipatia kipaumbele kiasi cha kuliundia idara yake inayojitegemea. Idara hii itajulikana kama Zone Marketing Department, yaani Idara ya Masoko ya Kanda, kwa kifupi ZMD itakayoongozwa na Mkurugenzi wa Masoko wa Kanda. Ndani ya ZMD kutakuwa na vitengo viwili ambavyo ni Kitengo cha Masoko ya Ndani, kwa kifupi DMS (*Domestic Marketing Section*) na Kitengo cha Masoko ya Nje, kwa kifupi EMS *(External Marketing Section)*. Hata hivyo, soko la ndani litamaanisha ni soko ndani ya kanda husika na soko la nje ni soko nje ya kanda husika pamoja na nje ya nchi. Hapa tunataka kuchochea biashara kutoka kanda moja hadi nyingine kwa bidhaa mbalimbali ili kukidhi soko la ndani."

"Ndugu Mwandishi, kama nilivyosema hapo awali, lengo letu ni kutenganisha shughuli za kiuchumi na siasa. Ili kukidhi lengo hilo, tunakusudia idara zote ziwe chini ya Mamlaka ya Kuendeleza Uchumi Tanzania, yaani *Natioanal Economic Development Authority*, kwa kifupi NEDA ambayo itakuwa chini ya Katibu Mkuu Mtendaji wa Maendeleo ya Uchumi nchini."

"Si hivyo tu, suala la uwajibikaji kwa watendaji serikalini nalo tumelitafutia dawa kwa kuliundia chombo kitakachoratibu utendaji wao. Chombo hiki kitaitwa Executive Performance Appraisal, yaani EPA. EPA itakuwa ni taasisi inayojitegemea ambayo kazi yake kuu ni kutathimini ufanisi wa watendaji mbalimbali wa idara zitakazoundwa. Watendaji hawa watapimwa kutokana na

mafanikio ya utendaji wao katika kufikia malengo yaliyowekwa kupitia nafasi zao. Watendaji hawa watakuwa wanaajiriwa kwa mkataba wa miaka mitatu mitatu. Hata hivyo, EPA itakuwa inafanyika kila mwaka na majumuisho ya miaka mitatu ndiyo yatakayoamua hatima ya mtendaji husika kwenye nafasi ayake. Ni bahati mbaya sana, ili kuondoa uwezekano wa kulindana ikiwa ni ugonjwa mwingine tulionao Watanzania, basi kuna kila uwezekano EPA ikawa inaongozwa na mgeni pale itakapobidi!" Baada ya kufika hapa, Mheshimiwa Najum Mchunda alitulia kidogo kisha akaendelea:

"Ndugu Mwandishi, ili serikali ya MUP iweze kufikia malengo ya kuondoa umaskini nchini, itawataka watendaji wa idara kuibua fursa mbalimbali za kiuchumi zilizopo kwenye kanda husika. Uwekezaji ukishafanyika, vitega uchumi hivyo vitakuwa vinapata ruzuku toka Hazina kwa kipindi maalumu kutegemea na ukubwa wa mradi. Baada ya hapo, miradi hiyo italazimika kujiendesha yenyewe kibiashara. Hata hivyo, miradi hii haitabaki serikalini milele, badala yake kila mradi utakaokidhi vigezo utakuwa unauza kiasi cha hisa zake kwa wananchi. Na kwavile miradi hii itakuwa imetoa ajira kwa wananchi wengi basi tuna imani kwamba wengi wao watakuwa na uwezo wa kununua hisa hizo na hivyo kuwapa fursa ya kumiliki uchumi wa nchi yao."

"Pamoja na idara hizo ambazo shughuli zake hata sasa zinafahamika, vilevile tunatarajia kuunda idara zitakazohusika na uibuaji wa miradi itakayotumia zaidi nguvu kazi za wananchi. Aidha, tunatarajia kufanya mabadiliko ya kisheria ambapo watuhumiwa watakaopatikana na hatia kwenye baadhi ya makosa wawe wanatumika kwenye miradi hii kama adhabu badala ya

kuwafunga jela. Idara hii itakayokuwapo katika kila kanda itajulikana kama *Micro Enterprises Labor Intensive Department*, kwa kifupi MELID. Watendaji kwenye idara hii watakuwa na wajibu wa kuibua miradi ambayo itashirikisha vikundi vidogo vidogo vya wananchi katika uendeshaji wake. Wananchi watakuwa ndio wamiliki wa miradi hiyo ambapo mchango wao utakuwa ni nguvu zao wenyewe. Wakati wananchi watakuwa ndo wamiliki, kazi ya watendaji wa serikali itakuwa ni kutoa huduma ya kiuongozi kwenye miradi hiyo. Aidha, kazi ya serikali itakuwa ni kutoa vitendea kazi vitakavyokuwa kwenye mfumo wa mashine za moto wakati wa mwanzo wa mradi. Hata hivyo, asilimia fulani ya mapato kwenye miradi hii itakuwa inaenda serikalini kwa ajili ya kuanzisha miradi mingine kama hiyo na hivyo kuufanya mpango mzima kuwa endelevu."Baada ya kufika hapa, Mheshimiwa Najum Mchunda alipepesa macho huku na huko kisha akaendelea: "Ndugu Mwandishi, endapo patatokea mtu atakayekosa shughuli maalumu ya kufanya chini ya mipango yote hii, basi naamini mtu huyo hastahili kuishi kwenye dunia ya wastaarabu. Aidha, ni matumaini yetu kwamba hata lile wimbi la vijana kukimbilia Dar es salaam litapungua kwa kiasi kikubwa kwavile nyingi ya shughuli hizi zitakuwa zinafanyika mikoani, hususani vijijini."Alimalizia.

"Bwana Mchunda, kimsingi hapa nchini tumeshauzika mfumo wa kijamaa na sasa tunafuata mfumo wa kibepari. Hata hivyo, nikiangalia maelezo yako na hata jina la chama chako inaonesha ni kama unaturudisha tena kwenye ujamaa!?" Hatimae Bon Mtambo alihoji!

"Sina uhakika endapo ni kweli tunakusudia kuirudisha nchi kwenye mfumo wa ujamaa lakini hata

kama ndivyo, bado ujamaa wetu utakuwa tofauti sana na ujamaa wa Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere! Falsafa yetu ni kuwawezesha Watanzania kumiliki uchumi wao wenyewe kwa kiasi kikubwa kadri itakavyowezekana. Kwa maana nyingine tunataka kutengeneza mabepari wa kitanzania. Hata hivyo, falsafa yetu hiyo inatuaminisha kwamba huwezi kufanikiwa kwenye mfumo wa kibepari kabla ya kufanikiwa kwenye mfumo wa ujamaa! Ukirukia kwenye ubepari kabla ya kufanikiwa kwenye mfumo wa ujamaa itakuwa ni kutengeneza ubepari wa kinyonyaji, utakaokandamiza wananchi walio wengi. Katika falsafa hii, serikali itakuwa inamiliki vitega uchumi mbalimbali kwa muda maalumu lakini kwa niaba ya wananchi. Wakati muafaka ukifika, serikali itakuwa inauza hisa za vitega uchumi hivyo kwa nyakati mbalimbali huku ikiendelea kuhodhi sehemu nyingine ya hisa hizo."

"Aidha, katika suala la serikali kumilikisha vitega uchumi vyake kwa wananchi halitaishia hapo bali litaenda mbali zaidi. Kuna mpango mwingine unaolenga kuwawezesha wafanyabiashara wa kati ili wafikie hatua ya juu kibiashara. Katika hili hatutaangalia ukubwa wa biashara peke yake bali safu ya uongozi inayosimamia kampuni husika. Kampuni ambazo zitakakidhi vigezo vitakavyowekwa zitasaidiwa kwa mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kudhaminiwa kwenye taasisi za fedha na suala zima la mafunzo ya uongozi wa biashara. Lengo letu hapa ni kwamba kampuni hizi zikishafikia sifa za kuweza kuendesha biashara kubwa basi ziweze kuuziwa sehemu ya hisa ambazo zilikuwa zinahodhiwa na serikali kwenye vitega uchumi vyake. Hivyo basi, utaona kwamba serikali itakuwa inajitoa kwenye umiliki wa uchumi wake kwa nyakati mbalimbali kwa kuuza hisa kwa wananchi na

kisha pesa zinazopatikana kuibua miradi mingine. Zoezi hili litakuwa endelevu hadi pale tutakaporidhika kwamba sekta binafsi imekuwa kiasi cha kuweza kujiendesha yenyewe. Tukifikia hapo, serikali itajitoa moja kwa moja kwenye suala zima la kumiliki njia kuu za uchumi na kumilikisha vitega uchumi hivyo kwa Watanzania wenyewe badala ya kuwamilikisha wageni kama ilivyo sasa. Hapo falsafa yetu itakuwa imetimia kwa kuondoka kwenye mfumo wa kijamaa kama ulivyoita na kuingia kwenye mfumo wa ubepari wenye manufaa kwa Watanzania walio wengi. Pamoja na hayo, ingawaje serikali itakuwa inajihusisha na suala la uwekezaji, sekta binafsi nayo itakuwa inaendelea na shughuli zake kama kawaida. *Modern Ujamaa* ni mfumo utakaoruhusu ushindani ulio sawa kati ya serikali na sekta binafsi katika kushiriki katika shughulia za kiuchumi. Labda tu niseme jambo moja, kimsingi, mipango na mikakati katika jambo hili ipo mingi ambayo siwezi yote kuileza hapa, lakini ukitaka nitakupatia kitabu kinachoelezea sera zetu za kiuchumi."

Mtu wa mwisho kuingia alikuwa ni Dunstan Mkundi, Katibu wa Umoja wa Vijana wa DRFA. Aliingia akiwa ni mwingi wa bashasha huku akionesha wazi kwamba alikuwa na jambo angependa kulizungumza!

"Ni matumaini yangu kwamba sijachelewa sana. Na ingawaje mwenyekiti ana jambo la kutuambia, ningependa mnipatie kwanza fursa ya kuwapatia habari njema za huko nitokako!" Dunstan Mkundi aliongea kwa furaha mara baada ya kuvuta kiti na kuketi.

“Tupatie hizo nyepesinyepesi!” Anatory Saibaba, katibu Mkuu wa DRFA aliongea kwa hamasa!

“Tumewamaliza!” Bwana Mkundi nae aliongea kwa mbwembwe, kisha akaendelea, “Yule jamaa amenionesha kila kitu ambacho tungehitaji kuanza nacho katika kuanzisha mashambulizi. Hata hivyo, nyaraka zote alizonipatia amezikata sehemu ambazo zina saini za wahusika na kwamba anaweza kutupatia nyaraka kamilifu pale tu tutakavyompatia pesa zake.” Alimalizia na kutoa hizo nyaraka na kumpatia Anatory Saibaba ambae baada ya kuziangalia kwa haraka haraka alitoa tabasamu la ushindi! Nae alizipitisha kwa wenzake na baada ya wote kuzipitia walimpatia mwenyekiti wao Bwana Bwana Hassan Muki.

Tofauti na viongozi wenzake, Bwana Hassan Muki alizingalia mara moja tu na kuzitupa mezani. Ajabu ni kwamba, hakuonesha furaha hata chembe, na badala yake alitoa karatasi fulani kwenye mkoba na kumpatia Anatory Saibaba!

*“Bravo Mr. Chairman!”* Bwana Saibaba aliongea kwa sauti huku akipunga ngumi juu kama ishara ya ushindi! Nyaraka alizopewa na Bwana Hassan Muki zilikuwa ni kama zile alizoonesha Dunstan Mkundi. Tofauti na za Mkundi, nyaraka za Bwana Muki zilikuwa zimekamilika!

*“You deserve to be Mr. President our excellence Mr. Chairman!”(*Unastahili kuwa rais wa nchi hii Bwana Mwenyekiti!)!” Mkundi nae aliongea kwa hamasa baada ya kuziangalia hizo nyaraka!

Hata hivyo, Bwana Hassan Muki bado alibaki akiwa mnyonge!

“Mwenyekiti inakuwaje katikati ya ushindi unakuwa mnyonge?!” Dunstan Mkundi aliuliza.

"Hiyo kashfa hatutakiwi kuitoa hadharani!"Bwana Hassan Muki alijibu huku akiwa katika hali hali ile ile ya unyonge!

"*What* (nini)?!" Mkundi aliuliza kwa kihoro.

"Kwanini na kwa maslahi ya nani?!"Anatory Saibaba nae aliuliza!

Hakika viongozi wote wa DRFA waliohudhuria hapa walimwangalia mwenyekiti wao kwa mshangao! Bwana Hassan Muki nae alishayasoma mawazo yao!

"Ni kweli wapiganaji wenzangu, kashfa hiyo hatutakiwi kuitoa hadharani kwa maslahi ya hao waliotuagiza kutofanya hivyo, na kwa maslahi yetu pia!"

"Ni nani hao waliotuagiza, na walijuaje suala hili? Ni vyombo vya usalama, au kuna msaliti miongoni mwetu?!"Dunstan Mkundi aliuliza kwa jazba!

"Si vyombo vya usalama. Nazani ni ama serikali au chama tawala, wameamua kufanya kazi zao kijasusi hivi sasa!"

"Hatukuelewi mwenyekiti!"

"Ni hivi ndugu zangu, jana wakati najiandaa kutoka ofisini nilitekwa na watu wasiojulikana na kunipeleka mahali ambako hadi hivi sasa sipajui! Nilipofikishwa kwa mabosi wa watekaji waliniambia wamepata taarifa za sisi kutaka kuibua kashfa ya kampuni ya TanEuro Energy. Wakanionya kwamba endapo tutaibua kashfa hiyo, nao wataibua kashfa ya sisi kupatiwa misaada kwa siri kutoka CDTPE. Wamesema wana ushahidi wote na hadi akaunti ambazo pesa kutoka CDTPE zinakopita."

"Umewaamini?" Anatory Saibaba aliuliza.

"Kuwaamini nini?"

"Kwamba ni kweli wana ushahidi?"

“Ni kweli wana ushahidi. Wamenionesha kanda za video za tukio lile la kuwekeana saini na CDTPE. Si hivyo tu, wamenionesha hadi baadhi ya nyaraka zilizotumika ile siku!” Alimalizia kisha akaingiza mkono kwenye mkoba na kutoa CD ya video ambayo moja kwa moja aliingiza kwenye mashine na kuwasha televisheni!

Picha za tukio zima la kutiliana saini kati ya CDTPE na DRFA zilianza kutokea! Wote wakabaki wamenywea!

“Haiwezekani! Ni njama za chama tawala hizi!” Dunstan Mkundi alifoka!

Hakika kila mmoja alikuwa amelowana asijue la kufanya! Wapo walioangaliana kwa namna ya kusutana, na wapo waliotoa ishara ya majuto!

“Ndugu zangu naomba tupunguze jazba na badala yake tujadili cha kufanya ili kukabiliana na hali hii. Hili ni tukio la kwanza tu, cha kujiuliza ni endapo hili ni tukio la mwanzo na la mwisho au ni la mwanzo endelevu!” Bwana Hassan Muki aliongea kwa simanzi.

“Naamini huu ni mwanzo tu wa hujuma hizi, na zitaendelea kila pale itakapoonekana tunataka kuingilia maslahi yao! Jambo la msingi hapa ni kujua ni nani aliye nyuma ya hujuma hizi! Inawezekana kabisa ikawa ni serikali au chama tawala, lakini inawezekana vilevile wakawa ni watu wengine kabisa. Itaeleweka endapo hujuma hizi zinafanywa na serikali au chama tawala, lakini kama ni watu wengine basi ni lazima tujue wanafanya kwa maslahi ya nani!” Hatimae Makamu Mwenyekiti, Bi Theresia Mwaipopo alitoa hoja baada ya kuwa kimya kwa muda mrefu.

“Lakini kwanini tusianze na hao wahusika wakuu waliomo kwenye hizo nyaraka za serikali? Inawezekana kabisa kwamba ni wao ndio walio nyuma ya njama hizi

kwavile wasingependa kuvuliwa nguo hadharani!" Fatma Mosha nae alitoa wazo.

"Hapana Bi. Fatma, hili jambo ni zito kuliko tunavyofikiria. Inawezekana ni kweli kwamba viongozi wa serikali walio ndani ya kashfa ya TanEuro Energy ndio walio nyuma ya sakata hili. Na inawezekana vilevile kwamba ni njama za serikali na chama tawala katika kutubana ili tusiwaumbue! Hata hivyo, jambo la kujiuliza hapa, je ni wapi hawa watu walipata picha za tukio la siri kati yetu na CDTPE. Lazima tukumbuke kwamba ile siku hapakua na upigaji picha uliofanyika! Ndugu zangu, lazima CDTPE nao tuwaangalie kwa jicho la tatu! Isije nayo ikawa ni mkono wa serikali na chama tawala ambao waliiunda mahususi ili kuubumoa upinzani kwa mtindo huu!" Dunstan Mkundi aliongea kwa uchungu!

Minong'ono ikaibuka miongoni mwao katika hali iliyoonekana kujadili jambo. Iliwachukuwa takribani nusu saa kujadiliana ili kupata muafaka wa nini hasa cha kufanya! Baada ya muda, Bwana Hassan Muki alisimama na kusema:

"Kama ambavyo wenyewe mlivyoona, nazani kwa sasa hatuna namna ya kufanya. Hakika tumeingia kwenye mtego ambao bado ni kitendawili, kwavile bado hatujafahamu kitanzi chake kimetegeshwa wapi. Hata hivyo, sisi kama wapiganaji hatutakiwi kukata tamaa. Lazima tujipange upya kukabiliana na hujuma hii mpya dhidi ya upinzani. Jambo la msingi kwetu ni kuifanya taarifa hii kuwa siri sana kwavile inaweza kuharibu taswira yetu. Hivyo basi, hatuna budi kuachana na suala la kuibua kashfa hii na badala yake tuanze kufanya uchunguzi wa siri kujua kiini cha hili jambo. Mimi nitaanza na Bwana George Malilo katika kufahamu chanzo cha tukio hili." Alimalizia.

Baada ya hitimisho hili fupi la Bwana Hassan Muki, walijadialiana mambo fulani fulani kisha wakafunga kikao.

“Karibu Wendy, karibu Mashaka!” Alikuwa ni Ngosha akiwakaribisha tayari kwa kupanga mikakati ya kukabiliana na Jonas Siyame. Kikao hiki kilitokana na maagizo ya Michael Mchupi ambapo alimteua Ngosha, mmoja wa vijana wake kuongoza kampeni hiyo!

“Ahsante bosi!” Mashaka aliitikia.

“Ok! Wendy, naomba tusipoteze muda. Bosi Mchupi amenieleza kila kitu kuhusu Jonas ni mtu wa namna gani. Hata hivyo, sio vibaya nami ukinisimulia na endapo kuna lingine lolote limetokea tangu uongee na bosi Mchupi kwa mara ya mwisho!”

“Sawa Ngosha, kama nilivyokueleza kwenye simu ni kwamba nimeshapata uhakika kwamba Jonas ni mfuasi mkubwa wa mambo ya kishirikina. Kila anapohisi kuna kitu ambacho si cha kawaida kimbilio lake huwa kwa mganga wake wa kienyeji. Pamoja na hayo, hivi sasa ameanzisha mtindo wa kunipaka dawa ya usingizi puani pale anapokusudia kuondoka!”

“Kazi nzuri Wendy, sasa kazi iliyobaki ni ndogo tu. Leo mwambie kwamba hutaweza kwenda kulala kwake na utarudi baada ya siku tatu. Siku ya pili baada ya wewe kurejea kwa Jonas, ndio tutakayotumia kumfuatilia ili kujua ni wapi huwa anaenda usiku! Jinsi ya kufanya ni kwamba wewe utaenda kwake na njiwa ambae tutamfunga kikaratasi chenye maandishi ya kiarabu. Njiwa huyu tutamlisha dawa ya usingizi na wewe utaenda kumweka uvunguni mwa kitanda kwa siri. Kwa kiwango

tutakachompulizia, ataweza kuzinduka usiku wa manane. Ni matumaini yangu kwamba, baada ya kuzinduka, humo ndani hamtakalika kutokana na vurugu za huyo njiwa. Sina shaka kwamba baada ya vurugu za njiwa huyo kitakachofuata ni Jonas kwenda kwa mganga wake! Wakati hayo yanafanyika, tayari Mashaka na mwenzake mmoja watakuwa wamejificha kwenye buti ya gari ambayo huwa anaitumia." Alitulia kidogo, kisha akaendelea:

"Tukishagundua kwa mganga ambako huwa anaenda, kazi itakayofuata kwetu ni kumtisha huyo mganga ili afanye kila tutakachomwagiza kufanya.!" Alimalizia.

Glory alikuwa makini kupita kiasi wakati akienda kukutana na George Kamau. Hofu yake ni kwamba hakutaka kwa namna yoyote ile aonekane na Bon Mtambo ambae alimdanganya kwamba anaumwa!

"Pita Glory!" George Kamau alimkaribisha Glory mara baada kumuona akigonga mlango.

" Ahsante George, habari yako!"

"Nipo sawa Glory, bila kupoteza muda ningependa kufahamu endapo hatua za awali za kumweleza Bon Mtambo kwamba unaumwa zimefanikiwa!"

"Bila shaka George, nilimjulisha juu ya jambo hilo leo alfajiri kwa simu na aliahidi kuja kuniangalia jioni hii!"

"Safi sana, sasa huyo mtu wako itabidi aje kukujulia hali Muhimbili. Itabidi ulazwe mchana huu, na tayari tumeshaongea na mtu wetu pale. Huyu mtu anaitwa Dokta Masawe na atakuandikia ripoti itakayoonesha kwamba ugonjwa wako hauwezi kutibika hapa nchini. Aidha, ukiwa

hapo Muhimbili utapatiwa matibabu ya kutuliza tu maumivu na kupatiwa ushauri wa kufanyiwa upasuaji mdogo ndani ya majuma mawili. Yeye atapendekeza hospitali zilizopo India, Ujerumani na Marekani na pia atakutajia majina ya hospitali husika. Hata hivyo, wewe utatumia uwezo wako kumshawishi Bon Mtambo ukatibiwe Chicago nchini Marekani kwavile ni sehemu unayoifahamu. Nazani New York pangekuwa ni mahali muafaka zaidi lakini kwavile ulituambia Bon Mtambo keshawahi kuishi New York basi Chicago ndio sehemu muafaka.”

“Unachotakiwa kukumbuka ni kwamba Mtambo ni ni mtambo kwelikweli; ni mtu hatari na mwerevu kupita kiasi! Chunguza sana nyendo zake, kwani wakati mwingine unaweza kuhisi umeshamteka akili kumbe ni yeye ndie amekuteka. Akishagundua kwamba kuna mchezo unamchezea usitarajie kwamba ataanza kukukwepa, badala yake anaweza kujifanya mjinga zaidi ili agundue kiini cha mchezo wako! Hivyo, kuwa makini sana na huyu mtu.”

# 7

Wengi walizoea kumwita Babu Linjembwa! Ni babu wa kimakonde ambae mtindo wa maisha yake ni wa kushangaza kama sio kuogofya! Pamoja na umri alionao, babu huyu alimudu kuishi peke yake tena sehemu ambayo ilikuwa ni mbali kabisa na wanajamii wenzake. Aliishi huku akifanya kazi zake za kuagua! Aidha, ni hodi toka mlangoni kwake ndiyo ambayo ilimrudisha babu huyu sebuleni baada ya kuwa tayari ameshaenda kulala! Ilikuwa inakaribia usiku wa saa nne, lakini kwa huku anakoishi ilionekana ni usiku mzito! Hata hivyo, hakushangazwa na hodi za muda kama huo kwani ilikuwa ni jambo la kawaida kabisa, hasa baada ya kuanza kufanya kazi na Jonas Siyame ambae aliweza kuja hata usiku wa manane!

Bila kupoteza muda, alijizoazoa na kwenda kufungua mlango.

Hamadi!

Mwanga wa mbalamwezi ulitosha kabisa kumuonesha Babu Linjembwa kisu kikubwa chenye makali pande zote mbili, maarufu kama sime! Alijaribu kurudi ndani, lakini alichelewa kwani kabla hajafanya hivyo Mashaka alimdaka na kuzunguka nae nyuma ya kibanda chake! Masumbuko aliyeongozana na Mashaka nae alifuata na hapo akabaki Nkuba aliyekuwa anaangalia usalama!

“Babu Linjembwa, unamjua huyu mtu?!” Mashaka alimuuliza mara baada ya kumwongoza nyuma kisha akampatia picha ya Jonas Siyame!

“Ndiyo namjua!” Alijibu huku akiwa ametawaliwa na hofu mwili mzima! Hofu yake iliongezeka zaidi pale Masumbuko alipofika huku akiwa amemwelekezea bunduki. Alitamani kukaa, ikashindikana, kuendelea kusimama nako ilielekea kuwa ni kibarua cha ziada kwake!

“Kwanini unafanya nae vitendo vya kishirikina wakati unafahamu ni kinyume cha sheria?!” Masumbuko nae aliuliza kwa ukali ambao ulikosa japo chembe ya masihara ndani yake!

“Tafadhali msiniue, sitarudia tena!” Babu Linjembwa aliomboleza kwa hofu.

“Lazima tukuue usiku huu huu kisha tunakukata vipande vipande na kuvitupa baharini! Hivi unajua ni namna gani huyo mtu wako anavyoharibu maisha ya wenzake kutokana na uchawi wako? Isitoshe tumepata habari kwamba unahusika na mauaji ya albino.” Masumbuko alizidi kutishia katika sauti ile ile isiyo na masihara! Ni dhahiri kwamba Babu huyu hivi sasa alikuwa anasubiria kudra za mwenyezi mungu tu ili zimwokoe!

“Wewe si mchawi uliekubuhu, jigeuze sisimizi basi ili utupotee!” Mashaka aliongea kwa kejeli.

“Jamani mimi si mchawi, ni mganga tu na hata huyo kijana nilikuwa nampa dawa za....!” Kabla hajamalizia hiyo sentensi yake Mashaka alirusha kofi lililomzoazoa Babu Linjembwa hadi chini. Kabla hajainuka, alimwahi kumwinua na kumpiga ngumi nyingine ambayo ilimrudisha chini na kumfanya aanze kulia kwa maumivu! Baada ya kipigo hicho, Mashaka alimbeba Babu Linjembwa

hadi kwenye shamba la mihogo ambako Masumbuko nae alifuata!

"Kaka, hebu nenda kwenye gari kalete ile sepetu kwani huyu mshenzi hana budi kufa kifo cha kinyama! Lazima tumzike angali hai!" Mashaka alimwamrisha Masumbuko, nae akaenda kufuata sepetu na kuchimba shimo la ukubwa wa wastani!

Haja ndogo ikamlowanisha Babu Linjembwa! Hakuwahi hata mara moja maishani mwake kuzani kwamba kifo chake kingekuwa cha kinyama hivi! Alilia hadi machozi yakaelekea kumkauka! Kufumba na kufumbua, Mashaka alimkata ngwala Babu Linjembwa kisha kichwa chake akakiegesha hapo kwenye shimo!

"Tafadhali msinichinje, nitawapa kitu chochote mkitakacho!" Babu Linjembwa alipiga kelele baada ya kumsikia Mashaka akiitisha jambia toka kwa Masumbuko!

"Bosi, hebu mwache kwanza huyo mzee! Mimi natoa wazo tumuhurumie lakini lazima atufanyie kazi yetu!" Masumbuko alitoa wazo wakati Mashaka alipoanza kuelekeza jambia lake kwenye shingo ya babu Linjembwa! Mashaka alisitisha zoezi, na kuinua kichwa chake na kumwangalia Masumbuko.

"Mbona sikuelewi?! Yaani unataka tumsamehe huyu mwanaharamu?! Hapana, huyu lazima alipie madhambi yake kwa mateso kama hivi!" Mashaka alijifanya kumshangaa Masumbuko huku akianza kulekeza tena jambia lake shingoni kwa Babu Linjembwa!

"Sikiliza Bosi, tumwache kwa masharti!"

"Hapana, kwanza endelea kuchimba hili shimo, urefu wa kwenda chini uwe sawa na kimo chake huyu shetani!" Mashaka alimwamrisha Masumbuko.

“Bosi tu....!” Masumbuko alijaribu kuongea kitu lakini kabla hajamalizia hicho alichotaka alipigwa kibao na Mashaka na hivyo kumfanya aanze tena kuchimba shimo. Hali hii moja kwa kwa moja ikamkatisha tamaa Babu Linjembwa!

“Haya ingia humo shimoni!” Mashaka alimwamrisha Babu Linjembwa mara baada ya Masumbuko kumaliza kuchimba shimo.

“Tafadhali msi...!” Babu Linjembwa alijaribu kujitetea lakini kabla hajamalizia sentensi yake alipigwa ngwala iliyomtupa moja kwa moja shimoni! Baada ya kudondokea humo shimoni, Mashaka alipokonya sepetu iliyokua mikononi mwa Masumbuko kisha akaanza kufukia shimo!

Ni kukosa uwezo wa kujitetea ndiko kunakomfanya binadamu asujudu na kukubali afe akiwa amekaa, au amelala! Babu Linjembwa bado alikuwa na afya kamilifu, hivyo hakukubali kufa akiwa amekaa humo shimoni. Alisimama na kujaribu kutoka lakini alibabatizwa kichwani kwa teke zito hivyo kumfanya ashindwe kutoka. Tamaa ya kunusurika ikayoyoma! Akaanza kuyarejea matukio yote aliyoyafanya na Jonas ambayo aliamini ndiyo yaliyomfikisha hapa. Awali, hata yeye Babu Linjembwa alikuwa akimshangaa jinsi ambavyo Jonas alivyohususdu vitendo vya kishirikina licha ya kuwa ni kijana msomi!

Kufumba na kufumbua Babu Linjembwa alijikuta mwili mzima umefukiwa hadi shingoni huku Mashaka akionesha dalili zote za kutaka kumfukia mzimamzima. Wakati akiendelea kufukia, ghafla Masumbuko alipokonya sepetu!

“Bosi, msamehe endapo atakubali kufanya ile kazi yetu!” Masumbuko alimwambia Mashaka kwa sauti ya

kubembeleza. Katika hali ya uigizaji wa hali ya juu, Mashaka alijifanya kumkata jicho Masumbuko!

“Sikiliza, ile kazi itafanywa na yule mbwa mwingine, na sio huyu shetani!” Mashaka alijifanya kutia ngumu.

“Hapana, atufanyie huyuhuyu!” Masumbuko alijifanya kusisitiza.

“Babu, wewe unaitwa nani?” Hatimae Mashaka aliuliza kwa upole!

“Naitwa Babu Linjembwa!”

“Ni mtu wa wapi wewe?”

“Newala!”

“Unaona sasa bosi, kumbe ni mtu wa kwenu!” Masumbuko aliingilia kati ingawaje hapa ilikuwa ni uigizaji mtupu kwani Mashaka yeye ni mwenyeji wa Morogoro!

“Sasa sikiliza Babu, nakuacha hai  kutokana na sababu kubwa mbili; kwanza ni kwavile ni mtu wa nyumbani na pili nitakuacha kwa sharti kwamba utakuwa tayari kufanya vile tutakavyokuagiza, sawa babu?” Mashaka aliongea kwa upole.

Babu Linjembwa hakuamini! Ingawaje alishaanza kupoteza nguvu lakini ghafla alirejewa na nguvu baada ya kupata matumaini ya kuendelea kuvuta pumzi!

“Nipo tayari kufanya chochote wajukuu wangu hata ikibidi kumuua!”

“Haina haja ya kumuua!”

“Nifanye nini sasa!?”Babu Linjembwa aliuliza kwa sauti ya upole.

“Je, ameshawahi kukuambia kwamba hivi sasa huwa analala na mwanamke ndani kwake?” Mashaka aliuliza.

“Hapana, kwanza Jonas anaogopa sana wanawake” Babu Linjembwa alijibu.

“Sasa sikiliza Babu Linjembwa,” Mashaka alianza kutoa maelekezo kisha akaendelea: “Kwanza itabidi wewe hivi sasa ukavae kwa namna ya kutaka kuagua na utachukua baadhi ya vifaa vyako vichache. Baada ya hapo tutaondoka usiku huu huu hadi kwa Jonas, tutakufungulia mlango wa nyumba yake na wewe utaenda hadi chumbani kwake. Hata hivyo, utajifanya umeingia humo ndani kiuchawi! Huko utamweleza kwamba mizimu imekasirishwa baada ya kugundua anafanya uchafu kwa kulala na mwanamke ndani bila ya ndoa. Utamwambia kwamba, leo leo itabidi atakaswe vinginevyo, yeye na huyo mwanamke wake watakufa baada ya muda mfupi. Utamweleza haya yote ukiwa katika hali ya kama umepandisha mashetani. Aidha, mwanamke utakayemkuta amelala nae utamwamrisha kwa ishara akalale kwenye kona moja ya chumba!” Alitulia kidogo na kumwangalia Babu Linjembwa, na alipoona anamsikiliza kwa makini aliendelea: “Utamweleza Jonas kwamba anatakiwa kutakaswa kwa kufanya mapenzi na mabinti wadogo ambao bado si wachafu! Na kwavile amelala na huyo mwanamke kwa siku tatu, basi itabidi afanye mapenzi na mabinti watatu! Na hayo mapenzi itabidi wafanyie kule nyuma ya nyumba yako na atakuwa anafanya mapenzi na binti mmoja mmoja! Bila shaka umenielewa!”Alimalizia Mashaka na kumwacha Babu Linjembwa akionekana kuwa na mambo ya kutaka kufahamu zaidi!

“Kiasi nimekuelewa kiasi sijakuelewa!”

“Ni wapi ambapo hujaelewa?”

“Kuna mengi sijaelewa, lakini nataka kwanza nifahamu ni wapi nitawatoa hao mabinti ghafla namna

hii!” Mashaka alitarajia swali hili, aliacha makusudi kueleza hapo awali ili afahamu endapo Babu Linjembwa alikuwa makini kumsikiliza.

“Sisi tayari tunao mabinti watatu. Utakachofanya baada ya kufika na Jonas hapa kwako, utajifanya unapiga manyanga kama dakika tano ya kumuita mtu kimiujiza. Baada ya kupita hizo dakika tano, utapiga filimbi kwa sauti ya kiasi. Baada ya wewe kupiga filimbi, subiria tu matokeo yake nawe utayaona. Jambo la msingi ni kwamba, mwambie kwa binti wa kwanza na wa pili asifike kileleni kwavile mizimu itakasirika. Akitaka kufika kileleni, afanye hivyo kwa binti wa tatu! Aidha, kwa kila binti wa kwanza na wa pili asitumie zaidi ya dakika tano. Ukiona ameshamaliza angalau dakika tano, utawasimamisha na kumruhusu binti huyo kuondoka kisha utaanza tena kupiga manyanga na kufanya kama ulivyofanya kwa huyu wa kwanza!” Alimalizia Mashaka na kumwuliza Babu Linjembwa kama alikuwa na swali lingine.

“Ndio ninalo, tutaenda vipi na kurudi vipi huko mjini hata tuweze kufanya mambo yote hayo kabla hakujapambazuka?”

“Wakati wa kwenda tutaenda na gari letu. Wakati wa kurudi, utamwuliza Jonas endapo atataka mrudi na ungo au kwa usafiri wa kawaida! Kwa vyovyote hatakubali kurudi na ungo na bila shaka atataka mrudi kwa usafiri wake. Sisi tutajua tutarudi vipi, kwani lazima tuwachunge kuanzia mwanzo hadi mwisho, na ninakuhakikishia,ukileta ujanja wowote tunawamiminia risasi hapo hapo!”

“Usiwe na wasiwasi babu, nitafanya kama mnavyotaka!” Babu Linjembwa aliongea kwa unyenyekevu.

Baada ya kutoa maelekezo mabalimbali, walirudi pale nyumbani kisha wakafunga kamera za siri karibu tatu hivi kwenye mti uliokuwa hapo nyumbani! Baada ya hapo walichukua kifaa cha kunasa na kurusha sauti na kumwamlisha babu Linjembwa akifiche sehemu yoyote mwilini mwake.

"Babu nakuonya, hicho kifaa ni hatari sana kwahiyo hapo utakapokiweka usiwe unakigusagusa! Aidha, ukileta ujanja tu, hicho kifaa kitajilipua chenyewe na kukuteketeza!" Mashaka alimtisha Babu Linjembwa kisha wakafunga safari ya kwenda kwa Jonas.

"Jambo la mwisho ni kwamba, Jonas akishamaliza kufanya mapenzi na binti wa tatu utamwambia aondoke mara moja na asigeuke nyuma hadi anafika nyumbani kwake!" Mashaka alihitimisha maelezo yake alipoona wamekaribia nyumbani kw Jonas.

Bon Mtambo na Glory walikuwa wanakata kwenye mitaa ya jiji la Chicago baada ya Glory kupata nafuu ya *operesheni* yake ya uongo na kweli!

"Sikufikiria endapo Chicago ni jiji kubwa na zuri namna hii!" Bon Mtambo alimweleza mpenzi wakati wanatoka Woodfield Shopping Malls walikoenda kununua bidhaa mbalimbali ikiwa ni maandalizi ya kurudi Tanzania.

"Kumbe ulivyokuwa unakataa kuja na mimi ungeliona saa ngapi?" Glory alimsuta mwenzake.

"Sio kukataa Glory, unajua safari yenyewe ilikuwa ya ghafla mno!"

"Ghafla vipi wakati haikuwa safari ya matembezi? Au ulitaka nife ndipo ufurahi sio."

“Si hivyo mpenzi, unajua nilikuwa bado siamini kwamba ugonjwa wako usingeweza kutibika sehemu yoyote Afrika Mashariki. Niliona kuja mbali kote huku ni kutowaamini wataalamu wetu, na mbaya zaidi ni matumizi mabaya ya pesa!” Bon Mtambo alijitetea.

“Wewe ndie unaelekea kutowaamini wataalamu wetu kwavile yule aliyetoa ushauri wa mimi kuja huku ni mtaalamu wa Kitanzania. Kwavile yeye ni daktari, anafahamu magonjwa ambayo wao wanatibu kwa ufanisi na magonjwa ambayo hawayawezi. Kuna baadhi ya magonjwa yanakuwa hayapatikani kwenye baadhi ya nchi, hivyo nao inakuwa sio rahisi kuwa na utaalamu nayo. Aidha suala la pesa nalo si jambo la msingi katika hili kwavile nilishakuambia nina akiba ya kutosha.”

“Samahani mpenzi wangu kama nilikuudhi!” Bon Mtambo alijitetea, na mara simu yake ya mkononi ilianza kuita walipokaribia kwenye kona ya independence. Aliichukuwa na kuiweka sikioni, lakini kabla hajaongea chochote, ghafla simu yake ilikwapuliwa na kijana mmoja mwenye asili ya kiafrika. Alijaribu kumkimbiza, lakini alishachelewa kwani yule kijana alishapotelea mtaa mwingine! Hata kelele za kuomba msaada kutoka kwa Glory nazo, hazikuwa na msaada wowote!

“Siamini, yaani hata Marekani nako kuna vibaka wa simu za mkononi!?” Bon Mtambo alilalamika.

“Hilo ndilo tatizo la Chicago Bon! Unajua huu mji unakaliwa na weusi wengi sana, na wengi wao ni maskini kwa kiwango cha maisha ya hapa Marekani. Kutokana na hilo, uhalifu umekuwa mwingi sana hapa Chicago! Nami naona ishakuwa nuksi, twende tuchukue taksi itufikishe hotelini.” Glory alieleza kisha wakachukuwa taksi kuwarudisha walikofikia.

“Unafikiri ni wapi naweza kupata simu nyingine nzuri lakini kwa bei nafuu!” Bon Mtambo aliuliza mara walipofika hotelini walikofikia. Hilo ndio haswa lililokuwa linalosubiriwa na Glory! Na ndio chanzo cha safari nzima toka Dar es salaam hadi Marekani!

“Ondoa hofu mpenzi, ina maana umeshasahau kwamba upo Marekani?” Glory aliongea kwa utani kidogo kisha akaendelea: “Wacha tupumzike kidogo kisha tutaenda madukani.”

“Hapana Glory, kama kuna uwezekano twende sasa hivi. Shughuli zangu haziniruhusu kukaaa bila ya simu japo kwa dakika moja. Hivyo nahitaji kupata simu nyingine mapema iwezekanavyo.”

“Mapenzi yako yatimie mpenzi, haya twende.” Glory alikubali kisha wakatoka na kupita mitaa miwili mitatu kisha wakatokeza kwenye duka moja. Simu nyingi kwenye duka hili zilikuwa zinauzwa kwa bei ya juu sana. Hata hivyo, kulikuwa na aina nyingine ya Panasonic za kisasa kabisa ambazo zilikuwa zinauzwa dola mia nane!

*“ I guess this type will fit your needs, because besides of being very cheap, it's of a new model as well!”(*Nazani aina hii itakufaa kwani licha ya kwamba bei yake ni nafuu lakini vilevile ni ya kisasa zaidi!) Muuza duka aliongea na kumkabidhi simu Glory, nae aliiangalia kisha akampatia Bon Mtambo ambae moja kwa moja alionekana kuvutiwa sana na simu hiyo! Kabla Bon Mtambo hajaongea lolote, Glory alichukuwa kadi yake ya malipo (Debit Card) na kulipia hiyo simu.

“Ni matumaini yangu umeipenda hiyo simu!” Glory alimtupia swali Bon Mtambo.

“Nimeipenda sana mpenzi!”

Baada ya kufanya malipo na kupata kadi nyingine ya simu (*sim card*) walirejea hotelini.

“Ahsante sana mpenzi kwa kuninunulia simu ya gharama kama hii!”

“Usijali mpenzi, Bon ni Glory na Glory ni Bon kwahiyo ni kama nimejinunulia mwenyewe tu!” Glory aliongea kwa maringo kidogo.

Waliongea mambo ya kimapenzi huku wakiendelea kujifunza kuitumia hiyo simu na baada ya kama robo saa hivi Bon Mtambo alielekea maliwatoni!

“Mtambo kwenye simu, je ni wewe ambae ulinipigia simu kiasi cha nusu saa iliyopita?” Bon alimuuliza mmoja wa wafanyakazi wenzake maalumu!

“Hapana bosi, sio mimi; kwani imekuwaje?” Huyo mtu alihoji.

“Hamna kitu isipokuwa kuna mtu alinipigia lakini kabla sijaipokea nikaporwa simu kwahiyo sikuwahi kufahamu mtu ambae alinipigia!”

Hata baada ya kuwapigia watu wengine kuwauliza endapo walimpigia, wote hao walikana!

Bon Mtambo akashangaa!

Jonas aligutuka toka usingizini baada ya kuhisi kuchapwa na kitu mithili ya fagio laini! Alitaka kupiga kelele, lakini alipewa ishara ya kutulia kisha akaashiriwa atoke kitandani na kusimama! Alijizoazoa hapo kitandani huku akiwa amekumbwa na hofu isiyo kifani! Isingekuwa ni muda mfupi tu uliopita kwamba alienda kujisaidia haja ndogo, basi huenda tungesema mengine hivi sasa!

“Hebu simama hapo pembeni!” Sauti kali ya Babu Linjembwa ilijipenyeza masikioni mwa Jonas. Tangu afahamiane na babu huyu, hajawahi kumshuhudia akiongea kwa ukali kiasi hicho kwake! Alizoea kumuona akiwa ni mnyenyekevu mno kwake, na si unyenyekevu wa mteja ni mfalme pekee, bali pia ni unyeyekevu dhidi ya mtu mwenye madaraka!

Akiwa bado mwenye hofu, Jonas alisogea pembeni huku akiangalia kitandani kuona kama Wendy anashuhudia haya yanayotokea! Ilikuwa ni heri kufa, kuliko msichana huyu kufahamu aibu hii! Hata hivyo, Wendy alikuwa ndo kwanza anaendelea kuvuta shuka huku akikoroma ingawaje ukweli ni kwamba kila kitu alikuwa akikishuhudia kwa jicho la pembeni!

Mwanga hafifu wa rangi ya kibluu humo chumbani ulitosha kabisa kumuonesha babu Linjembwa vile alivyokuwa amefura kwa ghadhabu! Akiwa hivyohivyo amekasirika, alienda karibu na kitanda na kumchapa Wendy kama alivyofanya kwa Jonas! Wendy alikurupuka na kutaka kupiga ukelele lakini akaonywa kutofanya hivyo! Aliamriwa kutoka hapo kitandani na kupewa ishara ya kwenda kwenye pembe moja ya hicho chumba! Bila kukaidi, alitoka na kwenda kwenye hiyo pembe kisha akajilaza huku akiwa amejikunja mithili ya kambale! Hazikupita hata sekunde tano, Wendy alianza kukoroma kama ishara ya kuelemewa na usingizi hapo hapo chini!

Jonas Siyame akaduwaa!

“Ni nani huyu?” Babu Linjembwa aliuliza kwa sauti ya chini lakini iliyoonesha kubeba ghadhabu za wazi!

Jonas Siyame hakujibu!

“Nimekuuliza ni nani huyu uliyekuwa unafanya nae uchafu?” Aliuliza tena kwa ukali.

“M..m...mpenzi wangu!”

“Umefunga nae ndoa?”

“Hapana!”

“Una habari umeniletea matatizo makubwa sana we kijana! Kwa taarifa yako, mizimu imechukizwa sana na suala la wewe kulala na malaya ndani bila kufuata taratibu. Na si ajabu jua la kesho mkashindwa kuliona wewe na huyo malaya wako!” Babu Linjembwa alifoka.

“Hapana babu, niombee kwa mizimu wanisamehe. Sitarudia tena nami nipo tayari kutoa chochote kwao ili wanisamehe! Tafadhali ba....!” Jonas hakumaliza maombi yake, kufumba na kufumbua Babu Linjembwa alikula mwereka hadi chini na kuanza kuhema! Kwa mtu mwingine, angetoka mbio lakini kwa Jonas alijua nini kinaendelea!

Maruhani!

Babu Linjembwa alikuwa amepandisha mashetani! Akaanza kupiga kelele, ingawaje si za kuweza kutoka nje! Jonas, alikuwa ameshazoea mambo haya! Akamsogelea na kuuliza matakwa ya maruhani!

“Wewe ni nani?!” Jonas aliyauliza maruhani ya Babu Linjembwa huku akiwa ametawaliwa na uoga!

“Mimi iko Sheikh Kareem toka Muscat!” Babu Linjembwa alijibu kimaruahani!

“Unataka nini Sheikh?”

“Takasa hiyo chafu! Takasa hiyo chafu! Takasa hiyo kijanaaaaaa! Kama hapana takasa leo leo nakufa yeye na bibi yake leo leo!” Babu Linjembwa alijibu huku akionekana kama asiejitambua! Hata hivyo, kwa wale wanaoamini mambo haya, ni kwamba aliyekua anajibu si babu Linjembwa mwenyewe, bali ni maruhani yake!

“Atakase na nini?” Jonas alimuuliza ruhani!

“Na binti tatu isiyo chafu! Ni binti safi ambayo ni dogodogo!” Babu Linjembwa akijifanya bado amepandwa na maruhani alijibu na ghafla aliend kujipigiza ukutani!

“Naomba maji!” Hatimae babu Linjembwa alimwambia Jonas baada ya kujiondoa hapo ukutani na bila kupoteza muda Jonas alifuata maagizo. Baada ya kunywa maji, Jonas alisimulia yote yaliyotokea wakati babu Linjembwa alipokuwa amepandwa na maruhani!

“Haya tuondoke haraka kabla hakujapambazuka!” Babu Linjembwa alimweleza Jonas mara baada ya kupewa maelezo kuhusu maruhani ambayo alipandisha.

“Kwa jinsi hali ilivyo inabidi tuwe pamoja hadi tunafika asije yule sheikh akakuibukia ukiwa peke yako! Je, umeshawahi kusafiri kwa ungo?” Babu Linjembwa alimuuliza Jonas! Jonas hakutarajia kuulizwa suala la kusafiri kwa ungo hali iliyomfanya atoe macho mithili ya mjusi aliyebanwa kwa mlango!

*“Kusafiri na ungo, hapana! Sijafikia kiwango hicho cha ushirikina, na isitoshe mimi sio mchawi ila ninachofanya ni kutafuta kinga!”* Jonas aliwaza huku akionekana kuwa na hofu ya kulazimishwa kusafiri kwa ungo! Akaanza kuzikumbuka simulizi kadhaa kuhusu wachawi kutunguliwa na nyungo zao kiasi cha kukutwa na raia wema asubuhi!

“Hapana babu, naomba tutumie gari yangu!” Jonas aliongea kwa hofu. Na bila kupoteza muda, waliingia garini na kiasi cha nusu saa baadae walikuwa wameshafika nyumbani kwa babu Linjembwa!

Kwa kufuata maelekezo ya Mashaka, Babu Linjembwa alianza kupiga manyanga kwa takribani dakika tano, kisha akapiga filimbi! Muda wote huo, Jonas alikuwa kawekwa chini huku akiwa amenyoosha miguu mbele!

Kufumba na kufumbua, binti mmoja wa makamo alitokeza toka kwenye shamba la mihogo huku akiwa amevaa sare za shule ya msingi! Alikuja moja kwa moja na kusimama mbele ya Jonas, huku akionesha dhahiri kwamba hajitambui! Akiwa katika hali hiyohiyo ya kutojitambua, alipandisha sketi yake juu na kulala chali! Ndani hakuwa amejisitiri kwa chochote!

Macho yalimtoka Jonas Siyame kiasi cha kutamani kutimua mbio!Alihisi kijasho chembamba kikimtoka huku akiwa hafahamu endapo yupo ndotoni au la!

"Hebu jitakase haraka!" Babu Linjembwa aliongea kwa ukali huku yule binti akiwa bado amelala. Ajabu ni kwamba alikuwa anakoroma kwa usingizi!

"Nijitakase vipi babu?" Jonas aliuliza, ingawaje tayari alishahisi ni nini hasa alichotakiwa kufanya!

"Wacha maswali ya kitoto, hebu lala na huyo binti! Fanya nae ulichokuwa unafanya na yule malaya wako lakini usifike kileleni!" Babu Linjembwa alifoka!

Huku akiwa amegubikwa na soni iliyoambatana na hofu, Jonas alifanya alichoamrishwa!

Haidhuru kwamba hakupata ushirikiano toka kwa hao mabinti wakati wa zoezi hilo la faragha! Hata hivyo, kiasi cha nusu saa baadae alikuwa amemaliza *kujitakasa* kwa mabinti wote watatu, kisha akaruhusiwa kwenda nyumbani bila kuangalia nyuma!

Njia nzima kuelekea nyumbani, Jonas alikuwa anawazia tukio lile! Aidha alistaajabishwa sana na uwezo wa Babu Linjembwa hususani tukio la kupiga manyanga na kutokea wasichana watatu wadogo, huku kila mmoja akitokea upande wake! Ingawaje hakufurahishwa na tukio lile, lakini vile vile alistaajabu wale mabinti walivyoweza kumudu wakati walionekana ni watoto wadogo tu!

“*Bila shaka watakuwa ni watoto toka ujinini wale*!” Jonas alijiambia huku akihisi kusisimkwa mwili kama ukweli wenyewe ndio huo!

Alipofika nyumbani, alimkuta Wendy amelala kitandani tofauti na alipomwacha! Hata hivyo, Jonas bado alikuwa na hofu ya huenda Wendy amegundua yale yaliyokuwa yametokea!

Alikosa raha!

Dakika tano tangu Jonas aondoke kwa Babu Linjembwa, Mashaka na mwenzake walijitokeza!

“Kazi nzuri babu!” Mashaka aliongea na kutoa kibunda cha pesa na kumpatia Babu Linjembwa!

“Hizi pesa ni ahsante yako, sisi tumeshamaliza kazi yetu! Lakini kumbuka kwamba hii inapaswa kuwa siri, kwani Jonas akigundua kwamba umemsaliti anaweza hata kukuua! Sisi hatuna shida nae tena na wewe tunakuacha huru!” Mashaka aliendelea kueleza kisha akaenda kwenye mti na kufungua vifaa vyake ambavyo alivitegesha kisha wakaondoka na kurudi walikoacha gari yao.

“Watoto wazuri mmefanya kazi nzuri sana kwani mmefanya kama tulivyowaelekeza! Lakini kumbukeni kwamba siri hii hamtakiwi kuitoa kwa mtu yeyote na mkifanya hivyo tunawaua mara moja! Kila mtu tutampatia shilingi laki tano kwahiyo naamini zitawatosha kuanzishia biashara ndogondogo na kuacha maisha yenu ya uchokoraa.” Mashaka aliwaeleza wale mabinti ambao alikuwa amewachukuwa kwenye dangulo moja maeneo ya Buguruni! Aliwafundisha kufanya walivyofanya na baada

ya kuwapa malipo yao aliwarudisha Buguruni na wao wakaendelea na hamsini zao.

# 8

Bon Mtambo na Glory waliwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es salaam majira ya saa kumi na moja kasorobo alfajiri. Wa kwanza kukaguliwa alikuwa ni Glory ambae baada ya kukamilisha taratibu alitoka nje kumsubiria mwenzake. Baada ya Bon Mtambo nae kukagauliwa, alielekea nje lakini kabla hajafika kwenye lango kuu, mwanamke mmoja alipita karibu yake na kumfanyia ishara fulani!

Bon Mtambo alielewa ishara hii!

Hamna yeyote mwingine ambae angeelewa hata kama angeona ishara hiyo! Ni ishara iliyomsisimua mwili na akili pia! Ni ishara ya kazi, na mara nyingi, kama sio zote, ni kazi ya hatari na ya kifo kiganjani!

Bila kupoteza muda, Bon Mtambo alimfuata kwa nyuma yule dada na kiasi cha kama hatua kumi kutoka hapo alikutana na mtu mwingine ambae alimfahamu kutokana na ishara zao! Alipomfikia, hawakuongea chochote zaidi ya huyo mtu kumpatia Bon Mtambo *brief case* na mfuko mdogo wa plastiki. Ndani ya mfuko alikuta hati ya kusafiria yenye jina la Joseph Kimathi, raia wa Kenya lakini ikiwa na picha yake! Mbali na hati, vilevile

kulikuwa na tiketi ya ndege kutoka Dar es salaam kwenda Geneva, nchini Uswisi na ndege ya saa kumi na moja alfajiri ya siku hiyohiyo! Kwa maana nyingine ni kwamba hakutakiwa hata kutoka nje ya uwanja, na badala yake alitakiwa kugeuzia hapo hapo! Aidha, hiyo ilimaanisha asingeweza hata kuonana na Glory kabla ya kuondoka!

Mwili ukiwa unamsisimka, alitaka kuchukua simu lakini akagundua mfuko wenye simu anao Glory!

"Tafadhali nipe simu yako mara moja!"Bon Mtambo alimweleza huyo mtu aliyekuwa nae.

"Lakini fanya haraka kwavile muda si mrefu ndege itaruka!" Huyo mtu alisema na kumpatia Bon Mtambo simu.

Bon Mtambo alichukua simu na kupiga namba za Glory!

"Bon hapa!" Bon Mtambo aliongea kwa sauti ya kitetemeshi mara baada ya Glory kupokea simu!

"Una nini Bon? Mbona unachelewa huko ndani?!" Glory alilalamika.

"Nisikilize kwa makini Glory, hivyo vitu vyangu kaviache nyumbani kwangu kisha utafunga mlango na kudondoshea funguo ndani. Mimi nipo mikononi mwa polisi, napelekwa kituoni, lakini usihofu nitaachiwa tu!"

"Mbona sikue.....!" Glory alitaka kuhoji, lakini kabla hajamalizia sentensi yake tayari Bon Mtambo alishakata simu na bila kupoteza muda aliwahi ndege tayari kuelekea Geneva!

Ingawaje Bwana Hassan Muki na wenzake walichukizwa na utaratibu wa wao kupekuliwa kila

sehemu lakini bado walijikuta wakilazimka kuwa wapole! Hata hivyo, Dunstan Mkundi alikata shauri kwamba asingekaa kimya kutokana na jambo hili ambalo aliliona ni kama udhalilishaji. Waliingia ukumbini na kumkuta tayari Bwana George Malilo wa CDTPE akiwasubiri.

“Karibuni wapiganaji wenzetu,” George Malilo alianza kuongea kisha akaendelea, “awali ya yote ningependa kutumia fursa hii kuwataka radhi kwa usumbufu mlioupata hapo mlangoni. Hata hivyo, hatukuwa na namna nyingine kutokana na hali iliyojitokeza hapa ofisini! Inaweza ikaonekana ni kama kitendo cha udhalilishaji lakini ningependa tu kuwaambia kwamba hivi sasa tupo kwenye matatizo makubwa dhidi ya serikali! Ni matatizo hayo ndiyo yaliyotusukuma sisi watu wa CDTPE kuwaita nyinyi kwavile ni matumaini yetu kwamba ama ninyi wote, au angalau mmoja wenu atakuwa anafahamu chanzo cha tatizo hili! Ndugu zangu, nyie nyote mnakumbuka jinsi ambavyo tulikubaliana suala la kuufanya mkataba ule kuwa ni siri. Nyinyi ni watu wazima, nasi ni watu wazima hivyo tuliridhika kwamba tulielewana! Hata hivyo, CDTPE imeshangazwa kwamba habari zile zimevuja na kufika kwenye mikono ya watawala! Hapa ninaposema kila siku tumekuwa tukitumiwa vitisho kwamba taasisi yetu itafungiwa endapo itathibitika kwamba tumewasaidia nyinyi kinyume na utaratibu. Na wamesema wanazo picha za video za tukio zima, na wanachofanya hivi sasa ni kuzichunguza kama ni za kweli kabla hatua kali hazijachukuliwa dhidi yetu. Kila siku imekuwa ikisemwa kwamba vyama vya upinzani havikomai kwavile miongoni mwenu kuna vibaraka wa chama tawala. Siku za nyuma nilihisi ni propaganda za kisiasa lakini kutokana na tukio hili, hatimae nimeamini!

Hivyo basi, ningependa tufahamishane ni nani miongoni mwenu aliyevujisha taarifa hizi na tuangalie ni namna gani tunaweza kukabiliana na hali hii kwa siku zijazo. Hili jambo ni zito sana kwavile linaweza kuleta hata mgogoro wa kidiplomasia kati ya nchi yetu na nchi marafiki wanaowasaidia nyinyi kupitia CDTPE! Aidha, hili ni bomu linalopaswa kuzimwa kwa gharama yoyote ile kabla halijalipuka! Hivyo basi, ningependa kupata ushirikiano kutoka kwenu kabla hatujaendelea na mkakati mwingine! Na labda kwa kumalizia, ndio maana leo mlivyoingia, ilibidi kwanza mkaguliwe ili kuhakikisha hakuna mtu atakayeingia na kifaa chochote chenye uwezo wa kurusha mawasiliano au kupiga picha." George Malilo alimaka na kuwaacha viongozi wa DRFA midomo wazi! Hakika walikuwa na kila sababu za kubaki midomo wazi! Baada ya wao kukutwa na lile sakata la kulazimishwa kutoibua kashfa za TanPurity walishaanza kuwa na wasiwasi na CDTPE. Baada ya sakata hilo, DRFA walikutana kujadili kwa kina suala hilo na wao wote walikubaliana kwamba lazima CDTPE walihusika katika suala hilo na waliamini ni wao ndio walipiga picha za siri. Hata hivyo, jambo ambalo walishindwa kupata jibu ni uhusiano uliopo kati ya CDTPE na TanPurity!

" Kwanini Bwana Malilo unaonesha ni kama umeshapata uhakika wa unachokisema wakati hata watu wenu wanaweza kufanya jambo hilo?! Sisi tutavujishaje taarifa ambazo tunajua zitaharibu taswira yetu kwa jamii?" Hatimae, Dunstan Mkundi aliuliza ghafla katika hali ambayo haikutarajiwa na yeyote miongoni mwao!

"Unamaanisha nini kijana?" George Malilo aliuliza huku akiwa ameyakaza macho yake kwa Mkundi!

Ingawaje alijitahidi kutojionesha lakini ukweli ni kwamba alichukizwa na swali hilo!

"Maana yangu ni kwamba taarifa hizi zinaweza kuvujishwa hata na miongoni mwa watu wa CDTPE. Wakati nyinyi mnadai mmetishiwa, sisi DRFA na watanzania kwa ujumla, tayari tumeshaathirika na suala hili. Ni hivi majuzi tu mwenyekiti wetu alitekwa nyara na watu wasiojulikana na kulazimishwa kutoibua bungeni kashfa ya TanPurity vinginevyo wangeitoa hadharani kashfa ya sisi kupokea misaada ya siri kutoka kwenu! Ajabu zaidi ni kwamba, watu hao wametuonesha picha za video za tukio zima! Sasa, ni nani basi kati yetu na nyinyi wanaoonekana kuwa katika nafasi kubwa ya kuvujisha taarifa hizi? Nyinyi mnafanya kazi kwa niaba ya taasisi za kisiasa, sisi tunafanya kazi kwa niaba ya wananchi! Sasa itakuwaje tuvujishe taarifa zitakazotoa taswira mbaya dhidi yetu kwa wananchi?" Dunstan Mkundi, alifafanua na kuwaacha wenzake midomo wazi! Hakuna hata mmoja miongoni mwao alietarajia kwamba angetoa msimamo huo kwa sasa! Hata wao wenyewe hawakuwa tayari kuongea waziwazi kwa kile walichokubaliana kwamba bado hawajapata ushahidi wa kutosha! Isitoshe, mamilioni waliyokabidhiwa ni kama tayari yalishawafunga mdomo!

"Mbona hamjatupa taarifa hizo mapema?" George Malilo aliuliza lakini akiwa amepooza kidogo!

"Isingekuwa rahisi kuanza kuwaambia wakati tayari tulishaanza kuwa na mashaka na.....!" Dunstan Mkundi alianza tena kueleza, lakini kabla hajaendelea, Bwana Bwana Hassan Muki aliingilia kati:

"Sikiliza Bwana Malilo, hili suala limeshaibua mkanganyiko kwa upande wetu na kwenu pia! Hivyo basi, badala ya kuanza kutuhumiana nazani jambo la busara ni

sisi kushirikiana ili kubaini ni nani hasa yupo nyuma ya jambo hili. Sisi tujichunguze, na nyinyi mjichunguze!"

"Ina maana na wewe Bwana Muki una wasiwasi na sisi?" George Malilo aliuliza kwa utulivu.

"Sina wasiwasi, ninachosema ni kwamba lazima tuchunguze nje na ndani. Tunapochunguza ndani, ni lazima tujichunguze wote tuliohusika, kwa maana ya DRFA na CDTPE!"

"Nimewaelewa, nitaufanyia kazi ushauri wenu kwani hata nami sasa nimeshaanza kupata mashaka kwavile ni kweli mchawi anaweza pia akatoka ndani ya CDTPE, ingawaje swali ni kwa manufaa ya nani!" George Malilo alianza kueleza kwa unyenyekevu wa hali ya juu, kisha akaendelea: "Pamoja na yote hayo, CDTPE imekuja na mkakati mwingine, ambao tunaamini endapo mtaufanya vizuri basi sina shaka yoyote kwamba kwenye uchaguzi ujao mnaweza kuwa na viti visivyopungua mia moja bungeni! Nazani hatuwezi kutetereshwa na wahujumu hawa wachache wasiotaka kuona watanzania wananasuka toka kwenye minyororo ya dhuluma! Katika hili lazima tukumbuke kwamba siasa ni ujasiliamali. Mjasiliamali ni yule anayegendua mapema mahali kuna tatizo na yeye akafanya jambo la kutatua tatizo lile huku akitengeneza *noti*! Hivyo basi, CDTPE imeandaa mkakati wa kuwasaidia nyinyi kujipenyeza ndani kabisa kwenye mikoa ile inayoonekana kusahaulika kimaendeleo. Mkakati huu utawawezesha nyinyi kujiimarisha kisiasa kwenye mikoa ya Lindi, Mtwara, Rukwa, Kigoma, Singida, Tabora, na Manyara. Mkakati uliopo ni kwamba itabidi kwanza muanzishe mfuko wa DRFA, yaani *DRFA Trust Fund* kisha mtaandika mchanganuo wa kuomba fedha ndani na nje. Sisi tutawaunganisha na baadhi ya mashirika ya misaada

yaliyopo nje ya nchi ambayo tutahakikisha baadhi ya misaada yao haitakuwa ya siri. Lengo hapa ni kwamba wasije watu wakaanza kuwa na mashaka ni wapi mnakopata pesa za kuendeshea DRFA Trust Fund. Hiyo DRFA Trust Fund mtaianzisha kwenye kila kata ya mikoa niliyoitaja na kwenye baadhi ya wilaya za mikoa ambayo hapo haijatajwa. Mfuko huu utajihusisha sana na shughuli za kimaendeleo na kijamii kwenye maeneo husika bila kujali itikadi za kisiasa ingawaje wakati huo huo mtakuwa mnahubiri siasa. Katika kufanikisha jambo hilo, mtakuwa mnaibua miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ambayo itawashirikisha wananchi katika kuiendesha! Na kwavile itafahamika wazi kwamba DRFA Trust ni ya kwenu, basi sina shaka yoyote wananchi wengi pia watataka kuwaunga mkono kisiasa. Hayo ndio mapendekezo ya CDTPE kwahiyo ningependa maoni yenu, nikianza kwa Bwana Mkundi!" George Malilo alimalizia .

"Mkakati huo ni mzuri, lakini awali ya yote ni lazima kwanza tufahamu ni nani walihusika na kuvuja kwa taarifa zile za awali kabla hatujaingia kwenye mkakati huu wa sasa! Hofu yangu ni kwamba, endapo hatujapata kiini basi kuna hatari hata habari hizi nazo zikavuja. Kama mjuavyo, katika msafara wa mamba kenge nao hawakosekani!" Mkundi alimalizia na kuwatupia macho wenzake kama ishara ya kutafuta uungwaji mkono!

Hakupata uungwaji!

Ni kama vile walishikwa na kigugumizi cha ghafla, hali ambayo hata George Malilo nae alishaigundua!

"Safi kabisa Bwana Mkundi, kwakweli nami nimewaeleza mkakati huo kirahisi ili niwaone mtaupokea vipi! Ni kama nilikuwa *nawatega*! Mngekubali kirahisi basi ningekuwa na hakika kwamba ni kweli ni nyinyi ndio

mlivujisha habari zile! Hii imenipa imani zaidi kwamba huenda siri hii imevujishwa na wasaliti fulani nje ya nyinyi. Hivyo basi, ningewaomba taarifa hii kwanza iwe siri wakati nanyi mnajaribu kutafuta mchawi. Hata upande wa CDTPE, ni watu wachache sana ambao tunafahamu juu ya mpango huu mpya!" George Malilo aliendeleza sanaa yake ya kuwachezea akili na baada ya majadilianao ya hapa na pale waliagana.

Glory hakutaka kuamini alichosikia! Alirudi ndani na kuangaza macho huku na huko, lakini hakuambua chochote! Alienda kituo cha polisi cha hapo uwanjani, lakini nako hakupata chochote! Akahisi kufanya kosa, hivyo alirudi nje haraka na kuangaza huku na huko huku akihakikisha anamwona kila anayetoka kwenye lango kuu!

Hakuambua kitu!

Akakumbuka kitu, akachukua simu yake na kuangalia namba iliyopigwa kwake na Bon Mtambo. Akakuta kumbe namba ilifichwa, yaani *private call*!

"*Damn it*!" Glory alifoka na kuondoka hapo uwanjani huku akiwa hajui ni nini hasa kilichotokea! Alikodi teksi ambayo ilimpeleka moja kwa moja nyumbani kwa Bon Mtambo. Baada ya kufika hapo alianza kukagua sehemu mbalimbali lakini hakuona dalili yoyote ya kuonesha angalau amepita hapo! Alisubiri hadi kiasi cha saa tano asubuhi bila ya kuwepo na dalili za Bon Mtambo kutokea! Baada ya kukata tamaa aliamua kuzunguka na kuulizia kwenye vituo mbalimbali vya polisi lakini kote huko hakukuwa na mtu mwenye jina alilotafuta! Alikata

tamaa na kuamua kurudi nyumbani kwake, na alipofika tu alichukua simu yake na kupiga mahali!

“Lete habari Glory, bila shaka kila kitu kipo sawa!” Upande wa pili wa simu uliongea. Glory alichukua sekunde kadhaa bila kuongea chochote, hali iliyomshangaza hata yule aliyepokea simu!

“Glory, upo sawa bibie?”

“Nipo sawa, lakini mambo si mazuri!”

“Kwanini!?”

“Bon Mtambo amenitoroka!”

“*What*?!”sauti upande wa pili iliuliza kwa hamaki, kisha Glory akaanza kuelezea tukio zima lilivyotokea!

“Ondoa shaka, tutamuonesha kwamba sisi tuna akili zaidi yake. Kuna kikao fulani kinafanyika Uswisi hivyo bila shaka atakuwa ameenda huko! Tumeweka watu wetu huko hivyo kama ndiko alikoenda basi tutamnasa tu!” George Kamau alieleza na kumwacha Glory akiwa ni kama aliyepigwa na bumbuwazi. Alianza kuingiwa na hofu kwamba huenda tayari Bon Mtambo alishamgundua kwamba yeye ni nani hasa kwake! Alianza kuingiwa na hofu baada ya kuhisi kwamba Bon Mtambo ni mtu hatari sana. Hakika tukio ambalo lilitokea uwanja wa ndege aliona ni  kama sinema!

“Unazani atakuwa ameshanigundua?” Hatimae Glory aliuliza.

“Sizani! Isikupe hofu hatua ya yeye kuondoka ghafla bila hata kukuarifu. Michezo kama hii wakati mwingine inatufanya tuwe ni wenye maamuzi ya kushangaza kidogo machoni mwa watu! Hivi sasa wewe njoo hapa ofisini bila kupoteza muda.” Kamau alihitimisha maelezo yake kisha Glory nae akachukua gari na kuelekea ofisini kwa Kamau.

Bon Mtambo aliwasili Uwanja wa Ndege wa Geneva majira ya saa nne usiku! Hapo uwanjani hakupata usumbufu wowote hivyo baada ya taratibu za hapa na pale alitoka nje ya uwanja ambako alikuta gari ikimsuburi.

"Pole na safari!" Dereva wa gari aliyopanda, ambae ni mzungu alianza maongezi.

"Ahsante, ni wapi umejifunza kiswahili!?" Bon Mtambo alishindwa kuuzuia mshangao wake.

"Unashangaa mimi kufahamu Kiswahili? Si unajua hizi kazi zetu wakati wote mtu inabidi uwe kama kinyonga!"

"Ni kweli!"Bon Mtambo aliunga mkono. Alitamani kuuliza nini chanzo cha kikao hiki cha ghafla lakini alikata shauri la kuwa mstahimilivu. Njia nzima, kila mmoja alionekana kuzama kwenye lindi zito la mawazo na mara chache chache tu ndipo walijitumbukiza kwenye maongezi.

Baada ya mwendo wa takribani dakika ishirini, walifika safari yao na kuegesha gari yao mbele ya jengo moja. Waliteremka, na mara macho ya Bon Mtambo yakagongana na macho ya msichana mmoja mwenye asili ya Kimanga. Msichana huyu alimwangalia Bon Mtambo mara moja tu kisha akatazama chini katika hali iliyoonesha ni mwingi wa aibu! Hata hivyo, akili ya Bon Mtambo iligoma kuhama kwa msichana huyu! Alimfuatilia kwa macho hadi alipopotelea kwenye hoteli iliyo jirani na hapo!

"Tufanye haraka, tunasubiriwa!" Bon Mtambo aligutushwa toka kwenye mawazo juu ya yule binti. Na bila kupoteza muda zaidi, walifanya haraka hadi kwenye chumba cha mikutano walichokuwa wanasubiriwa. Waliwakuta kiasi cha watu saba, na baada ya wao kuingia

walifanya idadi yao kutimia tisa. Baada ya kuketi kwenye kiti, Bon Mtambo alichukua kifaa maalumu na kuvaa masikioni. Ni kifaa kinachotumika kurahisisha maelewano ya lugha inapotokea lugha inayozungumzwa haifahamiki na wote.

*"Free Corrupt World!"* Mwenyekiti wa kikao, Peterson Paul alifungua kikao hicho kwa kauli mbiu ambayo hutumiwa na kila mtu anapohitajika kuongea!

*"Has no objection!"* Wajumbe wengine wote waliitikia kwa hamasa kubwa huku wakikunja ngumi na kupunga mikono juu kwa kuisiganisha!

*"Free Corrupt World!"*

*"Has No Objection!"*

"Bon Mtambo, kwanza kabisa pole na safari ndefu yenye uchovu mwingi. Tulipata habari kwamba ulikuwa Marekani, lakini hali halisi ilitunyima busara ya kukupa japo muda mfupi wa kupumzika pindi uliporejea Tanzania!" Peterson Paul, mwenyekiti wa kikao hiki alianza kuhutubia. Peterson hakuwa mgeni kwa Bon Mtambo, hii ni karibu mara ya tano anakutana nae kwenye vikao kama hiki. Akiwa na umri unaokaribia miaka hamsini na tano, Peterson amekuwa ndie kiongozi mwenye mafanikio makubwa zaidi katika historia ya Shirika la Uchunguzi Duniani Dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa, yaani World Investigation Bureau Against International Crimes , au WIBAIC kwa kifupi. Alijiunga na WIBAIC akitokea Scotland Yard nchini Uingereza ambako nako hadi anaondoka alikuwa ni mwenye mafanikio makubwa katika kupambana na uhalifu.

Kimsingi, WIBAIC ni taasisi ya kimataifa ambayo kazi yake kubwa ni kupambana na uhalifu wa kimataifa hususani wa aina zote za biashara haramu pamoja na

ubadhirifu wa kimataifa, yaani *cross boarder corruption*. Kwa upande wa ubadhirifu wa kimataifa, WIBAIC imefanikiwa kuwafichuwa viongozi mbalimbali duniani wenye akaunti za benki nje ya nchi zao zinazotokana na pesa haramu. Pamoja na kuwafichuwa viongozi hao, vilevile imepata kuzifichuwa kampuni kadhaa za kimataifa ambazo hujihusisha na rushwa katika upataji wa tenda za kibiashara katika nchi za kigeni. Na kwa sasa WIBAIC, inaendesha kampeni ya kutungwa sheria ya kimataifa ambayo itazizuia kampuni zote zinazojihusisha na rushwa za kimataifa kuwekewa vikwazo vya kushiriki kwenye zabuni za kimataifa. Kampeni yao hii, inapata uungwaji mkono mkubwa kutoka mashirika makubwa ya kupambana na rushwa duniani kama vile Transparency International. Tofauti na Transparency International, WIBAIC ni taasisi yenye nguvu za kisheria zinazoiwezesha kupambana na uhalifu kupitia mkondo wa kikachero na hata kuwafikisha mahakamani wahusika. Hata hivyo, tatizo kubwa linalowakabili ni kwamba wanaruhusiwa kuendesha shughuli zao kwenye zile nchi ambazo tu ndizo zimeridhia kufanya kazi na taasisi hiyo, Tanzania ikiwa moja wapo. Na hili ndilo lingine wanalopigania kwamba nchi zote duniani zisaini mkataba wa kufanya kazi na WIBAIC. Ndoto kubwa ya WIBAIC ni kuona siku moja dunia inakuwa eneo huru dhidi ya vitendo vya rushwa, ubadhirifu pamoja na vitendo vyote vya kihalifu!

“Kwa kifupi ni kwamba,” hatimae Peterson aliendelea, “kitengo chetu cha ujasusi, yaani WIBAIC Intelligence Unit kimegundua kuwepo kwa mtandao wa uhalifu wa kimataifa unaoelekea kutaka kuota mizizi nchini Tanzania. Mtandao huu ulianzishwa mara baada ya Tanzania kuanzisha sera ya ubinafsishaji wa mashirika ya

umma, na kwa sasa unashika kasi ya kutisha! Kimsingi, mtandao huu una lengo la kuwaweka chini ya himaya yao viongozi wa serikali na watu wengine wenye ushawishi kwa jamii. Wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali, na kubwa zaidi ni kuwahonga watu kadhaa, wakati mwingine hata pasipo na sababu za msingi za kuhonga lakini huku wakiamini kwamba ipo siku watawatumia watu hao! Taarifa hizi za kijasusi zinaendelea kudokeza kwamba, endapo hatua za makusudi hazitachukuliwa basi muda si mrefu mtandao huu utaotesha mizizi ukanda mzima wa maziwa makuu. Si hilo tu, kwavile wana uwezo wa kutumia kila njia ili kumpata wamtakae, kuna hatari siku moja serikali za nchi hizi zikawa si tena za wananchi bali zinazotumikia majahili hawa wa kimataifa. Hivyo basi, WIBAIC baada ya kupata taarifa hizi, ilikata shauri kwamba hatutaweza kuvumilia hali hii hata kidogo. Ndoto yetu ya kuwa na dunia isiyo na ubadhirifu, yaani *Free Corrupt World* lazima itimie, tena kwa gharama yoyote ile. Hivyo basi, napenda kutumia fursa hii kukutangazia rasmi kwamba WIBAIC inakupa jukumu la kwenda kuuvunja mtandao huu wa kishenzi mapema iwezekanavyo. Ukishafika Dar es salaam, utapatiwa mtu mmoja wa ziada atakayekuwa na wewe bega kwa bega kwenye operesheni hii. Na endapo utahitaji mtu mwingine zaidi hapo baadae, usisite kutuharifu nasi tutakupatia!"Alimalizia na kumuuliza Bon Mtambo kama alikuwa na swali lolote.

"Ningependa kufahamu endapo hadi sasa kuna fununu yoyote ya wahusika wa mtandao huu!" Hatimae Bon Mtambo aliuliza baada ya kuyatafakari maelezo ya Peterson.

"Hadi sasa tunasikitika kwamba hamna fununu yoyote ambayo inaweza kukusaidia. Hata hivyo, kilicho

dhahiri ni kwamba mtandao huu utakuwa na uhusiano na wafanyabiashara wakubwa wa kigeni."

*"Free Corrupt World!"* Bon Mtambo alianza kuhamasisha!

*"Has no objection!"* Wajumbe waliitikia kwa mtindo uleule!

*"Free Corrupt World!"*

*"Has No Objection!"*

"Awali ya yote ningependa kutoa shukurani zangu kwenu kwa kunipatia kazi hii ambayo lengo lake kubwa ni lile lile la kuhakikisha kunakuwa na dunia huru isiyo na ubadhirifu." Hatimae Bon Mtambo alianza kueleza, kisha akatoa ombi, "lakini hata hivyo, ningependa huyo msaidizi wangu msimlete kwa sasa na badala yake nitawaarifu pindi nitakapomuhitaji!" Bon Mtambo alimalizia, na baada ya majadiliano ya hapa na pale walikubaliana na ombi lake kisha wakaagana.

Uchovu wa safari ulimfanya Bon Mtambo achelewe kufika uwanja wa ndege tayari kwa kurejea Tanzania. Alikamilisha taratibu hapo uwanjani haraka haraka na kuwahi ndege ambayo ilikuwa inakaribia kuruka. Alipofika kwenye ndege, alikuta ni kiti kimoja tu kilichokuwa wazi ambacho bila kupoteza muda alienda kukaa. Aliyekuwa nae kwenye kiti hicho ni msichana ambae alishindwa kumtambua kwavile alikuwa amejifunika kitambaa usoni na kujiegemeza kwenye kiti katika hali iliyoonesha amelala!

Kiasi cha dakika tano baadae, ndege ilianza kutembea ili kuiacha ardhi ya Geneva. Hali hii ilimfanya

huyu msichana azinduke usingizini na kumfanya Bon Mtambo apatwe na kigumimizi cha ghafla mara baada ya kujifunua kitambaa chake!

Alikuwa ni yule binti wa Kimanga aliyemuona jana yake usiku!

"Naitwa Joseph Kimathi, mzaliwa wa Kenya lakini nimekulia na kuishi Dar es salaam." Bon Mtambo alijitambulisha kwa huyu msichana kwa kutumia jina lake la bandia lililotumika kwenye hati ya kusafiria. Msichana huyu aliyatuliza macho yake mazuri kwa Bon Mtambo kisha akatoa tabasamu ambalo lilitosha kabisa kuwa tiba kwa mwanaume yeyote mwenye hisia mfu za mapenzi!

"Naitwa Layla, mzaliwa wa Mombasa, na pia naishi huko na wazazi wangu!" Alijibu yule binti.

"Kwahiyo safari hii inakufikisha moja kwa moja hadi Mombasa?" Bon Mtambo aliuliza kwa huzuni kidogo kwavile alitamani safari yao hii iwafikishe sehemu moja.

"Hapana, kwa sasa inabidi nifike Dar es salaam kwanza kwavile nina safari ya Zanzibar ambako naenda kumwangalia shangazi yangu!"

"Natumaini wakati unaelekea Zanzibar utaweka kituo angalau kwa siku moja nyumbani kwangu!" Bon Mtambo alichokoza na kumfanya Layla atoe lile tabasamu lake ambalo mara zote limekuwa likimfanya Bon Mtambo akaribie kurukwa na akili!

"Na utanitambulisha vipi kwa mke wako, au mchumba, au hata mpenzi wako?" Hatimae Layla alimtupia swali Bon Mtambo lililomfanya ababaike kidogo na kumfanya amkumbuke Glory ambae ilielekea ni kama alishamsahau kwa muda! Swali la Layla likamfanya Bon Mtambo avute kumbukumbu kuhusu Glory na kuanza kumthaminisha kwa kumlinganisha na msichana huyu!

Jibu alilopata likamfanya avute pumzi ndefu ambazo kimsingi alishindwa kupata jibu la nani zaidi ya mwenzake!

"Naishi peke yangu Layla?"Hatimae Bon Mtambo alijibu lakini kwa kubabaika kidogo.

"Ni sawa, inawezekana unaishi peke yako nyumbani lakini huishi peke yako kwenye maisha yako!"

"Ni kweli, lakini...!" Bon Mtambo alijaribu kujitetea lakini Layla aliingilia kati:

"Tuyaache hayo Jose, nitaangalia uwezekano wa ombi lako. Kama sitaweka kituo wakati wa kwenda basi naweza kuweka kituo wakati wa kurudi ili mradi tu unihakikishie usalama wangu!"

Waliongea mambo mengi kiasi cha kuifanya safari yao ionekane fupi licha kwamba iliwachukuwa masaa kadhaa.

Layla na Bon Mtambo waliingia jijini Dar es salaam majira ya saa moja unusu asubuhi ya siku iliyofuata. Kwavile Layla alikuwa na mizigo mitatu, Bon Mtambo alimsaidia begi moja dogo baada ya kuombwa kufanya hivyo na Layla mwenyewe. Baada ya Layla kukaguliwa alitoka nje. Aliyefuata alikuwa ni raia wa kigeni kisha ikaja zamu ya Bon Mtambo, ama Joseph Kimathi.

Katika hali ya kushangaza, ilipofika zamu yake alikaguliwa kwa umakini zaidi kuliko abiria wengine! Baada ya kukaguliwa begi lake, likaanza kupekuliwa begi alilombebea Layla. Begi hili lilikuwa na mifuko mingi ya ndani, na wakati zoezi likiendelea mara lilisimama ghafla na kumfanya mpekuzi wake ainue kichwa kumtazama Bon

Mtambo! Bila kutarajia, alijikuta akiamriwa kuingia kwenye chumba kimoja kwa upekuzi zaidi!

*Chanzo cha upekuzi wote huu ilikuwa ni George Kamau aliyepenyeza taarifa kwa wanausalam akijifanya ni raia mwema!*

Kabla hajaingia humo chumbani, aliyatupa macho yake kule alikoelekea Layla. Katika hali ya kustaajabisha alimshuhudia akimpungia mkono na kisha kutokomea kwa gari ambayo iliondoka kwa kasi hapo uwanjani!

"*Kazi imeanza!"* Bon Mtambo aliwaza.

Baada ya kufanyiwa upekuzi zaidi, ndani ya begi la Layla zilikutwa paketi tano zilizoaminiwa kuwa ni madawa ya kulevya! Aidha, kulikuwa na kimkebe chenye madini fulani yaliyohisiwa kuwa ni uraniamu! Pamoja na hivyo vitu, vilevile kulikuwa na hati zingine mbili za kusafiria, moja yenye jina lake halisi lakini ikimuonesha kuwa ni raia wa Malawi, na nyingine ikiwa na jina Abdulhusein Awadhi, mzaliwa wa Lamu nchini Kenya!

"Haya tusaidie wewe mwenyewe, unaitwa Bon Mtambo, Joseph au Abdulhusein?! Ni raia wa Malawi au Kenya?" Askari polisi aliyekuwa anamfanyia upekuzi aliuliza kwa kejeli!

"Ni Joseph, na ni raia wa Kenya"

"Na hizi hati zenye jina la Bon Mtambo Kareem na Abdulhussein Awadhi Juma?"

"Sizifahamu!"

"Hufahamu wakati zimekutwa kwenye begi lako?"

Kimya!

Baada ya upekuzi huu, Bon Mtambo alitolewa kwenye hicho chumba na mara akagongana macho na yule mtu ambae alimpatia hati za kusafiria kwenda Geneva. Mtu huyo alikuwapo hapo kuchunguza endapo kuna yeyote aliyekuwa anamfuatilia Bon Mtambo wakati anawasili!

Pamoja na huyo mtu, vilevile alikutana na watu kiasi cha watatu waliionekana kama ni waandishi wa habari!

Layla alifika ofisini kwake majira ya saa tatu asubuhi. Bila kupoteza muda, aliwasha kompyuta na kuanza kuandika:

**HATARI - Jasusi Labambwa Uwanja wa Ndege Dar!**

- **Begi lake lakutwa na madini ya Kutengenezea Mabomu ya Nyuklia!**
- ***Lakutwa pia na Pakiti kadhaa za Madawa ya Kulevya,***
- ***Vilevile labambwa likiwa na hati tatu za kusafiria!*** ***Na Mwandishi Maalumu.***

*Tanzania, ukanda wa Maziwa Makuu na Afrika kwa ujumla imekumbwa na kihoro kufuatia Mtanzania mmoja aitwae Bon Mtambo Kareem (27) kukamatwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam akiwa na vitu vinavyohisiwa kuwa ni madini ya uraniamu. Madini hayo hatari ambayo hutumika kutengenezea mabomu hatari ya nyuklia yalikutwa kwenye begi la Mtanzania huyo ambae pia anahisiwa kulifanyia kazi za kijasusi kundi hatari la kigaidi la Al-Qaed. Habari za kuaminika zinasema kwamba kijana huyo alikutwa na sakata hilo wakati akitokea nchini Uswisi inakohisiwa kulikuwa na kikao cha siri cha majasusi wa kundi hilo hatari duniani.*

*Chanzo chetu cha kuaminika cha habari kilieleza pia kuwa, mtanzania huyo mwenye hati kadhaa za kusafiria vilevile alikamatwa na paketi kadhaa za madawa ya kulevya aina ya heroin na hivyo kusababisha hofu ya kuharibika kizazi cha vijana ambacho ndio nguvu kazi inayotegemewa duniani. Chanzo chetu hicho kikiongea na mwandishi wa habari hizi kilisema kwamba,*

*Bon Mtambo Kareem amekuwa akifuatiliwa na makachero wa Marekani kwa muda mrefu hivi sasa! Aidha, chanzo hicho kiliendelea kupasha kwamba Jasusi hilo hatari lina mpango wa kuanzisha mashambulizi kadhaa ya kigaidi hapa nchini dhidi ya makampuni kadhaa ya kigeni hususani yale ya Marekani na Ulaya.*

*Watu mbalimbali walioongoea na mwandishi wa habari hii wana hofu ya kwamba huenda magaidi wa Al-Qaeda wakaanzisha mashambulizi yao nchini siku chache zijazo yatakayolenga kutaka kumwokoa gaidi mwenzao!*

Baada ya kufika hapo, Layla alianza tena kuipitia hiyo habari kisha akatabasamu! Aliandika habari nyingine kama hii lakini katika lugha ya kiingereza. Baada ya kufanya mabadiliko mengine ya hapa na pale, alinyanyua simu na kupiga mahali:

“Halo, Layla naongea. Ningependa kukueleza kwamba tayari Bon Mtambo hivi sasa yupo mikononi mwa polisi.”

“Vizuri mrembo, lakini usisahau kuandaa taarifa kwa baadhi ya wahariri wetu wa magazeti.”

“Nimeshaandaa tayari!”

“Safi sana. Kwavile taarifa hii ni muhimu sana kila mhariri kampatie shilingi milioni mbili unusu na waambie habari ikishatoka watapatiwa milioni mbili unusu nyingine! Hata hivyo, kabla hujapeleka habari hiyo, naomba unitumie kwanza kwa barua pepe ili niione.”

# 9

Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Tanzania, DCI Humphrey Mwaiswelo alianza kupitia mafaili kadhaa yaliyokuwa mezani pake. Hata hivyo, kila faili aliloshika, alihisi kama ni la moto! Mafaili yalikuwa mengi mno!

Wakati akiendelea kupitia faili hili na lile mara mashine ya faksi iliyokuwa jirani yake ilitoa mlio kuashiria kuna faksi inaingia. Huku akionekana kuwa na mawazo mengi DCI Mwaiswelo alinyosha mkono na kuchukuwa faksi hiyo ambayo ilikuwa na maelezo mafupi sana:

*Rescue, WIBAIC TZ One under your forces!*

DCI Mwaiswelo alishusha pumzi kufuatia taarifa hiyo fupi ambayo alishaielewa ilikuwa na maana gani! Aliangalia namba ya faksi ya mtumaji, nayo akaitambua. Bila kupoteza muda, alivuta simu ya mezani na kuanza kupiga namba alizokusudia.

"Halo, OC-CID Abraham kwenye simu!" Upande wa pili wa simu ulijitambulisha.

"Ni DCI Mwaiswelo hapa, napenda kufahamu kama kuna mtu yeyote mnayemshikiria akitokea Geneva Uswisi!"

"Yupo afande, na sasa tunamuhoji hapa!"

"Sasa sikiliza, huyo mtu mleteni kwangu sasa hivi. Hata hivyo, hakikisheni hakuna mtu anayefahamu juu ya

kuja kwenu! Aidha ongozana na vijana wale tu unaowaamini kwamba wanazingatia maadili ya kazi yao."

*Ilichukuwa dakika kumi tu Bon Mtambo kuletwa mbele ya DCI Mwaiswelo.*

"Subirini hapo nje!" DCI Mwaiswelo aliwaamuru maofisa wa polisi waliomleta Bon Mtambo.

"Pole sana kijana!"

"Usijali mzee, ni mchezo ambao nilishaushuku mapema lakini nikaamua kujifanya mjinga!"

"Hebu tueleze ni nini hasa kimetokea!" DCI Mwaiswelo alihoji.

"Bila shaka unafahamu kuhusu kikao ambacho WIBAIC ilikifanya juzi jijini Geneva!" Bon Mtambo aliuliza.

"Yote nayafahamu na ndio maana hukupata shida wakati wa kusafiri. Napenda kufahamu ulivyoingia kwenye sakata lililokufikisha mikononi mwa polisi!"

"Ni hivi mzee, wakati narudi Dar es salaam, nilikutana na dada mmoja kwenye ndege ambae tulikaa kiti kimoja. Ingawaje alijitahidi kujionesha ni abiria wa kawaida, lakini tayari nilishaanza kuwa na wasiwasi nae! Wasiwasi wangu uliongezeka zaidi pale alipoamua nimbebee mkoba wake tulipofika uwanja wa ndege hapa Dar es salaam. Kwani, mara baada ya kunipatia mkoba huo, yeye alitangulia mbele kwa hatua za haraka kiasi kwamba ingekuwa ngumu kwa mtu yeyote kufahamu kwamba tulikuwa pamoja! Hata hivyo, niliamua kujifanya mjinga ili nifahamu lengo la mchezo wake!"

"Safi kijana, kwahiyo tukuachie sio?" DCI Mwaiswelo alihoji.

"Hapana, ningependelea kesho nifikishwe mahakamani na pale nitakanusha mashitaka ili nirudishwe mahabusu. Nikiwa mahabusu, nitafanya vurugu kidogo na

utawaagiza askari waniweke kwenye chumba cha peke yangu chenye ulinzi mkali. Baada ya kuwekwa chumba cha peke yangu, ndipo itabidi niachiwe, lakini kwa siri sana ili nianze kazi yangu iliyonipeleka Geneva. Hata hivyo, angalau mara moja kwa wiki, ningependa nirudishwe mahakamani kuendelea na kesi ili kuendelea kuwapumbaza wale walioniingiza mtegoni. Nitakuwa napelekwa mahakamani nikitokea mahabusu ili kuwaonesha kuwa bado nashikiliwa na vyombo vya usalama. Hivyo basi, jambo la msingi ni kuwapata askari waaminifu watakaohusika na ulinzi wa sehemu itakayoaminika kwamba ndiko nimeshikiliwa. Aidha, hata hakimu atayeendesha kesi hii nae inabidi awe mtu wetu! Hata hivyo, watu hao wasijue kiundani ni nini hasa ninachofanya!" Alitulia kidogo kisha akamalizia, "Kwa nyongeza tu ni kwamba naomba leo uitishe mkutano na waandishi wa habari lakini usiongelee kwa kina suala hili. Waambie tu kwamba nimekamatwa na vitu vinavyohisiwa ni madawa ya kuleva, basi. Kusiwe na maelezo marefu kwavile ningependa kufahamu ni vyombo gani vya habari vitakuwa na maelezo ya kina kuhusu sakata hili."

"Safi kijana, mkakati mzuri! Je, kuna msaada mwingine ambao ungeuhitaji ili kufanikisha kazi hii?" DCI Mwaiswelo aliuliza.

"Ni kweli mzee, ningeomba magari ambayo ni 4WD nitakayotumia kwa dharura. Magari mawili yaegeshwe kwenye maegesho ya ukumbi wa zamani wa Avalon, magari mawili yakaegeshwe kwenye maegesho ya Chuo Cha Usimamizi wa Fedha, IFM na mawili yakaegeshwe polisi Chang'ombe. Funguo za magari hayo zifichwe kwenye viti vya nyuma nami nitapatiwa tu namba na aina za magari husika." Bon Mtambo alimalizia.

*Baada ya maelekezo mafupi, DCI Mwaiswelo aliwaita vijana wake ambao hapo kabla aliwatoa nje.*

"Nimewaita kuwaambia kwamba huyu mtu sio mharifu, ni mtu wetu aliye katika kazi maalumu. Vitu alivyokamatwa navyo ulikuwa ni mtego aliotegeshewa na wahalifu waliogundua kwamba anawafuatilia. Hata hivyo sio kwamba hakufahamu kwamba ni mtego, alijua isipokuwa aliamua tu kujifanya mjinga! Hata hivyo nawaonya kwamba, mpango huu ni wa siri sana ambayo kuitoa kwake kunaweza kugharimu hata maisha yenu! Ni siri ambayo hampaswi kuwaeleza hata wake zenu, achilia mbali ndugu zenu! Aidha, nyie mliokuja hapa ndio mtahusika katika ulinzi wake gerezani. Kumbukeni kwamba habari hii ikivuja tu, mimi nitaanza na nyinyi kwavile hamna mwingine anayefahamu juu ya jambo hili!" DCI Mwaiswelo alihitimisha maelezo yake huku *akiwapiga mkwala* vijana wake!

Glory alipata taarifa za kukamatwa kwa Bon Mtambo kupitia kwa George Kamau. Taarifa hii ilimpa ahueni kufuatia kosa alilofanya la kubaki na simu ya Bon Mtambo ambayo ilikuwa ni mahususi kwa ajili ya kufuatilia nyendo yake. Aliamini kabisa kwamba Kamau na watu wake wasingemsamehe kwa kosa hilo. Walitumia maelfu ya dola kumsafirisha yeye Glory pamoja na Bon Mtambo hadi Marekani na kukaa huko kwa takribani juma moja. Wakati Bon Mtambo akiamini safari hiyo ni ya matibabu ya Glory lakini ukweli ni kwamba ilikuwa ni maalumu kwa ajili yake yeye mwenyewe ili akanunuliwe simu. Simu aliyonunuliwa ni zaidi ya simu, kwani ilikuwa

na vifaa maalumu vya kupokea na kusafirishia sauti na picha! Walifanya hayo yote baada ya kupata tetesi kwamba shughuli zao zilikuwa hatarini kuingiliwa na makachero. Aidha, waliambiwa uwezekano wa Bon Mtambo kuendesha kampeni hiyo dhidi yao. Ni kutokana na taarifa hizo za kikachero ndipo George Kamau na wenzake wakampenyeza Glory kwa Bon Mtambo na kufikia kumnununulia simu hiyo maalumu!

Magazeti mengi ya siku iliyofuata yalisheheni taarifa za kukamatwa kwa Bon Mtambo na madawa ya kulevya. Hata hivyo, magazeti yaliyotia fora zaidi ni yale ambayo yalipokea taarifa hii moja kwa moja toka kwa Layla. Kwa msomaji aliye makini, angeweza kugundua kwamba mwandishi wa habari hizo kwenye magazeti yote hayo ni mmoja, ingawaje kulikuwa na tofauti kiasi kutoka gazeti moja hadi jingine! Taarifa za magazeti haya zilisababisha Mahakama ya Kisutu ifurike watu kuja kusikiliza kesi hiyo, na zaidi kumfahamu huyo mtu aliyetajwa kuwa ni jasusi la kimataifa aishie kwenye viunga vya jiji la Dar es salaam! Glory nae alikuwa ni miongoni mwa waliokuja kuhudhuria mahakamani.

Baada ya Bon Mtambo kukanusha kuhusika na tuhuma alizosomewa aliingizwa garini tayari kwa kurudishwa mahabusu. Hata hivyo, kabla hajatolewa mahakamani alipata nafasi ya kuongea na Glory.

“Bon, pole sana mpenzi! Kwakweli nimeshitushwa sana na taarifa hizi ingawaje nashindwa kufahamu ni kwanini ulijiingiza kwenye mambo hatari kama haya?”

“Usijali Glory, ndio maisha yalivyo. Nimezaliwa mwanaume ili nipate kupambana na mambo kama haya!”

“Kwahiyo ni kweli umehusika kwenye hili jambo?”

“Nisamehe Glory, hata hivyo nakuahidi endapo nitatoka salama basi naachana kabisa na biashara hii!”

“Na suala la ugaidi je?”

“Kesi ya ugaidi nimesingiziwa mpenzi wangu!”

“Sawa mpenzi, lakini kumbuka bado nipo pamoja na wewe kwenye tatizo hili. Nami nakuahidi nitafanya kila liwezekanalo nikutoe nje pale dhamana yako itakapokuwa wazi!” Glory alimaliza na kuagana na Bon Mtambo.

Mara baada ya kuachana, Glory na Bon Mtambo kila mmoja alikuwa anawaza kivyake juu ya mwenzake! Hata hivyo, Glory alikuwa na hofu zaidi kuhusu hisia zake wakati Bon Mtambo yeye aliishia tu kujishangaa! Wakati Bon Mtambo alijishangaa ni kwanini hakumueleza ukweli Glory, yeye Glory alishangaa ni kwanini Bon Mtambo ameshindwa kumuamini.

“*Kwanini anataka niamini ni kweli amekamatwa na madawa ya kulevya wakati anajua si kweli*!” Glory alijiuliza huku akikosa amani ndani ya nafsi yake.

Tatizo lililokuwa linamkabili Glory ni nafsi mbili ndani ya mwili mmoja, ambazo zilikuwa zinashindania ufalme kwenye nafsi yake. Wakati alikuwa na jukumu la kuitekeleza kazi yake iliyomfanya akutane na Bon Mtambo, lakini kwa bahati mbaya akajikuta anatokea kumpenda kijana huyo. Kilichompeleka kwa Bon Mtambo hakikuwa mapenzi ya dhati, lakini akajikuta anashindwa kujimiliki na bila kutarajia mapenzi ya dhati yakaanza kumea taratibu ndani ya nafsi yake!

“*Kuna akina Bon Mtambo wengi sana duniani, lakini kazi zenye kipato kama hii ni chache au ni kama hakuna hususani kwa*

*hapa Tanzania!"* Glory alipiga moyo konde na kutoweka hapo mahakamani.

Bon Mtambo alitolewa kizuizini majira ya saa tano usiku tayari kwenda kuanza kazi yake! Aliingia kwenye gari ya polisi ambayo ingempeleka hadi sehemu ambayo angeona ni muafaka kwa usiku huo. Hata hivyo, alisita kidogo wakati dereva wa gari hiyo akijiandaa kuingia Sokoine Drive!

"Subiri mara moja SSP Faraji!" Bon Mtambo alimwambia huyo dereva.

Bon Mtambo aliteremka kwenye gari na kwenda kukagua baadhi ya daladala zilizokuwa zimeegeshwa hapo kituoni. Baada ya kumaliza alirudi kwa SSP Faraji Zegge na kumwamuru akamwitie OC-CID Miraji.

"Nasikia unanihitaji mkuu!" OC-CID Miraji aliuliza mara alipofika.

"Ndio afande, naomba kuondoka na daladala tatu kati ya zile zilizoegeshwa. Hata hivyo, nitazitumia kwa muda mfupi tu na zitarejeshwa mapema kesho asubuhi! Kati ya hizo, mimi nitaondoka na moja, nyingine ataondoka nayo SSP Faraji Zegge na ya mwisho ataondoka nayo Inspekta Mussa Ndimbu." Bon Mtambo alieleza kisha akaitwa Inspekta Mussa Ndimbu ili awapatie maelekezo.

"Kwahiyo mkishafika TAMECO mtaingia barabara ya kwenda Temeke na mbele mtakuta nimeegesha gari yangu maeneo ya Chang'ombe. Nanyi mtakuja kuegesha magari yenu hapo. Aidha, kazi yetu tukiwa hapo ni kufuatilia nyendo za mtu yeyote atakayeonekana kuwa na shauku na nyumba moja yenye ghorofa moja iliyo jirani na

hapo. Nyumba yenyewe imepakwa rangi ya zambarau nyepesi na ina geti la kijani." Bon Mtambo alimalizia maelekezo yake.

Nyumba aliyoimaanisha Bon Mtambo ni nyumba ya kwake mwenyewe.

*"Kwavile hawa majahiri wanaonekana wako makini kwenye mipango yao, basi sina shaka kwamba watakuja kupeleleza pale nyumbani! Wakifanya hivyo, nami watanipa mwanya wa kujua ni wapi pa kuanzia kwavile hadi sasa nipo gizani."* Bon Mtambo aliwaza wakati akipiga gari moto na kushika barabara ya Sokoine Drive.

Robo saa baadae Bon Mtambo, SSP Faraji Zegge na Inspekta Mussa Ndimbu walikuwa wameegesha magari yao kiasi cha meta mia moja toka ilipo nyumba ya Bon Mtambo. Yalionekana ni kama magari ya kawaida ya abiria ambayo yalikuwa yamerudishwa kwa tajiri baada ya kazi ya mchana kutwa!

Walitulia hapo huku wakipigana kiume na usingizi! Bon Mtambo hakutaka kuamini kwamba sehemu hiyo hapakuwa na mtu yeyote aliyekuwa anaichunga nyumba yake. Ili kujiridhisha, alikata shauri la kwenda moja kwa moja kujionea mwenyewe.

*"Naenda kuangalia huko ndani, nichungeni! Zikipita dakika kumi sijarejea, mtakuja kuangalia kulikoni."* Bon Mtambo alituma ujumbe mfupi wa simu kwa SSP Faraji Zegge na mwenzake Inspekta Mussa Ndimbu kisha bila kuchelewa aliteremka kwenye gari na kunyata upande mwingine. Si kwamba alihofia kuonekana na maadui, bali hakutaka kuonekana kuwa alitoka kwenye moja ya hayo

magari. Baada ya kuyaacha hayo magari, sasa alivuka barabara na kutembea bila wasiwasi kuelekea kwenye nyumba yake. Alitembea kwenye barabara iliyo mkabala na nyumba yake huku akichukua tahadhari ya hali ya juu. Alipoona hamna anayemfuata alishika ukuta wa uzio na kuanza kuparamia kwa juu kisha akachungulia kwa ndani.

Hakuona kitu!

*"Haiwezekani!"* Bon Mtambo aliwaza, na mara akapata akili.

Alidondokea ndani na kufanya kishindo kikubwa kwa makusudi! Baada ya kutua chini, alikimbia kwa kunyata na kujibanza karibu na tangi la maji. Kama alivyotarajia, kijana mmoja aliyegutuka kutoka usingizini alijitokeza huku akinyata! Kijana huyo alitembea kwa tahadhari huku akielekea kule kilikotokea kishindo. Hata hivyo, kabla hajafika kokote Bon Mtambo aliruka hewani na kudondokea sentimita chache kutoka aliposimama huyo kijana! Kabla hajasimama sawasawa aliachia teke kali lililomzoazoa huyo kijana hadi chini. Alijaribu kuinuka ili ajitetee lakini akarudishwa tena chini kwa teke kali la mbavuni, na kufuatiwa na teke lingine akiwa bado hapo hapo chini!

"Tafadhali usiniue!" Huyo kijana alipiga kelele za hofu baada ya kujikuta akichungulia mtutu wa bastola.

"Lazima nikuue, mshenzi mkubwa wee!" Bon Mtambo alifoka.

"Tafadhali mzee naomba unisamehe!"

"Unaitwa nani?" Bon Mtambo alimuuliza huyo mtu.

"Naitwa Ernest Masanja!"

"Umekuja kufanya nini hapa?"

"Tumetumwa kuja kufanya lindo!"

"Mwenzako yuko wapi?"

"Yeye analinda kwa nje!"

"Mwenzako anaitwa nani?"

"Ole!"

"Nyinyi ni walinzi au ni wezi?

"Ni walinzi mzee!"

"Ni wezi!" Bon Mtambo alizidi kumchemsha Masanja.

"Hapana ni walinzi!"

"Ni walinzi wa kampuni gani?"

"ISLIB!"

"Mkubwa wenu wa kazi aliwaambiaje?"

"Alituambia tukiona kuna mtu kaja na kuingia ndani basi tumjulishe!"

"Kwahiyo hata akija mwenye nyumba mtatoa taarifa kwa mkuu wenu!?"

"Alituambia mwenye nyumba amesafiri kwenda China, kwahiyo asingeweza kurudi karibuni!"

"Mkubwa wenu wa kazi anaitwa nani?"

"Joseph Marwa!"

"Anaishi wapi?"

"Sij....!"

Inavyoelekea alikusudia kusema *sijui*, lakini kabla hajamalizia sentensi yake Bon Mtambo alirusha kibao kizito cha uso kilichomfanya Masanja aone nyota!

"Unataka kuniletea utani sio?" Bon Mtambo alifoka.

"Ni kweli sijui mzee!"

"Kwanini unaficha anakokaa bosi wako?"

"Ni kweli mzee, sifahamu."

*Kibao kingine!*

Kibao hiki kilimzoazoa Masanja hadi chini na kumfanya aanze kulia kwa maumivu.

“Nakuambia usiposema ukweli nakuua!” Bon Mtambo alitishia.

“Ni kweli sifahamu mzee!”

Bon Mtambo alianza kuyapima maelezo ya huyu mtu, akagundua alikuwa hajui chochote.

“Ina maana Masanja aliwaambia endapo kuna mtu anakuja msimfanye chochote?”

“Alisema tumjulishe kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu na endapo huyo mtu angeondoka basi tumfuatilie kujua ni wapi anakwenda.”

“Una hakika kwamba yote uliyoniambia ni sahihi? Kama kuna kitu unajua umenidanganya, nakupa nafasi ya kurekebisha maelezo yako sasa kwavile endapo nitagundua mwenyewe kwamba umenidanganya basi sitakua na msamaha kwako hata chembe!”

“Yote niliyokuambia ni ukweli mtupu!”

“Ok! Sasa toa simu yako nikuambie cha kufanya.” Bon Mtambo aliamrisha.

“Leo sijatembea na si...!” Kabla hajamalizia sentensi yake Masanja alijikuta anatweta kwa kipigo huku akiwa amebwaga chini na ngumi nzito toka kwa Bon Mtambo!

“Sikiliza Masanja. Mimi ni mtu mwenye huruma sana, lakini vilevile ni mtu hatari na katili kupita maelezo ninapokutana na mtu anayejifanya jeuri kama wewe!”

“Samahani, sikukusudia kukudanganya!” Masanja alijitetea.

“Sawa, sasa nataka utume ujumbe kwa Marwa kumwambia kuna mtu ameingia ndani! Akikuuliza yupo vipi mwambie ni mwanamke! Usipofanya hivyo nakuua sasa hivi.” Bon Mtambo alitishia huku akiwa ameegemeza mdomo wa bastola kwenye paji la uso la Masanja. Masanja

nae huku akiwa anatetemeka alituma ujumbe kwa Joseph Marwa.

*"Sawa, hakikisheni mnachunguza kuona anafanya nini na akitoka mfuatilieni mjue anaenda wapi. Aidha hakikisheni mnanitaarifa kwa kila jambo ambalo mnahisi si la kawaida."* Joseph Marwa alijibu ujumbe aliotumiwa na Masanja.

"Vizuri, sasa nataka umtumie ujumbe Ole umwambie aje kuna kitu umeona. Hakikisha unatuma kwa namna mnayotumia kuwasiliana." Bon Mtambo alitoa amri nyingine kisha akatoa pingu na kumfunga Masanja mikono na miguu baada ya kuwa ameshatuma huo ujumbe. Baada ya kumfunga pingu na kumnyang'anya simu yake alimwamrisha akae nyuma ya tangi la maji.

Baada ya kama dakika moja unusu kupita alisikia mlio kuashiria kuna ujumbe umeingia kwenye simu yake.

*"Nyoka anaelekea uani!"* Ulikuwa ni ujumbe mfupi kutoka kwa SSP Faraji Zegge.

*"Mwacheni!"* Bon Mtambo alijibu huku akionekana kutabasamu kwa kuona vijana wake wanafanya kazi yao sawasawa!

Baada ya kujibu ujumbe huo, Bon Mtambo aliendа kujibanza kwenye pembe moja ya uzio. Haikupita muda, mara Ole aliparamia ukuta na kudondokea uani lakini kabla hajakaa sawasawa alishitukia akipigwa teke kali la mbavuni ambalo lilimzoazoa hadi chini!

Alijaribu kuinuka lakini akarudishwa tena chini kwa teke kali la tumbo, na lingine la mbavuni na kumfanya atoe ukelele mkali wa maumivu.

"Masanja, nisaidieee!" Ole alipiga kelele

"Nyamaza!" Bon Mtambo alifoka huku akiwa tayari ameelekeza bastola yake usoni kwa Ole.

“Sasa sikiliza Ole, nataka ujibu maswali yangu kwa usahihi kabisa. Ukijibu tofauti na vile alivyojibu Masanja basi nawaua wote hapahapa tena kwa kifo cha kikatili.”

“Masanja yupo wapi? Umemuua?”

“Sijamuua, twende ukamuone!” Bon Mtambo alijibu na kumuongoza Ole alipo Masanja.

“Mwenzako huyu hapa, nakuuliza maswali yaleyale niliyomuuliza Masanja. Majibu yako yakiwa tofauti na mwenzako basi nitajua mnanidanganya hivyo sitasita kuwaua!” Bon Mtambo aliendelea *kupiga mkwara* kwa Ole kisha akaanza kumuhoji maswali yaleyale aliyohoji kwa Masanja. Baada ya kuridhika na majibu yao aliwachukua hadi nje na kumwamuru Inspekta Mussa Ndimbu awapeleke kituo kikuu cha polisi.

“Hao watu wawekwe chini ya ulinzi kwa usalama wao wenyewe. Nitawasiliana na DCI Mwaiswelo kuhusu nini kitafuata! Hata hivyo, wasiojiwe chochote. Aidha, ukishawakabidhi hao watu rudi hapa haraka sana.” Bon Mtambo alitoa maagizo kwa Inspekta Mussa Ndimbu na hapo wakabaki yeye na SSP Faraji Zegge.

“*Bosi, kuna jambo ambalo si la kawaida hapa!*” Bon Mtambo alituma ujumbe mfupi wa simu kwa Joseph Marwa akitumia simu ya Masanja!

“*Si jambo la kawaida?! Jambo gani?*” Marwa alijibu huku akiamini anawasiliana na Masanja.

*“Huyu mwanamke anaonekana kila wakati akiwasiliana na simu, tena inaelekea anawasiliana na watu mbalimbali!”* Bon Mtambo aliendelea kucheza karata yake.

“*Mnhh..!*”Marwa aliguna.

*"Hata hivyo, kilichonitisha si hatua yake ya kuwasiliana na watu kila wakati!"* Bon Mtambo alizidi kumpumbaza Marwa.

*"Ni nini zaidi*!" Marwa aliuliza kwa taharuki.

*"Kama mara mbili au tatu hivi nimemsikia akilitaja jina lako na ISLIB, ingawaje sina hakika kama ni Joseph Marwa wewe au kuna mwingine! Na kutokana na maongezi yenyewe inaelekea kuna mtu anajaribu kumuelekeza ni wapi anakoishi huyo Joseph Marwa!"*

*"What?!"*

*"Ndiyo hivyo bosi"*

*"Ok, mchungeni sana huyo mtu, na mkiona anaelekea kuja huku kwangu basi nijulisheni mara moja!"* Joseph Marwa alituma ujumbe huo huku akiwa amejawa na hofu!

*"Sawa bosi, lakini hatufahamu ni wapi unakaa hivyo itatuwea vigumu kuhisi kama anakuja kwako au hapana!"* Bon Mtambo alitupa karata nyingine muhimu kabisa kwake na kumfanya apoteze utulivu wake wa kawaida wakati akisubiria jibu la swali hili. Ilichukuwa muda mrefu kidogo, lakini hatimae alisikia mlio wa kuashiria kuingia kwa ujumbe mfupi.

*"Mimi nakaa Kitunda. Nyumba yangu ipo karibu na Shule ya Sekondari Kitunda inatazamana na duka la vyakula vya kuku la Interchick. Mbele ya nyumba kuna mwembe uliopanguliwa matawi! Tafadhali endeleeni kumfuatilia kwa karibu*!" Joseph Marwa alijibu na kumfanya Bon Mtambo ashushe pumzi zilizoashiria kupata ahueni.

*"Ondoa shaka bosi, tutakabiliana na hatari yoyote ambayo itataka kuelekea kwako! Kwa sasa endelea kupumzika wakati nasi tunaendelea kumchunga huyu mtu!"* Bon Mtambo alijibu kisha akapiga namba za Inspekta Mussa Ndimbu.

“Sikiliza Inspekta, ukishawaacha hao watu, rudi hapa lindoni haraka sana. Mimi na SSP Faraji kuna mahali tunakwenda!” Alitoa maelezo kwa Inspekta Mussa Ndimbu na kumwelekeza kule wanakoenda ili awafuate endapo ataona wanachelewa kurudi. Baada ya mawasiliano hayo aliingia ndani kwake na kuchukua baadhi ya vitu alivyoona ni muhimu kwa kazi yake. Aliiangalia ile simu aliyonunuliwa na Glory, lakini akaamua kuiacha kwa kile alichoona asije akaipoteza kwenye pilikapilika zake hizi.

“Moja kwa moja Kitunda!” Bon Mtambo alimwamrisha SSP Faraji mara baada ya kuingia garini.

*Kiasi cha robo saa baadae Bon Mtambo na SSP Faraji Zegge walikuwa Kitunda jirani na nyumba ya Joseph Marwa*.

“Sikiliza Inspekta, mimi naingia ndani; wewe baki hapa nje kisha baada ya dakika moja ita jina la Joseph hadi usikie anaitika. Ita kwa namna kama hutaki watu wengine wasikie. Ukishasikia ameitika utakuja ndani mara moja!” Bon Mtambo alitoa maelekezo kwa SSP Zegge na hata kabla hajajibu tayari alikuwa mlangoni na funguo malaya. Aliingiza funguo lakini ikashindikana kwavile funguo zingine zilikuwa zinaning’inia hapo mlangoni kwa ndani!

Ikabidi abadilishe mbinu. Bila kupoteza muda alimwashiria SSP Faraji Zegge amfuate.

“Joseph! Joseph!” Bon Mtambo aliita.

Kimya!

“Joseph!” Alipandisha sauti kidogo.

“Nani?”

“Mimi *muraa*!”

“Nani, Mwita?”

“Ndiyo muraa, njoo mara moja kuna jambo huku nje! Toka na panga *muraa* manake sielewielewi!”Bon Mtambo aliongea katika lafudhi ya Kikulya ili kumteka

akili Joseph Marwa. Aliamini hiyo isingemtia wasiwasi Joseph kwavile eneo hilo linakaliwa na Wakulya wengi! Aidha, aliamini kwamba Marwa asingehisi yeye ni adui kwavile hamna adui ambae angemwambia atoke nje na silaha!

Ilipita kama dakika mbili hivi mara mlango ulisikika ukifunguliwa baada ya kuwashwa taa humo ndani. Kabla mlango hujafunguliwa sawaswa, tayari Bon Mtambo alikuwa ndani na bastola mkononi!

"Inua mikono yako juu, kisha onesha chumba chako! Ukijaribu kuleta ujanja wowote nakumiminia maelfu ya risasi sasa hivi!" Bon Mtambo aliamuru.

"Inspekta, nenda kamlete mke wa Marwa. Hakikisha hafanyi vurugu yoyote." Bon Mtambo alimwamuru SSP Faraji Zegge mara baada ya Marwa kuonesha chumba chake. Haikupita muda, mke wa Marwa alikuja mikono yake ikiwa juu huku mwili mzima ukiwa unatetemeka kwa hofu!

"Sasa sikiliza mama Marwa, tunaondoka na mumeo kwenda kituo cha polisi. Usiwe na wasiwasi, mumeo atarudi uraiani siku si nyingi! Hata hivyo nakuonya kutopiga kelele yoyote kwa sasa. Rudi chumbani kautafute usingizi, nasi tutakuwa hapo nje kwa muda sasa ole wako tukusikie unapiga kelele!" Bon Mtambo alimweleza mke wa Marwa kisha yeye na SSP Faraji wakaondoka na Joseph Marwa hadi garini na kuondoka.

"Sasa sikiliza Marwa, kwa usalama wa maisha yako naomba uyajibu maswali yangu kwa usahihi kabisa. Na endapo utajaribu kunidanganya kwa namna yoyote ile, nakuhakikishia sitasita kukuzawadia kifo chenye mateso makali!" Bon Mtambo alimtisha Joseph Marwa kisha akaendelea: "Nataka uniambie umeajiriwa na kampuni

gani hapa Dar es salaam na kazi yako ni nini kwenye hiyo kampuni?"

"Nimeajiriwa na kampuni ya ulinzi ya ISLIB kama *Site Manager*! Kazi yangu ni kupangia askari sehemu za kwenda kulinda."

"Una uhakika na ulichokisema?"

"Ndiyo mheshimiwa!"

"Nani anakaa na daftari la orodha ya walinzi wanaopangiwa vituo vya kazi?" Bon Mtambo aliuliza kwa kujiamini kabisa kana kwamba ana uhakika wa kuwapo kwa daftari la namna hiyo!

"Daftari nakaa nalo mwenyewe ofisini ili kukagua endapo walioenda lindoni wamerudi salama!"

"Ernest Masanja na Ole wamepangiwa kulinda nyumba au ofisi gani?"

"Wao wapo Chang'ombe kwa Ramesh Patel!" Marwa alijibu na kusababisha hali ya mshangao kwa Bon Mtambo!

"Una uhakika kwamba wanalinda kwa Ramesh Patel?"

Kimya!

"Una hakika kwamba nyumba uliyowapangia kulinda ni ya Patel?" Bon Mtambo aliuliza kwa ukali.

"Mimi ndivyo nilivyoambiwa!" Marwa alijibu!

"Ulivyoambiwa na nani?"

"Na Bosi Batenga!"

"Jina kamili la huyo Batenga ni nani?" Bon Mtambo alizidi kuhoji.

"Ni Crispin Nicolous Batenga!"

"Na yeye ni nani katika ISLIB?"

"Ni CSO, yaani *Chief Security Officer*!"

"Kwanini uliwaagiza akina Masanja wachunguze kila anayeingia kwenye nyumba ya Patel?"

"Kutokana na maelezo ya Batenga, Patel anajihusisha na biashara ya madawa ya kulevya. Hata hivyo, haijafahamika anashirikiana na nani na ndio maana tuliagizwa kuchunguza watu wote wanaoingia hapo."

"Lakini hiyo si kazi ya polisi, ilikuwaje mfanye nyinyi ambao ni kampuni ya ulinzi ?"

"ISLIB ni kampuni ya ulinzi na uchunguzi!"Marwa alijibu huku ikionekana hofu yake imepungua.

"Ni wapi anakokaa Batenga?"

Kimya!

"Nakuuliza ni wapi anakokaa Batenga?" Bon Mtambo aliuliza kwa ukali huku akimgongagonga kichwani kwa kutumia mtutu wa bastola.

"Si..si..sifaha...!"

Joseph Marwa alijikuta akigalagala chini baada ya kupigwa kofi kali la usoni kabla hajamalizia sentensi yake!

"Joseph, huwa sipendi masihara kwenye kazi. Mimi ni mtu katili ile mbaya ninapokutana na mtu jeuri kama wewe!" Bon Mtambo aliongea huku akionesha wazi kukasirika!

"Samahani mkuu!" Marwa alijibu kwa hofu akiwa bado hapo hapo chini.

"Niambie ni wapi anakoishi Batenga!"

"Anakaa Ilala Mtaa wa Arusha nyumba namba IL/Ar/20BT."

Baada ya kutaja nyumba anayoishi CSO Batenga, Bon Mtambo aliendelea kuhoji maswali kadhaa ambayo yalimfanya aridhike kabisa kwamba Marwa nae si miongoni mwa watu muhimu sana kwenye sakata hili.

"Ndiyo, anatumia gari dogo aina ya Suzuki Escudo,

rangi ya bluu yenye namba T.103 XXL!" Marwa alijibu baada ya kuulizwa gari inayotumiwa na Batenga.

"Sasa sikiliza Joseph, mimi na wewe tunatoka hapa hadi kituo cha polisi kwa mahojiano zaidi. Aidha, tunakupeleka huko kwa usalama wako wewe mwenyewe kwavile wakigundua tumekuhoji bila shaka watakuua!"Bon Mtambo alimalizia kisha akamwamuru SSP Faraji Zegge kuendesha gari hadi Kituo Kikuu cha Polisi ambako Marwa aliunganishwa na akina Ole.

Baada ya kuacha maagizo hapo polisi, Bon Mtambo aliangalia saa yake ya mkononi na kukuta inakaribia saa saa kumi kasorobo alfajiri.

"Sikiliza SSP Faraji, nenda nyumbani kapumzike kidogo, huenda kesho tukawa na kazi nyingi na pengine za hatari zaidi."

Baada ya maagizo hayo, Bon Mtambo alimpigia simu Inspekta Mussa Ndimbu na kumwambia nae akapumzike, kisha nae aliondoka na kwenda nyumbani kwake Chang'ombe! Pamoja na mambo mengine, aliamini huenda majahili wangekuja kuchunguza baada ya kuona Ole, Masanja na Marwa hawatokei!

# 10

Ilikua inakaribia saa kumi na mbili unusu asubuhi wakati Bon Mtambo alipowasili Ilala anakoishi Crispin Batenga. Alifikia kwenye baa moja jirani na hapo na kuagiza supu ya nyama ya mbuzi. Akiwa anajiburudisha na supu hiyo, mtu mmoja aliyemshuku kuwa ni Batenga alitokeza. Ili apate uhakika, alichukua simu yake na kuweka kadi ya simu *(simcard)* maalumu kisha akapiga namba ya Batenga! Kama alivyotarajia, Batenga alipokea simu lakini hata hivyo Bon Mtambo hakuongea chochote!

Alitulia hapo kwa muda hadi alipomwona Batenga akiingia kwenye gari na kuondoka kisha nae akaondoka na kwenda Chamanzi alikorudi na gari aina ya *Coaster Minibus* na kuanza safari ya kurudi nyumbani kwake Chang'ombe. Akiwa anaendesha kwa tahadhari kubwa kwavile alishakaribia kwake, aliweza kuiona gari moja aina ya Land Rover 110 ya polisi ikiwa inaegeshwa upande wa pili wa barabara. Muda mfupi baadae, vijana wawili waliteremka na kwenda upande wa pili wa nyumba yake! Huku akijionesha kutovutiwa na gari hiyo, Bon Mtambo aliipita kwa mwendo wa taratibu huku akitabasamu kutokana na mbinu waliyoitumia. Hakutaka kabisa kuamini kwamba watu wale ni polisi!

Baada ya kusimamisha gari, aliteremka na kuingia uvunguni mwa gari hiyo kisha akajifanya analikagua lakini huku akili yake yote ikiwa kule ilikoegeshwa gari ya *polisi*! Punde si punde aliwaona wale vijana wakirudi kwa haraka

na kwenda kuongea na mwenzao aliyekuwa kwenye gari kisha wote wakaondoaka kurejea kwenye nyumba ya Bon Mtambo. Bila kupoteza muda aliwafuata kwa mwendo wa mnyato na kukuta mtu wa mwisho akimalizia kuruka ukuta na kuingia ndani. Kabla hajawapa nafasi ya kujipanga huko ndani, Bon Mtambo alishika ukuta na kurukia ndani na bastola mkononi!

“Wote mikono juu!” Bon Mtambo aliwaamrisha, kisha akawauliza kwa sauti ya kipolisi: “Nyinyi ni nani na mmekuja kufanya nini hapa?”

Lilikuwa ni tukio la ghafla mno, lililotokea mithili ya mchezo wa sinema!

“Sisi ni askari polisi, na wewe ni nani na umekuja kufanya nini hapa?” Aliyeonekana ndie kiongozi wa kundi alijibu kijeuri!

“Mmetumwa na nani?”Bon Mtambo aliuliza tena.

“Sio juu ya..!” Huyo mtu alitaka kujibu kijeuri tena lakini kabla hajamalizia sentensi yake alipelekwa chini kwa teke kali la tumbo kutoka kwa Bon Mtambo. Alijaribu kuinuka lakini kabla hajakaa sawasawa alirudishwa na teke lingine la mbavuni na kufuatiwa na lingine la kichwani na kumfanya mtu huyo kutoa ukelele wa maumivu!

Kuona hivyo, mwenzake mmoja alichomoa bastola yake lakini lilikuwa ni tukio ambalo tayari lilishaotewa na Bon Mtambo! Kabla hajafanya chochote, Bon Mtambo aligeuka kwa kasi na kuupiga teke mkono ulioshika bastola; nayo ikapaa hewani na kwenda kudondokea pembeni mwa jahiri wa kwanza! Jahili huyo aliiwahi bastola hiyo na kuachia risasi mbili mfululizo ambazo moja kwa moja zilienda kuvunja kiuno cha mwenzake baada ya Bon Mtambo kuwahi kujiviringisha! Mwenzake huyu ni

yule ambae muda wote alikuwa bado amesimama akishangaa ikielekea alikuwa bado hajafahamu ni nini hasa kinatokea!

"Pumbavu, utanitambua mimi ni nani na kwanini IBU ilinipa ukamanda!" Huyo mtu alimaka na kwenda kumvaa Bon Mtambo akiwa bado na bastola yake mkononi. Wote wawili walidondoka chini na kuanza kubiringishana huku Bon Mtambo akiwa ameukamata mkono uliokuwa umeshikilia bastola!

*Sasa ikawa ni kunyang'anyana bastola!*

Wakiwa bado wananyang'anyana, mara yule jahili mwingine alikuja kwa kasi ili amvamie Bon Mtambo hapo chini. Hata hivyo alikosea mahesabu, kwani bila kutarajia Bon Mtambo alijikunja na kupiga teke kali kwa nyuma ambalo lilimzoazoa huyo mtu na kwenda kumtupa mbali. Tukio hili la haraka lilimfanya jahili mwenye bastola mkononi kukumbwa na mchecheto wa ghafla na hivyo kuufanya mkono wake kuondokewa umakini na kuruhusu kuiachia bastola yake kwa Bon Mtambo. Baada ya kuipokonya bastola hiyo, alimpekua sehemu zingine na kumpokonya bastola aliyokuwa ameificha kiunoni!

"Wote mikono juu na mkikaidi sitachelea kuvifumua vichwa vyenu sasa hivi!" Bon Mtambo aliamrisha kwa ukali!

"Narudia tena, nyinyi ni nani?"

"Polisi!" Yule jamaa alijibu tena kwa jeuri!

"Kuna jeshi la polisi Tanzania linaloitwa IBU?!" Bon Mtambo aliuliza na kumgutusha jamaa ambae awali alishajigamba kwamba yeye ni kamanda wa IBU!

"Kuna jeshi la IBU hapa nchini?!" Alirejea swali lake!

Kimya!

“Nazani nyinyi ni jeuri, hivyo ombeni sala zenu za mwisho kabla sijawafumua kwa risasi!” Bon Mtambo alitishia lakini hamna yeyote aliyeshituka! Kwa jinsi ilivyo, mwanaume yeyote anapotoa kitisho basi anataraji kitisho hicho kimtishe mlengwa vinginevyo inaumiza sana! Suala la *mkwala* wake kuonekana ni kama *kumtishia mtu mzima nyau* lilimkasirisha sana Bon Mtambo! Kwa kasi ya umeme, alifyatuka na kwenda kumshindilia yule jeuri ngumi tatu mfululizo ambazo moja kwa moja zilimng’oa meno mawili ya mbele! Na kwa kasi ileile alimvutia kwake na kumpeleka chini kwa kichwa kizito kilichovunja mshipa wa pua! Ilionekana kipigo hiki ni kama onyo toka kwa ziraili kwa huyu jahili mwingine kwani bila kutarajia, alianza kutimua mbio lakini kabla hajafika kokote alidakwa na kusindikizwa na ngumi mbili nzito zilizotua kwenye koromeo lake! Taratibu, uwezo wake wa kuvuta hewa ukapungua; sekunde chache baadae ukapotea kabisa na bila kutaka akapoteza fahamu hapohapo!

Baada ya kuona wote wako chini, Bon Mtambo alikoki bastola yake na kumwelekezea yule jahili aliyeonekana kuwa ni jeuri zaidi!

“Tafadhali usini....!” Kabla hajamalizia sentensi yake Bon Mtambo aliachia risasi na kukata vidole viwili vya mkononi na kulifanya jahili kupiga kelele za maumivu!

“Lazima nikuue kwa sababu ni jeuri!”

“Tafadhali, nipo tayari kukueleza kila kitu!”

“Ok! Niambie unaitwa nani na umetumwa na nani?”

“Naitwa Mashaka na nimetumwa na Ngosha!”

“Ngosha ni nani?”

“Kamanda wa IBU!”

“Ni nani hao IBU?”

“Kwakweli sifahamu kiu...!” Kabla hajamaliza, Bon Mtambo alitumia kitako cha bastola kumpiga nacho Mashaka kwenye mgongo wa pua yake ambayo tayari ilikuwa inachuruzika damu!

“Ni kweli sifahamu!” Alijibu na kumfanya Bon Mtambo aendelee kukandamiza pua yake hali iliyomfanya aendelee kupiga kelele za kuomba kuachiwa!

“Haya niambie ukweli!”

“IBU huwa inawatengenezea kashfa vigogo mbalimbali na baadae kuzitumia kashfa hizo kuwalazimisha kutekeleza matakwa ya IBU endapo watataka siri ya kashfa hizo zisitolewe hadharani!

“Nini kirefu cha IBU?”

*“International Blackmail Unit.”*

“Haya, sasa nitajie orodha ya watu ambao mmewahi kuwatengenezea kashfa!”

“Binafsi yangu nimewahi kuhusika mara moja tu, hivyo kama kuna orodha nyingine siifahamu!” Mashaka alijibu akiwa na hofu ya kutoaminika!

“Umehusika kwenye kashfa ya nani na anafanya kazi gani?”

“Namfahamu kwa jina moja tu; anaitwa Jonas na ni ofisa wa juu wa TAKUKURU” Mashaka alijibu kwa hofu.

“Hebu niambie, ilikuwaje!” Bon Mtambo aliuliza na kumfanya Mashaka aanze kusimulia tukio zima la Jonas kufanya mapenzi na wasichana wadogo kwa Babu Linjembwa!

“Sasa hapo lengo lenu lilikuwa nini?” Bon Mtambo aliuliza baada ya kugutuka toka kwenye mshangao uliotokana na simulizi ya Mashaka ingawaje hakutaka kuuonesha wazi mshangao wake!

"Kwakweli siwezi kufahamu kwavile sisi tuliagizwa tu na sina hakika endapo huyu Jonas alishawahi kufuatwa tena au hapana ingawaje lazima atakuja kufuatwa tu!"

"Mlitumwa na nani?!"

"Ngosha!"

"Pamoja na wewe, kulikuwa na nani tena!"

"Masumbuko, Nkuba na Wendy!"

"Je, unaifahamu kampuni inayoitwa ISLIB?"

"Ndio naifahamu!"

"Je, kuna uhusiano gani kati ya ISLIB na IBU?"

"Sizani kama kuna uhusiano wowote. ISLIB ni kampuni inayofahamika na kuheshimika wakati IBU ni kundi tu la kijambazi linalofanya kazi zake kwa kukodiwa!" Mashaka alijibu kwa kujiamini kwavile ni kweli hakufahamu endapo IBU na ISLIB ni kitu kimoja! Hii ilitokana na mkakati wa kutenganisha kazi za ISLIB na IBU!

"Je, unamfahamu mtu yeyote anayefanya kazi ISLIB?" Bon Mtambo aliendelea kuhoji.

"Hapana!"

"Je, unamfahamu mtu anayeitwa Crispin Batenga?"

"Ndio namfahamu!"

"Kwa mara ya mwisho umeonana nae lini?"

"Hata leo asubuhi nimemuona!"

"Wapi?"

"Nilimuona akitoka nyumbani kwa Ngosha ambako alienda kumweleza kuwasili kwa mzigo wake bandarini!"

"Ina maana Batenga anafanya kazi bandarini?"

"Ndio!"

Bon Mtambo aliendelea kumuhoji Mashaka maswali kadhaa ikiwa ni pamoja wanakokaa akina Wendy na baada ya kuridhika na mahojiano yao, alitoa pingu na kuwafunga wote wawili kisha akawaita akina SSP Faraji Zegge.

“Sasa sikilizeni, hawa watu wakawekwe chini ya ulinzi mkali sana hadi nitakapotoa maagizo mengine hapo baadae. Aidha, baada ya hapo mtarudi hapa mara moja kuna kazi muhimu tunatakiwa kuifanya kabla ya saa nne asubuhi hii!” Bon Mtambo alitoa maagizo kwa SSP Faraji Zegge na mwenzake mara walipowasili.

Baada ya SSP Faraji Zegge na Inspekta Ndimbu kuondoka, yeye aliingia ndani na kuwasha kompyuta yake ya mezani na kuanza kuandika:

**TAARIFA KWA VYOMBO YA HABARI:**

Ndivyo alivyoanza kuandika taarifa hiyo, kisha akaendelea:

*Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es salaam linawashikilia watu watatu wanaohisiwa kuwa ni washirika wa Bon Mtambo; Mtanzania anayetuhumiwa kujihusisha na ugaidi pamoja na usafirishaji wa madawa ya kulevya.*

*Miongoni mwao, mtuhumiwa aliyetambuliwa kwa jina la Joseph Marwa yupo mahututi hospitali ya jeshi akiwa chini ya ulinzi mkali wa polisi na wanajeshi wa JWTZ. Joseph Marwa alipigwa risasi tatu baada ya kujaribu kuwatoroka polisi pale walipoanza kumhoji! Marwa alikutwa na mkasa huo baada ya kuruka toka kwenye gari ya polisi na kuanza kukimbia kabla hajajibu chochote cha maana! Hata hivyo, kabla Joseph Marwa hajapigwa risasi alimtaja mtu mwingine kwa jina moja la Crispin ambae bado haijafahamika uhusiano wao. Aidha, pamoja na Joseph Marwa, wengine waliokamatwa wametambuliwa kama Ernest Masanja na Ole.*

*Wakati huohuo, polisi wameanza kufuatilia taarifa kwamba Ole, Masanja na Marwa ni waajiriwa wa kampuni moja ya ulinzi hapa jijini ili kuona endapo kampuni hiyo nayo inahusika kwa namna moja au nyingine.*

*Katika tukio lingine, majambazi yenye silaha yamevamia kituo cha mafuta na kufanikiwa kupora kiasi cha pesa ambacho hadi sasa hakijafahamika. Katika tukio hilo, polisi waliokuwa doria walifanikiwa kumuua kwa risasi jambazi mmoja, mwingine amejeruhiwa vibaya na wengine waliwahi kutoroka kabla hawajakamatwa. Jambazi aliyejeruhiwa amefahamika kwa jina moja la Mashaka na hivi sasa nae yupo kwenye chumba cha wagonjwa mahututi. Pamoja na hayo, polisi wanachunguza ili kufahamu mmiliki halali wa gari iliyokuwa inatumiwa na majambazi hayo ambayo ina namba za jeshi la polisi. Uchunguzi wa awali umeonesha gari hilo si miongoni mwa magari yanayomilikiwa na jeshi la polisi.*

**IMESAINIWA NA MKURUGENZI WA UPELELEZI WA MAKOSA YA JINAI NCHINI.**

Baada ya kuandika taarifa hii na kuihifadhi, aliwasha kifaa maalumu cha mawasiliano.

*"Drop two eagles in hurry!"* Bon Mtambo aliutuma ujumbe huu kwenda WIBAIC ukimaanisha kuhitaji msaada wa makachero wawili atakaoshirikiana nao.

Baada ya hapo, alifanya maandalizi muhimu kwa ajili ya kuanza kazi na baada ya muda mfupi SSP Faraji Zegge na Inspekta Mussa Ndimbu walirejea kisha akawaamuru waingize gari ya akina Mashaka uani. Waliichukua maiti ya mwenza wa akina Mashaka wakaiingiza mbele na kuikalisha kwenye kiti ya abiria!

"Sasa sikilizeni, Inspekta Mussa utondoka na gari mliyotoka nayo kituoni kisha utaelekea NasOil Ltd iliyopo barabara ya Mandela na utajifanya unataka kujaza mafuta. SSP Faraji utaondoka na hiyo gari ndogo halafu utanifuata mimi nyuma nyuma. Tukifika NasOil, nitawalaza usingizi kwa kipigo walinzi wa pale kisha nitapora pesa na wewe

utakuwa unarusha risasi hewani kuwazuia wananchi. Angalia, usije kuwajeruhi raia wasio na hatia. Nikishachukua hizo pesa nitarudi kwenye Land Rover ya akina Mashaka na hapo Inspekta Mussa utaanza kuishambulia kwa risasi sehemu tutakayokuwa tumemkalisha yule marehemu ambae wakati huo nitakuwa tayari nimeshamkalisha kwenye kiti cha dereva. Baada ya hapo mimi nitaruka na kuingia kwenye gari ya SSP Faraji Zegge atakayekuwa ananisubiri kisha ataiondoa kwa kasi! Hata hivyo, tunatakiwa kuwa makini sana kwavile tukifanya kosa ama tutauawa sisi au tutawaua raia wasio na hatia. Na kwavile Inspekta Mussa tutakuacha hapo NasOil, wewe utakuwa na wajibu wa kushughulika na mambo mengine yatakayofuatia hapo. Jambo la msingi kwako kukumbuka ni kwamba majambazi wamefanikiwa kutoroka nawe umefanikiwa kumuua mmoja wao! Vilevile hakikisha kwamba hutoi nafasi ya watu kuwahi kumchunguza marehemu hadi wakagundua kwamba hakuuawa kwenye tukio hilo. Aidha, baada ya tukio hilo utaiwaisha maiti Muhimbili na wewe utarudi hapa mara moja kuendelea na uchunguzi. Ni matumaini yangu kwamba watakuja tena kuchunguza baada ya kuona kwa mara nyingine akina Mashaka nao wameshindwa kurejea!" Bon Mtambo alimalizia maelekezo yake .

Baada ya kufanya tukio la uhalifu bandia kwenye kituo cha mafuta cha NasOil Bon Mtambo alifanya haraka kwenda kwa DCI Mwaiswelo ili kumpatia ile taarifa aliyoiandika kwa ajili ya vyombo vya habari.

“Nikusaidie nini kijana, na kwanini umeingia ofisini kwangu kienyeji?” DCI Mwaiswelo alifoka baada ya kuona mtu asiyemfahamu ameingia ofisini kwake bila kugonga!

“Samahani mzee, WIBAIC TZ One!” Bon Mtambo alijitetea na kumfanya DCI Mwaiswelo kugutuka na kuangua kicheko. Dakika chache alizotumia kujifanyia marekebisho madogo, zilitosha kabisa kumpumbaza DCI Mwaiswelo. Bila kupoteza muda, Bon Mtambo alichukua taarifa aliyoiandika na kumpatia DCI Mwaiswelo.

“Nini maana ya hii taarifa kijana?!” DCI Mwaiswelo aliuliza mara baada ya kumaliza kuisoma.

Bon Mtambo nae alitumia fursa hiyo kuelezea mkasa mzima tokea jana usiku na asubuhi hiyo.

“Hivyo basi, kwa taarifa hii nazani wahusika hawatashuku kwamba tayari tumeanza kuwatilia mashaka. Aidha, nimeamua kuonesha kwamba Marwa alipigwa risasi na yupo mahututi kabla hajaojiwa ili waendelee kuamini kwamba bado vyombo vya dola havijapata fununu ya kutosha kuhusu Batenga. Vilevile naamini taarifa kwamba majeruhi wapo Lugalo chini ya ulinzi mkali wa jeshi itawatisha kwenda huko kama wangefikiria kutaka kupeleleza! Hata wakienda, hawatakuwa wabishi endapo wataambiwa wapotee eneo hilo. Hata hivyo, kule Lugalo nitaweka vijana wawili sehemu ya mapokezi na kazi yao itakuwa ni kujua ni nani ataenda kufuatilia habari za majeruhi hao.” Bon Mtambo alifafanua.

“Nimekuelewa kijana, labda kama unahitaji msaada mwingine kutoka kwangu!”

“Ni kweli mzee, ningependa nipate vijana watatu wenye uwezo mkubwa kabisa wa kuweza kumfuatilia mtu! Vilevile usisahau kwamba kesho ni siku yangu ya kupelekwa Mahakamani!”

“Ondoa shaka, tunao vijana waliofuzu kwa kiwango cha juu na ambao wameshapata kufanya kazi na Interpol! Miongoni mwao, nitakupatia Kinyonga na Kifa Uwongo!” DCI Mwaiswelo alieleza kisha wote wakaangua kicheko baada ya kutaja majina ya Kinyonga na Kifa Uwongo!

Kinyonga na Kifa Uwongo ni majina ya utani ya Daniel Chacha na mwenzake Fareed Mwinyimkuu ambao licha kwamba wanafanya kazi idara moja lakini vilevile ni marafiki wakubwa. Inasemekana urafiki wao umechangiwa zaidi na wao kupenda zaidi watoto wa kike, huku wote wakivutiwa zaidi na watoto wa kike wenye maumbo makubwa! Simulizi kuhusu vijana hawa zinaendelea kueleza kwamba kuna siku Kinyonga, ama Daniel Chacha alikumbana na mwanamke ambae licha ya kwamba ana umbo kubwa lakini mambo yake ni makubwa pia! Hili lilithibitika baada ya kumfanya kijana wa DCI Mwaiswelo kuugua kwa karibu siku tatu! Aidha, kuna simulizi inayofanana na hiyo kwa Fareed Mwinyimkuu, lakini ukitaka kuifahamu zaidi basi nitafute kwa muda wako nikung’ate sikio!

Pamoja na yote hayo, majina yao haya ya utani yalitokana na umahiri wao katika kumfuatilia mtu! Inasemekana kwamba Daniel, au Kinyonga ana uwezo wa kumfuatilia mtu mwaka mzima bila kugundulika na hata pale utakapofanikiwa kumgundua alikuwa na uwezo wa kujibadilisha kwa haraka kutoka hali iliyomfanya atiliwe shaka hadi hali ya kuonekana ni mtu wa kawaida!

Baada ya muda mfupi, aliingia Inspekta Daniel Chacha, Inspekta Fareed Mwinyimkuu na msichana mrembo aitwae Inspekta Cecy. Huyu Inspekta Cecy alikuwa ni mrembo kwelikweli kiasi cha kukaribia kuivuruga akili ya Bon Mtambo!

“Sasa na wewe Inspekta Cecy kilichokufanya kujiingiza kwenye kazi za hatari kama hizi ni nini?” Bon Mtambo alitania mara baada ya kumaliza kuusoma wasifu wa Inspekta Cecy na kuwafanya wote kuangua kicheko!

Hakika vijana hawa walionekana ni wenye furaha zaidi baada ya kupata fursa hii adimu ya kufanya kazi na Bon Mtambo. Ni watu wachache sana Tanzania waliopata angalau bahati ya kufahamu machache kuhusu Bon Mtambo. Hivyo, kufanya nae kazi ilikuwa ni bahati kubwa ambayo ingewafanya kuboresha wasifu wao wa kazi.

“Sasa sikilizeni, Daniel na Fareed baadae mtaenda kupiga kambi pale ofisi za ISLIB na kuratibu kila kinachotokea. Mtaenda baada ya mimi kumaliza kazi zangu hapo na nitawajulisha punde nitakopomaliza ili nanyi mkazibe nafasi. Hata hivyo, mtafika pale kila mtu kivyake na atashughulika kivyake. Na inapotokea kuna mtu mnamshuku kiasi cha kutaka kumfuatilia nje ya hapo, basi hakikisheni mmoja anabaki ili aendelee na uratibu wa hali ya hapo. Aidha, SSP Faraji Zegge utafuatilia nyendo za Jonas, wakati Inspekta Cecy kuna kazi itabidi nimpatie pale......!” Kabla hajamalizia, mara simu yake ya mkononi iliita. Namba hii aliitumia wakati huu tu wa kazi hivyo kila ilipoita alijikuta mwili ukimsisimka! Alipoangalia, alikuta ni Inspekta Mussa Ndimbu !

“Ndiyo, nakupata Inspekta!”

“Toyota Escudo, T.103 XXL rangi ya bluu eneo la tukio!” Inspekta Ndimbu alimweleza Bon Mtambo na kumfanya asisimke kwani gari aliyotajiwa ni ya Batenga!

“Sasa sikiliza, akiondoka mfuatilie lakini hakikisha unaniambia mapema barabara atakazokuwa anapita!” Bon Mtambo aliongea na kukata simu.

“Tumemaliza maongezi hivyo kila mmoja ajiandae na kazi kwa kwenda kufanya kile nilichompangia. Inspekta Cecy, nifuate kwani kazi yetu inaanza sasa hivi! Aidha, Daniel na Fareed kaanzeni kazi yenu pale ISLIB sasa hivi kwavile kazi iliyotaka kunipeleka hapo ndio hii ninayoenda kuifanya sasa!” Bon Mtambo alimalizia.

“Sikiliza Inspekta Cecy, hapo maegesho ya Avalon kuna gari aina ya Nissan Safari rangi ya bluu namba T.550 XRT. Mimi nitakuwa kwenye Toyota Hilux Double Cabin nyekundu namba T.125 XGH. Tukitoka hapa, mimi nitaenda moja kwa moja hadi barabara ya Nyerere. Wewe utanifuata kwa nyuma huku ukihakikisha hamna anayejua kwamba tupo safari moja. Maelezo mengine nitakuwa nakupatia kadri safari inavyoendelea!” Bon Mtambo alitoa maelekezo kwa Inspekta Cecy kisha safari ikaanza.

Wakati Bon Mtambo anakaribia mzunguko wa Gerezani simu yake iliita, na alipoangalia namba ilikuwa ni ya Inspekta Mussa Ndimbu.

“Ni hivi mkuu, jamaa anaelekea mitaa ya Temeke.”

“Sawa Inspekta, endelea tu kumfuatilia!”

Baada ya kushika tu Barabara ya Nyerere Bon Mtambo aliarifiwa kuwa Batenga ameingia Barabara ya Mandela akiwa anaelekea TAZARA.

“Kazi nzuri Inspekta, sasa unaweza kuachana nae kwavile nishafahamu ni wapi anakoenda. Wewe rudi kisha kachunguze pale NatPrinters ili ufahamu ni wapi anakoishi Mhariri Mkuu wa gazeti la Nuru Yetu.”

Baada ya maagizo hayo, Bon Mtambo aliendelea kukanyaga mafuta ili akamuwahi Batenga eneo la

TAZARA. Kila wakati alikuwa anajaribu kuangalia nyuma ili amuone Inspekta Cecy lakini hakumuona! Wakati anaingia TAZARA, aliweza kuiona gari ya Batenga ikiendelea kukanyaga lami ambapo sasa walitenganishwa na gari tatu katikati yao. Safari ya Batenga iliendelea na kuishia nyumbani kwa Ngosha. Bon Mtambo aliinyatia nyumba ya Ngosha baada ya kuwa ameegesha gari yake mita kadhaa kutoka hapo. Aliangaza huku na huko na aliporidhika na usalama alinyata hadi dirishani!

"Ngosha, kwa jinsi ilivyo inaelekea wale vijana watakuwa wamekamatwa au wameuawa. Ni bora kama watakuwa wameuawa, lakini kama wamekamatwa basi bila shaka nawe utakamatwa tu. Ikitokea umekamatwa, basi usinitaje nami nitafanya kila liwezekanalo hadi unaachiwa. Kumbuka kwamba, kazi niliyokutuma ni ya wakubwa fulani hapa jijini hivyo kunitaja mimi itamaanisha ni kuwataja au kuwaumbua hao wakubwa. Na kwavile mimi nimetumwa tu na hao wakubwa basi ni wakubwa hao hao watakaotumia uwezo wao kukuokoa!" Bon Mtambo alimsikia Batenga akimweleza Ngosha.

"Ondoa hofu Batenga, bado ni mapema mno kuanza kukata tamaa."

"Sawa Ngosha, mimi naondoka lakini usisite kuniarifu pindi utakapogundua jambo lolote la maana."

Maongezi ya Batenga na Ngosha yalimwacha Bon Mtambo njia panda! Awali aliamini wote ni washirika wanaofanya kazi pamoja lakini maongezi yao yalionesha si wamoja hata kama wanacheza mchezo mmoja!

"*Sizani kama kuna uhusiano wowote. ISLIB ni kampuni inayofahamika na kuheshimika wakati IBU ni kundi tu la kijambazi linalofanya kazi zake kwa kukodiwa*!" Bon Mtambo aliyakumbuka maneno ya Mashaka wakati alipomhoji!

Bila kupoteza muda zaidi, alienda kujibanza mlangoni na Batenga alipoufungua tu alirudishwa ndani kwa ngumi kali ya shingo! Kufumba na kufumbua Bon Mtambo alikuwa tayari ndani na bastola yake mkononi!

"Wote mikono juu!" Bon Mtambo aliamrisha. Huku akionekana kutawaliwa na hofu, Batenga aliinua mikono yake lakini Ngosha alifanya kama hajasikia!

"Inua mikono yako juu Ngosha, ukijifanya kiburi nitakumiminia risasi kama nilivyofanya kwa Mashaka!" Bon Mtambo alifoka!

"*What*?(nini?) Umemuua Mashaka?! Pumbavu!" Ngosha aliongea kwa hasira na kwenda kumvamia Bon Mtambo, tukio ambalo tayari Bon Mtambo alishalinusa kabla na kufanikiwa kumkwepa! Kwavile alimwendea kwa kasi, Ngosha alijikuta anakula mwereka na alipojaribu kuinuka alipigwa ngumi tatu mfululizo ambazo zilimrudisha tena chini. Hapo hapo Bon Mtambo alijigeuza kwa haraka na kumfuata Batenga na kumshushia ngumi nzito ya shingoni ambayo ilimpeleka hadi chini!

"Kwanini umemuua Mashaka?" Hatimae Ngosha aliuliza kwa hasira.

"Nimemuua kwa sababu ni mshenzi, nawe ukiendelea na ushenzi wako sitachelea kukumiminia risasi kama mwenzako!" Bon Mtambo alijibu kwa kejeli, kisha akaendelea, "Sasa sikilizeni, nataka kila mmoja ayajibu maswali yangu kwa ufasaha kabisa bila kupindapinda!" Bon Mtambo alieleza na mara akahisi jambo baada ya kumuona Ngosha akiangalia dirishani kwa jicho la kuibia! Hali hiyo ikamfanya Bon Mtambo ageuke. Hilo likawa kosa kubwa kwani kabla hajarudisha akili yake alijikuta akirukiwa na kutandakikwa ngumi mzito ya mbavu iliyomfanya ajikunje kwa maumivu. Kabla hajakaaa sawa,

Ngosha alijirusha juu na kuachia pigo kali la kichwa ambalo nalo lilimzoazoa Bon Mtambo hadi chini. Alipoinua kichwa chake akajikuta akitazama ndani ya mtutu wa bastola ya Batenga!

"Sasa ni zamu yako kujibu maswali yetu!Wewe ni nani na umekuja kufanya nini?" Batenga aliuliza kwa kejeli!

"Naitwa Bon Mtambo, mpiganaji wa WIBAIC na nimo kazini kuliangamiza kundi la kijahili linaloongozwa chini ya mwavuli wa IBU na ISLIB!" Bon Mtambo alijibu kwa kujiamini hali iliyomfanya Batenga aonekane wazi kwamba ameshitushwa na kauli hiyo! Alichofahamu yeye ni kwamba bado Bon Mtambo anashikiliwa na vyombo vya dola! Kabla ya hapa, hakuwahi kumfahamu mtu huyu!

"Unazani utaweza?" Ngosha aliuliza kwa kejeli.

"Nimewaweza wanaume itakuwa mashoga kama nyi...!" Bon Mtambo alijibu kwa kejeli lakini kabla hajamalizia sentensi yake alishtukia akipigwa teke zito la mbavuni lililomfanya ajipinde kwa maumivu. Akiwa bado amejipinda, ghafla alifyatuka kama umeme na kuipiga teke bastola ya Batenga ambayo ilipaa hewani na kudondokea meta chache toka hapo. Kwa kasi ileile, alijigeuza kwa haraka na kumtwanga teke la ubavu Ngosha na kufuatia na lingine la tumbo lililomfanya asujudu sakafuni!

Kuona hivyo, Batenga aliikimbilia bastola yake lakini kabla hajaitia mikononi alipigwa teke zito la shingoni lililomfanya apepesuke na kwenda kujipigiza mezani. Alimwendea hapo mezani lakini ghafla Batenga alichukua kiti na kukirusha kwa nguvu zake zote! Kwa bahati, Bon Mtambo alikiona, hivyo kikapitiliza na kwenda kumbamiza Ngosha aliyekuwa akijiandaa kuinuka sakafuni!

“Unafanya nini Batenga!” Ngosha alipiga kelele baada ya kiti kumpata sawasawa kichwani na kusababisha avuje damu nyingi!

Wakati Batenga akiwa bado katika hali ya kiwewe, alishitukia akitandikwa kichwa kizito kilichomfanya anyong’onyee na kujibwaga chini kwa kishindo!

Hapo hapo akapoteza fahamu!

Kuona hivyo, Bon Mtambo aligeuka kwa kasi na kumkabili Ngosha aliyekuwa akijitahidi kujiinua hapo chini huku damu zikiendelea kumtoka. Kabla hajainuka sawaswa, aliinuliwa na kutishiwa kama anapigwa ngumi ya utosini. Ngosha alijaribu kuikwepa ngumi hiyo kwa kuinua kichwa chake kwa nyuma. Hapo alikuwa amefanya kosa kubwa la kiufundi, kwani kabla hajakirudisha alipigwa pigo zito la kareti usawa wa koromeo lake na hivyo kumwondolea uwezo wa kupitisha hewa kooni!

Alijaribu kupiga kelele lakini sauti haikutoka! Koo lake lilifunga na hivyo kushindwa kuvuta japo kiasi kidogo cha hewa! Alijaribu kukaa akashindwa, kusimama nako akashindwa! Huku akiwa ameshikilia shingo yake, alijikuta akipoteza nguvu kwa kukosa hewa na mara akajikuta akitumbukia ndani ya shimo refu lenye kiza totoro! Alijitahidi kukabiliana na hali hii lakini ilishindikana na bila kutarajia alijibwaga chini na kupoteza fahamu!

Baada ya kuona wote wamepoteza fahamu, Bon Mtambo alichukuwa pingu kisha akamchukua Ngosha na kumlaza kifudifudi juu ya meza kubwa iliyokuwa sebuleni. Pia, alimbeba Batenga na kumlaza chali juu ya mwili wa Ngosha! Alichukuwa pingu na kuwafunga miguu na mikono ambapo kila pingu ilifunga upande mmoja wa miguu na mikono yao kwa pamoja!

Kwa namna ile walivyofungwa, wangeweza hata kufia hapo hapo hata baada ya kurejewa na fahamu!

Baada ya kuridhika na hatua hiyo, aliwapekuwa mifukoni ambako hakukuta vitu vya maana zaidi ya simu zao za mkononi! Alichukuwa simu ya Ngosha na kuingia upande wa ujumbe mfupi lakini alikwama baada ya kukuta ametumia namba za siri, yaani *PIN code*! Hali kadhalika alikutana na hali hiyohiyo kwenye simu ya Batenga!

"Pumbavu!" Bon Mtambo alilaani!

Baada ya kuona amezidiwa maarifa, alianza kupekuwa sehemu mbalimbali hadi chumbani lakini hakuambua chochote cha maana! Akiwa bado anaendelea na upekuzi mara akasikia mtu akikooa kutokea sebuleni na hivyo akajua watakuwa wamerejewa na fahamu! Akiwa ameshika bastola yake mkononi alirudi sebuleni na kuvuta kiti na kukaa hatua chache kutoka kwenye meza aliyowalaza akina Ngosha!

"Ni ushenzi gani huu umetufanyia wewe? Unazani ukitufanyia hivi ndo utapata nini?" Ngosha alifoka.

"Jeuri na kiburi havitawasaidia hata chembe! Salama yenu ni kuyajibu maswali yangu vinginevyo hamtayaona machweo. Na wala msizani kwamba mtakufa kifo chepesi. Mkijifanya jeuri na kiburi nawaahidi kifo kibaya na kilichojaa mateso! Nitaanza kuua kiungo kimoja baada ya kingine, na cha mwisho ni roho zenu ambazo zitakufa zenyewe baada ya kukosa msaidizi kwavile viungo vyenu vyote vitakuwa mahututi! Hivyo basi, naanza kwako Batenga, nini uhusiano uliopo kati ya ISLIB na IBU!"

Kimya!

"Safi sana ISLIB CSO Batenga!" Bon Mtambo aliongea kwa kejeli kisha akachukuwa koleo toka kwenye mfuko wake wa suruali na kuwasogolea hapo mezani.

Kufuatia kuiona koleo hiyo, Batenga alitumbua macho kwa woga ! Hata hivyo Bon Mtambo hakujali na badala yake aliibana pua ya Batenga na kuanza kuivuta kwa nguvu!

"Haaaaaa! Su..su..subiri!" Batenga alipiga kelele za maumivu kufuatia kuvutwa pua yake kiasi cha kuhisi ilitaka kunyofoka! Bon Mtambo hakujali na badala yake alizidi kuivuta huku akiisokota! Ngosha aliyekuwa amelaliwa na Batenga, alikiona kifo cha mateso kikianza kumnyemelea. Kwavile yeye amekaa kijambazi zaidi basi aliamini mateso ambayo angepewa ni ya juu zaidi kuliko anayopewa Batenga ambae muonekano wake ni wa kiungwana! Kwa upande mwingine alikuwa akijiuliza kuhusu kazi rasmi ya Batenga baada ya kuona Bon Mtambo akimuhusisha na ISLIB! Ngosha hakuwa miongoni mwa wateule wachache waliofahamu uhusiano uliopo kati ya ISLIB na IBU!

"Ta..ta..tafadhali niache nita..taa..nitakujibu!" Batenga alizidi kulalamika huku akitokwa na makamasi yalichonganyika na damu!

"Haya nijibu." Bon Mtambo alilegeza mkono ulioshika koleo ili kumpa nafasi Batenga.

"Naifahamu ISLIB lakini siifahamu IBU!" Batenga alijibu huku akiwa bado anaugulia maumivu!

"*Ok*! Nazani huna haja na pua yako, nami nitakusaidia kuiondosha!" Bon Mtambo alieleza kwa kejeli kisha akaanza kukaza tena koleo!

"Mamaaaaaaaaa!" Batenga alianza tena kupiga yowe la maumivu, tena yowe kali kuliko la awali kutokana na ukweli kwamba hivi sasa alikuwa ameminywa kwelikweli! Hali hii ilimtisha zaidi Ngosha aliyekuwa bado amelaliwa na Batenga. Alifikiria ajifanye amekufa ili aepukane na mateso yaliyokuwa yanampigia hodi! Alijaribu kutafuta

akili ya kujinasua lakini hakuona ni namna gani angeweza kufanya lolote kutokana na vile walivyofungwa! Katika maisha yake aliamini kwamba angekuja kufa kifo ambacho si cha kawaida, lakini hakuwahi kujiandaa kukabiliana na kifo cha mateso makali kama kilichokuwa kinamnyemelea!

*"Sipo tayari kufa kifo cha mateso kiasi hiki*!" Ngosha aliwaza na kufikia maamuzi kuwa atayasema yale anayohisi hayatakuwa na athari kwa wenzake!

Wakati Batenga akitarajia Bon Mtambo angelegeza mkono wake lakini ndo kwanza alizidi kuukaza na kutoa dalili zote kwamba pua yake haikuwa na maisha marefu!

"Ta..ta..tafadhali niache nami nitakujibu kila kitu!" Batenga aliomboleza na kwa mara nyingine Bon Mtambo alilegeza mkono ili kumpa nafasi Batenga kuongea.

"Mimi ni Afisa Usal....!" Batenga alianza kueleza lakini sauti yake ilikatishwa ghafla bila yeyote kutarajia! Zilipita sekunde kadhaa kabla Bon Mtambo hajafahamu ni nini hasa kimetokea! Alifikicha macho yake ili aone endapo yupo ndotoni au la! Akili yake ilishindwa kabisa kutoa jibu muafaka! Alifikiria suala la kutimua mbio na kutokomea kusikojulikana, lakini tayari alishachelewa! Miguu yake alihisi ni mizito mithili ya mtu aliyefungiwa tani kadhaa za mawe kiunoni mwake! Hakuona namna nyingine na badala yake akafikiria suala la kupiga magoti ili amuombe mola amsamehe dhambi zake kabla hajajisalimisha kwa Izraili mtoa roho aliyepo milimeta chache tu toka kwenye pua yake!

Baada ya kuwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es salaam William Okello

na Jonathan Njoroge walienda kupanda daladala zitokazo Gongo la Mboto kwenda Mtoni Mtongani tayari kwa safari ya Chamanzi kukutana na Bon Mtambo! Mavazi na mabegi ya kawaida kabisa waliyobeba yaliwatofautisha moja kwa moja na abiria wenzao waliokuwa nao kwenye ndege moja! Hata pale walipotoka nje ya uwanja, hawakuonekana kama ni abiria na badala yake walionekana ni kama watu tu ambao ama walikuja kusindikiza au kuwapokea ndugu zao! Jambo lingine la kufurahisha ni kwamba ilitakiwa labda uwe na shahada ya ukachero ndipo angalau ungeweza kuwashuku kwamba walikuwa safari moja!

Wa kwanza kutoka nyumbani kwao alikuwa ni William Okello aliyesafiri kwa ndege ya shirika la ndege la Uganda hadi jijini Nairobi ambako aliungana na Jonathan Njoroge ambao wote kwa pamoja walikuwa wamekuja kuungana na Bon Mtambo kwenye vita dhidi ya hujuma iliyokuwa inafanyika nchini Tanzania. Wote watatu kwa pamoja, waliunda WIBAIC EA, yaani WIBAIC East Africa huku Bon Mtambo akiwa ndie bosi wao!

ઙ૭ઙ૭ઙ૭ઙ૭

Baada ya akili yake kukaa sawa ndipo Bon Mtambo alipokuja kubaini ni nini hasa kilichotokea! Awali alishindwa kabisa kuona damu zilizokuwa zikiruka hewani mithili ya lile jaribio maarufu la *Fountin's Experiment*! Si kwamba alikuwa amepata upofu wa ghafla, la hasha; bali mchecheto uliomkumba ulitosha kabisa kupoteza nuru ya kawaida ya macho yake! Alifikicha macho kwa mara ya pili na kushuhudia jinsi meza waliyolalia Batenga na Ngosha ilivyokuwa imechakazwa vibaya kwa risasi! Ni shambulio la ghafla na la kimyakimya lililofanywa kwa kutumia

bastola yenye kiwambo cha kuzuia sauti! Ni shambulio lililokusudia kuziba mdomo wa Crispin Batenga usitapike siri kwa Mtambo! Na wala haukuhitajika utaalamu wa kitabibu kujua kwamba viumbe vilivyokuwa vimelalia meza hiyo sekunde chache zilizopita vilikuwa tayari vimeshafunguliwa milango ya kuzimu!

Licha ya sasa kufahamu ni nini hasa kilichotokea lakini alikuwa bado hajajua ni nini alitakiwa kufanya! Kabla hajachukua hatua yoyote, ghafla mtu mmoja mwanaume alipiga teke mlango na kuingia ndani huku akimwaga risasi kadhaa kila upande huku akionesha wazi hajafafahamu ni wapi aliposimama adui yake! Punde si punde, ndani ya muda usiozidi hata sekunde tano huyo mtu alimwona Bon Mtambo aliyekuwa bado amesimama mithili ya mtu aliyepigwa na ganzi! Hapohapo alikoki bastola yake tayari kabisa kwa kufumua kichwa cha Bon Mtambo lakini kabla hajafanya hivyo, huyo mtu alionekana akipaa hewani! Baada ya kurudishwa alikotoka kwa msaada wa nguvu za mvutano, yaani *gravitaional force;* huyo mtu alijibwaga chini na kuruhusu mkono wake uachie bastola huku kiwiliwili nacho kikiruhusu mvua kubwa ya damu! Huu nao haukuwa ni mwili uliohitaji utaalamu wa kitabibu kuweza kuujua kwamba umeshakata shauri la kujumuika na wengine walioko kuzimu!

"Inspekta Cecy!" Bon Mtambo aliita katika namna ya kutoamini macho yake pale alipomuona Inspekta Cecy akiingia kwa kasi huku bastola yake ikiwa mkononi!

*Hakika alikuwa ameokoa maisha yake!*

Matukio yote haya, tangu kuuawa kwa akina Batenga hadi kuingia ndani kwa Insepkata Cecy hayakuchukua hata dakika moja!

“Ahsante mrembo, umeyaokoa maisha yangu!” Bon Mtambo aliongea huku akionekana bado kuwa kwenye mshangao! Bila kupoteza muda, alimwendea yule mtu aliyeuawa na Inspekta Cecy na kuanza kumpekua. Baada ya kuona hakuwa na chochote cha maana alipiga simu polisi kujulisha juu ya kuwapo kwa maiti hizo kisha bila kupoteza muda alimshika mkono Inspekta Cecy na kutoweka eneo hilo.

“Hebu niambie jinsi ulivyojua kwamba nilikuwa matatani hadi ukawahi kuniokoa!” Hatimae Bon Mtambo aliuliza mara baada ya Inspekta Cecy kupiga gari moto na kumwamuru waende Chamanzi! Inspekta Cecy nae akaanza kueleza:

“Kama ambavyo uliniagiza nilianza kukufuatilia nyumanyuma mara baada ya wewe kuondoka. Nilikufuatilia hadi pale nilipokuona unaegesha gari yako na kwenda kwenye ile nyumba. Nilipoona unaenda kwenye ile nyumba, nami niliegesha gari yangu pale ulipoikuta na kwenda kuagiza maji ya matunda lakini akili yangu yote ikiwa kwenye nyumba uliyoenda. Baada ya muda, nilikuona ukiingia ndani kijeshi, nami nikajua kazi imeshaanza hivyo nikajiweka tayari kwa lolote. Baada ya karibu robo saa kupita, nilimuona yule muuaji niliyemmiminia risasi akiwa anaielekea ile nyumba! Kuona hivyo nami nikaanza kumfuata kwa siri. Alipoifikia nilimuona akisita kidogo kisha akaja kujibanza dirishani

huku akichungulia ndani. Alitulia hapo kama dakika moja hivi na mara nikamuona akiangaza huku na huko na aliporidhika na usalama uliopo nilimuona akichomoa bastola na kuanza kuachia risasi kutokea dirishani. Wakati huo nami nilikuwa nimejibanza kwenye gari iliyokuwa imeegeshwa karibu na pale. Baada ya kumimina risasi tu, hapo hapo nilimuona akiingia ndani kwa kuupiga teke mlango. Nami bila kupoteza hata sekunde nilichomoka na kuja dirishani ambako nilimuona akirusha risasi bila mpangilio maalumu hadi pale alipokuona. Kwavile nilishajua ni nini kingefuata, niliwahi kummiminia risasi kupitia njia ileile aliyotumia yeye!" Alimalizia.

"Ahsante sana Inspekta Cecy!"

"Usijali, lakini vilevile nasikitika kwavile sikuwa na namna nyingine!" Inspekta Cecy aliitikia.

"Huna haja ya kusikitika!"

"Najua hatukwenda kule kufanya mauaji, bali kuhoji ili tuweze kuwapata wahusika wakuu waliotufanya tuingie kwenye *project* (mradi) hii. Badala yake, wote wamekufa huku wakiwa wametuacha palepale tulipokuwa dakika kadhaa zilizopita!" Inspekta Cecy alifafanua.

"Si kweli kwamba bado tupo palepale. Safari yetu ya Tabata imetusaidia kugundua kuwa tunapambana na watu hatari. Suala la kujua uwezo wa adui yako vitani ni hatua muhimu kuelekea kwenye ushindi!" Bon Mtambo alieleza.

[redacted]

"Habari za kutwa, nani mwenzangu!" Bon Mtambo aliipokea simu huku akikwepa kujitambulisha!

"DCI Mwaiswelo hapa, nimepigiwa simu kutoka Kituo Kikuu cha Polisi kwamba kuna dada mmoja anaitwa Glory anataka kuonana na wewe; ni muhimu sana!"

"Wamemjibu nini?" Bon Mtambo aliuliza.

"Niliwaagiza wamwambie atoweke kabisa eneo hilo na arejee baada ya nusu saa hadi pale watakapofanya mawasiliano na mpelelezi anayeisimamia kesi yako. Aidha, niliwaagiza wajaribu kumfuatilia huyo Glory kwa siri kuona anakoelekea. Hata hivyo, baada ya kumfuatilia wakagundua kuwapo kwa jambo ambalo si la kawaida kutoka kwake, je unamfahamu vizuri lakini?"

"Namfahamu mzee ingawaje si busara kwake kujua kwamba sipo mikononi mwa vyombo vya dola!" Bon Mtambo alieleza, kisha akahoji: "Ni kwanini umesema kuna jambo ambalo lilionekana si la kawaida?!"

"Hata baada ya kuambiwa atoweke eneo hilo, askari aliyemfuatilia alimuona akiingia kwenye gari kisha akafanya kama anaondoka lakini akarudi na kuja kuegesha gari yake kwenye maegesho finyu yaliyopo nje ya ofisi za TANESCO pale Kituo cha Daladala cha Stesheni. Alitulia kwa muda kisha akaenda kupanda daladala ya Mwananyamala iliyokuwa imeegeshwa hapo Stesheni. Hata hivyo, daladala ilipojaa na kukaribia kuondoka, aliteremka na kufanya kama kuna mtu anayemsubiria lakini baadae akaenda kupanda kwenye daladala nyingine iliyokuwa ndo imeanza kujaza abiria! Hii nayo ilipojaa na kukaribia kuondoka, alifanya kama alivyofanya ile ya awali. Na jambo la msingi kabisa ni kwamba wakati wote amekuwa akifuatilia kwa chati kila anayeingia na kutoka pale kituo cha polisi!" DCI Mwaiswelo alieleza na kumfanya Bon Mtambo ashushe pumzi kwa nguvu!

“Sawa mzee, waambie tu waendelee kufuatilia nyendo zake ingawaje sizani kama atakuwa na tatizo. Huenda ameamua kuisubiria hiyo nusu saa hapo hapo. Hata hivyo, waagize wale vijana wetu waiandae mahabusu yangu nami nitakuja kupumzika huko muda si mrefu. Nitakupigia baada ya robo saa kutoa maelekezo mengine!” Bon Mtambo alimalizia na kumwambia Inspekta Cecy kwenda kuegesha gari yake Halal Restaurant iliyopo hapo Mtoni kwa Azizi Ally.

“Tunahitaji kula kwa haraka Cecy kwavile itabidi turudi pale kituoni kwenu sasa hivi.” Bon Mtambo alimwambia Cecy.

Kiasi cha dakika kumi baadae walikuwa ndani ya gari tayari kwa kuanza safari ya kurejea mjini baada ya kuvunja ile ya kwenda Chamanzi!

“Ni hivi mzee, nazani zimesalia dakika chache tu ili Glory arejee kama alivyoambiwa kabla. Waagize kwamba, akija wamsindikize kwako kwa maelezo kwamba kutokana na uzito wa kesi yenyewe ni wewe tu mwenye mamlaka ya kutoa ruhusa. Aidha, akishafika kwako jifanye unamhoji katika namna ya kumshuku kwamba huenda anahusika kwenye kesi inayonikabili. Epuka kumshuku jambo lingine zaidi ya hilo. Aidha, utamchelewesha kwa takribani nusu saa kisha utatoa kibali cha yeye kuja kuonana nami kwani wakati huo nitakuwa tayari mahabusu yangu!” Bon Mtambo alimalizia maelekezo yake kwa DCI Mwaiswelo!

Inspekta Mussa Ndimbu alikuwa kwenye baa iliyo jirani kabisa na ilipoegeshwa gari ya Mathias Sinare, Mhariri wa Habari wa gazeti la Nuru Yetu.

*"Hakikisha unamteka na kumleta Rutamba Hotel, iliyopo Kariakoo Mtaa wa Livingstone. Mimi nitakuwa nawasubiri chumba namba 48 kilichopo ghorofa ya tatu."* Inspekta Mussa Ndimbu alikumbuka maagizo kutoka kwa Bon Mtambo. Alitulia hapo kwa takribani robo saa kabla hajatokea mtu mwenye wajihi sawa na ule alioelekezwa kwamba ndio wa Mathias Sinare. Huyo mtu aliingia garini na kulipiga moto lakini kabla hajafika popote, Inspekta Mussa Ndimbu alijitokeza mbele yake na kumsimamisha. Sare za jeshi la polisi zilizovaliwa na Inspekta Mussa Ndimbu zilimfanya Mathias Sinare asiwe na wasiwasi nae.

"Tafadhali naomba msaada uniache kituo cha polisi cha Kawe!" Inspekta Mussa Ndimbu aliomba. Dereva nae bila kinyongo alifungua mlango na kumruhusu Inspekta Ndimbu kuingia garini.

"Nazani nimeshawahi kukuona sehemu mbalimbali hapa jijini!" Inspekta Mussa Ndimbu alianzisha maongezi.

"Inawezekana afande, unajua mimi ni mwandishi wa habari hivyo kila penye matukio kwangu ni ofisi!"

"Oh! Nimefurahi kukutana na mtu muhimu kwa jamii." Inspekta Mussa Ndimbu aliongea kisha akaendelea, "Naitwa Inspekta Sudi, sijui mwenzagu unaitwa nani?"

"Naitwa Mathias Sinare, ni Mhariri wa Habari wa Nuru Yetu!" Mathias Sinare alijibu huku akiendelea kukanyaga mafuta.

"Kwahiyo endapo habari inatolewa na kuonekana sio ya ukweli bila shaka anayepaswa kuwajibika ni Mhariri zaidi kuliko mwandishi aliyeleta habari yenyewe!" Inspekta Mussa Ndimbu alihoji huku Mathias Sinare akiegesha gari baada ya kufika kituo cha polisi cha Kawe.

Karibu nusu dakika ilipita bila Inspekta Ndimbu kuonesha dalili yoyote ya kutaka kuteremka! Hali hii

ilimfanya Mathias Sinare kugeuka na kumwangalia lakini bila kutarajia alijikuta akichungulia mdomo wa bastola!

"Moja kwa moja Rutamba Hotel iliyoko mtaa wa Livingstone, Kariakoo! Ukileta ujanja wowote basi fahamu utakuwa unajikaribishia kifo!"

"U..u..unataka nini?!" Sinare aliongea kwa hofu.

"Endesha gari na sihitaji maswali zaidi!"

"Pole mpenzi, nilikuwa na hofu sana juu yako!" Glory alimweleza Bon Mtambo mara baada ya kuonana nae.

"Usijali Glory, naamini yataisha tu mpenzi!" Bon Mtambo alijibu kwa unyonge huku akimwangalia binti huyu mrembo kwa macho yaliyojaa huba!

"Mbona ni kama ulikuwa kwenye mapambano?!" Ghafla Glory aliuliza swali lililomfanya Bon Mtambo ababaike kidogo ingawaje alijitahidi kutojionesha!

"Ni kweli Glory, kitu kinachoitwa haki za binadamu hakipo kabisa kwa polisi wetu. Tangu niwekwe humu ndani nimekuwa ni mtu wa kupewa vipigo kila wakati wakinilazimisha nikubali eti nina uhusiano wa karibu na Osama Bin Laden!"

"Pole sana, hata hivyo, nimekuja kukuambia kwamba leo nimepita pale kwako kama mara mbili, na mara zote nimeshuhudia pilikapilika za watu ninaohisi wamekuwa wakiingia ndani kwako ingawaje sina hakika endapo ni wanausalama au wezi!" Glory alieleza.

"Sizani kama ni wezi, huenda ni wanausalama wanaojaribu kuchunguza endapo kutakuwa na watu wanaokuja hapo ambao wanaweza kuwa ni washirika

wangu! Si ajabu, hadi sasa wameshapekua nyumba nzima, lakini hainisumbui! Wakitaka wahamishie hata ofisi ya DCI palepale!" Bon Mtambo alijibu kwa upole!

"Washirika wa nini?" Glory aliuliza.

"Si wanasema mimi ni gaidi! Labda wanafuatilia kuona kama kuna hao magaidi wenzangu pale!"

"Na kwanini iwe washirika kwenye ugaidi na isiwe washirika wenzako wa madawa ya kulevya!?"

"Glory mpenzi, ina maana na wewe umegeuka kuwa askari wa upelelezi? Nilitarajia umekuja kuniliwaza kwa maneno matamu, kumbe nawe umekuja kwa shughuli za kikachero! Nami nilijua tu, watu wote, hata mama yangu mzazi wamekataliwa kuonana na mimi, inakuwaje DCI akuruhusu wewe pekee?! Ni mtu wao? Hebu niambie!" Bon Mtambo alijifanya kulalamika huku amekauka macho!

"Samahani mpenzi kama nimekuudhi!"

"Unanitisha mpenzi lakini tuyaache!" Bon Mtambo aliongea kwa unyonge lakini uliojaa umakini! Punde kidogo, walianza kuongea mambo kadhaa hadi pale walipoagana huku tena kila mmoja akiwaza kivyake juu ya mwenzake! Kwa mara nyingine, Bon Mtambo alijishangaa ni kwanini alishindwa kumuamini Glory na Glory nae ndie aliyeumia zaidi kuona Bon Mtambo aliendelea kujifanya anahusika na kesi wakati si kweli!

Baada ya Glory kuondoka, Bon Mtambo alifanya haraka kuwahi Rutamba Hotel!

Kama alivyoamrishwa, safari kati ya Inspekta Ndimbu na Mathias Sinare iliendelea hadi Rutamba Hotel.

“Sasa sikiliza, tunaongozana wewe mbele mimi nyuma hadi ghorofa ya tatu chumba namba 48. Usisahau kwamba nina bastola mkononi hivyo sitasita kukulipua pindi utakapojifanya mwerevu!” Inspekta Mussa Ndimbu aliongea mara Mathias Sinare alipoegesha gari hapo Rutamba Hotel.

“Karibu Mathias Sinare, mwandishi msaliti wa fani ya uandishi wa habari nchini!” Bon Mtambo, akiwa na bastola mkononi, alimkaribisha Mathias Sinare mara alipoingia na Inspekta Mussa Ndimbu, kisha akamwelekeza kiti cha kuketi.

“Sasa sikiliza Mathias, mimi sina shida na wewe endapo utaonesha ushirikiano. Hata hivyo sitachelea kukutia adabu endapo utaniletea kujua; hivyo nisingependa tupotezeane muda. Nimekuita hapa ili unipe maelezo kuhusu taarifa ambayo uliitoa kwenye gazeti lenu jumamosi iliyopita!” Bon Mtambo alieleza kisha akachukua kipande cha gazeti chenye habari husika na kumpatia Mathias. Habari aliyokua anaizungumizia ni ile ambayo iliandikwa na Layla kuhusu kukamatwa kwake kama gaidi kisha taarifa hiyo ikasambazwa kwenye vyombo vya habari.

*Moyo wa Mathias ulipiga mkamba baada ya kuiona habari yenyewe!*

“Naongea na wewe Mathias, au unataka kufahamu mimi ni nani ndipo uyajibu maswali yangu?” Bon Mtambo aliongea kwa ukali kisha akamuonesha kitambulisho chake.

Hofu ya Mathias iliongezeka maradufu kiasi cha kuongeza kasi ya mapigo ya moyo wake. Aliikumbuka siku alipoajiriwa kama mwandishi wa kawaida wa gazeti la Nuru Yetu hadi kufikia ngazi ya kuwa mhariri wa habari. Baada ya kuwa mhariri wa habari akapata fursa ya

kufahamiana na watu mbalimbali maarufu na mashuhuri nchini. Miongoni mwa watu ambao aliweza kufahamiana nao ni msichana mrembo ambae alijitambulisha kwake kama Layla Anwar Bayser. Baada ya maongezi ya hapa na pale, Layla alimweleza Mathias ni jinsi gani anavyoihusudu kazi ya uandishi wa habari. Kutokana na hilo, akamwomba amfanyie mpango kwa wakuu wake wa kazi ili awe anafanyia kazi hapo kama mwandishi wa habari wa kujitegemea kwa kupewa fursa ya kuleta habari mbalimbali, zikiwemo na uandishi wa makala. Kama ilivyo silika ya wanaume wengi wanapokutana na wasichana warembo; Mathias nae alijikuta akilipokea ombi la Layla kwa mikono miwili. Na kweli, Layla alianza kuleta habari mbalimbali ambazo nyingi ni za kiuchunguzi zaidi zikiihusu serikali na watendaji wake. Hata pale viongozi wa serikali walipokuja juu kuhusu habari zilizochapishwa, mara zote gazeti la Nuru Yetu liliibuka mshindi baada ya ushahidi wa habari hizo kutolewa. Hali hii ilijenga si jina la Layla pekee mbele ya Nuru Yetu, bali hata hadhi ya gazeti lenyewe ilipanda miongoni mwa magazeti mengine nchini! Hata hivyo, nyingi kama sio zote ya habari hizi zilipatikana kwa jitihada za IBU na kumpatia Layla ambae ni mtu wao, ingawaje Mathias hakufahamu juu ya jambo la hilo!

Kwa upande mwingine, uhusiano kati ya Layla na Mathias Sinare haukuishia hapo tu kwani Layla aligeuka na kuwa mfadhili mkubwa wa Mathias. Ufadhili wa Layla ulifikia kilele pale yeye Layla na watu wake walipokula njama zilizofanikisha kuchoma moto nyumba ya Mathias Sinare na hivyo kumwacha bila makazi! Baada ya mkasa huo, Mathias alimwendea Layla na kumwomba amkopeshe pesa ambazo zingemwezesha kukodi nyumba kwa mwaka mzima wakati akijaribu kuweka mambo yake sawa. Katika

hali ambayo Mathias hakuitarajia, Layla alimwahidi kumjengea nyumba nyingine kwa mkopo wa masharti nafuu. Awali, Mathias hakutaka kabisa kuamini lakini miezi mitatu baadae nyumba aliyoahidiwa ilijengwa!

“Nazani wewe ni jeuri, nami napenda sana watu wa aina yako.” Bon Mtambo aliongea kwa kejeli huku akiwa ameshika koleo na kumwelekea Mathias. Ni kauli hii ya Bon Mtambo ndiyo iliyomzindua Mathias Sinare!

“Habari hiyo ililetwa na mwandishi wetu sawa na habari zingine!” Mathias alijibu huku akiwa na hofu kwavile alijua kwamba anadanganya!

“Huyo mwandishi wenu anaitwa nani?”

Kimya!

“Nakuuliza wewe Mathias!”

“Kwakweli sifahamu!”

“Unanitania Mathias, ina maana huwafahamu waandishi wako?” Bon Mtambo alifoka kisha akaibana pua ya Mathias kwa koleo na kuanza kuisokota. Mathias alianza kupiga kelele za kuomba aachiwe!

“Sikuachii Mathias, kwavile unaonekana ni jeuri!”

“Niachie tafadhali nitakutajia!” Mathias alipiga kelele, kisha Bon Mtambo akalegeza mkono.

“Anaitwa Moses Ndumbalo!” Mathias aliongopa, hata hivyo, Bon Mtambo alijifanya kuukubali uwongo wake!

“Nani Mhariri Mkuu wa Nuru Yetu?”

“Hassan Lwa...!” Mathias alijibu bila kufikiri, huku kwa mara nyingine akijaribu kudanganya. Hata hivyo, kabla hajamalizia sentensi yake alipigwa ngumi mzito iliyompeleka hadi chini na kumng’oa meno mawili ya juu! Taratibu Mathias alijihisi kuishiwa na nuru machoni mwake na mara kiza totoro kikachukua nafasi.

Fahamu zikamruka!

Baada ya dakika tano, Mathias alirejewa na fahamu na kujikuta bado anachungulia ndani ya mtutu wa bastoal!

“Nazani sasa utaacha mchezo, na ukiendelea na upuuzi wako nakuua sasa hivi! Tena nitakuua kwa kifo cha mateso! Haya niambie, ni wapi ulizipata zile habari. Usizani sifahamu ni wapi ulizipata, hapa nataka kupima uaminifu wako kwa wana usalama.”

“Zililetwa na mwandishi wa kujitegemea!”

“Anaitwa nani?”

“Layla Anwar Bayser!”

“Afadhali, naona umeamua kuwa mtoto mzuri hivyo unaweza kwenda!”

Baada ya kuambiwa hivyo Mathias aliamka kwa haraka lakini ghafla akasita!

“Tafadhali, naomba usinitaje lakini!”

“Sikutaji!”

Baada ya kuhakikishiwa alianza kuondoka lakini kabla hajaufikia mlango, aliamriwa kurudi mara moja!

“Kwanini umeomba nisikutaje?”

“Layla ni rafiki yangu sana hivyo nami sijafahamu nini lengo lenu!” Mathias alijibu.

“Layla anaishi wapi?”

“Anakaa nyumba za msajili iliyopo eneo la Kitumbini.” Mathias alijibu na kuelekeza sehemu yenyewe.

Baada ya hapo aliendelea kumuhoji mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na kuchukua namba yake ya simu kisha bila kutarajia, Mathias alijikuta akipigwa pingu!

“Inspekta, kamuunganishe na akina Mashaka nami naenda kuonana na huyu mrembo hasidi!”

# 11

Matukio yaliyoikumba kambi ya George Kamau yaliwatisha mno kiasi cha kuhisi Bon Mtambo aliachiwa huru na kuendesha harakati dhidi yao kwa siri! Hofu hii ilipata nguvu zaidi pale walipopokea taarifa za kuuawa kwa Ngosha na wenzake ambapo waliamini wasingeweza kushindwa nguvu kwa polisi wa kawaida! Ili kujiridhisha, Kamau alimtuma Glory kwenda kuhakikisha kama Bon Mtambo bado anashikiliwa. Walipojiridhisha kwamba bado yupo mahabusu, walikata shauri la kufanya jambo la maana na la haraka dhidi ya wanausalama. Hata hivyo, walijiona walifanya kosa kwa kuwasahau watendaji wa jeshi la polisi pale walipoanza hujuma zao na badala yake kujikita zaidi kwa wanasiasa na watendaji wa serikali!

*"Hakikisha unafanya lolote liwezekanalo, na kwa gharama yoyote hadi tunaingilia maamuzi ya jeshi la polisi ndani ya saa ishirini na nne toka sasa!"* Kauli ya Fredrick De Souza ilikuwa inajirudiarudia kichwani mwa George Kamau.

Baada ya kuketi, aliwasha kompyuta yake kisha akachukua orodha ya maafisa wa jeshi la polisi pamoja na wale wa wizara ya mambo ya ndani! Alianza kwa kuingiza jina la kila mmoja kwenye *database* yao kuangalia endapo wamo kwenye orodha! Baada ya kuingiza majina yote ya maofisa wa polisi bila mafanikio ndipo alipokuja kuingiza jina la Mheshimiwa Bwana Elisante Josephat , Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kabla hajaingia kwenye siasa, Bwana Elisante Josephat alikuwa ni Katibu Mkuu wa iliyokuwa Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji.

Baada ya kuchukua taarifa zote muhimu ikiwa ni pamoja na kupata mkanda wa video, aliwaita watu wake ni kuwaelekeza nini cha kufanya. Ilimlazimu kutoa maelekezo ya kutosha kwavile alifahamu kazi ambayo alitaka kulazimishwa Bwana Elisante Josephat ni kazi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini!

Baada ya kufika eneo la Kitumbini Bon Mtambo alienda kubana kwenye duka moja la vinywaji baridi na kutoka hapo aliweza kuiona waziwazi nyumba anayoishi Layla Bayser. Hata hivyo taa za nje na za ndani zilikuwa hazijawashwa, hali iliyomjulisha kwamba mwenyewe hakuwapo. Akiwa bado ametulia, mara aliona gari moja aina ya Suzuki Rav 4 ikija na kugeshwa jirani kabisa na hiyo nyumba kisha sekunde chache baadae, alimuona Layla akiteremka na kwenda kwenye hiyo nyumba. Bila kupoteza muda, alianza kumfuatilia. Kwa hatua za kunyata alipanda ngazi na alipofika mlangoni kwa nje, aligundua Layla alikuwa anaongea na simu!

*"...yah, imethibitika kwamba Bon Mtambo bado yupo mikononi mwa vyombo vya dola.....Wendy na Mchupi wanaenda kwa waziri wa mambo ya ndani kumshinikiza amwagize mkuu wa jeshi la polisi achukue hatua dhidi ya wanausalama.....ni kweli, na huo ni mkakati wa muda mfupi tu wakati tunajipanga kwa mkakati wa kudumu....ok, usiku mwema!"* Layla alimalizia maongezi yaliyomwacha Bon Mtambo mdomo wazi!

*"Ni nani kawathibitishia kwamba bado nipo mikononi mwa vyombo vya dola!? Inawezekana Glory ni mmoja wao?! Hapana, it can't be (haiwezekani)! Ni hatua gani wanayotaka*

*ichukuliwe dhidi ya wanausalama!?"* Bon Mtambo alijikuta akijiuliza maswali kadhaa yasiyo na majibu!

*"IBU inajihusisha na kuwatengenezea kashfa watu walio na mamlaka serikalini na kuzitumia kashfa hizo kuwalazimisha hao watu watekeleze matakwa ya IBU! Hata hivyo, mara nyingi zinakuwa si kashfa za kutunga.......!"* Bon Mtambo aliyakumbuka maelezo ya Mashaka!

*"Ina maana Bwana Elisante Josephat nae alishawahi kuingia kwenye mtego wa IBU...!!"* Bon Mtambo aliendelea kujiuliza maswali kadhaa hadi alipogutushwa na mlio wa radio iliyoanza kusikika kutoka ndani!

Aliirudisha akili kazini kisha akatafuta upenyo na kuchungulia ndani. Akiwa hapo alimuona Layla akiwa amejifunga taulo fupi kabisa huku akielekea sehemu ambayo Bon Mtambo aliamini ni bafuni. Alitulia hapo mlangoni kwa sekunde kadhaa hadi aliposikia kumwagika kwa maji. Bila kupoteza muda, alichukua funguo malaya na kuingia ndani kisha akaenda kuketi kwenye sofa moja lililoelekea kule alikoenda Layla!

Zilipita kama dakika kumi hivi ndipo Layla alimaliza kujiswafi na kuelekea sebuleni. Akiwa hana hili wala lile, alikuja kwa hatua za taratibu huku akijifuta maji kwa taulo lake fupi na hivyo kufanya sehemu kubwa ya maungo yake kuwa tupu!

"Vipi mpenzi wangu, umeniachia sabuni?" Bon Mtambo aliongea kwa kejeli na kumfanya Layla apigwe na mshituko! Alitulia kimya! Haendi mbele wala nyuma! Ilikuwa ni kama aliyepigwa na shoti ya umeme! Alijiuliza endapo anaota, au yupo kwenye maisha halisi!

"Sikufikiria kama umeumbika kiasi hicho *Lay*!" Bon Mtambo aliendeleza kejeli zilizomzindua Layla na kugundua kwamba kumbe hata taulo lake lilishamponyoka

kitambo huku likiwa limemwacha mtupu kama alivyozaliwa!

“Mshenzi mkubwa wee! Ondoka haraka ama sivyo nitakuitia watu kwamba unataka kunibaka!” Layla aliongea kwa hasira huku akiokota taulo lake ambalo hata hivyo lilishindwa kabisa kusitiri maungo yake kutokana na ufupi wa taulo hilo! Ilikuwa ni lazima ama ayaache matiti nje, au aache kuyafunika maeneo nyeti zaidi ya mwili wake!

Layla alichagua kuyaacha matiti yake nje huku akimwangalia Bon Mtambo kwa jicho lililojaa chuki!

“Tulia hapohapo mwanamke, unaenda wapi?” Bon Mtambo aliongea kwa utulivu baada ya kuona Layla anaanza kuondoka. Hata hivyo, Layla hakusikiliza hadi pale Bon Mtambo alipochomoa bastola na kumwelekezea!

“Hasira za nini Layla, hukumbuki tulikubaliana kwamba ukitoka Zanzibar ungekuja kwangu?! Nimeona unachelewa na ndio maana nikaamua nikutafute mwenyewe!” Bon Mtambo aliongea kwa kejeli, hata hivyo alikuwa katika wakati mgumu kuliko kawaida! Hali ya joto la mwili wake ilikuwa inapanda na kushuka bila mpangalio maalumu!

“Unataka nini kutoka kwangu?”Layla aliuliza huku akiwa bado na donge la chuki na hasira dhidi ya Bon Mtambo! Suala la yeye kujianika mtupu mbele yake lilimkera kupita maelezo.

Badala ya kujibu, Bon Mtambo alichukua kitambaa kilichokuwa mezani na kumrushia na kumfanya ayasitiri maungo yake vizuri!

“Nani alikudanganya kwamba bado nipo mikononi mwa polisi? Mimi bado nadunda tu mtaani huku nikiwashikisha adabu mafedhuli wenzako. Hapa unaponiona, natoka kumshikisha adabu bwana ‘ako

Mathias Sinare, na sasa ni zamu yako! Siku ile pale uwanja wa ndege ulijiona mwerevu sana na leo werevu wako umeshafika tamati! Nilikuwa na hasira sana na wewe, na lazima nikakulaze kwenye mahabusu ya wanaume usiku huu!" Bon Mtambo alitishia na kumfanya Layla atoe macho ya woga!

"Eti!?" Layla aliuliza kwa taharuki!

"Ndiyo Layla, lazima ukalale kwenye mahabusu ya wanaume kwavile wewe ni mshenzi usiyepaswa kuwekwa na wanawake wenzako! Kwa kawaida wanawake washenzi kama wewe wanakuwa wasagaji. Kwahiyo nikikupeleka mahabusu ya wanawake, nachelea utaenda kupeleka vitendo vya kisagaji kule!"

"Acha kunitisha Bon, unajua wazi kwamba hakuna magereza yoyote nchini itakayokukubalia huo upuuzi unaoongea!" Layla alijibu kwa jeuri.

"Safi sana mrembo, napenda watu wakaidi kama wewe, na kwavile ilishasemwa kwamba mkaidi hafaidi hadi siku ya iddi, basi sina shaka kwamba iddi yako leo imewadia! Na hakika leo utafaidi kwelikweli kwani wanaume wote utakaowakuta watakua halali yako! Na sijui ni nani alikudanganya mimi nafanya kazi zangu kwa niaba ya nchi hii? Hivi hushangai ni kwanini maagizo ya kazi zangu nayapata toka Ulaya badala ya Tanzania? Sasa sikiliza, nazani si......!" Bon Mtambo aliongea lakini ghafla simu yake ikaita. Hata hivyo, muito wenyewe alishaujua. Si kwamba kuna mtu alikua anapiga, bali ni mlio wa kumkumbusha jambo kwamba muda wa kufanya jambo fulani umefika; yaani *alarm*! Hata hivyo, mlio uliotoka ulikuwa ni kama muito wa kawaida wa simu, hivyo Bon Mtambo aliamua kujifanya kuipokea!

“Ndio kapteni nakupata...yah! nipo nae hapa! Ebu niambie, vipi boti umeiacha palepale?.....OK! Sasa ni hivi kapteni, kaegeshe boti pale rasi ya Kurasini, kwenye bandari ya kwenda Vijibweni kwavile kuna waharifu wengine sita wapo pale Kituo Cha Polisi Cha Barabara ya Kilwa. Vilevile waambie watu wa Bongoyo waandae chakula kwa ajili ya hawa watu....Ndiyo ndiyo!…Kwani kule kuna waharifu wangapi?….Ni nane? Basi wataenea kwavile hawa huku ni saba na jumla watakuwa kumi na tano na ile mahabusu ina uwezo wa kuchukua watu ishirini kwa wakati mmoja....hapana, hamna jinsi kapteni, hilo jambo lipo nje ya uwezo wetu kwa sasa....ndiyo, kwa leo hatutawatenganisha, isitoshe ujenzi wa ile mahabusu ya wanawake haujafikia hata nusu.....ndiyo hivyo kapteni, kwa leo wote watalala maha....!” Kabla hajamalizia sentensi yake, ghafla Layla alikurupuka na kumrukia Bon Mtambo! Hata hivyo, Bon Mtambo alikwepa na kumruhusu apitilize na kwenda kujibamiza mezani!

“Sikiliza mwanamke, utaumia; mimi si mtu wa kufanyiwa michezo ya kitoto kama hiyo! Naomba urudi haraka pale kwenye sofa!” Bon Mtambo alimweleza Layla kwa sauti ya utulivu huku akiwa amemlenga bastoal yake sawia na paji la uso. Huku akiwa amefura kwa hasira, alijiinua na kurudi kwenye sofa, kisha Bon Mtambo akajifanya tena kupiga simu na kumalizia maongezi yake ambayo kimsingi hakuwa akiongea na yeyote! Alichokua anafanya ni kumtisha tu Layla!

“Samahani kapteni, huyu mwanamke alitaka kunilitea utoto wakati anatakiwa kuhifadhi nguvu zake kwa ajili ya kwenda kupambana na majahili wenzake atakaokuwa nao mahabusu.....!!Sawasawa, hata hivyo usichelewe kwavile kuna kazi pale ISLIB na IBU!” Bon

Mtambo aliongea na kumtupia jicho la pembeni Layla aliyekuwa amepigwa na mshituko baada ya kutajwa IBU!

"Sasa sikiliza mwanamke, nakuonya usiniletee ujanja wowote. Hivi sasa tunakwenda kisiwa cha Bongoyo ambako ndiko iliko mahabusu ya watu kama ninyi! Kule ndiko kuna maofisa watakaokuhoji ifikapo kesho. Mimi sitakuhoji kwavile bado nina hisia za mapenzi juu yako hivyo nitashindwa kukufanyia ukatili wa kukulazimisha kuongea unayopaswa kuongea!" Bon Mtambo alimtisha Layla kwa sauti ya utulivu lakini iliyokosa japo chembe ya masihara! Hofu ilidhihirika wazi usoni pa Layla.

"Kwanini unataka kunifanyia ukatili namna hiyo lakini!" Layla alihoji kwa unyonge.

"Ni ukatili gani mwanamke wakati tangu nimeingia humu ndani hata kukugusa sijakugusa?!"

"Kama ni kunihoji ni kwanini usinihoji wewe mwenyewe halafu tukamalizana hapahapa?" Layla alitupa karata ya kujiokoa! Taarifa kwamba alitaka kwenda kufungiwa mahabusu moja na wanaume ilikuwa ni habari iliyomtisha kuliko kifo! Na sizani kama kuna mwanamke yeyote duniani ambae angekuwa na ujasiri wa kuwa tayari kwa hilo! Kufuatia kauli ya Layla, Bon Mtambo alimtupia jicho lililobeba angalau kiasi fulani cha huruma ya bandia kisha akatikisa kichwa kwa masikitiko na kuongea:

"Nazani umenielewa Layla, siwezi kupata ujasiri wa kukutesa ili uongee unachotakiwa kuongea, hivyo tusipotezeane muda, inuka twende!" Bon Mtambo aliongea na kuelekea mlangoni huku akiwa bado ameelekeza bastola yake kwa Layla! Bila kutarajia, Layla aliinuka na kumfuata Bon Mtambo kisha kwa makusudi akajifungua kitambaa alichofunika maungo yake na kubaki mtupu kama

alivyozaliwa! Aliendelea kumfuata huku akirembua macho katika namna ya kumtamanisha!

"Simama hapo hapo mwanamke! Usijidanganye kwamba unaweza kunilaghai kwa huo upuuzi wako! Hapa nilipo sina hisia zozote za kingono!" Bon Mtambo alifoka hali iliyomtisha hata Layla mwenyewe!

"Ok, twenzetu, labda umechagua kwenda tuendako ukiwa uchi wa mnyama!" Hatimae Bon Mtambo aliongea huku akimvutia Layla nje, hali iliyomfanya Layla agome!

"Tafadhali Bon, nipo tayari kuongea lolote hapa hapa!"

Bon Mtambo alimwangalia Layla kwa jicho kali kwa takribani nusu dakika hivi!

"Sikiliza Layla, usitake kunipotezea muda wangu. Kila kitu utaenda kuongea huko huko!"

"*Please!* (tafadhali) Bon, naomba unihurumie jamani!" Ujanja ulimwisha Layla na badala yake akaanza kuongea kwa sauti ya kuomboleza!

"Sawa, nakupa nafasi moja tu na ukiichezea usitarajie kupata nafasi nyingine kama hiyo! Kwanza naomba tuongozane chumbani kwako!" Bon Mtambo alimwambia Layla na kuongozana nae chumbani ambako alichukua nguo na kumpatia ili avae.

"Una hati ya kusafiria iliyo hai!" Hatimae Bon Mtambo alimuuliza Layla kwa upole.

"Ndiyo!"

"Una ndugu yoyote anayeishi nchi za mashariki ya mbali, au Asia ya Kusini?"

"Hapana!" Layla alijibu huku akijiuliza nini maana ya maswali haya ambayo hakuyatarajia kabisa!

“Unaweza kuwa na pesa ya kukuwezesha kuishi hotelini kwenye hizo nchi kwa angalau mwezi mmoja?” Bon Mtambo aliendelea kuhoji.

“Mwezi mmoja sio rahisi, labda kama wiki mbili hivi.” Alijibu kisha akaendelea, “Kwanini unaniuliza hayo maswali lakini?” Hatimae Layla alihoji.

“Sasa nisikilize kwa makini, kama nilivyokuambia hapo awali, nimeamua kukupa fursa hii kwa ajili yako na yangu pia. Baada ya maongezi yetu, nataka kabla ya saa kumi na mbili kesho asubuhi uwe umetoweka hapa nchini. Nitakufanyia mipango ya usafiri na utaenda Indonesia ambako mimi nitakukuta huko mara baada ya kumaliza jukumu lililo mbele yangu!”

“Na vipi kuhusu huyo kapteni uliyemwambia umenitia mikononi?”Layla alihoji.

“Suala hilo niachie mimi, isitoshe mimi ni bosi wake hivyo naweza kumweleza chochote na yeye asihoji!” Bon Mtambo aliongea na kumpatia Layla nafasi ya kuyatafakari mapendekezo yake.

“Sikuamini Bon, naona ni kama unanichezea akili!”

“Sikiliza Layla, ukiamini hivyo utakuwa unajidanganya bibie. Lazima ujue kwamba nikitaka kukulazimisha utapike siri zote fahamu kwamba utazitapika tu. Huna uwezo wa kuhimili mateso yangu endapo nitaamua kufanya hivyo. Vilevile huna uwezo wa kuhimili mateso toka kwa makachero wa Kikaburu waliopo Bongoyo! Hata hivyo, sioni kama ni busara kwavile najua wewe umeingia kwenye uhalifu kwa kurubuniwa tu! Hivyo basi, tusicheleweshane, niambie mara moja kama upo tayari na au hapana!” Bon Mtambo alieleza kwa sauti kavu na kumtupia jicho la unasemaje!

“Nipo tayari, ni matumaini yangu kwamba hunichezei akili!”

“Usihofu, chukua hati yako ya kusafiria pamoja na vitu vichache unavyohisi ni muhimu katika safari! Tafadhali, fanya haraka tusije kukutwa na watu wako na kujua kwamba nimekutorosha!”

Dakika tano baadae, walikuwa kwenye gari wakielekea Chamanzi, shambani kwa Bon Mtambo.

“Karibuni, niwasaidie nini vijana?” Bwana Elisante Josephat , Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliwakaribisha, Michael Mchupi na Wendy mara walipoingia ofisini wake.

“Ahsante Mheshimiwa, mimi naitwa Latifa, na mwenzangu anaitwa Muhsin na tumekuja kwako kwavile tuna kazi tunaomba utusaidie!” Wendy alianza maongezi kwa kujitambulisha kwa majina ya uwongo!

“Sawa binti, hilo ni jukumu langu, sijui mnataka niwasaidie nini.” Bwana Elisante Josephat alijinadi.

“Ahsante mheshimiwa, kwa kifupi tumegundua kwamba vijana walio chini ya wizara yako wanazihujumu shughuli zetu, kwahiyo tunakuomba uwaamuru kuacha hujuma zao mara moja!” Wendy aliongea huku akikosa japo chembe ya masihara machoni mwake!

“Mbona sikuelewi binti, ni vijana gani hao na ni shughuli zipi wanazozihujumu!” Bwana Elisante Josephat aliuliza kwa utulivu ingawaje alichukizwa na namna msichana huyu alivyowasilisha hoja yake.

“Hatuwafahamu majina yao mzee, hata hivyo tuna picha za video zinazoonesha hujuma zao hivyo endapo hutajali tunaweza kukuonesha ili uwatambue!”

“Hamna shaka, nionesheni! Nami napenda sana mambo kama hayo ambayo mtu anayaongea akiwa tayari na ushahidi wake mkononi! Tunapata shida sana na watu wanaokuja hapa kuwalalamikia watendaji wa serikali na jeshi la polisi kwamba wanawasumbua. Utakuta wengine wanakuja kulalamika kwamba wanaombwa rushwa lakini ukiwataka ushahidi japo wa mazingira wanashindwa kufanya hivyo na badala yake wanaishia kuilaumu serikali!” Bwana Elisante Josephat aliongea kwa kujiamini kabisa.

Baada ya Bwana Elisante kukubali kuziona picha hizo, Wendy aliwasha kompyuta yake ya mkononi, yaani *laptop* kisha akafungua picha alizozitaka na kumgeuzia Jackson kompyuta hiyo ili aziangalie vizuri!

Picha, au tuseme filamu hiyo ilionesha ni kama ilipigwa sehemu fulani barani Ulaya kutokana na idadi ya wazungu walioonekana kupitapita. Sekunde chache baadae, picha hizo zilionesha jengo kubwa ambalo kulikuwa na bango lililosomeka NasBank Ltd! Bwana Elisante akagutuka kidogo kwavile ni kama anaifahamu benki yenye jina sawa na hili iliyopo nchi za ng’ambo! Kutoka hapo, filamu hii ilihamia ndani ya benki na mara alitokea mwanaume mmoja wa makamo huku akiwa ameshika mkoba mkononi! Alimwangalia kwa makini mtu huyo, kisha akahisi kama ameshapata kuonana nae mahali!

*“Sikiliza Jose, mmoja wa wale jamaa mkewe ni meneja wa tawi moja la benki kwenye visiwa fulani nchini Italia. Mpango huu tutaumalizia kulekule nawe utarudi Tanzania salama kabisa.Hivyo basi, tumia mamlaka yako kuandaa hati ya kusafiria*

*yenye jina tofauti na hilo lililozoeleka na wale jamaa watakusaidia kukutafutia hati ya kuingilia Italia.Utaondoka Tanzania kama Elisante Josephat na ukiwa ndani ya mitaa ya Italia utatumia jina lingine. Aidha, utamwagiza daktari wako akuandikie rufaa ya kwenda nje ya nchi kuchunguza afya. Tutaitumia nafasi hiyo kwenda Italia ambako utafunguliwa akaunti yako hapo NasBank kwa jina litakalokuwa kwenye hiyo hati mpya. Ukumbuke kwamba, NasBank wana matawi yao nchini Kenya na Uganda. Tafuta watu wawili unaowaamini, mmoja afungue akaunti ya biashara NasBank Kenya na mwingine NasBank Uganda! Wafungue akaunti kama mawakala wa kampuni moja kutoka Italia inayohusika na ununuzi wa mazao Ukanda wa Maziwa Makuu. Baada ya hapo, utaacha* ***Agizo la Benki,*** *yaani* ***Bank Order*** *pale NasBank Italia itakayoagiza kuamisha kiasi fulani cha pesa kila baada ya muda fulani na pesa hizo kuingizwa kwenye akaunti za NasBank zitakazofunguliwa Kenya na Uganda na hapo utaziingiza kwenye mzunguko wa kawaida wa biashara zako! "*

Bwana Bwana Elisante Josephat anakumbuka kuambiwa maneno haya na mtu anayefanana na yule aliyebeba mkoba kwenye filamu hii!

Muda mfupi baadae akatokea mtu mwingine aliyekuwa amevaa suti nadhifu huku akitembea kwa majivuno! Hata hivyo, Bwana Elisante alishindwa kumfahamu mtu huyu kwavile alikuwa anaonekana mgongoni. Lakini pamoja na hayo, macho ya Bwana Elisante yalitua kwa sekunde kadhaa kwa huyu mtu hasa baada ya kukumbuka kwamba, nae alikuwa na suti na viatu kama hivi miaka kadhaa iliyopita!

Mtu huyu mwenye suti nadhifu na yule mwenye mkoba waliongozana na kuingia kwenye chumba kimoja humohumo ndani ya jengo la NasBank! Ghafla, macho ya

Bwana Elisante yakatua tena kwa mama wa makamo wa kizungu aliyekutwa humo ofisini! Nae, alihisi ni kama alishapata kuonana nae mahali fulani! Bila kupoteza muda, hawa wageni na yule mama mzungu wakaanza kuelekezana kujaza fomu fulani. Ilichukuwa kama robo saa hivi na mara yule mtu mwenye suti nadhifu akafungua mkoba na kutoa kitu mithili ya hundi na kumkabidhi yule mama wa kizungu! Baada ya hapo, mtu huyuhuyu tena akaingiza mkono kwenye mkoba wake na kuibuka na mabunda mawili makubwa yenye dola mia mia na hapohapo ikaelekea ni kama kamera iligeuzwa na kumuonesha waziwazi huku akiwa ameshika mabunda ya dola za kimarekani!

*"Ni matumaini yangu kwamba zimetimia dola laki mbili!"* Huyo mtu aliyevaa suti aliongea kwa sauti ya utulivu akimuuliza yule mama wa kizungu!

Kijasho chembamba kilianza kumtoka mheshimiwa Elisante! Sasa akaikumbuka barabara siku hii, ikiwa ni miaka kadhaa iliyopita! Mwanzo wa filamu ulipaswa kuwa pale alipotembelewa nyumbani kwake na rafiki yake wa muda mrefu. Rafiki yake huyu aliyejulikana kama Steven Senya alimweleza kwamba kuna marafiki zake wapo nje ya nchi ambao wamepanga kuja kuwekeza Tanzania baada ya kusikia sera za uwekezaji zimeboreshwa. Hata hivyo, walitaka kufahamu endapo kuna mashirika ya umma yaliyo mbioni kubinafsishwa ili nao walete zabuni zao. Kutokana na urafiki wao, Bwana Elisante Josephat alimpatia Bwana Senya orodha ya makampuni yaliyokuwa mbioni kubinafsishwa. Baada ya kupatiwa orodha hiyo, nae akaipeleka kwa marafiki zake aliodai walikuwa nje ya nchi na siku ya pili tu wakarudisha majibu kwamba hayakuwa miongoni mwa biashara walizotaka kuwekeza.

Kufuatia hali hiyo, marafiki hao walileta aina ya mashirika ambayo wangependa kuyanunua na kuwekeza zaidi. Kwa bahati mbaya, aina ya mashirika waliyoyataka wao hayakuwa yale ambayo serikali ilipanga kuyauza! Hata hivyo, marafiki wa Steven Senya walisisitiza kuyahitaji hayo mashirika na kwamba walikuwa tayari *kuongea nao biashara*!

Na kweli, biashara ikaongelewa!

Kuanzia hapo ukaanza mkakati wa kuyaingiza mashirika mengine mawili kinyemela; yote yakiwa ni yale yaliyopendekezwa na rafiki zake Steven Senya! Mkakati huu ulifanywa na Bwana Elisante Josephat kwa kushirikiana na Dokta Joselyn Kimario!

Baada ya kufanikiwa zoezi hilo, akatafutwa mthamini ili afanye uthaminishaji! Hapa tena, ikafanyika *biashara* kati ya mthaminishaji na watendaji hawa wakuu wa serikali ambapo mthaminishaji alitakiwa kutaja nusu tu ya thamani halisi ya mashirika hayo!

Kufanikiwa kwa hujuma hiyo, ikafuata hujuma nyingine ya namna gani wangehakikisha kuwa mashirika hayo yananunuliwa na hao watu wao. Ili kuhakikisha kwamba hayaangukii mikononi mwa watu wengine, waliingiza baadhi ya masharti ya kipuuzi kabisa lakini waliyoamini wazabuni wengi wangeshindwa kuyatimiza ingawaje hayakuwa masharti yenye maslahi kwa taifa! Na kimsingi, masharti hayo yalikuwa yamependekezwa na hao hao watu wao rafiki zake Steven Senya. Kama walivyotarajia, masharti yaliyoongezewa yalikuwa mwiba mkali kwa wazabuni wengine na hivyo kupunguza kabisa nguvu za ushindani!

"Ndio hao mheshimiwa tunaotaka uwashughulike!" Ghafla Wendy aliongea kwa kejeli na kumzindua Bwana

Elisante Josephat toka kwenye lindi la kumbukumbu la tukio lile!

“Sikuelewi binti!” Hatimae Bwana Elisante alijikakamua na kuongea japo kwa sauti inayokwaruza!

“Ni nini hujaelewa mheshimiwa?”

“Nyinyi ni akina nani?” Mheshimiwa alijikuta akiuliza swali badala ya kujibu swali!

“Sikiliza Mheshimiwa, hatutakuwa watu wabaya kwako endapo utaamua kushirikiana na sisi. Hata hivyo, tutakuwa mwiba mkali kwako endapo hutataka kushirikiana kwavile hatutasita kuzisambaza picha hizi za video kwenye vyombo vya habari!” Michael Mchupi aliyekuwa kimya kwa muda mrefu aliongea kwa utulivu na kuyafanya matumbo ya Bwana Elisante kutoa mngurumo wa hofu!

Kuzisambaza kwenye vyombo vya habari!

Hili lisingekuwa jambo ambalo yeyote angependa hata kulifikiria litokee dhidi yake. Heshima ambayo Bwana Elisante Josephat alikuwa amejijengea kwa jamii ilikuwa ni kubwa mno kiasi kwamba wapo waliotabiri huenda siku moja akaja kuwa rais wa nchi hii! Kwa namna yoyote, asingependa heshima hiyo itoweke kirahisi hata kidogo.

“Mnataka tushirikiane nini?” Hatimae Bwana Mlaponi aliuliza kwa umakini huku akijaribu kutafakari kwa haraka mambo yote yanayotokea !

“Tunataka maafisa wote wa jeshi la polisi pamoja na askari wa upelelezi waliopo kwenye vituo vyote vikubwa jijini waamishwe ndani ya saa ishirini na nne!”

“*What*?!”(Nini?) Bwana Elisante aliuliza kwa taharuki kubwa!

“Umesikia mheshimiwa, litekeleze hilo ndani ya saa ishirini na nne zijazo nasi tutaendelea kukutunzia siri yako!” Wendy aliongea kwa upole kabisa.

“Mnataka kufanya uhalifu gani hapa jijini hadi mtake polisi wote wahamishwe?!”

“Sikiliza mheshimiwa, hatujasema jiji lisiwe na polisi, bali hawa waliopo wahamishwe kwavile wanaingilia maslahi yetu. Hata wewe bila shaka huwezi kuwa tayari kuona mtu anaingilia maslahi yako, na kama upo tayari basi tupe ruhusa ya kuzisambaza hizi picha kwa waandishi wa habari!” Wendy aliendelea kuongea kwa sauti ya utulivu kabisa lakini iliyokosa masihara!

“Sipo tayari kwa hilo, kwani huo ni usaliti mkubwa kwa nchi yangu!” Bwana Elisante alijitutumua kinaume!

“Huna aibu mheshimiwa, usaliti uliofanya ni mkubwa kuliko huu! Hata hivyo, hatukulazimishi kukubaliana na sisi katika hili. Hivyo basi, kwavile umekataa kufanya biashara na sisi, basi hatuna budi kukutakia jioni njema, nasi tunaondoka lakini sizani kama utakuja kupata nafasi nyingine mzuri kama hii!”Wendy aliongea kwa upole kisha akampa ishara Michael Mchupi kwamba waondoke. Hata hivyo, kabla hawajaufikia mlango, Bwana Elisante aliwaomba wasubiri!

“Naomba mnielewe, mimi sijakataa, bali mwenye uwezo huo katika mazingira kama hayo ni mkuu wa jeshi la polisi!” Bwana Elisante aliongea kwa unyonge.

“Ni kweli mheshimiwa, hata hivyo yeye yupo chini ya wizara yako na hivyo unaweza kumwagiza kutekeleza suala hilo!”

“Hilo unalosema lingewezekana endapo kungekuwa na sababu ambayo nae angeihafiki katika kutekeleza jukumu hilo.” Bwana Elisante alijitetea.

“Kama upo tayari tunaweza kukupa mbinu ambazo zitamfanya mkuu wa jeshi la polisi akubaliane na agizo lako.” Mchupi nae alieleza.

“Ok, nipo tayari endapo mnazani mbinu yenyewe itasaidia kuficha lengo halisi!” Bwana Elisante Josephat aliongea kwa utulivu na hivyo kutoa nafasi kwa Wendy kuanza kutoa maelekezo ya nini hasa anatakiwa kufanya kwa mkuu wa jeshi la polisi!

“Karibu Layla, jisikie nyumbani!” Bon Mtambo alimkaribisha Layla mara baada ya kufika safari yao. William Okello aliyekuwa ameketi kwenye sofa akiangalia televisheni alipigwa na butwaa kufuatia ujio wa Layla ambae alimuona ni kama malaika!

“Inakuwaje Bon, una kampuni ya uwakala wa urembo hapa jijini!?” Okello aliuliza katika namna ya utani.

“Nyinyi Waganda mkishakijua kiswahili tu mnakua na taabu sana! Hebu kutana na Layla hapa, huyu ndie Mrs. Bon Mtambo!” Bon Mtambo nae alijibu kwa utani!

“*What*?! (Nini?!)” Ghafla Jonathan Njoroge ambae alikuwa ndo anaingia hapo sebuleni aliuliza kwa kihoro! *It can’t be, is she really your wife?! Oh, my god*! (Haiwezekani, huyu msichana kweli ni mke wako? Mungu wangu!)!”

Njoroge aliendelea kuhoji huku akionekana kushitushwa na habari kwamba Layla ni mke wa Bon Mtambo! Bon Mtambo nae, alipotupa jicho kwa Layla, alikuta nae akiwa anatetemeka kwa hofu kiasi kwamba hata begi lililokuwa mikononi mwake lilishamponyoka kitambo!

Bon Mtambo na Okello wakabaki wameduwaa!

“Vipi tena? Mmefumaniana vijana wa Peterson Paul?!”Okello aliendeleza utani wake huku akicheka!

“Kuna nini kati yenu?! Mbona siwaelewi? Niambie Njoroge, Layla ni mchumba wako? Au ni mkeo?” Bon Mtambo nae alijikuta akiuliza maswali mfululizo, tena hata bila ya mpangilio! Bon Mtambo anakumbuka Layla aliwahi kumwambia kwamba yeye ni Mkenya, wakati Jonathan nae ni Mkenya! Hapa alipata picha kwamba inawezekana Layla na Jonathan wamewahi kuwa na uhusiano wa kimapenzi!

“Hebu niambie bosi, ni kweli huyu mwanamke ni mke wako?!”Jonathan Njoroge aliendelea kuhoji!

“Ni kama nilivyokueleza Jonathan, au nikuletee cheti cha ndoa?” Bon Mtambo alieleza huku akiamini Jonathan hawezi kuwa mbishi kiasi cha kutaka hadi kuthibitishiwa kwa cheti cha ndoa!

“Haina haja Bosi!” Jonathan aliongea kwa unyonge huku akishusha pumzi ndefu.

Bado Bon Mtambo na Okello hawakujua kinachoendelea kati ya Jonathan na Layla!

“Sasa tatizo ni nini Njoroge? Manake nakuona umekosa raha kabisa!” Bon Mtambo aliuza kwa utulivu.

“Muulize tu huyo mkeo, atakuambia! Ni matumaini yangu atakuambia ukweli!” Jonathan alijibu.

“Sawa Jonathan, ningependa tu kukuhakikishia kwa mara nyingine kwamba Layla ni mke wangu na ninampenda kuliko kitu chochote kile hapa duniani! Kwa kifupi nipo tayari hata kupoteza kila nilichonacho, ikiwa ni pamoja na kazi kwa ajili yake!” Bon Mtambo aliongea kwa hisia kali hali iliyomfanya hata Layla ashushe pumzi ndefu za kupata ahueni! Hata hivyo, Jonathan alianza kuwa na mashaka na kauli hii ya Bon Mtambo, kwani kwa jinsi alivyomfahamu, hakuwa ni mtu rahisi hivyo! Akaamua

kuacha kama yalivyo ili aone mwisho wake! Kwa upande mwingine, baada ya maelezo hayo, Bon Mtambo aliinuka na kwenda chumbani kisha akategesha kamera yake ya siri kabla ya kurejea tena kujumuika tena na wenzake.

"Okello na Njoroge," hatimae Bon Mtambo alianza kueleza, "kama mjuavyo hii kazi ni ya hatari sana hivyo mtaniwia radhi kwa hatua ya kumleta mke wangu kwenye makazi haya ya siri! Maharamia wananisaka mimi pamoja na wote wanaonihusu, na hapa mnaponiona ndo nimetoka kumwokoa toka mikono ya majahili! Kwa maana hiyo basi, naomba tuvumiliane. Aidha kwa upande wa Jonathan, hata kama Layla mlipata kukosana huko nyuma, basi naomba umsamehe hata kama jambo lenyewe ni la kikazi. Sikufanya ujinga kufunga ndoa na huyu msichana, kwakweli ni mtu ambae amenisaidia sana maishani mwangu! Lazima niseme wazi kwamba, kama si Layla huenda hivi sasa ningekuwa kaburini!" Bon Mtambo aliongea kwa hisia kali, hali iliyomfanya hata Layla mwenyewe aanze kudondosha machozi!

Sasa Layla akaamini wazi kwamba ni kweli Bon Mtambo alikusudia kuwa nae!

"Nimekuelewa bosi, samahani sana kwa yote!" Jonathan alijibu kisha wakaanza kuongea mambo mbalimbali kabla Bon Mtambo na Layla hawajatoka hapo sebuleni na kuelekea chumbani!

"Ahsante sana Bon, yaani nashindwa kuamini kama kweli umeamua kunisamehe!" Layla aliongea huku akibubujikwa machozi mara walipofika chumbani. Ilibidi Bon Mtambo afanye kazi ya ziada ya kumtoa kifuani pake!

"Usijali Layla, hata hivyo, najisikia wivu sana kwavile nahisi ama ulikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Jonathan, au na mtu wake wa karibu! Nahisi Jonathan

ameshindwa kusema ukweli kwavile ananionea aibu bosi wake. Hata hivyo, nina amini tutakapokua wawili mimi na yeye, ataniambia ukweli. Hivyo basi, nisingependa kusikia ukweli kwa mara ya kwanza kutoka kwake, bali ningependa kuusikia kutoka kwako! Je, Jonathan ni mpenzi wako?" Bon Mtambo alijifanya kulalamika!

"Ondoa hofu Bon, Njoroge sio mpenzi wangu na wala hajawahi kuwa mpenzi wangu. Na wala sijawahi kuwa mpenzi wa yeyote miongoni mwa watu wake!" Layla aliongea kwa utulivu akiwa amekaa kitandani.

"Sasa ni nini chanzo cha yote yale?"

"Ni hadithi ndefu Bon, lakini kama hutajali nitakusimulia mkasa mzima na hapo ndipo utakapogundua ni kwanini niliingia kwenye mtandao wa uhalifu wa akina George Kamau!"

"Bila shaka, nipo tayari kuisikia simulizi hiyo. Hata hivyo, ningependa kwanza kupata simulizi ya Wendy na Mchupi kwenda kwa waziri wa mambo ya ndani!" Bon Mtambo alieleza kwa utulivu huku akionekana kama hakua na shida sana na habari hiyo! Ili kuanza kujijengea uaminifu mbele ya Bon Mtambo, Layla alitumia nafasi hiyo kueleza mkakati mzima wa kumshinikiza waziri aingilie utendaji wa jeshi la polisi!

"Kwahiyo kesho tutarajie uhamisho wa kushitukiza wa watendaji mbalimbali wa jeshi la polisi?" Hatimae Bon Mtambo aliuliza huku akionekana wazi kuchanganyikiwa na habari hiyo!

"Ndio maana yake Bon!" Layla alijibu.

Bon Mtambo aliinuka na kumpiga busu Layla kisha akaelekea sebuleni.

"Bila shaka nazani mngehitaji kupata kazi nyepesi itakayouchangamsha ubongo wenu kabla ya mshikimshike

wenyewe!" Bon Mtambo aliwaambia Okello na Njoroge mara baada ya kufika sebuleni!

"Tunakusikiliza wewe bosi!"

"Ok, sasa ni hivi, nataka mkamteke nyara Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini na mje nae hapa usiku huu huu! Hakikisheni hamumdhuru na wala kuleta uharibifu wowote nyumbani kwake! Nyumba yake inalindwa na polisi wa kawaida tu ambao kwa watu kama ninyi hawatawasumbua. Aidha, pitieni kituo kikuu cha polisi na muulizieni SSP Faraji Zegge. Nyinyi jitambulisheni kwake kama WIB K (kifupi na utambulisho kwa mwakilishi wa WIBAIC Kenya)na WIB U (WIBAIC Uganda), nae atajitambulisha kwenu kama AST. Yeye mtaenda nae kwa mkuu wa polisi na mtakuwa pamoja kwenye hiyo operesheni. Nitafanya mawasiliano na AST hivi punde! Kwa upande wangu, mimi nitabaki hapa kwa muda nikiendelea kumhoji huyu msichana!" Bon Mtambo alitoa maelekezo kwa akina Okello.

"Ni mahojiano gani hayo ya kufanyia chumbani ambako hata meza hamna!" Hatimae Okello aliongea kwa utani na kuwafanya wote waangue kicheko.

Jaffery Minga, Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, aliziparamia kwa haraka ngazi za ofisi ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Bwana Elisante Josephat . Awali ya yote, labda kutokana na hali ya utulivu iliyopo nchini, haikuwahi kutokea kuitwa na waziri muda kama huo! Aidha, kubwa zaidi ni lile sharti la kwamba ahakikishe hakuna mtu anayefahamu juu ya kuja kwake kwa kile alichoambiwa ni kwa ajili ya *usalama wa taifa*!. Kutokana na

wito huo jinsi ulivyokuwa, IGP Minga aliamini bila shaka kuna jambo zito limetokea!

“Karibu Bwana Minga, najua ulishitushwa sana na wito huu wa ghafla lakini ilibidi iwe hivyo kabla mambo hayajaharibika zaidi.” Bwana Elisante Josephat , waziri wa mambo ya ndani alimkaribisha IGP Minga.

“Ahsante mheshimiwa! Kwa mtu kama mimi kuitwa muda wowote ni jambo la kawaida kwangu, hata kama ingekua usiku wa manane!”

“Ok, nazani tusipoteze muda, kwa kifupi ni kwamba, kuna jambo zito lipo njiani kutokea ambalo moja kwa moja linakuhusu wewe binafsi! Kutokana na unyeti na uzito wa jambo lenyewe, nilikata shauri la kukudokeza ili ikiwezekana uchukue hatua ingawaje tunachofanya ni kinyume na maadili ya utendaji. Hata hivyo, punguza hofu kwavile tumeshapata baraka zote kutoka juu za kushughulikia suala lenyewe ili lisiharibu taswira ya jeshi letu.” Bwana Elisante Josephat alifungua maongezi katika hali ya kirafiki zaidi kuliko kikazi, kisha akamalizia na swali: “Sasa niambie Minga, kuna biashara yoyote unayofanya ambayo si halali kwa mujibu wa sheria?”

“Mbona sikuelewi mheshimiwa!” IGP Minga aliuliza huku akionesha wazi kushitushwa na swali la Bwana Elisante Josephat .

“Ni kweli huelewi?”

“Kweli kabisa mheshimiwa!”

“Sasa sijui tufanye nini IGP, unajua hata mimi niliposikia hili jambo nilishangaa sana! Kwakweli itabidi tusaidieni akili manake hata mzee anasubiri jibu toka kwangu!” Bwana Elisante Josephat aliongea kwa sauti ya upole!

“Mbone sikuelewi mheshimiwa?!”

"Sikiliza Minga, kwa kifupi ni kwamba, jeshi la polisi nchini Rwanda kwa kushirikiana na Interpol wamekuwa wakifuatilia mtandao mmoja unaojihusisha na usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya pamoja na silaha nchini Rwanda na Kongo DRC. Serikali ya Rwanda na Interpol wanadai mtandao huo una uhusiano wa moja kwa moja na vigogo wa jeshi letu la polisi! Baada ya kuendelea na uchunguzi wao, wakabaini kwamba Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania ndie anayeulinda mtandao huo haramu! Baada ya ugunduzi huo, wakaona kazi iliyokuwa mbele yao ilishakuwa ngumu kwavile waliamini endapo mkuu wa jeshi la polisi anahusika basi hata vigogo wa serikali, au serikali yenyewe nayo inahusika! Kutokana na hisia hizo wakaamua kutoa taarifa kwa serikali ya Rwanda na kuomba ushauri wa nini cha kufanya. Serikali ya Rwanda ilipopata taarifa hiyo, nayo ikaamua kuwasiliana na serikali ya Tanzania kupitia wizara yangu! Hapa ninapokuambia, tayari wana usalama kutoka Rwanda na wale wa Interpol wapo nchini wakisubiria ruhusa kutoka kwangu ili waje kukufanyia upekuzi kwa kushirikiana na polisi wa hapa nchini!" Waziri wa Mambo ya Ndani, Bwana Elisante Josephat alimalizia maelezo yake na kumtupia jicho la udadisi ili aone endapo karata yake ilikuwa na dalili za kufua dafu!

"Kwahiyo ina maana ni mimi ndie niliye na uhusiano na huo mtandao?" Hatimae IGP Minga aliuliza baada ya kushusha pumzi mzito huku uso wake ukiwa umesawajika kwa taharuki! Hakika taarifa hii ilimshitua mno kuliko kitu chochote kilichopata kutokea ndani ya utumishi wake ndani ya jeshi la polisi.

"Ndio manake IGP!" Bwana Elisante Josephat aliongea kwa kwa kifupi na kujiamini kabisa!

“Na wewe umeziamini mheshimiwa?” IGP  Minga aliuliza kwa simanzi kubwa!

“Ni wewe mwenyewe ndie mwenye jibu kamili kuhusu tuhuma hizo, na ndio maana mimi nimekuita kwa siri ili uniambie ukweli. Mimi nimekuita kwa ajili yako binafsi na mustakabali mzima wa taswira ya jeshi letu na nchi kwa ujumla. Hata mzee ameniagiza nilishughulikie suala hili kabla mambo hayajaharibika zaidi!” Bwana Elisante Josephat  aliendelea kuzichanga karata zake.

“Mzee yupi?” IGP aliuliza kwa taharuki.

“Unazani ni nani niwezae kumwita mzee?! Kwa taarifa yako ni kwamba hata rais wa nchi amezipata taarifa hizi na ni yeye ndie aliyeniagiza tulishughulikie suala hili mapema iwezekanavyo. Kimsingi, mzee amechukizwa sana na habari kwamba wewe unahusika na mtandao huo lakini nikampoza kwa kumwambia inawezekana ikawa si kweli.”

“Kwakweli mheshimiwa, nakuhakikishia kwa majina ya miungu yote kwamba mimi sihusiki hata chembe na mtandao wowote wa uhalifu hapa nchini na hata nje ya nchi!” IGP  Minga alijitetea huku ujasiri wake wa kipolisi ukiwa umeshatoweka kitambo!

“Sasa unazani nini chanzo cha taarifa hizi?” Bwana Elisante Josephat  aliuliza kwa upole.

“Siwezi kufahamu mheshimiwa. Hata hivyo lazima ujue kwamba kwa mtu kama mimi si jambo la ajabu kuwa na maadui wa ndani na hata nje ya nchi. Kila mmoja anafahamu ni namna gani nilivyo mstari wa mbele katika upigaji vita vitendo vyote vya kihalifu nchini. Kwa maana hiyo si ajabu kuona tayari nimejitengenezea maadui kadhaa ndani na nje ya nchi kwavile uhalifu wa zama hizi hauna mipaka!” IGP  Minga alijaribu kujitetea.

“Sasa sikiliza Minga, huna haja ya kujitetea sana kwani serikali tayari imeenda mbali kidogo ya hapa. Baada ya mzee kuzipata habari hizi, aliagiza watu walio ndani kabisa ya usalama wa taifa wafanye uchunguzi wa haraka sana ili angalau tu kubaini ukweli wa jambo hili. Baada ya kufanya uchunguzi huo walibaini kuwepo kwa mtandao mmoja wa kihalifu wenye makao yake jijini Nairobi nchini Kenya na tawi lake hapa Dar es salaam. Aidha, mtandao huo una watu wake wengi katika jeshi la polisi, hususani Dar es salaam pamoja na miji mingine mikubwa nchini kama Arusha na Mwanza! Vilevile wanausalama wetu wamebaini kwamba kuna mkakati kabambe unaosukwa wa kukung’oa ili awekwe mtu wao. Hawana wasiwasi kwamba endapo wewe utaondolewa basi mwingine yeyote ambae atawekwa anaweza kuwa ni mtu wao. Hii ni kwavile tayari kuna orodha ndefu ya vigogo wa jeshi la polisi nchini wanaolipwa na mtandao huu! Aidha, uchunguzi huo umeweka bayana kwamba, kwa jinsi walivyojiandaa na kujipanga, basi kuna uwezekano mkubwa sana wa wewe kuingia mtegoni kupitia kwa vijana wa polisi tulionao. Kutokana na hilo, nina hofu hata habari hizi za wewe kuhusika na biashara haramu ni moja ya mikakati hiyo ya kukumaliza! Nahisi kuna kitu wamepanga kufanya kupitia tuhuma hizo, hivyo kuwa makini sana na usithubutu kumuamini mtu yeyote kwa sasa, hususani toka ndani ya jeshi lako!” Waziri wa Mambo ya Ndani, Bwana Elisante Josephat alimalizia maelezo aliyoelekezwa na Wendy kwamba ayatoe kwa IGP Jaffery Minga! Baada ya maelezo hayo, alimtupia jicho IGP Minga ambae alionesha wazi kuwa amechanganywa na taarifa hii.

“Sasa unazani nini kifanyike mheshimiwa?” Hatimae IGP Minga aliuliza kwa unyonge.

“Kwavile hadi sasa hatujui orodha ya walipwao na mtandao huu, basi hatuna budi kuchukua tahadhali kwa vijana wetu wote wa polisi. Na ili tusionekane tunachelewa kutoa maamuzi ya wao kufanya kazi yao na hivyo kutafsirika kwamba tunajaribu kukulinda basi hatuna budi kuchukua hatua za maana mapema iwezekanavyo. Hatua ya kwanza, ni kuhamisha maafisa wote wa jeshi la polisi waliopo kwenye miji hiyo niliyotaja pamoja na askari wa upelelezi. Hata hivyo, maafisa watakaohusika hapa ni wale walio kwenye vituo vikubwa tu! Na kuhusu wale wa Makao Makuu, tunasubiria maagizo kutoka watu wa usalama wa taifa! Na kazi hiyo inabidi ifanyike ndani ya saa ishirini na nne zijazo. Ni matumaini yetu kwamba, hakuna raia atakayehoji kwavile wengi wanachukulia uhamisho wa ghafla wa watendaji wa polisi ni kama njia ya kusafisha jeshi. Bila shaka umenielewa!” Alimalizia.

“Ndio mheshimiwa, nimekuelewa na lazima nitumie fursa hii kuishukuru serikali kwa kuniamini kwamba siwezi nahusika na uhalifu!” IGP Minga alieleza.

“Serikali inakuamini sana Inspekta na ndio maana imejitoa muhanga kukulinda. Hata hivyo, ukumbuke kwamba hatutakiwi kuongea wala kufanya chochote kitakachoashiria kwamba mzee alitia mkono kwenye jambo hili. Na endapo kutatokea jambo au aina ya fitina yoyote ya kisiasa kuhusu jambo hili, mimi nitakuwa na jukumu la kulifanyia kazi!” Bwana Elisante aliongea kwa utulivu huku nafsi yake ikishangilia ushindi huku akistaajabia akili za Wendy!

“Nilipomaliza masomo ya upili niliamua kusoma diploma ya uandishi wa habari kwavile ni kazi ambayo niliipenda tangu utotoni!” Hatimae Layla alianza kueleza kisa chake: “Baada ya kutunukiwa diploma nilifanya kazi ya uandishi wa habari kwa takribani miaka miwili lakini nikaona hailipi hivyo nikaamua kusomea fani ya utalii na usimamizi wa hoteli na kufanikiwa kuajiriwa kwenye hoteli moja ya kitalii iliyopo Mombasa.“

“Nilifanya kazi hapo hotelini kwa miaka miwili hadi nilipokutana na Muitaliano mmoja aliyejulikana kama Roberto. Bila kutarajia, mimi na Roberto tukajikuta tumetumbukia kwenye mapenzi na pale yalipokolea akaniachisha kazi na yeye kuamua kufanya makazi hapohapo Mombasa ambako alijenga hoteli mbili za kitalii.”

“Siku moja Roberto aliniaga anaenda Italia na kwamba angerudi baada ya juma moja! Alipoondoka, nami nikapata dharura, nikaenda Zanzibar na siku niliyorudi na kufika nyumbani nilikuta mkoba wa Roberto ukiwa kitandani hali iliyoonesha kwamba alikuwa amerudi safari yake kimyakimya! Hata hivyo, sikushangaa kwavile nilifahamu tabia yake ya wivu!”

“Nilimsubiria Roberto kwa muda mrefu bila ya yeye kutokea! Ajabu, hata nilipoijaribu simu yake ya mkononi ilikuwa haipatikani! Nilisubiri zaidi lakini mara nikaingiwa na hamu ya kufungua mkoba wake!Nilifanya hivyo huku nikifahamu fika ni jinsi gani Roberto hapendi mtu afungue mkoba wake!”

“Baada ya kufungua, sikuamini macho yangu baada ya kukuta mkoba umejaa paketi za dawa za kulevya! Nikiwa bado kwenye mshangao huo ghafla Roberto aliingia chumbani na kunikuta nikiwa nazikodolea macho

paketi hizo! Kuona hivyo, Roberto alinivamia akiwa amefura kwa hasira na kuanza kunishushia kipigo kikali! Pamoja na kwamba nililia kwa maumivu na kumuomba aniachie lakini ilikuwa ni kazi bure kwani aliendelea kunishushia kipigo kisha akachukua bastola ili animalize. Na vile alivyokuwa amechukia nina hakika angeniua kweli! Na katika kujitetea, niliwahi kuokota chuma kizito kilichokuwa humo chumbani na kumtwanga nacho kichwani! Hakika sikuwahi kujiuliza nini yangekuwa matokeo ya kipigo hicho, na hadi leo bado sijui matokeo ya pigo lile hasa yalikuwa nini! Hata hivyo, baada ya pigo lile Roberto alidondoka chini huku akivuja damu nyingi huku mwenyewe akionekana kuwa kati ya uhai na umauti! Kufuatia taharuki ambayo ilinikumba kwa kuamini nimeua, nilijikuta nikidondoka chini na kupoteza fahamu kwa kihoro! Pale nilipozinduka karibu nusu saa baadae, nilijikuta nikiwa nimekaa kitini huku nikiwa nimeshika bastola mkononi! Aidha, kichwa cha Roberto nacho kilikuwa kimefumuliwa vibaya kwa risasi! Si hivyo tu, mkoba uliokuwa na dawa za kulevya nao, ulikuwa umetoweka!

"Bon, siwezi kukueleza ni namna gani nilichanganyikiwa baada ya hali hiyo! Hapohapo nikahisi akili yangu ni kama imesimama na hivyo kukosa uwezo wa kutafakari! Nikiwa bado sijafahamu nini cha kufanya mara simu ya mezani iliita! Baada ya kuipokea simu hiyo, mtu ambae alijitambulisha kwangu kama Inspekta Jonathan Njoroge alisema kwamba amepata taarifa ya kutokea mauaji; hivyo alitaka uthibitisho! Kwakweli nilichanganyikiwa sana kiasi kwamba sikutaka hata kuendelea kuisikiliza hiyo simu. Nilikuwa namfahamu vilivyo Njoroge hususani katika kupambana na wahalifu!

Nilijua lazima angenisaka kwa gharama yoyote ile! Hapo hapo nilizoazoa kila kilicho changu na kwenda kukodi mashua ambayo muda huo huo ilinipeleka Pemba. Hapo Pemba sikukaa, nikaenda Zanzibar kisha nikasafiri hadi Comoro ambako niliweka makazi yangu kwa takribani miaka mitatu. Nilipohisi huenda kesi yangu imepoa kidogo niliamua kurudi Zanzibar na hatimae kuja Dar es salaam. Nilipofika Dar es salaam na kukaa kwa takribani miezi mitatu nikakutana na mtu mmoja aitwae George Kamau ambae ni raia wa Kenya. Ni huyu George Kamau ndie alinishinikiza kujiingiza kwenye kazi hii iliyonikutanisha na wewe. Na hata pale nilipokataa, alitishia kwamba angetoa taarifa polisi kwamba nimekimbia kesi ya mauaji ya mfanyabiashara maarufu mjini Mombasa. Na ili kuthibitisha madai yake, alitoa picha zilizonionesha nikiwa nimesimama nimeegemea meza na bastola mkononi huku nikiangalia maiti ya Roberto! Usoni nilikuwa nimevaa miwani ya giza iliyoshindwa kuonesha endapo macho yangu yalikuwa yamefumba au hapana! Hata hivyo, sina shaka yoyote kwamba nilikuwa nimefumba na ndio maana walinivisha miwani ya giza ili kuyaficha! Si hivyo tu, hapo mezani ulionekana ule mkoba uliokuwa na dawa za kulevya huku paketi zake zikionekana waziwazi! Hakika picha hizi zilithibitisha wazi kwamba nilimuua Roberto kwa risasi labda ili nimdhurumu hizo dawa! Baada ya kutoa ushahidi huo wa picha, George akaniambia wazi kwamba endapo sitakubali matakwa yake basi atazivujisha picha hizo kwa wanausalama, hususani kwa Jonathan Njoroge aliyekuwa mpelelezi wa kesi yangu. Hivyo basi, nazani umefahamu ni kwanini Jonathan alishituka aliposikia mimi ni mke wako kwavile ananisaka ili nikajibu tuhuma za mauaji! Aidha, hiyo ndio sababu iliyonifanya

niingie kwenye uhalifu huu wa sasa!" Layla alimalizia simulizi yake na kumfanya Bon Mtambo ashushe pumzi!

"Pole sana Layla, hata hivyo naamini utaendelea kuwa mtumwa wa George Kamau hadi kundi lao litakapotoweka duniani!" Bon Mtambo alieleza kwa utulivu.

"Ni kweli Bon, nami nipo tayari kushirikiana na wewe kwa kila hatua. Lakini huzani akishagundua kwamba mimi nipo nanyi kwa sasa anaweza kuzitoa hizo picha?" Hatimae Layla alitoa dukuduku lake!

"Hawezi kufahamu, na hata pale atakapokuja kufahamu, tayari atakuwa hana uwezo tena wa kufanya chochote. Hata hivyo, bado kuna mengi ninayohitaji kufahamu kuhusu George Kamau hususani nafasi yake ndani ya IBU." Mtambo alihoji.

"George ndie bosi wa IBU anayefahamika!"

"Kwanini unasema ndie anayefahamika?"

"Yupo bosi mkuu ambae ndie anatoa maagizo kwa George lakini hamna mtu yeyote anayemfahamu bosi huyo zaidi ya George mwenyewe! Hata hivyo, inasemekana kwamba huyo bosi ni mzungu!" Layla alijibu.

"Kazi ya IBU hasa ni nini?"

"IBU ni mtandao wa kihalifu uliopo nchini na kuna mkakati wa kusambaza shughuli zake ukanda wote wa afrika mashariki na maziwa makuu. Kikweli sina mengi sana ninayofahamu kwani hata utendaji wake wa kazi unafanyika kwa umakini wa hali ya juu. Mathalani, ingawaje mtandao huu ni mkubwa sana lakini hata sisi kwa sisi hatufahamiani. Utapata fursa ya kufahamiana na wenzako endapo tu utakuwa umepata kupangiwa kazi nao." Layla alieleza kisha akaelezea hatua mbalimbali zinazofanywa na IBU katika kuwatumia watu wenye

ushawishi mkubwa katika kutekeleza matakwa yao. Ingawaje hakutaka kujionesha, lakini Bon Mtambo alishitushwa sana na maelezo hayo ya Layla!

"Mbali na George Kamau, ni nani mwingine unayemfahamu kuhusika na IBU?" Bon Mtambo aliuliza.

"Nawafahamu Wendy na Mchupi pekee! Hata hivyo, wapo wengine wengi ila ni kama nilivyokuambia hapo awali ni namna gani inakuwa ngumu kufahamiana."

"George Kamau anatambulika kwa shughuli gani machoni mwa jamii?"

"Anamiliki kampuni ya ushauri juu ya masuala ya uwekezaji inayoitwa East Africa Opportunities & Consultancy (EA-O&C) iliyo na ofisi zake Sokoine Drive. Tena umenikumbusha Bon, kupitia kampuni yake hii, George Kamau amekuwa akikutana na wawekezaji kutoka nje wenye nia ya kuwekeza hapa nchini na kuwaelekeza njia zisizo halali za namna gani wanaweza kushinda zabuni au kupata mikataba ya kuwekeza. Huo nao unakuwa ni moja ya ushauri anaoutoa kwa wateja wake! Na kwavile tayari IBU ina orodha ya viongozi kadhaa, basi inawawea rahisi kuwafuata na kuwaomba waendelee kukiuka taratibu na pale wanapobisha wanatishia kufichua siri zao! Na kwa mtindo huo, unakuta viongozi walewale wakiendelea kuitia hasara serikali. Na ninakuhakikishia Bon, endapo serikali haitashituka mapema na kuanza kuchuka hatua, basi ipo siku utakuja kusikia limefanyika hata jaribio la kuuza benki kuu!" Layla alimalizia na kumfanya Bon Mtambo aangue kicheko cha huzuni!

"Je, kuna kampuni yoyote ambayo unaifahamu ambayo imewahi kuhusika katika haya mambo?"

"Hapana Bon, labda ukianzia pale ISLIB na EA-O&C huenda ukapata lolote la kukusaidia." Layla alijibu na

kumpatia Bon Mtambo nafasi ya kutafakari maelezo yake kwa kina.

“Kamau huwa anaondoka ofisini saa ngapi?”

“Kwakweli Kamau ni mchapa kazi hasa! Hususani siku hizi ambazo wewe umeingilia kazi za IBU, huwa anakuwepo ofisini hadi saa nne usiku, na wakati mwingine zaidi ya hapo!” Layla alijibu bila wasiwasi.

“Na vipi kuhusu mazoea kati yako na Kamau?” Bon Mtambo aliuliza na kumuona Layla akibabaika kidogo hali iliyomfanya ahisi kuwepo na jambo fulani kati yao. Hisia hizi zilimpa nguvu zaidi akizingatia uzuri wa Layla ambao ungeweza kumzuzua mwanaume yeyote.

“Mbona hujibu Layla?” Hatimae Bon Mtambo alikumbusha baada ya kuona bado Layla yupo kimya!

“Samahani, nilikuwa mbali kidogo kimawazo! Ni kweli Bon, nina mazoea na uhusiano wa karibu sana na George, lakini naomba usiulize maswali mengi zaidi!”Layla alijibu huku akionekana kukosa raha ghafla!

“Usihofu Layla, hapa ninachofanya ni kupata taarifa muhimu zitakazotuwezesha kuwatokomeza akina Kamau!” Bon Mtambo aliongea kwa sauti ya utulivu katika namna iliyoonesha kutaka maelezo zaidi.

“George ni mpenzi wangu, hata hivyo ni mapenzi ambayo hayakutokana na utashi wangu! George kashika mpini nami nimeshika makali hivyo anaweza kunitumia vyovyote atakavyo!” Layla aliongea kwa uchungu.

“Pole sana Layla.”

“ Ahsante Bon.”

“Je, una mazoea ya kwenda ofisini kwa Kamau nyakati za usiku?”

“Huwa naenda wakati wowote ninaojisikia!”

“Je, Kamau ana mazoea ya kulala kwako?”

"Mara nyingi tu anafanya hivyo!"

"Ok Layla, sasa hebu nieleze muundo wa ofisi hii ya Kamau endapo mtu anataka kuingia kwa siri. Usisahau muundo wa madirisha vilevile!"

"Jengo lenyewe ni dogo tu lenye ghorofa moja na linalindwa na walinzi watatu wa kampuni moja ya ulinzi lakini sio ISLIB! Hata hivyo, walinzi hao ni waaminifu sana kwa George kwavile mbali na kulipwa na kampuni yao, lakini pia mara kwa mara George huwa anawapa bakshishi ya kutosha! Na walinzi hao wamekuwa ni kama wameajiriwa kabisa na George kwani wakati wote wanakuwa wao!" Layla alieleza kisha akaanza kuelekeza muundo wa ofisi yenywe!

"Sasa Layla, nataka mimi na wewe tushirikiane usiku huu, je upo tayari?" Hatimae Bon Mtambo aliuliza.

"Ina maana niende na wewe hadi kwa George, au!?"

"Hapana, hatutaenda pamoja!"

"Sasa tutashirikiana vipi?"

"Nijibu kwanza kama upo tayari!"

"Si nilishakuambia kwamba mimi hivi sasa nipo upande wako? Au huniamini? Narudia tena, mimi nitakuwa na wewe bega kwa bega kwavile nimeshachoshwa na utumwa toka kwa Kamau!"

"Nimefurahi kusikia hivyo mpenzi, sasa sikiliza, kwanza itabidi umpigie simu kumuuliza yupo wapi, na kama bado yupo ofisini mwambie akusubiri hapo kwa vile una jambo muhimu unataka kumweleza! Ukishafika tumia mbinu zako zote umshawishi akalale kwako. Aidha, kabla hujaondoka hapo ofisini hakikisha unafanya hila za kufungua dirisha la upande wa kulia na kuliegesha ili isijulikane kwamba limefunguliwa. Fanya zoezi hilo wakati mpo tayari kuondoka ili asipate nafasi ya kuchunguza!

Vilevile, kabla ya kuondoka jipe jukumu la kuyakagua madirisha kuangalia kama yamefungwa. Tena fanya hivyo wakati anakuona! Aidha, nitakupatia kichupa kidogo chenye dawa za usingizi. Dawa hii haina harufu, rangi wala madhara kwa mtumiaji na huanza kufanya kazi baada ya robo saa tangu mtu aivute dawa hiyo! Dawa hiyo ni ya kupuliza mithili ya dawa ya mbu, na ina uwezo wa kubakia na nguvu kwa dakika kumi tangu kupuliziwa. Yaani, endapo utapulizia chumbani, mtu yeyote atakayeingia ndani ya dakika kumi tangu kupulizia, basi lazima atalala baada ya robo saa tu kupita! Hivyo basi, mkishafika nyumbani hakikisha Kamau anakuwa ndie mtu wa kwanza kwenda kuoga. Na muda mfupi kabla ya kutoka bafuni, pulizia hiyo dawa chumbani na ukishafanya hivyo usiingie tena. Ni matumaini yangu kuwa, akishatoka bafuni ataenda moja kwa moja chumbani ambako atakuta bado dawa ina nguvu. Mvuto mmoja tu wa hewa unatosha kabisa kumlaza zaidi ya masaa matatu hadi manne! Akishaingia chumbani, nawe mara moja utaenda bafuni ili kumnyima nafasi ya endapo atataka uende chumbani kwa shughuli yoyote ile kwa wakati huo! Tumia si chini ya robo saa huko bafuni! Je, utaiweza hiyo kazi?" Bon Mtambo alimalizia maelezo yake kwa swali.

"Hata sasa tunaweza kuanza kuitekeleza ingawaje hujanieleza nini kitafuata mara baada ya yeye kulala!"

"Hayo yatafanyika wakati mimi nikiwa jirani na pale kwako! Ukishathibitisha kwamba amelala fofofo, utamwibia funguo zake kisha utaniletea sehemu nitakayokuwa nakusubiri nami nitazirudisha funguo hizo mara baada ya kumaliza kazi yangu pale! Aidha, hakikisha asubuhi unaongozana nae hadi ofisini ili ukawahi kulirekebisha dirisha kabla hajagundua kwamba lilikuwa

wazi halafu akaanza kupata mashaka! Mimi nitafanya upekuzi wangu kwa umakini kabisa na ninaamini hatafahamu kwamba kuna upekuzi ulifanyika!"

"Sawa Bon, twende tukaanze hiyo kazi sasa hivi ili tumwahi kabla hajatoka ofisini."

"Ni kweli mpenzi, kwani akishawahi kutoka itanilazimu tupangue utaratibu wote! Hata hivyo, sina budi kukuonya kwamba usijaribu kunichezea akili kwa kuusaliti mpango wetu na kurudi tena upande wa Kamau. Nimelazimika kufanya ufedhuli kidogo kwa kurekodi maongezi yetu mimi na wewe tangu tumeingia humu chumbani! Aidha nimelazimika kuchukua picha za siri vilevile. Hata hivyo, nakuhakikishia kwamba sitarajii kutumia picha na maongezi haya kwa ajili ya kukusaliti lakini sitasita kufanya hivyo endapo wewe utaanza kunisaliti!" Bon Mtambo aliongea na kumpiga busu moja lililomsisimua Layla kiasi cha kumfanya akae tena kitandani ingawaje alishainuka kwa ajili ya kuondoka!

"Unamaanisha nini Bon?" Hatimae Layla aliuliza baada ya kukaa sawa kiakili.

"Maana yangu ni kwamba endapo utajaribu kunisaliti basi picha na maongezi haya nitaziwasilisha kwenye vyombo vya habari na vyombo vya usalama!"

"Sasa una tofauti gani hapo kati yako na IBU?" Layla aliuliza kwa utulivu huku akionekana kuhamanika.

"Kuna tofauti kubwa sana Layla. IBU wanafanya haya kwa maslahi yao binafsi lakini mimi nimelazimika kufanya hayo kwa maslahi ya taifa!"

"Hofu yako tu Bon, mimi hivi sasa ni mtu mwingine kabisa. Na wala siogopi tena hata ukiamua kunifikisha kwenye vyombo vya usalama kwa mauaji ya Roberto

kwavile nitakuwa nimefikishwa na mtu aliyeujua ukweli!"

Ilikuwa inakaribia saa tano kasorobo usiku wakati Bon Mtambo alipofika jirani na ofisi ya East Africa Opportunities & Consultancy; kwa kifupi EA-O&C inayomilikiwa na George Kamau. Alifika hapa akitumia gari ya polisi ambayo kwa kawaida hutumika kwa doria! Hii ilikuwa ni baada ya kupata funguo toka kwa Layla! Mtaa wote ulikuwa kimya kabisa. Hata hivyo, kabla hajafika hapa alikuwa amewasiliana na DCI Mwaiswelo kumuomba awaagize TANESCO wakate umeme maeneo yote ya posta ifikapo saa tano kasoro dakika kumi! Aliagiza umeme ukatwe kwa robo saa kabla ya kuurejesha tena!

Kabla hajateremka kwenye gari akakumbuka kitu! Kwamba alitakiwa amwagize Layla ampigie pindi atakapofika hapa ili apate sababu ya kuwaingia walinzi waliopo. Akafikiri kwa haraka haraka akapata jibu! Akachukua simu yake na kutafuta namba ya SSP Faraji Zegge kisha akamtumia ujumbe mfupi wa maneno kwamba ampigie simu baada ya dakika tano. Alipomaliza kutuma ujumbe huo, alirekebisha jina la mwenye hiyo namba; badala ya SSP Faraji Zegge akaandika jina la George Kamau! Baada ya kumaliza zoezi hilo, alisogeza gari mbele kidogo na kusimamisha upande wa pili wa barabara kutoka ilipo ofisi ya Kamau. Aliteremka huku akiongea kwa simu ingawaje kiukweli alikua haongei na yeyote! Alikuwa tu anawapumbaza hawa walinzi!

"Ndo nafika hapa ofisini lakini inaonekana bado hajafika kwani ofisi imefungwa....Ndio, walinzi wapo na wanaendelea na kazi kama kawaida....Hapana, kama

wanakufahamu basi ni vizuri waulize wewe mwenyewe...Sawa, kata halafu piga baada ya dakika kama moja hivi!" Bon Mtambo alimaliza kuongea na simu yake ya hadaa kisha akawakabili walinzi!

"Habari zenu za kazi!" Bon Mtambo aliwasalimia.

"Safi afande, sijui tukusaidie nini?" Mmoja alijibu kwa niaba ya wenzake kwa unyenyekevu wa hali ya juu baada ya kuhisi kuwa Bon Mtambo ni polisi wa doria kutokana na gari aliyokuja nayo na nguo alizovaa!

"Bila shaka mnamfahamu Bwana George Kamau?"

"Ndio!"Wote waliitikia kwa unyenyekevu!

"Kwa kifupi mimi naitwa Sajini Meja Sylvester Mokiwa toka kituo kikuu cha polisi! Nipo hapa kwavile kuna suala tunataka kufanya na Kamau pindi atakapofika. Yeye aliondoka hapa ofisini majira ya saa tatu usiku huu akiwa na mchumba wake. Sasa kuna tatizo limewakuta kwahiyo wanakuja hapa muda si mrefu! Chukua hii simu, huyo mchumba wake atapiga muda si mrefu anataka kuongea na mmoja wenu!" Bon Mtambo aliongea huku akimkabidhi simu mmoja wao. Haikupita muda, mara simu yake ilianza kuita.

*Aliyekuwa anapiga ni SSP Faraji Zegge!*

"Naona anayepiga ni Bosi Kamau mwenyewe!" Mlinzi ambae alikuwa ameshika hiyo simu aliongea mara baada ya kuona jina lililojitokeza kwenye kioo cha simu ni la George Kamau badala ya Layla kama alivyotarajia!

"Kama ni Kamau basi nipe niongee nae!" Bon Mtambo alijibu na kuipokea hiyo simu kisha akasogea pembeni kidogo!

"Halo Bwana Kamau. Mimi tayari nipo hapa ofisini kwako...Sawa, lakini usichelewe kwavile bado nahitajika kuwahi Polisi Oysterbay kabla ya saa tano unusu....!Ndio

ndio George! Haahaaahaaa! Haina haja bwana, mimi nitakaa tu hapahapa na hawa rafiki zangu!” Bon Mtambo alijifanya kuongea ingawaje hakuwa anaongea na yeyote!

Walinzi wakajenga imani kwa Bon Mtambo! Maongezi yakachukua nafasi na mara ghafla umeme ulikatika eneo lote la katikati ya mji!

“*Shit*!” Bon Mtambo akajifanya kulaani na hapo hapo akajipiga kwa nguvu mkononi kama ishara ya kufukuza mbu! Alifanya hivyo kama mara mbili tena!

“Pole sana afande, tatizo la hapa ndo hili la mbu!” Mmoja wa hawa walinzi aliongea kisha akamwagiza mwenzake akachukue dawa ya mbu ya kuchoma!

“Usisumbuke afande, hapa nilipo natembea na dawa ya mbu kila ninakoenda!” Bon Mtambo alimwambia mlinzi aliyetumwa kufuata dawa ya kuchoma kiasi cha mlinzi huyo kuvimba kichwa kufuatia kuitwa afande! Baada ya kuongea hayo, Bon Mtambo alitoa dawa aliyodai ni ya mbu wakati ni ya usingizi, kisha akavuta pumzi ndefu ndani na kuanza kupulizia hapo walipokaa! Wangekua makini, wangegundua kuwa upulizaji wenyewe ulikuwa unawalenga wao lakini walipuuza kutokana na dawa yenyewe kukosa harufu! Ilikuwa ni kama hamna kilichopuliziwa ingawaje dawa hii ilikuwa na uwezo kuanza kufanya kazi baada ya dakika tatu tu!

Baada ya zoezi hili, Bon Mtambo alijibaraguza kidogo kisha akatoweka na kwenda kwenye gari kwa madai ya kufuata sigara! Na kama alivyotarajia, baada ya dakika chache tu walinzi wote walikuwa wameegemea silaha zao wakiuchapa usingizi pasi na hofu yoyote! Aliwainua na kwenda kuwalaza sehemu ambayo wasingeonekana kwa urahisi kisha bila kupoteza muda alirudi kwenye gari na kubeba mkoba wake ambao ndani

kulikuwa na vitu kadhaa zikiwemo santuri tupu pamoja na kompyuta ya mkononi! Bila kupoteza muda zaidi, alifanya haraka akaingia ndani ya ofisi ya EA-O&C kupitia dirisha ambalo alielekezwa na Layla.

Akiwa ndani ya Ofisi ya Kamau alianza kwa kuyakagua makaratasi na vijarida mbalimbali vilivyokuwa mezani lakini hakupata chochote cha maana! Alifungua mtoto wa meza kisha akakutana na ramani iliyoonesha ni ya jengo fulani! Hata hivyo, alishindwa kufahamu jengo hilo lilikuwa wapi! Pamoja na yote hayo kulikuwa na kitu ambacho kilimvuta zaidi kwenye ramani hii!

Namba, au tarakimu ukipenda!

Kwa mfano, sehemu ya nyuma ya ramani hii ilionesha uwanja mkubwa ambao katikati yake paliandikwa: 9’19’12’9’2 - 20’18’1’9’14’9’14’7-19’17’21’1’18’5

Alijaribu kujiuliza nini maana ya tarakimu hizi lakini hakupata jibu! Alitumia karibu dakika tatu kujaribu kutafakari lakini hakuambua chochote!

Pamoja na hili alivutiwa na sehemu nyingine ya ramani hiyo ambayo ilionesha ni kama handaki! Hapa napo paliandikwa tarakimu zilizofanana sana zikiwa zimetofautiana kidogo tu na zile za awali! Hata hivyo, tarakimu hizi zilikuwa nyingi zaidi ukilinganisha na zile za awali! Hizi za sasa zilisomeka: 9’19’12’9’2-21’14’4’5’18’7’18’15’21’14’4–13’9’12’9’20’1’18’25-20’18’1’9’14’9’14’7-19’17’21’1’18’5

Alijaribu kutafuta uhusiano kati ya namba hizi na zile za awali lakini bado alijikuta akitwanga maji kwenye kinu! Pamoja na hizi, namba zilizokuwa kwenye mtindo huu zilionekana sehemu mbalimbali za ramani hii. Kutanabahi, alijikuta amepoteza karibu robo saa kwenye

namba hizi na hapo ndipo aliposhituka kwamba anatakiwa kuondoka humo ndani mara moja!

Aliikunja ramani vizuri na kuirudisha alipoikuta kisha akaaanza kufanya upekuzi kwenye sehemu zingine!

Alifungua kabati moja ambako alikuta vitu mbalimbali lakini macho yake yalivutika kwenye kasha la kuhifadhia santuri (CDs). Pembeni ya kasha hilo kulikua na CD ambayo ama ilikosa nafasi kwenye hilo kasha au aliyeiweka alikuwa na haraka kiasi kwamba akakosa muda wa kuirudisha sehemu yake! Huku mikono yake ikitetemeka, aliichukua CD hiyo kisha akawasha kompyuta yake ya mkononi na kuingiza CD hiyo.

Ilikuwa ni ile iliyoonesha matukio ya Bwana Elisante Josephat alipokuwa kwenye benki moja barani Ulaya! Bon Mtambo alishindwa kuamini matukio yaliyooneshwa kwenye filamu hiyo! Awali alipokuwa anaelezwa na Layla alihisi ni kama masihara!

Baada ya kuzinduka kwenye bumbuwazi hilo aliamua kurekodi picha hizo na kuzihifadhi kwenye kompyuta yake ya mkononi! Alichukua na CD zingine toka kwenye lile kasha, na picha zake nazo akaziamishia kwenye kompyuta yake. Aliamua kuziamishia tu kwenye kompyuta yake bila kuangalia zilihusu nini na alipomaliza hiyo kazi, alirudisha kasha kama alivyokuta awali!

Alipokuwa anajiandaa kuondoka mara macho yake yakavutika kwenye mashine ya faksi iliyokuwa humo ofisini! Kilichomvutia ni karatasi iliyokuwa kwenye mashine hiyo ambayo ilionekana imetumwa baada ya Kamau kuondoka. Aliichukua karatasi hiyo na kuvutiwa na kitu kingine zaidi!

Tarakimu!

Karatasi hii nayo ilikuwa haijaandikwa chochote mbali na tarakimu! Kitu pekee alichoelewa kutoka kwenye karatasi hilo ni neno la kiingereza lililoandikwa kwa herufi kubwa *ACKNOWLEDGED*! Hii ilimaanisha mtu aliyetuma alikuwa anakiri kupokea ujumbe huo wa tarakimu!

Tarakimu za kwenye karatasi hii zikamkumbusha ile ramani ya awali!

"Lazima hizi tarakimu zitakuwa zinaficha kitu!" Bon Mtambo alijiambia na kuamua kuichukua tena ile ramani! Aliwasha mashine ya kudurufu (*photocopier*) ya humo ofisini kisha zote akazidurufu nakala moja moja kisha zote akazirudisha alipozikuta!

Alipekua tena sehemu zingine kwa haraka haraka lakini hakuambua chochote cha maana! Aliangaza macho yake sehemu mbalimbali humo ofisini na aliporidhika kila kitu kipo sawa alitoweka bila kupoteza muda zaidi.

Hata hivyo, akili yake yote ilikuwa kwenye tarakimu!

Baada ya kuweka vitu vyake kwenye gari akawarudia tena wale walinzi kisha akawasugulia dawa fulani puani na baada ya dakika kama mbili, wote walianza kupiga chafya na kuzinduka!

"Sasa sikilizeni nyie watu, mimi sikuja hapa kumsubiria George Kamau kama nilivyowaambia hapo awali. Nilikuja kufanya upelelezi pale Benki Kuu kuhusu *ufisadi* dhidi ya majengo pacha na EPA! Upelelezi huu nimetumwa na rais na ndio maana nilipofika tu umeme maeneo haya ulikatwa ili mimi niweze kufanya kazi zangu bila kuonekana na watu! Kwavile nyinyi niliona mnaweza kuniletea *gozigozi* nikaamua kuwapulizia dawa ya usingizi niliyowadanganya kwamba ni ya mbu! Hivyo basi, hamtakiwi kutoa siri hii kwa yeyote yule kwa jili ya

usalama wa taifa! Isitoshe mkitoa siri na Kamau akajua kwamba mlimkaribisha mtu msiyemjua basi hapohapo atawafukuza kazi nyote. Si hivyo tu, inabidi niwachukue alama za vidole ili siri hii ikivuja tu tuweze kuwasaka popote pale duniani!" Bon Mtambo aliwaeleza hao walinzi kisha akatoa mkebe wa wino pamoja na karatasi kisha akachukua alama za vidole za kila mmoja!

Hata hivyo, wala hakuwa na shida na alama hizi za vidole isipokuwa alitaka tu kuwatisha ili wasije kuropoka hapo baadae! Hakutaka Kamau ashuku kwamba kuna upekuzi umefanyika ofisini kwake! Hakutaka washituke mapema wakati bado hajafahamu mtandao mzima.

"Pole na samahani sana mkuu!" Bon Mtambo alitaka radhi mara baada ya kufika Chamanzi na kumkuta IGP Minga akiwa chini ya ulinzi wa akina Njoroge!

"Ni kwanini umenifanyia upuuzi kama huu kijana?!" IGP Minga aliuliza huku akionesha wazi kughadhibishwa na kitendo hicho!

"Ni maongezi yako uliyoyafanya masaa machache yaliyopita na waziri wa mambo ya ndani ndiyo yaliyosababisha wewe uletwe hapa!" Bon Mtambo aliongea kwa utulivu na kutupa jicho la udadisi kwa IGP Minga ambae alionesha dhahiri kushtuka kutokana na kauli hiyo!

"Ina maana na wewe upo katika mtandao unaotaka kunichafulia jina langu?" IGP aliuliza kwa taharuki kidogo!

"Sipo katika mtandao wa kukuchafulia jina lako bali nipo kwenye mtandao wa kuwashikisha adabu wahujumu wa nchi hii! Hivyo basi, ni salama zaidi kwako ukiwa mtulivu kuliko vingenevyo!" Bon Mtambo aliendelea

kuongea kwa sauti yake tulivu kisha akamwagiza SSP Faraji Zegge ampeleke IGP  Minga kwenye chumba kimoja humo ndani!

“Sasa ni hivi mzee, kwa usalama wako wewe binafsi na usalama wa taifa hili, utalazimika kubaki humu ndani hadi hapo utakapofikishwa kunakohusika.” Bon Mtambo alimweleza IGP  Minga wakati akipelekwa kwenye moja ya vyumba vilivyomo humo ndani!

Baada ya kukamilisha zoezi hilo, alimpigia simu Inspekta Cecy na kumpatia namba ya faksi ambayo ilitokea kwenye faksi aliyoipata ofisini kwa George Kamau.

“Sasa sikiliza Inspekta Cecy, kesho kabla ya saa nne asubuhi naomba nipate taarifa rasmi juu ya mtu anayemiliki hiyo namba. Taarifa yako ieleze jina la mtu au kampuni, sehemu anakopatikana huyo mtu, au hiyo kampuni, na kama ni mtu binafsi jitahidi ufahamu shughuli zake na wapi anakofanyia.”

“Ondoa shaka bosi, hiyo ni kazi nyepesi kwangu kama kufumba na kufumbua!” Inspekta Cecy nae alijibu kwa kujiamini.”

# 12

Mahakama ya Kisutu ilikuwa imefurika watu kama ilivyokuwa kwa siku zilizotangulia. Wote hawa, walikuja kusikiliza maendeleo ya kesi dhidi ya Bon Mtambo anayetuhumiwa kuhusika na ugaidi pamoja na usafirishaji wa madawa ya kulevya! Kila mmoja, alitaka kumuona huyo Mtanzania mwenye uhusiano wa karibu na Osama Bin Laden!

Pamoja na Bon Mtambo, pia Ernest Masanja, Joseph Marwa na Ole waliunganishwa kwenye kesi hii kwa maelekezo ya Bon Mtambo mwenyewe!

Baada ya mashitaka kusomwa, Masanja, Marwa na Ole walikanusha mashitaka dhidi yao na hivyo kesi kuahirishwa hadi uchunguzi utakapokamilika! Baada ya hapo, waliunganishwa na Bon Mtambo tayari kwa kurudishwa mahabusu. Hata hivyo, kabla hawajafika kokote ghafla kishindo kizito kilitokea na kutetemesha eneo lote la Mahakama ya Kisutu na maeneo ya jirani! Gari moja aina ya Landrover 110 lililokuwa limeegeshwa hapo mahakamani, lilirushwa juu na liliporudi chini lilikuwa vipandevipande huku likiwaka moto! Kufuatia tukio hilo, Masanja, Ole na Marwa walikimbizwa kuelekea ilikoegeshwa karandinga la polisi, lakini hata hivyo walichelewa! Kabla hawajawahi kupanda mara ilisikika mirindimo ya risasi kutoka pande tatu tofauti!

Kutanabahi, wote watatu walikuwa wamelala chini wakiwa wamefumiliwa vibaya kwa risasi.

Harufu ya damu ilisambaa eneo zima na kuwafanya wananchi waliokuja hapo kupiga mayowe bila mpangilio! Eneo lote lilitawaliwa na vurugu huku kila mmoja akijaribu kuokoa nafsi yake! Hekaheka hizi hazikuishia hapo tu! Magari yaligongana hovyohovyo kwenye barabara za Bibi Titi, Ally Hassani Mwinyi na Maktaba! Hekaheka na sintofahamu hususani iliyosababishwa na mlipuko mkubwa wa bomu iliwawezesha Nkuba, Masumbuko na Michael Mchupi kutoweka eneo hilo bila kutiliwa shaka na yeyote! Walitoweka baada ya kufanikiwa kuwaua Marwa, Masanja na Ole mara baada ya mlipuko uliotokea! Hata hivyo, haukuwa mlipuko wa bahati mbaya! Ni mpango ambao ulipangwa na Kamau kwa kushirikiana na Mchupi. Waliamua waanze kwa kulipua bomu lililokuwa limetegeshwa kwenye gari ili kujenga hofu kwa watu kabla hawajawaua akina Marwa!

Aidha, baada ya hekaheka hizo, Bon Mtambo alijaribu kutaka kukimbia lakini kabla hajapiga hatua yoyote alidakwa na polisi na kupelekwa mahabusu!

Ukumbi ulikuwa umeshaenea wahusika huku kila mmoja akiwa na shauku ya kujua ni nini hasa madhumuni ya kikao hiki cha dharura! Wakati wengine wakisubiri kwa shauku kubwa, wengine walikuwa wamejawa na hofu! Hofu yao ilitokana na nini; ni siri yao na mungu wao lakini hawa walitamani hata itangazawe kwamba kikao kimeahirishwa hadi hapo itakapotangazwa tena! Huenda walishapata fununu ya nini hasa kinachotaka kuzungumzwa kwenye kikao hiki!

Pamoja na yote hayo, inaelekea bahati haikua upande wao, kwani baada ya muda mfupi, mgeni rasmi alitokea huku lile tabasamu lake lililozoeleka likiwa limepotea kabisa usoni pake! Ajabu zaidi ni kwamba, kulikuwa na kitu mithili ya ndita zilizokunjamana kwenye paji la uso la mgeni huyu! Hii haikuwa ishara nzuri hata kidogo, kwani si kitu kilichozoeleka kuona lundo la ndita likiwa limekusanyika kwenye paji la uso la bwana huyu! Ingekuwa ni yule mtendaji wake mkuu, basi hakuna ambae angeshangaa wala kuhofia kwani hata pale tabasamu linapokolea usoni pake, ndita nazo zingekuwa sawia kulisindikiza tabasamu hilo! Lakini huyu; hapana, lazima kuna jambo lililomchukiza kuliko lolote lile lililopata kutokea maishani mwake, angalau kwa kipindi hiki!

Kila mmoja hivi sasa alianza kushikwa na mchecheto! Hata wale waliokuwa wakimsubiria kwa shauku, hivi sasa waliekea kusutana na shauku yao! Ukumbi uligeuka na kuwa kimya; kimya kabisa! Hata sisimizi angeweza kusikika endapo angeweza kupita jirani na mtu yeyote mingoni mwao! Sio ukimya wa nidhamu kwa *mkulu*, la hasha, bali ni ukimya wa hofu! Hofu ambayo iliongezeka maradufu baada ya mgeni huyu kuingia na kukaa kwenye kiti chake bila kuonesha dalili kwamba ana nia ya kuzungumza!

Sekunde na hatimae dakika kadhaa wa kadhaa zikapita! Kutanabahi, robo ya saa hiyoo ikayoyoma; bila mgeni huyu kuongea lolote! Hata ile sura yake ya kupendeza ikaelekea kutoweka taratibu na kukaribia kufanana na yule mheshimiwa mwenzake anayetokea ukanda wa mahindi mengi!

Endapo pangetokea mtu akaenda kusoma kiwango cha joto kilichopo humu ndani basi angeweza kukuta

kiyoyozi kinasoma nyuzi joto ishirini tu! Hata hivyo, hali hii haikuwazuia baadhi yao kutumia vifaa vingine vilivyo jirani yao walivyoona vingefaa kuwatengenezea hali ya ubaridi zaidi! Haifahamiki ni kwavipi mkazi na mzoefu wa jiji la Dar es salaam aone nyuzi joto ishirini ni hali ya joto la kupindukia kiasi cha kuanza kujipepea mwenyewe! Wapo waliotumia magazeti kama vipepeo, na wapo pia waliofikia kujipepea hata kwa viganja vyao vya mikono! Ili mradi ni hofu, hofu, hofu kupindukia! Mbaya zaidi, hata kwa wale ambao hawakua na hofu wakati walipoingia humu ndani na hata alipowasili mkuu wao, hivi sasa nao walionekana kuwa na hofu! Hofu ya kwanini basi hazungumzi na wala haoneshi dalili ya kutaka kuzungumza!

*"Au kuna mwingine zaidi anayekuja kuzungumza badala yake?!"* Baadhi walijiuliza! Swali ambalo wengine bila shaka waliona ni upuuzi kwavile yeye ndie mkuu wa nchi!

Kiongozi mmoja mkubwa kwenye meza kuu alionesha dalili ya kutaka kusimama ili aongee jambo. Ilionesha kwamba alitaka kumkaribisha rasmi kiongozi wa nchi kwavile alihisi ndio sababu kiongozi huyu hadi sasa asiwe ameongea chochote. Kwamba, anasubiri kukaribishwa! Hata hivyo, kabla hajasimama aliashiriwa kukaa chini, tena kwa upendo kabisa hali iliyoonesha kwamba kinachomfanya kiongozi huyu asiongee hadi hivi sasa sio kwamba hajakaribishwa! La hasha!

*"Ni nini basi?!"*

Ndio swali lililowaumiza wengi na kusababisha hofu izidi kusambaa mithili ya moto wa petroli! Hofu si kitu kizuri! Hofu huondoa ujasiri! Hofu huondoa uwezo wa kufikiri. Hofu ushambulia milango ya fahamu! Mbaya zaidi, hofu imebeba silika ya kunyong'onyesha kibofu cha haja ndogo!

Ghafla, tena pasipo na matarajio, safari za kwenda maliwatoni ziliongezeka miongoni mwa vigogo hawa wa serikali! Wengine walitamani kutimka na kutokomea kusikojulikana. Wapo waliofika mbali zaidi! Hawa walihisi huenda Baba wa Taifa, amefufuka na ndie anayesubiriwa hapo kuongea lolote! Hata hivyo, baada ya kurejewa na ufahamu japo kwa sekunde; walijikuta wakijicheka wenyewe! Wapo ambao walianza kumtazama kwa makini kiongozi huyu wa nchi. Walihisi si yeye, bali ni kiumbe tu cha kimiujiza ambacho kimekuja katika sura yake!

Hofu!

Ghafla, na pasipo kutarajia, mgeni alisimama huku akiwa na hali ileile ya kupoteza tabasamu lake lililozoeleka.

Mbaya zaidi, alionesha kukasirika!

Kila mmoja akajiweka tayari kumsikiliza, ingawaje hofu miongoni mwao iliongezeka maradufu! Kilichowatisha zaidi ni hatua yake ya kuanza kumtupia macho mmoja baada ya mwingine kana kwamba anawahesabu kimoyomoyo; au alitaka kujua ni nani hajahudhuria wito ule!

"Wote turudi sehemu zetu za kazi hadi hapo uchunguzi utakapokamilika!" Hatimae alizungumza akiwa katika hali ile ile, kisha bila kupoteza hata sekunde akaondoka na kuwaacha vigogo hawa wakiwa wametumbua macho! Macho ya hofu! Hakuna aliyeamini. Badala ya hofu kupungua kwavile alishaondoka; hivi sasa iliongezeka mara dufu ya ile maradufu iliyotangulia! *Hadi hapo uchunguzi utakapokamilika!?* Tamko hili halikuwa tamko rafiki hata chembe! Ni tamko la kuogofya kuliko maelezo! Aidha, haikuwaingia akilini kiongozi wa nchi aitishe kikao cha dharura halafu asiongee jambo lolote! Kikao hiki alikiitisha katikati ya tuhuma na malalamiko

yaliyokuwa yanatokea kuhusiana na kuongezeka kwa matukio yaliyo kinyume na maadili ya uongozi hususani tuhuma za rushwa na *ufisadi*. Baada ya tuhuma hizi kuzidi kuongezeka, kiongozi wa nchi alikata shauri la kuwaita watendaji wote wakuu wa wizara mbalimbali pamoja na idara zingine zinazojitegemea. Hata hivyo, kwa mshangao wa wengi, kama sio wote, hakuongea chochote na badala yake aliondoka!

Baada ya kutoka *mahabusu,* Bon Mtambo alikanyaga mafuta kuelekea Chamanzi kukutana na wenzake. Akiwa ameenda umbali mfupi mara simu yake ya mkononi iliita na alipoangalia namba ya mpigaji alikuta ni Inspekta Cecy.

"Ndiyo Inspekta, lete habari!"

"Hofu kwako wewe uliyenusurika na mabomu!" Inspekta Cecy aliongea kwa utani kisha wote wakacheka!

"Nawashangaa wale jamaa, walitaka nife sijui ili warembo kama nyinyi nimwachie nani!"

"Wasiwasi wako tu bosi, huko peponi kuna warembo kuwazidi malaika, lakini kwa watu waliokuwa watenda mema hapa duniani!"

"Watenda mema kama mimi hapa! Haya niambie Inspekta manake najua kuna jambo muhimu unataka kunipasha!" Bon Mtambo alibadilisha mada.

"Ni kweli bosi, ile namba uliyonipatia jana ilitumwa kutokea nyumba ya mzungu mmoja aitwae Fredrick De Souza aishie Upanga. Huyu bwana ni raia wa Afrika ya Kusini na ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni moja ya uchimbaji wa madini hapa nchini. Kwa hapa Dar es salaam huyu Bwana anaishi Upanga Mtaa wa Mindu, nyumba

namba IL/UPM/MF0101. Aidha, ofisi yake kwa hapa Dar es salaam ipo Mtaa wa Samora jirani na Extelcom Building!" Inspekta Cecy alimalizia maelezo yake.

"Kazi nzuri sana Inspekta! Kwakweli umefanya kama ambavyo nilitaka!" Bon Mtambo alipongeza na baada ya maongezi ya hapa na pale, waliagana kwa miadi kwamba watawasiliana baadae.

Baada ya kufanikisha mauaji pale Mahakama ya Kisutu Michael Mchupi alifanya haraka kwenda kukutana na George Kamau. Suala la kukutana na Kamau lilikuja dakika chache tu zilizopita baada ya Mchupi kupokea simu toka kwa Kamau kwamba anamuhitaji haraka sana!

"Michael, nimekuita hapa kuna jambo muhimu inabidi tulishughulikie mapema iwezekanavyo. Kwanza kabisa, hongereni kwa kazi nzuri mliyofanya ambayo bila shaka itazidi kumweka Bon Mtambo matatani. Hata hivyo, bado kuna kazi kubwa mbele yetu ambayo naamini kutokana na uwezo wako bila shaka tutaifanikisha." George Kamau alianza kueleza mara baada ya kukutana na Michael Mchupi kwenye hoteli moja iliyopo katikati ya jiji, kisha akaendelea huku akionekana kuwa makini zaidi: "Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Jaffery Minga ametoweka na hadi hivi sasa haijulikani alipo! Inawezekana kutoweka kwake kumetokana na yeye kutokubaliana na maagizo aliyopewa na Waziri au inawezekana ni waziri mwenyewe ametuchezea akili. Lakini vyovyote iwavyo, lazima tufanye jambo la maana leo hii hii kabla ya saa kumi vinginevyo tutakuwa kwenye matatizo makubwa! Hofu iliyopo mbele yetu ni hatari ya

kugundulika kwa ISLIB kuwa inacheza mchezo mchafu. Nasi kama wadau wakuu wa ISLIB hatuna budi kutengeneza mazingira ambayo itaifanya ISLIB ionekane ipo kwa maslahi ya taifa hili. Tukishaliweza hilo, basi yeyote atakayeanza kuichokonoa ISLIB ataonekana ni mtu mwenye nia mbaya na ISLIB. Hivyo basi, ili kufanikisha jambo hili hatuna budi kuwatoa kafara viongozi wawili walio kwenye orodha yetu leo hii hii! Nimepitia orodha tuliyonayo na kukuta kuna mawaziri wawili ambao zamani walikuwa kwenye idara nyeti za serikali. Hata hivyo, kwa sasa wapo kwenye wizara ambazo hazina msaada sana kwetu. Mawaziri hawa ni Godfrey Makali na Austine Ishengoma!" George Kamau, huku akionekana kuwa makini zaidi alimweleza Michael Mchupi kazi iliyokuwa mbele yao. Alitumia kiasi cha karibu nusu saa kumuelekeza nini kinatakiwa kufanywa ili kufanikisha zoezi hilo! Baada ya kuona Michael Mchupi yupo makini kumsikiliza, aliendelea: "Hivyo basi, Senti Kumi atawasili hapa hivi punde ambapo utaondoka nae hadi kwa Jonas Siyame. Leo hii Wendy atakuwa na Masumbuko na wataenda kwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Bwana Elisante Josephat mara baada ya wewe kuwaeleza kuwa mpo njiani kwenda kwa waziri huyo. Hata hivyo, kabla wewe hujaondoka kwenda kwa Siyame itabidi umpigie simu Bwana Elisante na kumwambia asitoke kwavile una mazungumzo na yeye. Aidha, kuna vijana wetu wengine wawili tutawatuma waende kwa Makali na Ishengoma. Vijana hawa wataenda kuwashinikiza Ishengoma na mwenzake wasafiri kwenda Nairobi leo leo! Lengo ni kuwafanya waonekane ni wenye pilikapilika za kutaka kusafiri ili wajihalalishie kukamatwa leo leo!"George Kamau alimalizia maelezo yake kisha akaanza kuelekeza nini cha kufanya!

ꕥꕥꕥ

Baada ya kumaliza kuongea na Inspekta Cecy, Bon Mtambo alimpitia Layla ambae alimwongopea Kamau kwamba anaenda Kibaha!Wakati anaendelea kukanyaga mafuta mara akamuona kijana anayeuza magazeti. Alisimamisha gari na kuchukua magazeti mawili yatokayo jioni.

**Shambulio la kigaidi laitikisa Mahakama ya Kisutu!**

- *Lililenga kuja kumtorosha gaidi Bon Mtambo,*
- *Washirika wake watatu wauawa!*

Kilikuwa ni kichwa cha habari kilichopamba moja ya magazeti hayo! Hata hivyo, hakuwa na muda wa kuyasoma na badala yake aliyahifadhi kisha akaendelea na safari ambayo ilimfikisha shambani kwake!

Baada ya kuwasalimia aliowakuta alipitiliza chumbani ili kuzuia masihara kutoka kwa akina Okello! Bila kupoteza muda, alichukua karatasi ambazo alizichukua ofisini kwa Kamau na kuanza kuzipitia upya akijaribu kutambua maana ya zile tarakimu. Awali alianza na ile ramani kwa kile alichoamini uchache wa namba zilizomo ungemrahisishia kutegua kitendawili kilichofichwa! Hata hivyo, alitumia zaidi ya robo saa bila kuambua chochote! Aliiacha ramani kisha akachukua ile faksi ambayo ilikuwa na rundo la tarakimu ambazo nazo ni kama zilizidi kumchanganya badala ya kumfumbulia fumbo! Hapa napo alitumia zaidi ya robo saa nyingine bila ya mafanikio yoyote! Nayo akaitupa pembeni kisha akachukua yale magazeti na kuanza kuyasoma!

Mbali na kushtushwa jinsi ilivyoandikwa habari ya mlipuko wa bomu pale makamani Kisutu, habari nyingine ni ile iliyohusu kutoweka kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini! Katika habari hiyo, iliandikwa kwamba Mkuu wa Jeshi la Polisi ametekwa na watu inaodhaniwa ni magaidi wanaoshinikiza kuachiwa huru kwa gaidi mwenzao Bon Mtambo! Aidha, kwa mujibu wa habari hiyo, hadi gazeti linaingia mitamboni ilikuwa bado haijafahamika ni wapi alikopelekwa mkuu huyo wa jeshi la polisi. Habari hiyo, iliendelea kueleza kwamba kuna hatari utekaji nyara zaidi wa viongozi mbalimbali ukaendelea nchini. Aidha kutokana na uchunguzi uliofanywa na mwandishi, kampuni moja ya ulinzi jijini inayojulikana kama ISLIB imejitolea kutoa ulinzi kwa viongozi mbalimbali kwa kushirikiana na jeshi la polisi ili kuzima uwezekano wa kutokea matukio mengine ya utekaji nyara!

Alipomaliza kuisoma habari hiyo, akawapelekea magazeti wenzake. Huko alikuta mjadala mkali!

“Afadhali umekuja Bon, hebu nawe tuambie enzi zako za uanafunzi! Imegundulika kwamba wote walio hapa walikuwa *wakali* wa hisabati *primary* (shule ya msingi) lakini wakageuka wabovu wa hisabati mara walipojiunga shule za upili!” Alikuwa ni Layla aliyeanza kumchokoza Bon Mtambo mara alipowafikia!

“Mimi nilikuwa natisha binti! Sikuwa mkali wa hisabati shule ya msingi tu, bali hadi chuo kikuu! Nilikuwa natisha hadi kwenye *calculus* na aljeb....!” Bon Mtambo alijibu kwa majigambo lakini akasita ghafla na kubaki ni kama mtu aliyepigwa na bumbuwazi la ghafla!

“Ulitaka kutupiga *fiksi* kwamba ulikuwa mkali kwenye *aljebra* sio?” William Okello aliongea kwa kejeli na kuwafanya wenzake waangue kicheko! Hata hivyo, Bon

Mtambo hakuweza kuyasikia maongezi hayo, na badala yake alibaki akiwa bado ameganda!

"Samahani waungwana, nakuja mara moja!" Bon Mtambo aliwataka radhi wenzake na mara moja akainuka huku akiwa amewaacha wenzake kwenye mshangao! Alienda moja kwa moja chumbani huku lile neno *aljebra* likiendelea kujirudiarudia kichwani mwake!

"*Aljebra, ni herufi badala ya namba*!" Bon Mtambo aliwaza huku akiichukua tena ile ramani na faksi na kuanza kuzipitia tena zile tarakimu!

"*Ni herufi badala ya namba au ni namba badala ya herufi!*" Aliendelea kujiuliza na kuzikumbuka tena zile tarakimu!

*9'19'12'9'2 - 20'18'1'9'14'9'14'7-19'17'21'1'18'5*

Mithili ya mtu aliyezinduka usingizini, alichukua karatasi na kalamu na kuanza kuziandika alphabeti zote, tangu A hadi Z ! Alizitupia macho ya udadisi mithili ya mtu anayeziuliza kitu herufi hizo! Hata hivyo herufi hizi hazikutoa ushirikiano alioutarajia! Aliweka kando hizi herufi kisha akaichukua tena ile ramani na kuanza kuziangalia upya zile tarakimu lakini hivi sasa akiziangalia kwa umakini zaidi! Baada ya kuzidadisi tarakimu zilizokuwa kwenye ramani alichukua ile faksi ambayo ndo ilikuwa na tarakimu nyingi zaidi! Nazo akaanza kuzichunguza kwa udadisi zaidi!

Akahisi kama aliyegundua kitu! Namba zote zilikua ni kati ya moja na ishirini na sita! Ingawaje alikuwa anafahamu idadi kamili ya alphabeti A hadi Z ni ishirini na sita lakini akaamua kuzihesabu tena ili kuthibitisha! Kabla ya hapo hakuwahi kuthibitisha jambo hili!

"Moja, mbili, tatu, nne.....!" Alianza kuhesabu na mwisho akafikia jibu lilelile kwamba ni ishirini na sita tu!

“Kwanini nilihesabu A ni moja, B ni mbili, C ni tatu...........na Z ni ishirini na sita?” Alijiuliza kisha akatoa tabasamu la mbali alilohisi linamsuta kwa ujinga!

Akaamua kutengeneza jedwali ambalo aliandika alphabeti zote kisha kila chini ya herufi aliweka na namba sawa na vile alivyokuwa anahesabu! A aliiwakilisha na moja, B mbili, C tatu na zingine zote kwa mtiririko huu!

Baada ya kazi hii kisha akaichukua tena ile ramani na kuzichunguza upya zile tarakimu!

9’19’12’9’2 - 20’18’1’9’14’9’14’7-19’17’21’1’18’5

Namba hizi sasa akaanza kuziwakilisha na herufi kama zilivyokuwa kwenye jedwali lake! 9 akaiwakilisha na I, 19 akaiwakilisha na S na alipomaliza zoezi hili na kusoma akajikuta ni kama aliyepigwa na shoti ya umeme!

ISLIB TRAINING SQUARE!

Baada ya zile namba kuziwekea herufi mbadala, akakutana na neno ISLIB TRAINING SQUARE, likiwa na maana kwamba ni Uwanja wa Mafunzo wa ISLIB!

Baada ya hapo alizigeukia tarakimu zingine kwenye hiyo ramani na kuanza kuziwekea herufi!

9’19’12’9’2 - 21’14’4’5’18’7’18’15’21’14’4 – 13’9’12’9’20’1’18’25 - 20’18’1’9’14’9’14’7-19’17’21’1’18’5

Hizo nazo zikamwacha na mshituko wa hofu!

ISLIB UNDERGROUND MILITARY TRAINING SQUARE!

Hilo ndilo neno lililopatikana lililokuwa limefichwa na hizo tarakimu, likimaanisha ni Uwanja wa Mafunzo ya Kijeshi wa ISLIB ulikokuwa chini ya ardhi!

“*Hii sasa ni vita*” Bon Mtambo alijikuta akijisemea peke yake. Baada ya kuzichunguza na namba zingine akakutana na vitu kama ISLIB UNDERGROUND

CONFERENCE ROOM, (yaani ukumbi wa mikutano uliokuwa chini ya ardhi)!

Baada ya hapo aliweka ramani pembeni na kuchukua ile faksi ambayo ilikuwa na tarakimu nyingi zaidi ambazo zilisomeka kama ifuatavyo:

13’5’5’20’9’14’7’- 4’1’25’- 1’6’20’5’18’-
20’15’13’15’18’18’15’23’- 19’20’1’18’20’9’14’7’- 23’9’20’8-
4’15’13’5’19’20’9’3’- 19’20’18’1’20’5’7’9’3’ –
3’15’13’13’9’20’20’5’5’- 1’20’- 6’15’18’20’5’5’14’-
6’15’12’12’15’23’5’4’- 2’25’- 15’21’18- 14’15’14 – 7’22’20 –
1’12’12’9’5’19’- 1’20’- 5’9’7’8’20’5’5’14’- 9’14’ -
21’14’4’5’18’7’18’15’21’14’4 – 3’15’14’6’5’18’5’14’3’5’ –
18’15’15’13.

Kwakuwa hivi sasa alikuwa ameshapa uzoefu katika ghiliba hii, ilimchukua kiasi cha dakika moja tu kupata kifungu cha maneno kilichosomeka:

*Meeting day after tommorrow starting with Domestic Strategic Committee at forteen followed by our non gvt allies at Eighteen, in underground conference room.*

Baada ya kuisoma habari hii Bon Mtambo alishusha pumzi ndefu na kujikuta akiwa katika hali mbili tofauti! Wakati kwa upande mmoja alikuwa amejawa na furaha kwa kutegua kitendawili cha tarakimu lakini kwa upande mwingine alikosa amani baada ya kuona uzito wa kazi iliyopo mbele yao! Suala la kuwepo uwanja wa mafunzo ya kijeshi chini ya ardhi unaomilikiwa na ISLIB lilimpa tahadhari ya kwamba anapambana na kikosi cha jeshi tena chenye mafunzo ya kutosha. Aidha, kabla hajawagutusha, alihitaji kutegua kitendawili cha hao waliotajwa kuwa ni *Domestic Strategic Committee* au Kamati ya Ndani ya Mikakati! Aliamini kwamba watu waliomo kwenye kamati hiyo ndio bila shaka wanaoratibu mipango yote ya hujuma

zinazoendelea nchini! Vilevile suala la kufanyika huo mkutano kwa nyakati mbili tofauti lilikuwa ni pigo lingine! Isingekuwa busara kufanya mashambulizi kwavile hiyo ingeruhusu wahusika wengine kutoroka! Aidha alihitaji kuwafahamu hao waliotajwa kuwa ni *non gvt allies*, au washirika walio nje ya vyombo vya serikali.

Baada ya kufanikiwa kutegua kitendawili cha tarakimu, aliwasha kompyuta yake ya mkononi na kuanza kuziangalia picha za video ambazo alizichukua ofisini kwa Kamau usiku uliopita! Ilikua ni vigumu kwake kuamini matukio yaliyokuwa yanatokea kwenye picha hizi! Labda usahihi ni kusema kwamba, ilimwea vigumu kuamini watu waliokuwa wanaonekana kwenye picha hizo! Wengi ni viongozi na watendaji waandamizi wa serikali ambao baadhi yao walikuwa wanaheshimika mno kwa jamii! Mshangao wake hakuishia kwa viongozi hawa peke yake. Alizidi kushangaa zaidi alipokutana na viongozi wa vyama vya upinzani, viongozi wa vyama vya wafanyakazi pamoja na viongozi wa vyama vya kiraia!

*"Bila shaka hawa ndio non gvt allies!"* Bon Mtambo alijisemea peke yake alipokuwa anaangalia picha za viongozi wa vyama vya upinzani, vyama vya wafanyakazi pamoja na viongozi asasi za kiraia! Hakika alichoka kiasi cha kuanza kuzitilia mashaka picha hizo! Ili kuondokana na shaka aliyokuwa nayo, alikata shauri ya kuzituma picha hizo Makao Makuu ya WIBAIC ili zikaguliwe na wataalamu wao wa masuala ya picha ili kuona kama sio za kugushi!Aidha, baada ya kazi hiyo, picha hizo hizo akajitumia mwenyewe kwenye barua pepe yake kama njia ya kuzihifadhi!

Baada ya kumaliza zoezi hilo, alichukua simu na kumpigia Inspekta Daniel Chacha:

“Sikiliza Kinyonga, fanya uchunguzi uniambie ni wapi ISLIB inakotolea mafunzo ya uaskari kwa askari wake!”

“ISLIB wanatolea mafunzo yao kwenye kambi yao iliyopo Vikindu!” Inspekta Chacha alitoa jibu hapohapo.

“ Ala! Kumbe unafahamu?”

“Ndiyo bosi, mimi nilishawahi kwenda pale mara kadhaa!”

“Kwahiyo bila shaka unapafahamu kidogo!”

“Ni kweli kabisa bosi, na si kupafahamu tu, vilevile kwa kiasi fulani nafahamika na baadhi ya watu wa pale!”

“Safi Inspekta, nazani baadae tunaweza kwenda huko!”

Baada ya maongezi hayo mafupi, Inspekta Daniel alimwelekeza Bon Mtambo ilipo hiyo kambi na baada ya hapo alienda na kujumuika na akina Layla.

“Lete habari bosi!” Layla alichokoza baada ya Bon Mtambo kuja kujumuika nao lakini bila kuongea chochote.

“Habari sio mzuri mrembo wangu! Nimegundua kwamba Kamau na wenzake ni watu hatari kuliko Osama!” Bon Mtambo aliongea na kuwafanya wenzake kucheka kisha akaendelea, “Sasa sikiliza Layla, itabidi urudi mjini sasa hivi na huko kajitahidi kila uwezavyo kujiweka karibu zaidi na Kamau. Jitahidi kuchunguza mienendo yake yote. Hata hivyo, usiwe unalazimisha asije akakushitukia!” Alimalizia na kuanza kuwaeleza wenzake mambo kadhaa aliyoyagundua ofisini kwa Kamau.

Michael Mchupi akiwa na mwenzake walifika ofisini kwa Jonas Siyame majira ya saa saba kasorobo mchana. Bila

kupoteza muda, alifungua kibegi chake na kutoa makarabrasha mawili pamoja na kanda mbili za video na vyote hivyo akaviweka mezani.

“Samahani Bwana Siyame kwa kukujia ghafla, tunasikitika kwamba muda haukuturuhusu kufanya miadi na wewe. Hata hivyo, tumekuja na habari njema ambayo hatuna shaka yoyote kwamba utaifurahia!” Michael Mchupi alifungua maongezi kwa sauti ya utulivu kabisa!

“Habari gani hiyo ndugu?”

“Awali ya yote, mimi naitwa Michael na huyu mwenzangu anaitwa Mohamed. Kuhusu habari njema, anzia kwa kuyapitia haya makarabrasha kwa haraka.”

Nusu saa baadae, Siyame alishamaliza kuyapitia!

“Sijaelewa vizuri, ni nini hasa mnacholenga kufanya na mimi mnataka nifanye nini!” Jonas Siyame aliuliza mara baada ya kumaliza kuyapitia hayo makarabrasha.

Sikiliza Siyame, taarifa hizi ni ushahidi juu ya vitendo vya rushwa vilivyofanywa na viongozi wawili wa serikali. Hizi kanda za video zinaonesha matukio yote yalivyotokea. Hao watu kwa sasa wapo mbioni kuikimbia nchi, hivyo basi, tunakushauri majalada haya uyapeleke kwa Mkurugenzi wa Mashitaka sasa hivi ili nae atoe kibali cha kukamatwa kwa watuhumiwa hawa kabla hawajatoroka!” Michael Mchupi alimalizia maelezo yake.

“Wewe unazani jambo hilo linawezekana?” Hatimae Siyame aliuliza kwa utaratibu.

“Hakuna kisichowezekana Siyame, hii ni kwa maslahi ya taifa. Hatuwezi kuwaacha watu walioitafuna nchi watoroke wakati tumekuletea ushahidi wote.”

“Mimi kama kiongozi siwezi kuutumia ushahidi ulioletwa na watu wengine bila ya kuufanyia uchunguzi! Ile tu kuleta, tayari mmeshakamilisha wajibu wenu,

niachieni mimi nifanye yaliyosalia kwa mujibu wa taratibu. Hata kama wanatoroka, acheni watoroke kwani hakuna usikofika mkono wa serikali!" Jonas Siyame aliongea kwa sauti yake ile ile tulivu.

"Sikiliza Siyame, naona unataka tupoteze muda bila ya sababu. Najua, hofu yako ni kuhusu ushahidi tulioleta. Lazima ujue kwamba, kazi hii imefanywa na watu makini katika nyanja ya uchunguzi na kamwe hawawezi kupika ushahidi. Labda tukuoneshe tukio moja ambalo hata wewe mwenyewe unalifahamu. Ukishauona ushahidi wa tukio hilo, ndipo utakapothibitisha kwamba sisi sio wababaishaji!" Michael Mchupi aliongea kwa sauti ya upole kisha akawasha kompyuta yake ya mkononi na kuweka CD. Baada ya picha kuanza kuonekana, alimgeuzia Jonas Siyame ili aweze kuona vizuri!

Mshituko alioupata Jonas Siyame alikuwa hajawahi kukutana nao hata mara moja maishani mwake! Alibaki akiwa anaikodolea macho filamu hiyo ya ajabu huku akihisi midomo kumkauka. Alitaka kuongea kitu lakini alishindwa! Alitamani ainuke kitini, lakini miguu yake haikuwa na ubavu wa kuhimili kiwiliwili chake! Awali alijihisi yupo ndotoni, hali iliyomfanya ajitikise kidogo na kubaini kwamba hakuwa akiota!

Alikuwa akiangalia picha za tukio ambalo lilimuonesha yeye akifanya mapenzi na mabinti wadogo wa shule! Alilikumbuka tukio hili, na hakua na shaka hata kidogo kwa yale yaliyokuwa yanaonekana!

Mwili ukajawa na hofu!

Nafsi ikajawa na aibu!

Kichwa kikapoteza uwezo wa kufikiri!

"Tuambie Jonas, hata picha kama hizo nazo unahitaji kuzichunguza ili uthibitishe kama ni za kweli au hapana?"

Hatimae Mohamed Salehe, au Senti Kumi alimuuliza Jonas Siyame baada ya kumuona amepigwa na bumbuwazi!

Hata hivyo, swali hili halikusikika masikioni mwa Jonas Siyame! Taswira ya watu waliokuwa wakimzomea kila apitapo ilianza kujengeka akilini mwake. Akaanza kwa kuikumbuka kesi ya Maumba, kisha ya Babu Seya na hatimae akaona inayofuata ni ya kwake yeye! Aliamini kesi yake haitachukua muda mrefu kwavile tayari kulikuwa na ushahidi usio shaka yoyote!

Akailaani nafsi yake!

Akailaani tabia yake ya kuendekeza ushirikina!

Akamlaani pia Babu Linjembwa!

Hapohapo akajihisi hana tena thamani mbele ya jamii! Hapo hapo akabaini kwamba sifa alizojizolea katika kupiga vita rushwa zitakuwa zimefikia tamati!

"Tujibu Siyame, hata picha hizo nazo zinahitaji kufanyiwa uchunguzi?" Senti Kumi alimkumbusha!

"Kwani nyinyi ni akina nani?" Hatimae Jonas Siyame alijitahidi kufungua mdomo na kuuliza swali!

"Nazani tulishajitambulisha kwako, sasa chagua moja, kuyapeleka haya majalada kwa DPP sasa hivi ili atoe kibali au usitekeleze matakwa yetu na sisi tuzivujishe picha zako kwa wanahabari!" Michael Mchupi aliuliza.

"Unamaanisha nini?"

"Maana yangu ni kwamba endapo utafanya kama tulivyokuagiza basi tutakutunzia siri yako. Lakini endapo utaenda kinyume na matakwa yetu, basi picha zako tutazisambaza kila sehemu!"

"Mimi nitaamini vipi kwamba nikitekeleza matakwa yenu hamtavujisha picha zangu?"

"Tunakuhakikishia kwamba tutakutunzia siri hii hadi mwisho wa dunia." Mchupi alitoa uthibitisho.

“Sasa nyinyi lengo lenu hasa ni nini? Sio siri, binafsi naona ni kama mna lengo maalumu katika hili vinginevyo sioni ni kwanini mnashinikiza mawaziri hao wakamatwe!” Jonas Siyame aliongea katika namna iliyotia simanzi sana!

“Sikiliza Siyame, awali ya yote lazima ufahamu kwamba ushahidi uliopatiwa kuhusu hao mawaziri ni ushahidi halali kabisa. Uchunguzi wa tukio hili ulifanywa na kampuni ya ISLIB na hauna shaka yoyote. Baada ya ISLIB kufanya uchunguzi wake, ikagundua viongozi kadhaa waandamizi waliopo madarakani na wale ambao kwa sasa hawapo madarakani wamejihusisha na vitendo vya rushwa. ISLIB imetumia mamilioni ya pesa katika kuendesha uchunguzi huu. Wakati uchunguzi dhidi ya mawaziri hawa ukiwa unafikia tamati, mara taarifa juu ya uchunguzi zikavuja. Baada ya kuvuja kwa taarifa hizo, mawaziri wanaohusika wakaanza harakati za kutaka kutoroka na wengine kutaka kuihujumu ISLIB. Na si ajabu hapa tunapoongea wakawa uwanja wa ndege. Baada ya kuona kuna uwezekano mkubwa wa viongozi hao kutoroka, ndipo ISLIB ilipoamua kukufuata wewe ili uzuie kutoroka kwao. ISLIB isingependa kuona mamilioni waliyotumia kwenye uchunguzi huu yakipotea hivihivi tu! Walijuwa utakataa, na hapo ndipo walipofikia muafaka wa kufanya *biashara* na wewe! Uwafanyie kazi yao, nao wakulindie siri yako! Kazi hii ni muhimu sana kwa kampuni yao, kwani kama nilivyokuambia wameshatumia mamilioni ya pesa! Na baada ya kufanyika kwa biashara hiyo, hawatakuwa na shida na wewe tena! Isitoshe, wao hawakuona taabu sana kupoteza ushahidi wa vitendo vyako kwavile wao malengo yao makubwa ni kupigana na vitendo dhidi ya rushwa na si vinginevyo! ISLIB wana hasira sana na wala rushwa wa nchi hii, kwavile kabla ya

kupata kibali cha kuendesha shughuli zao nchini walikwamishwa mara kadhaa na watendaji wapenda rushwa. Na miongoni mwa watu hawa, ni Bwana Makali. Hivyo basi, ISLIB wanaona wakati wa kumtia adabu Makali ndio sasa wakati wana ushahidi wote dhidi yake!"Michael Mchupi alimalizia maelezo yake na kumpatia Siyame nafasi ya kuyatafakari!

"Na ilikuwaje wakawa na hizi picha zangu?"Hatimae Siyame aliuliza.

"Sikiliza Siyame, ISLIB inahusika na kuchunguza vitendo vyote vilivyo kinyume na maadili ya uongozi. Hivyo basi, wewe ukiwa kama kiongozi mwandamizi kwenye taasisi nyeti kabisa nchini unapaswa kuwa mfano bora wa kuwa kiongozi unayeheshimu maadili. Kwavile ulikiuka maadili, sioni sababu kwanini ushangae kujikuta umeingia mikononi mwa ISLIB wanaopiga vita vitendo vyote viovu kwa jamii. Ikiwa umeweza kufanya ngono na vibinti vidogo kama hivi, sijui utashindwa nini kuongwa ngono na wasichana warembo ili upindishe sheria." Michael Mchupi aliongea kwa hisia kali huku akiwa amemkazia macho Siyame.

Baada ya kufikiri sana Jonas Siyame alichukua majalada yaliyokuwa mbele yake na kuanza kuyapitia upya harakaharaka. Baada ya kuyamaliza alichukua kanda za video na kuzitumbikiza kwenye kompyuta kisha nazo akaanza kuzipitia upya, lakini sasa kwa uangalifu kidogo!

"Kwa upande wangu nimekubaliana na nyinyi lakini DPP huwezi kumwingia kirahisi hivi!" Hatimae Siyame aliongea katika namna ya mtu aliyekata tamaa!

"Ondoa hofu Siyame, sisi tumeliona hilo kabla, hivyo kwa DPP utaongozana na waziri wa mambo ya ndani! Hata hivyo, baada ya zoezi hili itabidi muitishe

mkutano na waandishi wa habari kuelezea ni kwanini mlilazimika kulifanyia kazi haraka suala hili kiasi cha hata kukiuka taratibu zingine. Aidha, usisahau kueleza wazi kwamba uchunguzi wa kesi umefanywa na ISLIB!"

Wakati haya yanatokea, SSP Faraji Zegge alikua akiendelea na kazi ya kung'arisha viatu huku akihakikisha anamuona kila anayeingia na kutoka kwenye ofisi za TAKUKURU! Pamoja na kuangalia kila anayeingia na kutoka, lakini alivutiwa zaidi na ujio wa Michael Mchupi na mwenzake. Kilichomvutia zaidi kutoka kwao ni vile walivyokuwa wamevaa suti safi, nadhifu na za gharama lakini huku miendo yao ikiwa haishabihiani hata chembe na mavazi yao! Ulikuwa ni mwendo wa *kisela* mno wakati mavazi yaliwaonesha ni kama wakurugenzi!

Baada ya kuona watu hawa wakiingia kwenye ofisi za TAKUKURU, aliacha kazi ya kung'arisha viatu na badala yake akaagiza chakula kutoka kwa mama lishe! Hakutaka mtu mwingine aje na kumpa kazi wakati yeye hivi sasa alitaka afanye kazi iliyomleta hapo!

Muda mrefu kidogo ulipita na mara akawaona wale watu wakitoka wakiwa wameongozana na Jonas Siyame! Mara moja, SSP Zegge akabaini kuwa msafara ule haukuwa wa amani!

Bon Mtambo alikuwa anakaribia Mnazi Mmoja wakati simu yake ilipoita. Alipoangalia namba akakuta ni ya SSP Faraji Zegge.

Mwili ukamsisimka!

"Lete habari Inspekta!"

"Naona Jonas Siyame ameongozana na watu wawili hapa! Nina mashaka juu ya huu msafara kwavile Jonas anaonekana kama mtu asiye na amani usoni pake!"

"Sawa, wafuatilie uone wanaelekea wapi na usisite….!" Bon Mtambo alijibu lakini kabla hajamalizia sentensi yake simu ikakatika ghafla!

"*Shit*!" Bon Mtambo alilaani baada ya kugundua simu yake imekatika kutokana na kuishiwa umeme(*charge*)!

"Nazani hapa panatosha Layla! Lakini kumbuka kwamba unajiweka karibu na Kamau kwa kadri uwezavyo na usisite kunijulisha chochote kitakachotokea! Aidha, kumbuka kwamba nina kanda za picha na maelezo yako!" Bon Mtambo alimweleza Layla huku akimtisha kidogo kwa hofu ya kumsaliti!

Alimteremsha kwenye kituo cha Baridi, hapo hapo Mnazi Mmoja.

"Karibuni vijana, sijui niwasaidie nini ?" Alikuwa ni Godfrey Makali akiwakaribisha Wendy na Nkuba.

"Ahsante mheshimiwa, tuna muda mfupi sana wa kukaa ofisini kwako, lakini muda huo ni muhimu sana kwako!" Wendy aliongea huku akipepesa macho huku na huko kama anayechelea mazungumzo yake kusikika!

"Unamaanisha nini binti?" Makali aliuliza huku akionesha wazi kutoelewa alichoambiwa na Wendy.

"Una hakika maongezi yetu hapa hayataweza kusikika na yeyote?" Badala ya kujibu, Wendy nae alirusha swali katika hali ile ile ya kuonesha ni kama ana hofu!

"Hakuna yeyote atakayesikia!" Godfrey Makali alijibu huku nae akianza kushikwa na hofu kidogo.

"*Ok!* Ni hivi mheshimiwa, mimi nisingependa kukuzungusha sana kwani kufanya hivyo itakuwa ni kutaka kukutia matatani bure! Kwa kifupi ni kwamba, wakati ulipokuwa kwenye wizara ya ujenzi miaka kadhaa iliyopita ulikuwa umejiundia maadui wengi ikiwa ni wafanya biashara wakubwa na vigogo wenzako! Uadui huo ulitokana na imani kwamba zabuni nyingi wizarani kwako zilikuwa zinatolewa kwa kujuana kuliko kuzingatia vigezo! Tangu wakati huo, baadhi ya maadui zako hawa wakaapa kukumaliza kwa gharama yoyote ile! Na kwa bahati, karata ya ushindi imeangukia upande wao na wameshapata mtaji wa kukumaliza. Mtaji walionao umetokana na wao kupata ushahidi unaokuhusisha wewe kupokea rushwa wa.....!"

"*What*?Mimi kupokea....! Binti, lakini unajua unaongea na nani wewe?" Godfrey Makali alifoka huku akiwa amefura kwa hasira!

"Sikiliza mheshimiwa, mimi sikujui na wala wewe hunijui! Mimi nina akili zangu timamu hapa hivyo...!"

"Siwezi kusikiliza upuuzi wenu msichana, hebu ondokeni mara moja la sivyo nitawaitia polisi!"

"Sawa mheshimiwa, sisi tunaondoka sasa hivi lakini hata hivyo tunaomba tukuoneshe kitu kimoja bila shaka utakipenda na kuamua kututegea sikio lako!"

"Nionesheni huo upuuzi wenu kisha muondoke mara moja!" Godfrey Makali aliendelea kufoka. Kufuatia ruhusa hiyo, Wendy aliwasha kompyuta yake ya mkononi na kuweka CD ambapo alimgeuzia kompyuta Godfrey Makali na kumpa nafasi ya kuangalia!

Haikumchukua muda mrefu Bwana Godfrey Makali kuanza kutumbua macho mithili ya mjusi aliyebanwa na mlango! Kama ilivyo kwa wenzake, nae alikumbuka matukio haya moja baada ya lingine! Lilikua ni tukio lililokuja baada ya kutoa zabuni kwa kampuni moja ya ujenzi wa barabara. Zabuni zilizoipatia ushindi kampuni hii iliendeshwa kwa uwazi na uhalali kabisa. Aidha, kampuni hiyo iliyoshinda, ilitekeleza vipengele vyote vilivyohitajika kama masharti ya zabuni husika. Hata hivyo, baada ya kampuni hiyo kushinda zabuni, wao wenyewe wakajua kwamba hawakua na uwezo wa kufanya kazi waliyoomba! Si kwamba hawakuwa na vifaa vya kutosha tu tofauti na walivyoeleza, bali hata wataalamu wa kufanya kazi hiyo hawakuwa nao! Ili kuziba pengo hilo, wakaamua *kufanya biashara* na mheshimiwa waziri pamoja na watendaji wengine serikalini! Hadi wakati anaoneshwa filamu yake hiyo, miaka zaidi ya saba ilishapita na ujenzi wa barabara ulikuwa haujafikia hata robo ya kazi, na wala haikuelekea kwamba ungeisha! Na kwa muda wote ambao yeye alikuwa kama kiongozi mwenye dhamana alishindwa hata kuuliza, kwani kila alipofikiria kufanya hivyo, alikumbuka takrima aliyopewa na hivyo kuamua kuwa bubu!

Takrima, ikamfunga mdomo mheshimiwa waziri!

“Bila shaka mheshimiwa hivi sasa upo tayari kutusikiliza?” Hatimae Nkuba alimgutusha Bwana Godfrey Makali kutoka lindi zito la mawazo! Hata hivyo, inaelekea sauti hii ilikosa kupeleka ujumbe uliokusudiwa kwa mheshimiwa!

“Mheshimiwa, vipi utatusikiliza au tuondoke kama ulivyotuamuru hapo kabla?” Nkuba alikumbushia!

“Hao watu ni akina nani?” Hatimae Mheshimiwa Godfrey Makali akafanikiwa kufungua mdomo! Jeuri yote, mfukoni!

“Sikiliza Mheshimiwa, tunasikitika kusema kwamba maswali yakiwa mengi basi unaweza kutiwa mikononi mwa wabaya wako kabla hujafika popote. Salama yako wewe ni kufuata maelekezo yetu, ambapo rafiki yako mmoja ametuamuru tuje kukushauri uende Nairobi leo hii hii! Sio kwamba unatoroka nchini la hasha! Kinachotaka kufanyika ni kukuweka mbali na hujuma iliyopangwa kufanywa dhidi yako muda si mrefu. Wakati wewe ukiwa safarini kuna timu imepangwa ambayo itashughulika na hao watu na kuwapoteza kabisa. Hao watu wakija ni lazima watakutafuta, na watakulazimisha kusaini baadhi ya nyaraka fulani chini ya mtutu wa bunduki. Ukishasaini nyaraka hizo zitakuwa zinawatia hatiani hata hawa waliopanga njama za kukutorosha. Hapo maaana yake ni kwamba tayari itabainika ni nani walikupatia rushwa hiyo. Na mbaya zaidi,kampuni ambayo ilikupatia takrima ina uhusiano wa karibu kabisa na kigogo mmoja wa juu kabisa serikalini. Hivyo basi, ukishaingia kwenye mtego wa kusaini nyaraka hizo maana yake ni kwamba tayari itakuwa umeshamuweka kigogo huyo matatani! Sasa jambo hilo hatuwezi kuliruhusu kutokea ili kulinda maslahi ya taifa! Hivyo basi, wewe kukuambia uende Nairobi ni kukunusuru wewe binafsi na kulinda maslahi ya taifa hili kwa ujumla!” Wendy alimalizia maelezo yake kisha akaingiza mkono mfukoni na kutoa kadi ya simu(*sim card*) ambayo ilikuwa bado haijatumika na kumpatia Godfrey Makali. Kadi hii ilikuwa ni ya kampuni ya SafariCom inayotumika sana nchini Kenya!

“Sasa hii kadi ni ya nini?” Godfrey Makali aliuliza.

“Ukifika Nairobi utaitumia hiyo kadi na ifikapo saa nne usiku mheshimiwa atakupigia kukueleza hali halisi!” Wendy aliendelea kucheza na akili za Godfrey Makali!

“Mheshimiwa nani?”

“Acha maswali ya kitoto Makali! Unafikiri ni mheshimiwa gani awezaye kukupigia simu kwa kutumia namba ya siri?” Wendy aliongea kwa sauti kavu kisha akaingiza mkono kwenye kibegi chake na kutoa tiketi ya ndege ya kwenda na kurudi Nairobi siku inayofuata!

“Tunakutakia safari njema Mheshimiwa, sisi tupo nje tunakusubiri kwavile inabidi tukuwekee ulinzi kila utakapoenda hadi utakapofanikiwa kupanda ndege! Weka vitu vyako vizuri na kwavile itabidi uende nyumbani basi fanya hivyo haraka. Ondoa wasiwasi, serikali inakulinda! Na wala hakuna atakayeuliza Godfrey Makali ameenda wapi kwavile suala hili linafahamika kwa viongozi wa juu wa nchi hii!” Wendy alimalizia maelezo yake.

Godfrey Makali hakua na namna nyingine zaidi ya kukubali! Kwanza suala la zile picha za video zinazomuonesha akifanya mambo yasiyofaa ziliifanya akili yake igome kufanya kazi. Aidha, aliamini hawa watu hawakua na nia mbaya kwake, kwani wangekuwa na nia mbaya basi wangeweza kumfanyia kutokana na ushahidi walionao dhidi yake. Na kwa upande mwingine, maelezo ya akina Wendy yalimfanya aamini kuwa watakuwa ni watu wa usalama wa taifa waliotumwa na uongozi wa juu wa nchi ili kulinda maslahi ya nchi!

Akakumbuka kikao na mkuu wa nchi ambacho mkuu huyo hakuongea chochote!

*“Wote turudi sehemu zetu za kazi hadi hapo uchunguzi utakapokamilika!”* Mheshimiwa Makali akakumbuka kauli

ya mwisho na pekee ya rais! Hapo hapo akapata jibu kwamba kumbe kikao kile cha rais kilimuhusu yeye!

Wakati Godfrey Makali akikumbana na ghiriba ya akina Wendy, kijana mwingine wa George Kamau akiongozwa na Glory walikuwa kwa Austine Ishengoma wakifanya yaleyale yaliyokuwa yanafanywa na akina Wendy kwa Godfrey Makali!

Austine Ishengoma alikuwa ni miongoni mwa watendaji wa serikali ambao walikuwa wamejilimbikizia utajiri mkubwa kabisa kinyume na sheria. Pamoja na utajiri uliotokana na upokeaji wa rushwa, kuna wakati fulani, kwa kutumia nafasi yake alipokuwa Wizara ya Ardhi na Makazi, Ishengoma alifanikiwa kufanya hujuma kubwa dhidi ya serikali. Hujuma hii ilikuja pale serikali ilipokusudia kugeuza matumizi ya ardhi ya maeneo kadhaa jijini kama vile Kurasini na Kigamboni. Kabla jambo hili halijafahamika kwa wakazi wa maeneo hayo, Austine Ishengoma alikula njama na kuchukua mkopo mkubwa benki pamoja na taasisi zingine za fedha. Baada ya kufanikisha hilo, aliwatumia ndugu na watu wake wa karibu kununua nyumba na viwanja kadhaa kwenye maeneo hayo. Aidha, aliunda mtandao wa siri uliotumika kuwatisha wakazi wa maeneo hayo kwamba serikali ilikuwa na mpango wa kuyatwaa maeneo hayo kwa nguvu na isingelipa fidia yoyote. Mtandao huu ulifikia hatua ya kuonesha hadi ramani za kughushi za matumizi sahihi ya maeneo hayo kabla wakazi hao *hawajayavamia*! Ramani hizi ambazo zilipandikizwa hadi wizara ya ardhi zilionesha kwamba eneo kubwa la Kurasini ni mali ya Mamlaka ya

Bandari na lile la Kigamboni ni mali ya Jeshi la Wananchi Tanzania! Ikiwa mtu angeenda wizara ya ardhi na kuomba kuoneshwa ramani ya matumizi ya ardhi ya Kigamboni na Kurasini basi angeoneshwa ramani hii ya kughushi! Hivyo basi, kutokana na hofu waliyokuwa nayo ya kukosa haki zao, wengi wao wakalazimika kuyauza maeneo yao, tena kwa bei ya kutupa kabisa! Na ili kuhakikisha anavuna zaidi kupitia hiyo hujuma yake, Ishengoma alihakikisha nyingi ya nyumba anazonunua ni zile tunazoweza kuziita za mbavu za mbwa. Kwa kutumia mikopo aliyopata na pesa kutoka kwenye baadhi ya biashara zake na kutoka kwenye hujuma zingine, Austine Ishengoma alifanikiwa kununua nyumba na viwanja kadhaa! Baada ya kufanikiwa zoezi hilo, lilifuata zoezi la kuviendeleza viwanja hivyo ambapo alijenga nyumba na majengo kadhaa ya biashara. Muda ulienda, na huku akifanya kila aliloweza ili kuharakisha mpango huo, hatimae wakati aliokuwa anausubiri kwa hamu uliwadia! Zoezi la kufanya uthaminishaji wa mali za watu kwenye maeneo hayo likaanza. Huku serikali ikiamini kwamba majengo na mali zote zilizokuwepo hapo ni za wananchi wa kawaida lakini ukweli ni kwamba kulikuwa na idadi kubwa kabisa ya mali za Austine Ishengoma! Na kwa kutumia maafisa wa uthaminishaji, majengo yake yote yalipewa thamani zaidi ya mara mbili hadi tatu ya ile thamani yake halisi! Zoezi lilikamilika likiwa limemwacha Austine Ishengoma akibakiwa na ukwasi wa kutisha!

Hii ilikuwa ni moja tu ya matumizi yake mabaya ya dhamana ambayo alipewa na serikali!

# 13

“Karibuni Bwana Siyame!” Bwana Elisante Josephat aliwakaribisha Jonas Siyame na akina Michael Mchupi mara walipoingia ofisini kwake. Hakika alipowaona tu, moyo wake ulipiga mkamba kwa taharuki! Alianza kukosa amani tangu alipoachwa kwenye mataa na IGP Jaffery Minga kiasi kwamba akawa tu anasubiria ujio wa shari wa Michael Mchupi! Hata hivyo, hivi sasa hofu yake iliongezeka maradufu kufuatia msafara huu kuongozwa na kigogo wa TAKUKURU! Taswira ya waandishi wa habari waliokuwa wakipigana vikumbo kumpiga picha kwa fujo ilianza kupitia akilini mwake!

*“Wote turudi sehemu zetu za kazi hadi hapo uchunguzi utakapokamilika!”* Kauli ya mkuu wa nchi ikahirudia tena na tena akilini mwake! Kuja kwa mkubwa wa TAKUKURU ofisini mwake kulimwashiria ule uchunguzi uliosemwa na mheshimwa rais tayari umeshakamilika! Hisia hizi zikamjengea taswira ya wananchi waliokuwa wakimzomea wakati anatolewa kwenye Mahakama ya Kisutu na kurudishwa mahabusu!

“Ahsante Mheshimiwa, mimi naona tusipoteze muda. Hawa jamaa wanatoka kampuni ya ulinzi na uchunguzi ya ISLIB. Kwa maana nyingine, ni wadau wa TAKUKURU na ni wadau wa wizara yako vilevile!” Jonas Siyame alianza kueleza. Hakufahamu kwamba tayari Michael Mchupi alishawahi kukutana na Bwana Elisante kabla yake! Baada ya utambulisha huo, Siyame aliendelea:

“Hawa mabwana kupitia ISLIB wametuletea ushahidi kuhusu mawaziri wawili waliopokea rushwa. Mimi na timu yangu tumeupitia ushahidi wote na tumeridhika nao! Hata hivyo, mawaziri hao wapo mbioni kuikimbia nchi, na si ajabu mawio ya leo yasiwakute Tanzania! Kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na watu hawa, TAKUKURU imeonelea kuchukua hatua za haraka kabla waheshimiwa hao hawajatoroka na lawama kuangukia kwetu. Hivyo basi, nimekuja kwako kwavile inabidi tushirikiane na Mkurugenzi wa Mashitaka leo hii ili kuzima jaribio la hao mabwana kutoroka! Najua ni uamuzi wa ghafla lakini kutokana na unyeti wenyewe nina hofu hawa watu wanaweza kupotea wakati tuna uwezo wa kuzuia jambo hilo kutokea!” Jonas Siyame alimalizia maelezo yake na kumfanya Bwana Elisante Josephat kumtupia Michael Mchupi jicho la wizi! Huko alikutana na jicho kali la Mchupi ambalo lilimtisha kiasi cha kukaribia kuachia haja ndogo hapohapo!

“Una hakika na ushahidi wenyewe Siyame?” Hatimae Bwana Elisante Josephat alijibaraguza kwa swali ili mradi tu asionekanae yupo rahisi!

Wakati upande mmoja akijitahidi kujibaraguza, kwa upande wa pili Bwana Elisante alishindwa kupata picha halisi za tukio hili hususani kuhusika kwa Jonas Siyame! Alijiuliza endapo Siyame nae aliingia kwenye mtego kama wa kwake au ilikuwa ni katika utekelezaji tu wa kazi yake!

“Kwahiyo mheshimiwa, hiyo ndio njia pekee ya kusahihisha makosa yako!” Michael Mchupi aliongea kwa sauti kavu iliyomtisha vilivyo Bwana Elisante Josephat ambae moja kwa moja alielewa alilenga nini! Hisia za utumwa wa kudumu ikampitia akilini mwake!

Bon Mtambo alikuwa nyumbani kwake Chang'ombe na kilichomsukuma zaidi kwenda huko ni kufuata simu baada ya ile aliyokua anaitumia kuishiwa *chaji*. Bila kupoteza muda aliichukua simu ambayo alinunuliwa na Glory walipokuwa Marekani na kuanza kuandika namba za SSP Faraji Zegge lakini ghafla akahisi ubaridi fulani ukipita akilini mwake baada ya kukumbuka maneno ya DCI Mwaiswelo: *".......Hata hivyo, baada ya kumfuatilia wakagundua kuwapo kwa jambo ambalo si la kawaida kidogo kutoka kwake, je unamfahamu vizuri lakini huyo binti?"*

Hajui ni kwanini, lakini sauti hii hivi sasa aliiona ni kama taadhari ingawaje alipoambiwa siku ya kwanza aliipuuza! Ghafla akajikuta akisitisha zoezi la kupiga simu na badala yake akawasha kompyuta iliyounganishwa na intaneti. Alichukua vielelezo vilivyoihusu simu hii na kuanza kutafuta habari zake kwenye intanet!

"*Bitch*!" Bon Mtambo alilaani huku akimtusi Glory kwa kumfananisha na mwanamke malaya! Ghadhabu hizi za Bon Mtambo zilikuja baada ya kusoma habari kwamba simu ile ilikuwa na uwezo tofauti na simu za kawaida! Hapa ndipo alipokuja kugundua ni kwanini Glory alimbembeleza sana waende Marekani! Na hapa ndipo akaja kubaini kwamba hata kuporwa kwa simu yake kule Marekani kulipangwa ili Glory apate sababu ya kumnunulia simu hii! Aliamini kwamba hata lile duka walilonunua simu lilikuwa ni miongoni mwa maduka ya watu wao, au la mmoja wa hawa majahili!

Kufuatia hali hii, Bon Mtambo alizirejesha kumbukumbu zake siku ya kwanza alipokutana na Glory baada ya kutokea ajali pale Chang'ombe maeneo ya

TAMECO! Hapo ndipo akaja kubaini kuwa hata ile ajali nayo ilikuwa ni ya kupanga!

*"Kama wanazani wao ni werevu basi nitawaonesha mimi ni mwerevu zaidi yao*!" Bon Mtambo aliongea peke yake na kukata shauri la kuendelea kuitumia simu hiyo bila kujali kwamba hiyo itasababisha aweze kufuatiliwa kirahisi zaidi!

"Ndiyo bosi, naona simu yako ilikatika. Taarifa za karibuni ni kwamba Jonas Siyame na wageni wake walikua ofisini kwa waziri wa mambo ya ndani na sasa wale watu wameondoka lakini Jonas na mheshimiwa waziri wameingia ofisini kwa Mkurugenzi wa Mashitaka,!" SSP Faraji Zegge alieleza mara baada ya kupigiwa simu na Bon Mtambo kwa kutumia simu ileile aliyonunuliwa na Glory! Aidha, kabla hajafanya kitu chochote mara tena simu yake ikaita. Alipoangalia namba, zilikuwa ni za DCI Mwaiswelo!

"Ndiyo mzee, nakupata!"

"Ni hivi kijana, muda mfupi uliopita nilipigiwa simu na Bwana Elisante akiagiza kuchunguzwa kwa nyendo za mawaziri wawili; Bwana Godfrey Makali na Austine Ishengoma. Na taarifa nilizozipata hivi punde ni kwamba mawaziri hao wapo katika harakati za kusafiri nje ya nchi, ingawaje sina maelezo ya kutosha kuhusu chanzo cha safari hiyo. Nimeamua kukujulisha kwavile nina shaka nao wakawa ni walengwa wako!"

"Sawa mzee, mimi nazani itakuwa busara endapo mheshimiwa waziri ataarifiwa suala la wao kuhisiwa kutaka kusafiri nje ya nchi, isije ikawa wanataka kutoroka. Akishaarifiwa, bila shaka atajua nini cha kufanya!" Bon Mtambo alijibu na kukata simu kabla ya kushusha pumzi ndefu! Hakika alishindwa kufahamu ni nini maana ya mchezo huo! Hakua na shaka kwamba George Kamau

yupo nyuma ya mchezo huo ingawaje hakufahamu lengo lake.

Baada ya kuongea na DCI Mwaiswelo, Bon Mtambo alimpigia simu Inspekta Mussa Ndimbu na Insepkta Cecy kisha mmoja akamwagiza akafanye doria Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Nyerere na mwingine uwanja wa ndege wa zamani, maarufu kama *Terminal One*! Aidha, alimpigia simu Inspekta Fareed na kumwagiza akafanye doria yake kituo cha mabasi cha Ubungo! Bon Mtambo alikua na hakika kwamba mawaziri hao wasingeweza kutoroka bila kutiwa mikononi. Alichotaka yeye ni kufahamu mazingira ya kukamatwa kwao!

Baada ya kutoa maagizo hayo, alichukua kadi nyingine ya simu na kuiingiza kwenye simu ambayo alikuwa anaitumia zamani kabisa kabla hajaiacha baada ya kuona imeshapitwa na wakati. Baada ya kazi hiyo, akaamua kuwapigia baadhi ya watu wake kuwaambia kwamba endapo wangetaka kumpigia basi watumie namba hiyo. Miongoni mwa watu aliowaambia ni Layla. Bon Mtambo alikusudia kwamba namba aliyoweka kwenye simu aliyonunuliwa na Glory, awe anapiga yeye tu kwa wakati na sababu maalumu!

Ujio wa ghafla wa Bwana Elisante Josephat na Jonas Siyame ulimshtua Bi. Natalia Kudilu, Mkurugenzi wa Mashitaka ya Umma nchini Tanzania. Hiki kilikuwa ni kipindi ambacho mara kwa mara, yeye kama DPP, alikuwa akishutumiwa kuchelewa kuzifikisha mahakamani kesi za vigogo wanaotuhumiwa kwa ulaji rushwa.

“Samahani Bi. Natalia kwa kukuvamia ghafla, mazingira ya kazi iliyopo mbele yetu ndiyo yametulazimisha kufanya hivi!” Bwana Elisante Josephat alifungua maongezi mara baada ya kuketi!

“Bila samahani mheshimiwa, ni matarajio yangu kwamba kuna jambo kubwa lililowasukuma kufanya hivyo!”Bi. Natalia Kudilu alijibu kwa sauti tulivu lakini huku akionekana kuwa makini zaidi.

“Ni kweli Bi. Natalia, kuna jambo kubwa limetokea ambalo ofisi yangu imelazimika kukiuka taratibu ili jambo hilo liweze kushughulikiwa kwa ajili ya kulinda maslahi ya taifa. Nilijikuta katika wakati mgumu wa kufanya maamuzi hadi nilipoletewa maagizo kutoka kwa mzee kushughulikia suala hilo na kwamba taratibu zingefuata baadae. Kwa kifupi tu ni kwamba, kuna mawaziri wawili wanatuhumiwa kupokea rushwa kufuatia uchunguzi uliofanywa na kampuni ya ISLIB. Mbaya zaidi, taarifa za uchunguzi huu zimevuja na hapa ninapoongea mawaziri hao wapo mbioni kutoroka nchi. Kutokana na hofu hiyo ya kutoroka, ndio maana zimekuja taarifa kutoka juu kwamba ofisi yangu na yako ihakikishe watu hao wanakamatwa leo leo na kupelekwa mahakamani mapema iwezekanavyo. Hivyo basi, tumekuja kwako kukueleza uandae hati ya mashitaka sasa hivi kwa.....!” Kabla hajamalizia malelezo yake, mara simu yake ya mkononi iliita. Alipoangalia namba zake akagundua ni za Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai nchini; DCI Mwaiswelo!

“Mkurugenzi wa upelelezi anapiga!” Bwana Elisante Josephat aliwaambia wenzake ambao nao wakajiweka tayari kusikiliza! Mithili ya mtu aliyezisoma akili zao, Bwana Elisante Josephat aliweka kipaza sauti ili maongezi kutoka kwa DCI yasikike kwao pia:

"Ni hivi mzee, kufuatia taarifa za Bwana Godfrey Makali na Austine Ishengoma kutaka kutoroka, tuliwatuma vijana wetu kufuatilia na wametuthibitishia kwamba kuna kila dalili za wao kutaka kusafiri. Na kutokana na sababu ambazo tuliambiwa basi kuna uwezekano mkubwa kwamba ni kweli wanataka kuikimbia nchi na..!"

"Sikiliza DCI, hakikisha hao watu wanatiwa mbaroni kabla hawajatoroka!" Ghafla Bwana Elisante Josephat aliingilia kati maongezi kwavile alijua hiyo ndio karata yake ya mwisho aliyopewa na Mchupi!

"Sawa mheshimiwa, tulikua tunataka ruhusa kutoka juu kwavile kumkamata waziri ni tofauti na kumkamata raia wa kawaida!" DCI Mwaiswelo alijitetea.

"Tekelezeni kazi yenu, hapa tuna ushahidi wote wa ushenzi wao! Nyinyi fanyeni kazi yenu wakati sisi huku tunaandaa taratibu za kisheria! Lazima ujue kwamba endapo watatoroka basi msalaba wote utakuwa juu yenu kwavile mlishataarifiwa mapema! Hata hivyo, jitahidini muwakamate wakati wanaelekea kupanda ndege ili kuwe na ushahidi wa kutosha kwamba walitaka kutoroka!" Bwana Elisante Josephat alimweleza DCI Mwaiswelo kwa ukali kidogo huku akitumia na vitisho ndani yake!

"Bi. Natalia, hiyo ndio hali halisi!" Hatimae Bwana Elisante alimgeukia DPP kisha akachukua na kanda za video za akina Godfrey Makali na kumpatia ili azichunguze. Na hata kama alikusudia kupinga maelezo ya Bwana Elisante, simu ya DCI Mwaiswelo ilielekea kulainisha msimamo wa Bi. Natalia Kubilu!

George Kamau alikuwa ametulia ofisini kwake wakati kifaa maalumu kwenye simu yake kilipotoa mlio! Aliangaza macho yake huku na huko kama anayetaka kuthibitisha kwamba yupo peke yake au hapana! Kimsingi, hakutarajia kabisa mlio huo kutokea kwa sasa kwavile alijua kwamba tayari Bon Mtambo walishamweza! Hisia kwamba Bon Mtambo alisharudi mtaani, zisingekuwa hisia za kufurahisha hata chembe akilini mwa Kamau pamoja na watu wake!

*"Sawa mzee, nazani itakuwa busara endapo mheshimiwa waziri ataarifiwa suala la wao kuhisiwa kutaka kusafiri nje ya nchi. Hofu yangu ni kwamba inawezekana ikawa wanataka kutoroka, bila shaka yeye atajua nini cha kufanya!"* George Kamau aliyarejea maongezi ya Bon Mtambo baada ya kurushwa kwa kutumia kifaa maalumu cha kusafirisha mawasiliano kutoka kwenye simu ya Bon Mtambo hadi kwenye simu yake!

*"Ni nani huyu mzee?!"* George Kamau alijiuliza .

Baada ya kujiuliza maswali kadhaa bila kupata majibu, alinyanyua simu na kuwapigia baadhi ya watu wake ili akutane nao kwenye chumba cha hoteli moja iliyopo nje kidogo ya jiji. Huu ndio ulikuwa utaratibu kwao, kwamba kila ilipolazimika kukutana na watu basi wangekutana hotelini.

ଓ৯ഈ৵ഈ৶ଔ৺

Bon Mtambo alikuwa amebana mahali ndani ya gari jirani kabisa na zilipo ofisi za Mkuregenzi wa Mashitaka nchini, Bi. Natalia Kudilu. Haikumchukua muda mrefu kabla hajamuona Bi. Kudilu akitoka ofisini akiwa ameongozana na Bwana Elisante Josephat na Jonas Siyame.

Walikuwa wakitembea kwa hatua fupi fupi huku kila mmoja akionekana kuongea na simu! Jambo moja lilimshangaza Bon Mtambo! Kila mmoja alipomaliza kuongea na mtu mmoja, alionekana kumpigia mtu mwingine. Wakiwa katika harakati hizo, mara alimwona SSP Faraji Zegge akipita karibu yao lakini huku akionekana kama asiye na habari na wao!

SSP Faraji Zegge alitembea kwa hatua za taratibu lakini ghafla akajikwaa na kudondoka! Ilimchukua karibu dakika moja kujipangusa vumbi! Waheshimiwa waliokuwa wanaongea na simu wakaonekana kutokuwa na habari nae, labda walichokuwa wanaongea hakikuwa siri!

Bon Mtambo akatabasamu!

Akiwa bado amebana humo garini, mara simu yake ikaita. Kwa kuhofiwa mazungumzo yao kunaswa na akina Kamau, alikata simu na kuchukua simu nyingine kisha akampigia SSP Faraji Zegge ambae ndie aliyepiga awali.

"Pole Inspekta kwa kudondoka!" Bon Mtambo aliongea kwa utani hali iliyomfanya SSP Faraji Zegge aangue kicheko.

"Ahsante bosi, kumbe uliniona! Mbona umebadilisha namba ghafla?!" SSP Faraji Zegge aliuliza.

"Kuanzia sasa ukitaka kunipigia tumia namba hii." Bon Mtambo alieleza kisha akaendelea: "Haya Inspekta, lete umbeya, bila shaka una mengi!" Alimalizia.

"Ni hivi bosi, waheshimiwa wanataka kukutana na vyombo vya habari hivi punde. Nimewasikia wakiwapigia wahariri kadhaa wa vyombo vya habari wakiwaomba wawaruhusu waandishi wao mara moja kwavile kuna jambo muhimu limetokea. Na kwa inavyoelekea, hakutakuwa na utaratibu maalumu wa kuingia kwani wanataka wawepo waandishi wengi iwezekanavyo wakati

muda wa maandalizi ni mfupi. Aidha, mkutano huo utafanyika kwenye ukumbi wa Idara ya Habari, Maelezo!”

“Kazi nzuri Inspekta.” Bon Mtambo alimpongeza kisha akaendelea, “Sasa wewe nenda kacheze jirani na pale ukumbi wa maelezo kuangalia usalama kwavile mimi nitakuwa ndani pamoja na waandishi wengine wa habari. Lakini kuwa makini kwavile hufahamu ni nani na nani amekuona ulipokuwa unacheza jirani na ofisi za TAKUKURU na pale ulipojikwaa!”

Baada ya kumaliza kuongea na SSP Faraji Zegge, Bon Mtambo alipiga gari moto lakini kabla hajaliondoa, mara simu yake ya kawaida ikaita. Alikua ni Layla!

“Lete habari mrembo!”

“Hapa nipo uwanja wa ndege, nazani unafahamu ni kwanini nipo hapa kwa sasa! Wakati nikiwa nasubiri, Kamau alinipigia simu kuniambia nitakapomaliza kazi yangu basi niwahi pale ukumbi wa Idara ya Habari.“ Layla aliongea kisha akatoa taarifa kuhusu kuwapo kwa mkutano na waandishi wa habari hapo Maelezo.

“Hongera, natarajia nitafahamu mengi kutoka kwako pindi utakaporudi!” Bon Mtambo aliongea bila kuonesha kwamba nae alikuwa na taarifa hizo kisha wakaagana.

Huku akifahamu fika kwamba maongezi yake yangenaswa na George Kamau, Bon Mtambo alichukua simu yake na kumpigia Inspekta Daniel Chacha. Simu aliyotumia ni ileile aliyonunuliwa na Glory!

“Sikiliza kijana, nimeshagundua kwamba ISLIB inahusika moja kwa moja na hujuma zinazoendelea.

Pamoja na ISLIB vilevile kuna watu wenye ushawishi ambao pia wanafanya kazi pamoja na ISLIB, ama kwa kupenda au kwa kushinikizwa. Ni wajibu wetu kuwafahamu watu hao mara moja. Hivyo basi, wewe endelea kumfuatilia huyo Kamau kwa kila hatua anayopiga, lakini hakikisha hakuoni…! Unasema? Hata hapo haupo mbali na yeye?! Safi sana, endelea hivyohivyo! Mimi na baadhi ya makachero tunaelekea kwenye hotel moja pale Ubungo kupanga mikakati ya kukabiliana nao!" Bon Mtambo alimalizia kisha akapiga gari moto hadi kwa DCI Mwaiswelo. Maelezo haya yalimchanganya sana Inspekta Daniel na kuhisi kwamba huenda Bon Mtambo alikosea kumpigia yeye. Huku akiwa bado anaendelea kujiuliza maana ya simu ile mara simu yake ikaita.

"Achana na maelezo niliyokupatia hivi punde, nilikua nampumbaza Kamau ambae nimegundua kwamba anayanasa maongezi yangu ya simu. Aidha, kuanzia sasa ukitaka kunipigia utatumia namba hii na usithubutu kutumia ile ambayo nilikupea maelezo kuhusu Kamau!" Bon Mtambo alimweleza Inspekta Daniel wakati akiingia ofisini kwa DCI Mwaiswelo.

"Mzee, nimekuja kuiacha hii simu yangu hapa na nitaifuata baada ya muda mfupi!" Bon Mtambo alimweleza DCI Mwaiswelo mara alipoingia ofisini mwake.

"Isije ikawa imetegwa bomu kijana!" DCI Mwaiswelo alitania!

George Kamau alikumbwa na mshituko mkubwa ulioambatana na taharuki wakati kifaa chake cha mawasiliano kiliponasa maongezi ya Bon Mtambo na

Inspekta Daniel! Habari kwamba Bon Mtambo alimgundua yeye na ISLIB ilikuwa ni habari mbaya sana kuliko yoyote ile katika kipindi chote cha kazi hii. Taarifa hii ilimlazimisha kubadili ratiba na utaratibu wa kupambana huku hivi sasa akiweka mkazo kwenye kummaliza Bon Mtambo mapema iwezekanavyo! Aidha, suala kwamba kuna mtu anamfuatilia kila hatua anayopiga wakati yeye hajashuku chochote ilikua ni taarifa nyingine ya kuogofya, sawa na kunyemelewa na ziraili kwa kila hatua unayopiga! Taarifa hii ilimfanya George Kamau awe anageuka kila wakati ili ajaribu kumshuku huyo mtu anayemfuatilia.

Hakuambua chochote!

Wakati Kamau akiwa katika hali ya taharuki, Bon Mtambo kwa upande wake alikuwa ameshapata taarifa kuhusu idadi kubwa ya waandishi wa habari waliokuwa wamefika pale Ukumbi wa Habari wa Maelezo. Kwavile hakuwa mbali sana na hapo, alifanya haraka na kufanikiwa kuingia ndani bila usumbufu wowote. Muda si mrefu baadae, Bwana Elisante Josephat , Bi. Natalia Kudilu na Jonas Siyame waliwasili. Aidha walikuwa wameongozana na mtu mwingine ambae baadae alijitambulisha kama Msemaji Mkuu wa ISLIB. Iliwachukuwa tena kiasi cha dakika tano za maandalizi ndipo Jonas Siyame akaanza kuongea:

“Ndugu waandishi wa habari, awali ya yote poleni na majukumu yanayowakabili ambayo wakati mwingine mnajikuta mkilazimika kukatisha ratiba zenu ili kufuatilia mambo makubwa yanayolikabili taifa letu. Sina shaka kwamba wengi wenu kama sio wote mpo kwenye mshangao wa ni kwanini kikao hiki kimeitishwa ghafla hivi! Kwakweli kuna jambo limetokea ambalo lisingehitaji tena ngojangoja ya kuuharifu umma kupitia nyinyi. Kwa

kifupi tu ni kwamba, nazani mnafahamu uwepo wa kampuni moja ya ulinzi hapa nchini iitwayo ISLIB. Pamoja na kujihusisha na masuala ya ulinzi, kampuni hii vilevile inajihusisha na mambo ya uchunguzi dhidi ya aina yoyote ya uhalifu. Katika hili, ISLIB imekuwa ikifanya kazi hiyo kwa kukodiwa na watu au taasisi wanaotaka wafanyiwe uchunguzi dhidi ya uhalifu uliotokea kwenye maeneo yao. Aidha, ISLIB imekuwa ikiendesha uchunguzi kwa mambo yenye maslahi ya taifa ama kwa utashi wao wenyewe au kwa kuagizwa na mamlaka husika. Katika suala hili la kuendesha uchunguzi katika mambo yenye maslahi ya taifa, leo hii ISLIB imekuja na matokeo ya uchunguzi muhimu kabisa. Kama mjuavyo, nchi yetu hivi sasa ipo katika mapambano makali dhidi ya vitendo vyote vya hujuma, rushwa na ufisadi unaotokea. TAKUKURU peke yake haiwezi kukomesha vitendo hivi, na ndio maana tungependa kutumia fursa hii kuipongeza ISLIB kwa hatua yake ya kupambana na vitendo vya hujuma dhidi ya mali ya umma.” Alitulia kidogo na kuanza kupitisha macho yake huku na huko, kisha akaendelea:

“Ndugu zangu, leo hii ISLIB imetuletea ushahidi wa kutosha kabisa dhidi ya mawaziri wawili; Bwana Godfrey Makali na Austine Ishengoma. Kwa bahati mbaya kabisa, habari za uchunguzi huu zilivuja na kuwafikia mawaziri husika; hali iliyowafanya mawaziri hao waanze kufanya harakati za kutaka kutoroka. Na hapa tunapoongea tayari tumepata habari kwamba mawaziri hawa wapo njiani kutaka kuikimbia nchi! Ni kuto.....!” Kabla hajaendelea na maelezo yake, alisita baada ya kuona Mheshimiwa Elisante akipokea simu huku akimwashiria atulie kidogo.

Mheshimiwa Elisante aliongea na simu kwa sekunde chache kisha akamgeukia Jonas Siyame na kuanza kumnong'oneza jambo!

"Ndugu waandishi wa habari, mheshimiwa alikuwa ananinong'oneza hapa kwamba tayari Bwana Godfrey Makali na Austine Ishengoma wamekamatwa uwanja wa ndege wakati wakijaribu kutoroka! Hapa wameudhihirishia umma kwamba wao ni watu wa namna gani. Na kwakweli ningependa kuitumia fursa hii kuipongeza kampuni ya ISLIB kwa kazi yake mzuri iliyofanya kwa maslahi ya taifa......!"

Maelezo ya Jonas Siyame na Bwana Elisante Josephat kwa waandishi wa habari yalikuwa marefu huku yakitoa sifa lukuki kwa ISLIB. Aidha, waliwataka waandishi wa habari na wananchi kwa ujumla wawaunge mkono ISLIB katika vita vyao hivi walivyovianzisha.

"Ndugu waandishi, kama mjuavyo leo hii ISLIB ndio imetangaza rasmi vita dhidi ya wahujumu nchini mwetu. Sina shaka kwamba, baada ya tukio hili tayari ISLIB itakuwa imeshajingea uadui mkubwa toka kwa wahujumu wa nchi hii. Lazima ieleweke kwamba ISLIB imeingilia maslahi ya watu wazito nchini ambao si wanasiasa pekee, bali hata watendaji wengine wakuu wa serikali pamoja na wafanya biashara wakubwa. Hivyo tusishangae endapo siku chache za usoni tukiona kampuni hii ikianza kupigwa vita na mapapa wa hujuma hapa nchini. Hata hivyo, sisi wana ISLIB tunawaahidi wananchi wa nchi hii kwamba kampuni yetu haitatishika na yeyote na bado tutaiendeleza vita hii hadi nchi yetu inakuwa huru dhidi ya vitendo haramu. Na kwa taarifa yenu tu ni kwamba, kuna kesi nyingine zinazowahusu wahujumu wakubwa ambao zitatolewa taarifa zake hivi karibuni.

Hivyo basi, tunahitaji ushirikiano wenu hususani wa ari ili ISLIB iweze kuiendeleza vita hii. Milango yetu ipo wazi kwa waandishi wa habari watakaotaka kufahamu zaidi kuhusu kazi za ISLIB."

" Pamoja na hilo, ISLIB inamkaribisha mtu yeyote mwenye taarifa zitakazotuwezesha kufuatilia kwa urahisi tukio lililotokea pale Mahakamani Kisutu. Moja ya malengo yetu makuu ni kuhakikisha dunia inakuwa huru na vitendo vya kigaidi. Ugaidi na rushwa, ni ndugu mmoja. Kuna habari ambazo hazijathibitishwa kwamba tukio lile limefanywa na watu wenye uhusiano na Bon Mtambo; kijana wa Kitanzania anaetuhumiwa kujihusisha na ugaidi. Ni bahati mbaya sana kwamba hadi hivi sasa watanzania wanaamini huyu kijana bado yumo mikononi mwa polisi! Hata hivyo, habari za kiuchunguzi nilizozipokea hivi punde ni zinasema kwamba Bon Mtambo hayumo tena mikononi mwa polisi! Sina shaka yoyote kwamba Bwana Mtambo atakuwa ama ametoroshwa au ameachiwa kutokana na shinikizo zilizotolewa na magaidi wenzake. Yote hayo yasingeweza kutokea endapo jamii yetu ingekuwa si jamii ya wala rushwa. Hivyo basi, natumia fursa hii kuwatangazia Watanzania kwamba ISLIB itaisaidia serikali kuchunguza kutoweka kwa Bon Mtambo na chanzo cha mlipuko uliotokea pale Kisutu." Mtu ambae awali alijitambulisha kwamba ni msemaji mkuu wa ISLIB nae alitoa maelezo kwa upande wake. Maelezo haya ndiyo yaliyompa Bon Mtambo picha halisi ya nini maana ya mkutano huu na waandishi wa habari. Ghafla, ukumbi mzima ulitawaliwa na minong'ono ya hapa na pale baada ya kutolewa kwa taarifa za kutoweka kwa Bon Mtambo! Bon Mtambo nae hakuona umuhimu wa kuendelea kuwa hapo kwavile alishafahamu lengo la mkutano huo.

Alitumia mwanya wa minong'ono iliyotawala hapo ukumbini kuweza kutoweka bila kutiliwa shaka .

Muda ulizidi kuyoyoma bila George Kamau kupata taarifa yoyote za maana zilizohusu kuonekana kwa Bon Mtambo sehemu yoyote jijini. Kamau alikuwa ametuma vijana wake maeneo mbalimbali ya Ubungo baada ya kunasa maongezi kwamba Bon Mtambo angekua kwenye hoteli moja maeneo hayo. Kukosekana huko kwa taarifa za hoteli gani aliyokuwepo ndiyo sababu iliyomfanya ampigie simu Glory na kumwitaji haraka sana!

"Glory, hivi sasa tumeshapata uhakika kwamba Bon Mtambo hayupo mahabusu na anaendelea na kazi yake kama kawaida. Hapa ninapozungumza tayari ameshaanza kuitumia simu ambayo ulimnunulia na maongezi yake yanaonesha ameshaanza kutilia shaka nyendo zetu. Sina shaka yoyote kwamba muda si mrefu harakati zetu zinaweza kufikia ukingoni na wote kuishia jela. Hata hivyo, jambo zuri ni kwamba bado hajafahamu lolote kuhusu wewe na hivyo bado una nafasi mzuri ya kumwangamiza. Mipango kamambe imeshaandaliwa ambapo baada ya kummaliza itabidi tutoweke nchini na kwenda kula raha nchi za ng'ambo!" Baada ya kusema hayo, Kamau alifungua mtoto wa meza na kutoa hati ya kusafiria yenye jina la Happiness Mathew Mushi lakini ikiwa na picha ya Glory pamoja na viza ya kuingia Japan na nyingine ya kuingia Brazil. Aidha, alitoa na hundi ya thamani ya dola za kimarekani laki moja ikiwa na jina kamili la Glory! Hata hivyo, hundi hii ilikuwa imeandikwa tarehe ya siku tano

mbele; kwa maana nyingine ni kwamba asingeweza kutoa pesa benki hadi baada ya hizo siku tano!

“Sasa ni hivi Glory,” hatimae Kamau alianzisha tena maongezi, “kwa jinsi hali ilivyo sina shaka kwamba kazi yetu tunaweza kuihitimisha ndani ya siku tatu hadi tano kutoka sasa. Mara baada ya kuhitimisha kazi hiyo, tutalazimika kuondoka nchini mara moja ambapo wewe utaanza kwa kwenda Brazil ambako utakaa kwa muda. Ukishatoka Brazili, utaenda kuishi Japan na baada ya hapo utaanza kujaribu kuishi maisha ya kawaida ya kwenda kule utakapopenda. Maisha haya ya kujificha utaishi nayo angalau mwaka mmoja huku ukiwa unafahamika kama Happiness Mathew Mushi. Kwa kipindi chote hicho, bado utakuwa kwenye uangalizi wetu na utasaidiwa kwa kila kitu hadi pale utakapoanza kuishi maisha ya kawaida. Aidha, tunakupatia kiasi cha dola laki moja za marekani kwa ajili ya kuanzia maisha. Ni matarajio yetu kwamba zitaweza kukusukuma angalau kwa miezi mitatu.” Baada ya kufikia hapo, Kamau alichukua ile hati ya kusafiria, viza pamoja na hundi kisha akamkabidhi Glory, kisha akaendelea, “Itabidi uweke hivi vitu sehemu ya usalama zaidi kama maandalizi ya kutoweka siku yoyote mara baada ya kuhitimisha kazi. Hata hivyo, hayo ni maandalizi tu ya jinsi ya kutoweka hapa nchini. Kwa upande wa majukumu yako kwa sasa ni kwamba itabidi utumie mbinu zote ili urudi kwa Bon Mtambo. Sisi tumeandaa taarifa tutakayoipeleka kwenye vyombo vya habari kuonesha kwamba Bon Mtambo ametoroka au ametoroshwa gerezani. Wewe utaitumia taarifa hiyo kumtafuta Bon Mtambo kwavile utamwambia umesikia kwamba ametoroka na ndio maana ulikata shauri la kumtafuta ni wapi alipo!” Kamau alimalizia maelezo yake ya namna

ambavyo Glory angeweza kujiunga tena na mpenzi wake kisha akatumia muda mrefu kumwelekeza nini atatakiwa kufanya pindi atakaporudi kwa Bon Mtambo!

Hata hivyo, Glory alishindwa kabisa kufahamu kwamba mpango wenyewe ulibeba ghiriba tupu yake!

Ilikuwa ni kama anajipeleka mwenyewe, lakini inaelekea alikuwa anajua nini anafanya! Aliitazama saa yake ya mkononi na ilikuwa inakaribia kabisa kutimia saa moja kasorobo jioni.

“Oh! Bon, siamini mpenzi wangu kama ni wewe!Umetokaje mpenzi? Nani kakutolea dhamana?” Glory alimlaki Bon Mtambo kwa maswali mfululizo yaliyobebwa na furaha ya kuigiza! Hakika hakutarajia kwamba mtu aliyekuwa anagonga mlango wake angekuwa Bon Mtambo ambae kwa dakika kadhaa sasa alikuwa akijiuliza ataanza vipi kujirudisha kwake!

“Ahsante mpenzi, nilikuwa na hamu sana na wewe!” Bon Mtambo alijibu kwa furaha.

“Ahsante kwa kunijali mpenzi, lakini kabla ya yote ningependa kufahamu kama hapo ulipo una angalau shilingi laki tatu?” Glory alimtupia swali Bon Mtambo!

“Hata ukitaka milioni kumi!” Bon Mtambo alijibu kwa majigambo lakini huku akiwa makini zaidi kwavile hakufahamu nini msingi wa swali la Glory!

“Ahsante mpenzi; je kutokana na hali ilivyo unazani unaweza kunisindikiza mahali. Sio mbali sana na hapa!”

“Kama hakuna wambeya nitakusindikiza! Sikiliza mpenzi, unajua mimi nimetoroka na si ajabu huko waliko wameshaanza kunisaka!” Bon Mtambo alidanganya huku

akiamini kwamba hata Glory nae anajua kwamba anadanganywa! Kufuatia kauli hiyo, Glory aliingia chumbani na kutoka na kofia kubwa aina ya pama na kumpatia Bon Mtambo!

“Swadakta mrembo wangu! Sasa naweza kukusindikiza hata Kituo Kikuu cha Polisi bila wasiwasi!” Bon Mtambo aliongea kwa hamasa!

Safari ya Glory na Bon Mtambo iliishia kwenye duka moja kubwa la vito vya thamani lililokuwa na bidhaa mbalimbali kama vile mikufu, pete, bangili na vito vingine! Jambo ambalo halikufahamika kwa Glory ni safari yao kufuatiliwa nyuma nyuma na SSP Faraji Zegge pamoja na Jonathan Njoroge waliokuwa wanahakikisha usalama wa Bon Mtambo!

“Sikiliza mpenzi, hii sehemu nilipita jana na kukuta mkufu ambao niliupenda sana. Ingawaje nilikuwa na pesa, lakini nilihisi mkufu ule nitaufurahia zaidi endapo nitanunuliwa na wewe ili uwe ukumbusho wangu kutoka kwako! Hiyo ndio sababu iliyonifanya nikulete hapa mpenzi!” Glory aliongea kwa deko huku akiwa amemwegemea Bon Mtambo. Hapo hapo Bon Mtambo alihisi kama damu zikimtembea mwilini! Hakufahamu ni kwanini, lakini alilifananisha suala hili ni sawa na lile la yeye kununuliwa simu walipokuwa Marekani! Kwamba Glory alikuwa anatafuta mbinu za kulipizia pesa zake alizotumia Marekani kununulia simu ilikuwa ni hoja nyingine iliyopita akilini mwake lakini ilikosa nguvu!

“Uko wapi mkufu wenyewe?”Hatimae Bon Mtambo aliuliza na mara mkufu ulitolewa na kuoneshwa! Machale yakamcheza lakini akaamua kujikausha kama hamna kitu chochote alichohisi kutoka kwenye mkufu huo! Kwa kifupi ulikuwa ni mkufu mzuri sana uliopambwa na kidani

chenye muundo wa moyo! Ni hicho kidani ndicho kilichomsisimua zaidi Bon Mtambo. Hakujua ni kwanini, lakini alihisi kama hakikuwa ni kidani cha kawaida, labda kwavile tayari alikuwa na kumbukumbu ya jinsi alivyoingia kwenye mtego wa simu ya msichana huyuhuyu! Hata hivyo, Bon Mtambo alilipa shilingi laki nane zote ingawaje Glory alikuwa amependekeza yeye mwenyewe angelipa laki tano na itakayobaki ndio ilipwe na Bon Mtambo!

“Usijali mpenzi, kwavile umetaka kuufanya uwe ni kumbukumbu kutoka kwangu basi sina budi kulipia kiasi chote mimi mwenyewe!”Bon Mtambo alijinadi.

“Lakini hiki kiwango kinaninyima raha kwavile inakuwa ni kama nimefanya njama za kulipiza ile simu!” Glory alijifanya kulalamika!

Hata hivyo, bei halisi ya mkufu ni zaidi ya hiyo laki nane, lakini ni Kamau ndie aliyependekeza kutajwa bei hiyo ili kumpumbaza Bon Mtambo azanie ni mbinu ya Glory kutaka kurudisha pesa alizotumia kumnunulia simu! Hakutaka Bon Mtambo ahisi kuwapo na kitu kuhusu huo mkufu mbali ya kwamba Glory ameamua kujilipa kijanja!

“Haya mpenzi, hebu niambie jinsi ulivyofanikiwa kuachiwa manake siamini kama kweli ulitoroka!” Hatimae Glory alianzisha maongezi mara waliporejea nyumbani. Maongezi haya yalianza baada ya Glory kuingia maliwatoni na kutulia huko kwa dakika chache kisha akarejea huku akiwa ameuvaa mkufu wake! Hali hii ilimfanya Bon Mtambo kuwa makini zaidi!

"Sikiliza Glory, nilikuwa na hamu sana na wewe na ndio maana nimekuja kukuona. Hata hivyo nasikitika kwamba sitakaa sana kwavile nina kazi maalumu ninayotakiwa kuikamilisha. Kama ujuavyo, natuhumiwa kujihusisha na ugaidi lakini nafurahi kwamba kwa namna moja au nyingine mungu yupo upande wangu. Kwa uweza wake, nimefanikiwa kupata kanda kadhaa za video kutoka kwenye ofisi ya mtu mmoja aitwae George ambae anamiliki kampuni ya ushauri juu ya masuala ya uwekezaji hapa jijini. Huyu George ana ushirikiano wa karibu na kampuni moja ya ulinzi inayoitwa ISLIB. Na ni hawa ISLIB ndio wanaonipiga vita kila uchao! Hata hivyo ISLIB wenyewe ni wachafu kuliko maelezo ingawaje wanataka jamii iwaone ni kampuni safi! Kutokana na hilo nafahamu fika kwamba endapo nitashindwa kutoroka basi nitaishia jela, lakini kabla sijafungwa nitahakikisha na wao nimeshaumbua! Nitaenda jela na vibaraka wao ambao ni watu wanaoheshimika huku wakijifanya ni watetezi wa wanyonge wakati ni wahujumu wakubwa!" Alitulia kidogo kiasi cha kulegeza koo kisha akamalizia, "Glory mpenzi, napenda kutumia fursa hii kukueleza kwamba kuna wakati nitaomba ushirikiano wako! Kwa sasa mathalani, nakuomba utumie kila hila kumzoea huyu George, lakini hakikisha hufanyi nae mapenzi! Mimi nitakuwa na jukumu la kukuelekeza ni namna gani unaweza kukutana nae!"

Baada ya maelezo hayo, Bon Mtambo alitumia takribani robo saa akijifanya kumwelekeza Glory namna anavyoweza kuzoeana na George Kamau! Glory nae, huku akiamini anamteka Bon Mtambo, alisikiliza kwa makini huku wakati mwingine na yeye akijifanya kutoa mapendekezo yake!

Ilikuwa ni kama mchezo wa paka na panya!

Gibson Mayanja alitembea kwa hatua za tahadhali hadi alipoifikia gari aliyoelekezwa. Ndani ya gari walikuwamo pia Michael Mchupi pamoja na Nkuba. Si kwamba alikuja kukutana na akina Michael Mchupi kwa kupenda yeye mwenyewe, bali alishinikizwa sawa na vile walivyokuwa wakishinikizwa watu wengine sawa na yeye!

Gibson Mayanja ni Mkurugenzi Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali linalopigania haki ya elimu na afya kwa wote, yaani Health and Education For All, kwa kifupi linaitwa HEFA. Akiwa na umri usiozidi hata miaka arobaini, Gibson Mayanja alikuwa ni miongoni mwa vijana wenye maisha ya juu kabisa huku akimiliki biashara mbalimbali nchini! Hata hivyo, ni watu wachache sana hususani wale walio ndani ya IBU ndio waliozifahamu biashara hizi pamoja na vyanzo vya mapato vya Gibson Mayanja tofauti na vile vinavyotokana na kazi yake!

Safari ya Gibson na watekaji wake iliishia Vikindu iliko kambi ya ISLIB! Na pale alipofunguliwa kitambaa usoni, alijikuta akiwa ndani ya ukumbi mkubwa wastani. Ndani ya ukumbi huo, kulikua na vyumba vidogovidogo vilivyozungushiwa vioo vya giza, yaani *tinted*! Ilionekana ni kama mgahawa wa intaneti, yaani *Internet Cafe*!

Baada ya kuamriwa kuingia kwenye moja ya vyumba hivyo, mtu ambae hakufahamika kwake alipuliza kitu mithili ya dawa ya wadudu lakini iliyo kali zaidi puani!

Chafya zikasikika toka kila kona!

"Awali ya yote poleni sana kwa chafya! Hiyo ilikuwa ni njia tu ya kumjuza kila mmoja wenu kuwa

hayupo peke yake! Pamoja na hayo, ningependa kutumia fursa hii kumwambia kila mmoja wenu kufungua faili lenye jina RAFIKI kwenye kompyuta yake! Nawapatia dakika tano kufuatilia kwa umakini filamu hiyo!"

Hiyo ilikuwa ni sauti ya George Kamau!

Pamoja na Gibson Mayanja, kulikuwa na watu wengine kadhaa walioletwa kwa mtindo uleule alioletwa nao yeye! Kamau alikuwa anaendesha kikao ambacho Bon Mtambo alifanikiwa kuiona *faksi* yake kabla huku wajumbe wake wakiwa ni wale waliotajwa kama *non gvt allies*! Hata hivyo, kikao hiki kiliitishwa mapema zaidi kuliko ilivyokuwa imepangwa na hivyo kusababisha Bon Mtambo *kuachwa kwenye mataa*! Kubwa kuliko yote, kabla ya tukio la kuwakusanya wanaharakati hawa, George Kamau alikuwa ametega bomu kwenye ofisi za utawala za ISLIB ambalo baadae alilipua akiwa mbali na hapo na kusababisha uharibifu mkubwa kwenye jengo hilo!

Baada ya dakika tano walizopewa na Kamau kupita, kila mmoja alihisi kijasho chembamba kikimtoka! Hali hii ilikuja baada ya kushuhudia picha za video zilizoonesha baadhi ya matukio ambayo kila mmoja kwa wakati wake akipata ufadhili haramu kutoka CDTPE na watu wengine wenye uhusiano nao!

"Ni matumaini yangu kwamba wote mmeshitushwa na *clips* (vipande vya filamu) mlizoziona hivi punde!" Hatimae George Kamau alianza kueleza, kisha akaendelea, "Aidha, ni matumaini yangu kwamba wote tuliopo hapa ni watu wazima! Kama hivyo ndivyo, nazani haina haja ya kuzungukazunguka na badala yake hatuna budi kuambiana ukweli kwanini tumejumuika hapa! Kama mjuavyo, wote nyinyi mmefaidika kwa kiasi kikubwa na misaada mbalimbali kama inavyoonekana kwenye hizo

filamu. Na ni bahati mbaya sana, kutokana na sheria za nchi hii misaada hiyo ilitolewa kwenu kinyume cha sheria za nch! Na mbaya zaidi, mtindo uliotumika kwa nyinyi kufaidika na misaada hiyo, unaleta taswira ya rushwa ingawaje hiyo haikuwa dhamira ya wafadhili wetu! Jambo ambalo halikufahamika na wafadhili hawa ni kwamba miongoni mwa watendaji wao kulikuwa na vibaraka ama wa serikali au wa TAKUKURU! Aidha, kuna shaka kwamba huenda pia kuna na vibaraka wa chama tawala! Vibaraka au wasaliti hawa wa ukombozi walifanikiwa kupiga picha za siri kila pale wafadhili wenu walipojaribu kuwawezesha kiuchumi. Na hapa ninapozungumza tayari picha hizo zimeangukia mikononi mwa Gaidi Bon Mtambo anayekusudia kuzitumia picha hizo ili kujisafisha!"

"Ndugu zangu, nazani mtajiuliza ilikuwaje hadi gaidi hili likajipenyeza kwenye hili suala! Kwa kifupi tu ni kwamba, Bon Mtambo ni mtu hatari sana duniani kuliko vile inavyofahamika. Ni watu wachache sana wanaofahamu kwamba ni kijana huyu huyu ndie ambae alikuwa mpangaji mkuu wa milipuko ya mabomu kwenye balozi za Marekani za Dar es salaam na Nairobi miaka kadhaa iliyopita! Wakati anapanga hujuma hizo dhidi ya nchi yake alikuwa ni kijana mdogo tu wa miaka kumi na nane! Na tangu wakati huo amehusika na matukio mbalimbali ya kigaidi likiwamo lile la Bali nchini Indonesia! Hata hivyo, imekuwa ni vigumu sana kumtia mbaroni kwavile ni mjanja sana huku akiwa amejaaliwa akili ambazo hata hivyo anazitumia vibaya! Pamoja na ujanja wake huo, Ubalozi wa Australia jijini Nairobi ulipata fununu za kuhusika kwa Bon Mtambo katika milipuko ya mabomu kule Bali. Kama mtakumbuka vizuri, raia kadhaa wa Australia walipoteza maisha yao kwenye shambulio lile

kiasi cha kuifanya Australia kuapa kuwatafuta popote duniani wahusika wote wa shambulizi la Bali!"

"Ndugu zangu, Ubalozi wa Australia ulipopata fununu za kuhusika kwa Bon Mtambo, iliipa kazi kampuni ya upelelezi ya ISLIB ili kufuatilia nyendo zake. Na ni kampuni hii ya ISLIB ndio ilifanikisha kukamatwa kwa Bon Mtambo pale uwanja wa ndege wiki chache zilizopita. Baada ya kukamatwa, magaidi wenzake walifanya jaribio la kumtorosha pale Mahakama ya Kisutu lakini hata hivyo jaribio lao lilishindwa. Kufuatia kushindwa kwa jaribio hilo, ndipo wakaamua kumteka Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, IGP Jaffery Minga ili kushinikiza kuachiwa kwa gaidi mwenzao! Licha ya kwamba wizara husika ilifanya jitihada za kukanusha juu ya jambo hilo, lakini lililo dhahiri hivi sasa ni kwamba ni kweli Bon Mtambo ameachiwa huru kutokana na shinikizo za magaidi! Kwakweli inasikitisha kuona nchi yetu bado ina viongozi ambao wapo tayari kuziweka rehani mabilioni ya roho za watu duniani kwa ajili ya kuinusuru roho ya mtu mmoja! Inasikitisha kuona bado tuna viongozi ambao wapo tayari kuwasujudia magaidi wakubwa duniani ili kujinusuru wao! Pamoja na kwamba kulikuwa na uwezekano wa kumuokoa mkuu wa polisi, lakini viongozi wetu waandamizi wakachagua njia ya mkato. Walichagua njia ya mkato kwavile walitaka kufanya siri suala la IGP kutekwa na magaidi!"

"Baada ya Bon Mtambo kuachiwa, alivamia ofisi za ISLIB na kuiba kanda za video zenye picha ambazo mmeziona hivi punde! Kama mlivyoona, nyingi ya kanda hizo zinawaonesha mkipokea ufadhili ulio kinyume cha sheria za nchi hii. Kutokana na hilo ISLIB ilikusudia kuwafikisha mahakamani kwa mashtaka ya hujuma. Hatua hiyo ya ISLIB ilikuja baada ya kugundulika kwamba taasisi

ya CDTPE iliyokuwa imewafadhili ina lengo la kuanzisha vuguvugu la uasi dhidi ya serikali! Na kwavile misaada ya CDTPE kwenu ilikuwa inatolewa kwa siri basi ilionekana kwamba nyinyi mlikuwa mnashirikiana nao ili kutekeleza uasi huo muda utakapofika! Hata hivyo, kwa bahati, kuna wakati hawa watu wa ISLIB nao kumbe walishawahi kufadhiliwa na CDTPE, na mkanda wa ushahidi dhidi yao upo! Hiyo ndio sababu iliyowafanya ISLIB washikwe na kigugumizi cha kulifikisha shauri hilo mahakamani!"

"Ndugu zangu, wakati ISLIB ikishikwa na kigugumizi hicho ndipo walipogundua kwamba kanda za video walizokuwa nazo zimeibiwa na Bon Mtambo! Ni bahati tu kwamba baadhi ya picha hizo za video zilikuwa zimehifadhiwa kwenye kompyuta na ndio hizo ambazo nyinyi mmefanikiwa kuziona. Pamoja na wizi alioufanya, kabla hajaondoka ofisini hapo alitega bomu ambalo limeharibu vibaya jengo la ofisi za ISLIB! Aidha, taarifa tulizonazo ni kwamba Bon Mtambo ana mpango wa kumtumia IGP ambae bado yupo mikononi mwao ili wauhadae umma kwamba yeye si gaidi! Njama zao ni kutaka kutangaza kwamba Bon Mtambo alikuwa anafuatilia vitendo vya hujuma vilivyokuwa vinaendelea nchini. Hapa wanataka kuonesha kwamba baada ya wahujumu na mafisadi kugundua harakati hizo za Bon Mtambo ndipo wakaamua kumwandama na kumpakazia shutuma za kigaidi ili malengo yake yasifanikiwe. Na katika kuthibitisha madai hayo, bila shaka Bon Mtambo atazitumia kanda alizoziiba ISLIB ili kuonesha hujuma alizozigundua! Na kwa taarifa yenu, vilevile Bon Mtambo amefanikiwa kuiba vithibitisho vinavyowahusisha vigogo watatu serikalini waliokuwa wanachunguzwa na ISLIB! Hivyo basi, pindi atakapowasilisha kanda na vithibitisho

hivyo, kila mmoja atamwamini na itaonekana ni kweli alikuwa anapakwa matope na wahujumu wa nchi hii. Hapo maana yake ni kwamba habari zenu za kupokea ufadhili wa siri kutoka CDTPE zitakuwa wazi. Aidha, msisahau kwamba Bon Mtambo anamiliki leseni ya bandia inayomuonesha yeye ni mpelelezi wa kujitegemea!"

"Ndugu zangu, baada ya kuhisi Bon Mtambo atakuwa ameiba kanda hizo, ISLIB ilimtumia dada mmoja ambae yupo karibu sana na huyu kijana. Huyu dada alielekezwa namna anavyoweza kuzipata habari nyeti kuhusu Bon Mtambo na kwakweli amefanikiwa sana katika hilo. Ningependa kuchukuwa nafasi hii niwawekee maongezi ya Bon Mtambo ambayo huyu dada alifanikiwa kuyanasa!" Baada ya kufika hapa, Kamau alifungua faili la kompyuta alilohifadhi maongezi yaliyorekodiwa na Glory. Maongezi haya ni yale waliyofanya baada ya Bon Mtambo na Glory kurudi kununua mkufu wenye kidani cha kunasia sauti! Bada ya kufungua faili lenye maongezi hayo, aliweka sauti ya juu ili kila mmoja asikie, na baada ya kwisha maongezi hayo aliendelea:

"Kufuatia hali hiyo, ISLIB ilikuja kwangu na kunipatia hadithi yote. Walikuja kwangu kwavile mimi ninamiliki hisa kwenye hiyo kampuni. Waliponieleza, sikutaka kuzunguka na badala yake niliwaambia wazi kwamba hawana budi kukaa nanyi ili kumdhibiti huyu kijana. Hii ni kwavile, endapo hamtafanya jambo la maana basi muda si mrefu mtaumbuliwa na kumwacha yeye akiendelea kufanya uhalifu wake huku akionekana ni shujaa na nyinyi mashujaa mkionekana waovu!"

"Ndugu zangu, kutokana na hilo wanahisa na watendaji wakuu wa ISLIB waliketi na kuangalia nini kifanyike ili kukabiliana na mtu huyu mwovu. Baada ya

majadiliano, ikafikiwa mwafaka kwamba viongozi wa asasi za kiraia, vyama vya wafanyakazi, vyama vya kisiasa na vyama visivyo vya kiserikali tuliopo hapa, tuitishe maandamano kulaani kuachiwa kwa Bon Mtambo kinyume cha sheria. Aidha, waandishi wa habari, watumie kalamu zao kuandika na kutangaza mambo kadhaa yatakayoashiria kulaani kuachiwa kwa muovu huyu. Vilevile, itabidi tulaani kwa nguvu zote mashambulizi ya mabomu yaliyotokea kwenye ofisi za ISLIB. Na endapo tutajipanga vizuri basi nina uhakika kwamba huyu muovu atarudi nyuma tu kwavile atajua njama zake zimegundulika! Na kwavile kila pande ya nchi hii itakuwa linatajwa jina lake basi sina shaka kwamba njia atakayoiona ni salama kwake ni kutoroka. Kutoroka kwake ndio salama yenu! Nafahamu kwamba jambo hili ni gumu, lakini hii ndio njia pekee ya kujinasua kwenye kashfa hii! Na kwavile mkubwa mmoja wa jeshi la polisi ana uhusiano wa karibu na kampuni ya ISLIB, yeye ameahidi kutoa kibali cha kufanyika kwa maandamano hayo." Baada ya kufika hapo, alitulia kidogo kisha akamalizia. "Hivyo basi, kwavile tunashindana na muda, ningependa kuishia hapa ili kama kuna mtu miongoni mwenu mwenye maoni aweze kuyatoa! Tusisahau kwamba, maandalizi ya jambo hili yanabidi yafanyike mara moja na maandamano yafanyike ndani ya saa ishirini na nne toka sasa! Aidha, nyinyi mliopo hapa mtaanza kujenga hoja kwa viongozi wenzenu ambao hapa hawapo. Tumieni kila mbinu ili muwe kitu kimoja kisha wote tuweze kukutana kesho majira ya saa nne asubuhi pale ukumbi wa Idara ya Habari, Maelezo! Pale ISLIB itakuwa tayari imeshawasiliana na waandishi wa habari ili kuelezea suala la wao kuhujumiwa na mtu wanayemshuku ni Bon Mtambo. Wao watasema wazi

kwamba wana wasiwasi kwamba kijana huyu anashirikiana na baadhi ya wakubwa ili kuihujumu ISLIB. Kuanzia hapo itaomba uungwaji mkono katika vita yake dhidi ya hujuma na ulaji rushwa hapa nchini. Nanyi mtatumia nafasi hiyo kutangaza azma yenu ya kuitishwa maandamano endapo hapatatolewa taarifa za kueleweka kuhusiana na wapi alipo Bon Mtambo!" Alimalizia na kuacha minong'ono ikitokea kila mahali.

Kwa hakika, Gibson Mayanja na wenzake walijikuta katika wakati mgumu na kuona ni namna gani walivyowekwa pabaya! Maelezo ya Kamau yaliwaingia barabara akilini mwao na hivyo kubaini wazi hatari iliyopo mbele yao! Watu pekee ambao hawakushangazwa sana na jambo hili ni viongozi wa DRFA! Kwao, waliona huu ni mwendelezo wa mchezo uleule ambao siku za nyuma uliwalazimisha kukaa kimya dhidi ya kampuni ya TanEuro! Hata hivyo, hawakuwa na la kufanya!

"Kwanza wewe ni nani na kwanini umetufungia kwenye hivi vichumba katika hali inayoonesha hutaki tufahamiane?!" Hatimae, Dunstan Mkundi, Katibu wa Vijana wa DRFA aliuliza kwa ukali, na hivyo kuibua minong'ono iliyoashiria wenzake kumkubalia hoja yake. Kwa yakini, Mkundi alishachoshwa na hali hii ya utumwa lakini mara kwa mara aliaswa na mwenyekiti wake kuwa mstahimilivu kwavile wanashughulikia suala hilo!

"Nimefanya hivyo kwa makusudi." Hatimae Kamau alianza kueleza kisha akaendelea: "Kwanza lazima tukubali kwamba ni kweli tuna hatia katika suala zima la upokeaji wa misaada ile ambayo imeshabainika kwamba CDTPE haina nia nzuri kwa nchi yetu. Ingawaje wote hapa ni wachawi, lakini nilihisi itakua si busara kila mmoja kufahamu kwamba kumbe fulani nae ni mchawi! Nilizani

inatosha kujua tu kwamba, si wewe peke yako bali upo na wenzako, lakini si busara kujua hao wenzako ni nani na nani! Unapokuwa nyumbani ukaiba mnofu jikoni kisha ukakimbilia chooni, utajikuta na fadhaa sana endapo huko chooni nako utakutana na mwanao ambae nae kaiba mnofu na kakimbilia huko! Si kwamba hutajisikia fadhaa eti tu kwavile wote mmeiba mnofu! Hata hivyo, endapo mtataka kufahamiana, basi naweza kuwafa....!"

"Hapana!Hapana!" Hatimae kila mmoja alipinga pendekezo la kwamba wafahamiane! Kila mmoja alipenda bado iwe siri yake moyoni kwamba ni miongoni mwa watu wanaotuhumiwa kuhujumu nchi yao!

"Sasa tuna hakika gani kwamba baada ya kummaliza Bon Mtambo ISLIB haitatugeuka na kutupeleka tena mahakamani?" Gibson Mayanja nae aliuliza.

"Swali lako ni zuri! Kwa kifupi tu ni kwamba, tayari tumeaandaa picha za video za matukio yote mliyoyaona kabla na kuyahifadhi kwenye vitunza kumbukumbu (*flash disk*s). Humo yapo na matukio yaliyofanywa na ISLIB wenyewe. Kila mmoja wetu, ataondoka hapa na kitunza kumbukumbu chake. Hata hivyo, vitunza kumbukumbu hivyo vitakuwa vinafunguliwa na namba za siri, yaani *password* ili kujilinda sisi wenyewe endapo itatokea mmoja wetu amepoteza kitunza kumbukumbu chake. Aidha, namba hiyo ya siri itafahamika na Mkurugenzi wa ISLIB peke yake lakini hatujakurupuka kumwachia jukumu hilo mtu wa ISLIB. Tumefanya hivyo kwavile mtu pekee ambae anaweza kutiliwa shaka ya kuwageuka wenzake ni ISLIB. Waswahili wanasema, mwenzako akimwaga mboga, wewe mwaga ugali! Si hivyo tu, dawa ya mchawi ni kumpa mtoto alee! Hivyo basi, endapo ISLIB itaamua kuwasaliti na kuzipeleka kanda za video kwenye vyombo vya usalama

maana yake ni kwamba picha zake haitazipeleka! Na kama watafanya hivyo, nyinyi mtakuwa na uwezo wa kuviwasilisha vitunza kumbukumbu hivyo kwenye vyombo vya usalama ambavyo ndivyo vitakavyokuwa na picha za matukio yote. Kwavile nyinyi mtakuwa tayari mmeshaumbuliwa na ISLIB, bila shaka hamtaona shida kwenda kwenye vyombo hivyo vya usalama na vitunzia kumbukumbu vyenu ili pia kuwaumbua wao! Huko mtakuwa na uwezo wa kuwaambia watu wa usalama kwamba ofisa wa ISLIB ndie mwenye namba za siri za kufungulia picha hizo. Hata kama atajaribu kubisha, sina shaka yoyote kwamba baada ya mateso ya polisi lazima ataitaja. Na kwavile ISLIB inafahamu kwamba nanyi mna picha za kashfa yake basi nina hakika kwamba hawatathubutu kutoa siri ya picha hizi kwavile itakuwa inajiandaa kujiumbua na yenyewe! Na ili kuwaondoa wasiwasi, kila mmoja wenu atapata fursa ya kuoneshwa picha hizo harakaharaka hususani kipande kinachowahusu watu wa ISLIB!" George Kamau alimalizia utetezi wake wa kuwaondoa hofu mateka wake!

Baada ya majadiliano ya hapa na pale, muafaka ulifikiwa na hivyo kiasi cha robo saa baadae, Bon Mayanja na wenzake walitolewa kwa namna ileile waliyokuja nayo.

"Ni matumaini yangu kwamba umeandika taarifa yako kama nilivyokueleza, au unasemaje mpenzi?" Hatimae George Kamau alimuuliza Layla baada ya kuwa wamebaki wawili tu humo ndani!

“Bila shaka mpenzi, nina hakika habari hii itakapotoka Bon Mtambo atanuka kila atakapopita!” Layla nae alijibu kwa hamasa!

“Nimefurahi kusikia hivyo, lakini usisahau kwamba nimeamua kukushirikisha kikamilifu kwavile hivi sasa nakuamini kwa asilimia zote! Nakuhakikishia Layla, baada ya kadhia hii nauza kampuni yangu na hisa nilizonazo ISLIB kisha tunatoweka hapa Afrika. Hii ni kadhia ndogo sana kwetu, na tumejizatiti vya kutosha katika kujilinda hivyo si Bon Mtambo wala jeshi la wananchi wenye uwezo wa kuivunja ngome yetu!” George Kamau alijigamba mbele ya Layla kisha akaanza kumpitisha sehemu mbalimbali ili kudhihirisha nguvu walizonazo! Pamoja na yote, sehemu ambayo ilimshitua zaidi Layla ni kambi ya mafunzo ya kijeshi iliyopo chini ya ardhi!

Dokta Joselyn Kimario, mmoja wa vigogo serikalini alikuwa anajiandaa kuondoka pale simu yake ilipoita.

“Dokta Joselyn Kimario hapa, nani mwenzangu!?”

“Ni rafiki yako hapa, naomba kuonana na wewe leo hii mahala pa faragha!” Sauti toka upande wa pili wa simu ilijipenyeza masikioni mwa Dokta Kimario.

“Wewe ni nani?” Dokta Joselyn Kimario aliuliza kwa ghadhabu kidogo.

“Nimeshakuambia kwamba ni rafiki yako!”

“Rafiki yangu yupi?”

“Utanifahamu tukishakutana!”

“Hivi unajuwa unaongea na nani wewe?”

“Najua kwamba naongea na Dokta Joselyn Kimario, kigogo wa serikali!”

“Sasa kwanini unataka kuleta upumbavu wako hapa?” Dokta Kimario alifoka.

“Kiburi hakitakusaidia Dok.......!” Kabla hajamaliza tayari Dokta Joselyn Kimario alishakata simu!

Wazo la kuondoka likayeyuka na badala yake akaketi na kutafakari ni nani aliyepiga simu ile. Alijiuliza ni nani huyo mwenye ujasiri wa kupiga simu kama ile kwa mtu mzito kama yeye! Akiwa anaendelea kutafakari mara simu yake ilitoa mlio ulioashiria kuingia kwa ujumbe mfupi. Alisita kwa muda kisha akaamua kufungua kisanduku cha ujumbe kwenye simu yake:

*“Dokta, baada ya ujumbe huu nakutumia zawadi mzuri kwenye simu yako sasa hivi. Baada ya kuipata zawadi hiyo basi sina shaka yoyote kwamba utafanya jitihada za kunitafuta!”*

Baada ya kuusoma huo ujumbe alisonya kwa hasira na kuanza kuondoka ofisini huku akiapa kumsaka huyo mtu kwa udi na uvumba! Wakati anakaribia mlangoni mara mlio ulioashiria kuingia kwa ujumbe kwenye simu yake ulisikika tena. Alijishauri endapo auangalie au aufute kabla ya kuusoma! Baada ya kufikiri kidogo, akakata shauri la kuusoma.

Ulikuwa ni ujumbe wa picha! Ile kuufungua tu na kuanza kuuangalia, hamadi! Dokta Joselyn Kimario alibaki ameganda mithili ya sanamu! Alitamani kukaa, akashindwa! Hata alipotaka kuendelea kusimama, alihisi miguu yake kuelemewa na uzito wa kiwiliwili chake mwenyewe! Alijaribu kuvuta hatua lakini hakuna mguu wowote ulioelekea kutii amri! Hatimae, akili yake ikamshawishi kwamba alichoangalia sicho; kwamba aliangalia vibaya! Hisia hizo zikamrejeshea kiasi cha nguvu zake na kuamua kuungalia tena picha hizo! Hata hivyo, badala ya kupata nafuu, alijikuta akipiga mweleka hadi

chini na kupoteza fahamu kwa karibu dakika tatu hivi na ushee hadi alipogutushwa tena na mlio wa simu yake!Alipoangalia namba, alikuta ni ileile!

Hapohapo akakumbuka kikao kati ya vigogo wa serikali na mkuu wa nchi; kikao ambacho mkuu huyo wa nchi hakuongea chochote zaidi ya kuonesha jinsi gani alighadhibika! Hapo ndipo alipogundua dhamira ya kikao kile kwamba kilimuhusu yeye!

*"Wote turudi sehemu zetu za kazi hadi hapo uchunguzi utakapokamilika!"* Dokta Joselyn Kimario akakumbuka kauli ya mwisho ya Mheshimiwa Rais! Kwamba mheshimiwa rais anasubiria uchunguzi kukamilika ili ndipo labda atoe tamko rasmi kuhusu yeye! Taswira ya wananchi wa Dar es salaam wakimzomea wakati akiwa kwenye viunga vya Mahakama ya Kisutu ilianza kupita akilini mwake! Hapo hapo akahisi kijasho chembamba kikimtoka kiasi cha kutamani kutimua mbio! Akapuuza wazo hilo baada ya kugundua kwamba anataka kukikimbia kivuli chake mwenyewe!

*"Ni bora kufa kuliko kashfa hii kufichuka kwa wananchi nikiwa bado hai!"* Dokta Kimario aliwaza na hapohapo akajilaani ni kwanini hakutembea na bastola yake!

"Kriiiiiii!! Kriiiiiii! Kriiiiii......!" Simu iliendelea kuita huku ikionekana kama inayomwambia, *umelikoroga mwenyewe hilo; lazima ulinywe!*

Alijiuliza endapo aipokee au aachane nayo!

"Ha..ha..haloo!"Hatimae Dokta Kimario alipokea simu huku sauti yake ikiwa imetawaliwa na mchecheto!

"Nazani hivi sasa unaweza kunisikiliza kwa makini!" Sauti toka upande wa pili wa simu ilijipenyeza masikioni mwa Dokta Joselyn Kimario: "Kama nilivyokuambia, mimi ni rafiki yako hivyo basi endapo

ungependa picha nilizokuonesha zisiwafikie wana usalama pamoja na wana habari, basi huna budi kufuata maelekezo yangu."

"Maelekezo gani?" Dokta Joselyn Kimario aliuliza huku ujasiri wake wote ukiwa umeyeyuka! Suala la picha alizooneshwa kwamba eti ziwafikie wana habari halikuwa jambo jema hata kidogo!

"Ni hivi Dokta, ukitoka hapo nje utakuta gari moja aina ya Nissan Safari rangi ya udongo. Hiyo ndio gari itakayokuleta kwa rafiki yako. Huna haja ya kuwa na hofu. Hata hivyo, jaribio lolote la kumtaarifu yeyote litakugharimu, hivyo chunga sana!"

Ingawaje Dokta Joselyn Kimario aliichukia tabia ya kupewa amri, lakini kwa sasa hakuwa na mbadala!

Uamuzi wa Kamau kumshirikisha Layla ulikuja baada ya kuona yeye anawindwa zaidi na Bon Mtambo. Kutokana na hilo, akakata shauri la kuteua mtu atakayeaminika kwake ili awe anafanya shughuli zingine ambazo angezifanya yeye. Hata suala la kuitisha kikao kilichokuwa kimemalizika punde, ilikuwa ni baada ya mashauriano ya kina na Layla. Na ni Layla ndie alipewa jukumu la kuwaongoza vijana waliopewa jukumu la kuwaleta wakina Gibson Mayanja hapo ISLIB. Ni Layla ndie alikuwa anafahamu kila mmoja alipokuwa anaishi au kufanyia kazi!

Gari iliyomchukua Dokta Joselyn Kimario ilikatiza mitaa mbalimbali ya jiji la Dar es salaam huku wakionekana kuwa na lengo la kumpoteza yeyote aliyetaka kuwafuatilia! Hata hivyo, Dokta Joselyn Kimario hakuweza kufahamu sehemu walizokuwa wanapita kwavile alikua amefungwa kitambaa cheusi usoni!

Baada ya kuzunguka hapa na pale, walikanyaga mafuta hadi Kurasini!

"Karibu sana Dokta !" Alikuwa ni Michael Mchupi akimkaribisha Dokta Joselyn Kimario.

Dokta Joselyn Kimario hakujibu!

"Najua umeghadhibika kutokana na mtindo uliotumika kukufikisha hapa lakini hapakua na namna! Hata hivyo, tunakuomba uwe msikivu kwavile, kama tulivyokwisha kukueleza hapo awali, sisi ni rafiki zako."

"Mnataka nini kutoka kwangu?"Dokta Joselyn Kimario aliuliza kwa hasira.

"Punguza jazba dokta, vinginevyo tutashindwa kuangalia ni namna gani ya kusaidiana."

"Sina nafasi ya kusaidiana na wahalifu mimi!"

"Sikiliza dokta, jeuri ya madaraka haitakusaidia hata chembe. Kama hujisikii kushirikiana na sisi tunaweza kukuruhusu uende zako na hatutakufuata tena. Lazima ujue kwamba kazi tunayotaka utufanyie wewe inaweza kufanywa na mtu mwingine yeyote miongoni mwa wahujumu wenzako." Michael Mchupi aliongea lakini hivi sasa akionesha kukerwa na jeuri ya Dokta Joselyn Kimario. Hali hii ilimfanya Dokta Joselyn Kimario anywee! Alitulia mithili ya kinda la ndege lililolomwagiwa maji ya baridi. Afadhali angeitwa *fisadi*, kwani ni neno ambalo limeshazoeleka! Lakini kuitwa mhujumu, halikuwa jambo jema! Hilo ni jambo la kuogofya! Jambo la kutisha, na la

kutia hofu pia! Leo hii hawa watu wanamwita yeye ni mhujumu, bila shaka mhujumu uchumi. Kwa maana nyingine, ni mhujumu wa jasho la wananchi maskini wa nchi hii!

Dokta Joselyn Kimario alizirejesha kumbukumbu zake nyuma akiikumbuka siku iliyozaa picha zile za video alizotumiwa kwenye simu yake. Picha ambazo leo hii zimeyeyusha kabisa ujasiri wa asili alionao!

Ilikuwa ni jumamosi moja akiwa amepumzika nyumbani kwake na mara akatokea bwana mmoja anayeitwa Lyimo ambae ni shemeji yake; Lyimo akiwa ndie mwenye dada! Huyu Lyimo ni mfanyabiashara, lakini pamoja na biashara ni mjanja wa mjini huku akiwa anafahamiana na watu mbalimbali; wageni na wenyeji. Siku hiyo Lyimo alikuja huku uso wake ukiwa umechanua kwa furaha ambayo ingeweza kuonekana hata na mtoto mdogo! Baada ya kusalimiana, Lyimo alimuomba shemeji yake watoke nje kwa faragha!

Aliendelea kuvuta kumbukumbu tangu mwanzo wa tukio hadi mwisho. Akiwa katika hali hiyo, mara akapata wazo!

“Mnataka niwafanyie nini?” Dokta Joselyn Kimario alifanikiwa kuuliza, tena kwa kujiamini kabisa!

“Nazani itakua vizuri tukianza kufahamiana, angalau kwa majina. Mimi naitwa Michael Mchupi, na hao wenzangu watajitambulisha wenyewe hapo baadae.” Michael Mchupi alijitambulisha kisha akachukua jalada moja na kumkabidhi Dokta Joselyn Kimario!

TANPURITY LTD!

Pamoja na maneno mengine yaliyosomeka juu ya hilo jalada, neno TanPurity Ltd ndilo lililoonekana kwa uwazi zaidi!

“Dokta Joselyn Kimario, hebu nieleze chochote unachofahamu kuhusu TanPurity Limited!” Hatimae Michael Mchupi aliuliza mara baada ya kukabidhi hilo jalada! Alijiuliza kwa haraka nini maana ya swali hili lakini hakuona mantiki yake, hivyo Dokta Joselyn Kimario akaamua kukaa kimya!

“Dokta Joselyn Kimario, ina maana hujasikia nilichokuhoji?” Michael Mchupi alifoka!

“Sina chochote ninachofahamu zaidi ya kujua kwamba hii ni kampuni ya serikali ambayo malengo yake ni kusafisha madini yachimbwayo hapa nchini!”

“Safi Dokta, sasa ningependa kutumia fursa hii kukuomba kwamba fanya lolote uwezalo hadi kampuni hiyo inaingia kabur...!”

“*What?*” Ghafla Dokta Joselyn Kimario alimkatiza Michael Mchupi kabla hajamalizia sentensi yake! Taharuki ya wazi ilionekana machoni na usoni pake pia!

“Usijifanye hujasikia Dokta, nimesema kwamba hakikisha hiyo kampuni inaingia kaburini mapema iwezekanavyo!” Michael Mchupi alirejea maelezo yake!

“Kwa maslahi ya nani?”

“Kwa maslahi ya wale wanaokutuma na wewe mwenyewe Dokta!”

“Ni nani wanaonituma?”

“Sikiliza Dokta, tusipotezeane muda hapa. Kama hutaki sema ili tuangalie ni nani kati yetu na wewe aliye mwerevu kumzidi mwenzake!”

“Unamaanisha nini?”

“Hii ni biashara kati yetu na wewe; tufanyie kazi yetu nasi tukufichie madhambi yako uliyoifanyia serikali na wananchi kwa ujumla! Acha kutufanyia kazi yetu nasi

tufichue maovu yako!" Michael Mchupi aliongea kwa utulivu lakini kwa kujiamini!

Dokta Kimario alibaki kimya kisha akavuta pumzi ndefu za kihoro! Pamoja na kwamba kiyoyozi kilikuwa kinafanya kazi humo ndani, lakini bado alihisi kiwango cha joto kilikuwa kinapanda kadri muda ulivyoenda! Kulikuwa na kila dalili kwamba amekaliwa pabaya!

" Wewe unazani jambo unalotaka nilifanye lipo ndani ya uwezo wangu?!"Hatimae Dokta Joselyn Kimario alijikuta akiuliza swali ambalo hakulitarajia kabisa!

"Sikiliza dokta, wewe peke yako huwezi lakini kwa kushirikiana na wenzako utaweza!"

"Wenzangu gani?"

"Wahujumu wenzako!"

"Kwanini unapenda kuniita mhujumu wewe?!"Dokta Joselyn Kimario alifoka.

"Sikiliza dokta, ninaekuita mhujumu sio mimi!"

"Kama si wewe ni nani wakati unayeongea hapa ni wewe?!" Dokta Joselyn Kimario aliuliza huku ghadhabu ikiwa bado inajidhihirisha machoni mwake! Kufuatia swali la Dokta Kimario, Michael Mchupi alichukua jalada lingine na kuliweka mbele yake!

PCCB: CONFIDENTIAL REPORT!

Hayo ndio maneno yaliyosomeka juu ya jalada hilo!

*"Wote turudi sehemu zetu za kazi hadi hapo uchunguzi utakapokamilika!"* Kauli ya mkuu wa nchi ikajirudia tena akilini mwa Dokta! Kauli pekee ambayo aliitoa ndani ya ukumbi waliokuwa wamekaa kwa karibu nusu saa! Ilionekana hatua ya mkuu wa nchi kukaa kimya bila kuzungumza chochote kwenye kikao hicho ilikuwa ni kama amechoma sindano ya kuua taratibu!

“Mbona sikuelewi?!” Dokta Kimario aliuliza baada ya kuirejesha akili yake kwenye jalada hilo lililomaanisha ni taarifa ya siri iliyoandaliwa na TAKUKURU, yaani Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini!

“Ni kweli huwezi kunielewa, ila kwa kifupi ni kwamba ni hao TAKUKURU ndio wanaokuita wewe na wenzako kwamba ni WAHUJUMU! Kimsingi, TAKUKURU walikua wanaendesha uchunguzi dhidi yako pamoja na vigogo wenzako watano bila ya nyinyi kujua. Ilibidi wiki ijayo ilikuwa mfikishwe mahakamani kujibu mashtaka; si ya matumizi mabaya ya ofisi kama ilivyozoeleka bali ya HUJUMA! Walishapata ushahidi wote ikiwa ni pamoja na wa picha za video! Hata hivyo, kwa kushirikiana na wenzangu, tulifanikiwa kuiba ushahidi ikiwa pamoja na majalada ambayo yalikuwa yapelekwe kwa Mkurugenzi wa Mashtaka siku chache zijazo.” Baada ya kufika hapa, Michael Mchupi alitoa majalada sita, moja dhidi ya Dokta Joselyn Kimario na mengine ya vigogo wenzake. Majalada haya ni yale yaliyodaiwa kutaka kufikishwa kwa DPP! Huku akiwa anatetemeka, Dokta Kimario alichukua jalada lililomuhusu na kuanza kulipitia kwa haraka haraka. Yote yaliyomo, yalimkumbusha tukio lile ambalo lilisukwa na shemeji yake!

*“Shemeji hebu niambie, ni nini hasa malengo yako kisiasa kwa siku zijazo hasa ukizingatia kwamba umri ndio hivyo tena unakutupa mkono.”* Dokta Joselyn Kimario alikumbuka jinsi ambavyo shemeji yake alianzisha maongezi yaliyomfanya hivi sasa awe amelowana mithili ya kinda la ndege!

*“Una maana gani shemeji?”* Anakumbuka ndivyo alivyomjibu shemeji yake huyo.

*“Je, una ndoto siku moja ya kuwa rais au waziri mkuu wa nchi hii?!”*Lyimo alizidi kumhoji shemeji yake.

*"Shemeji, mimi na wewe tumeshapata kuongea mipango mingi tu, sasa kwanini leo unaonekana kuzungukazunguka!?"*

*"Sikiliza shemeji, tufupishe maongezi. Kwa kifupi ni kwamba kuna rafiki zangu wanataka uwasaidie. Awali, waliniomba mimi lakini kwavile shida yenyewe ni ya kiutendaji niliwaambia wanipe muda ili niwatafutie mtu ambae angeweza kuwasaidia."*

*"Wanataka msaada gani?"* Dokta Joselyn Kimario anakumbuka kumuuliza shemeji yake hiyo siku.

*"Kuna mzigo unatarajiwa kupita nchini siku chache zijazo kupitia mpaka wa Tunduma. Hata hivyo, pasipo na msaada wa watu kama nyinyi, mzigo huo utapata upinzani kutoka kwa watu wa forodha. Lengo ni kwamba, mzigo huu usikaguliwe mpakani."* Lyimo alimwambia shemeji yake.

*"Ni mzigo gani?"*

*"Hawajaniambia!"*

*"Sasa wanataka mimi nifanye nini?"* Dokta Joselyn Kimario anakumbuka kuhoji.

*"Sikiliza shemeji, usifanye kama hujui nina maanisha nini. Tumia madaraka uliyonayo ili mzigo huu upite mpakani. Endapo mzigo huo hautaruhusiwa kuna hatari ya wao kupata hasara ya mamilioni ya dola. Aidha, wamesema faida inayotarajiwa kupatikana baada ya kuuzwa kwa mzigo huo ni kiasi cha shilingi bilioni tatu na kwavile utakua umewasaidia kuwaokoa kupata hasara, basi wapo tayari kuacha kiasi cha shilingi nusu bilioni kama ahsante yao kwako."*

*"Shilingi milioni mia tano?"*

*"Ndio shemeji!"*

*"Lazima utakua ni mzigo haramu huo!"*Dokta Joselyn Kimario anakumbuka kumtahadharisha shemeji yake!

*"Hilo unasema wewe shemeji, lakini hata kama ni hivyo, jambo la msingi hapa ni biashara iliyopo mbele yetu!"*

*"Kwanini nipuuze uwezekano wa kuwa ni mzigo haramu?Je kama ni silaha za maangamizi?!"*

*"Usinichekeshe sehemeji, silaha za maangamizi zije Tanzania kufanya nini? Tangu lini Kusini mwa Afrika kukatengenezwa silaha za maangamizi!? Isitoshe, huo mzigo unapita tu hapa kwahiyo hata kama ni silaha za maangamizi wataangamia kwingineko duniani na sio hapa Tanzania."* Dokta Joselyn Kimario alikumbuka msisitizo wa shemeji yake hiyo siku!

*"Lakini shemeji si unaona mambo yenyewe siku hizi yalivyo?"* Dokta Joselyn Kimario anakumbuka kuuliza kwa upole.

*"Na ndio maana nilikuuliza endapo una ndoto za kuwa rais siku moja kiasi kwamba unaogopa kufifisha matarajio yako pale mpango huu utakapovuja!"*

*"Unachoona wewe ni urais tu shemeji?! Na je suala la kuozea jela kwa makosa ya rushwa katika umri mkubwa kama huu!?Huoni kama wapwa zako bado wanahitaji malezi ya baba yao pia? "* Anakumbuka kumtahadhalisha shemeji yake.

*"Usinichekeshe Shem, hivi tangu nchi hii ipate uhuru kuna vigogo wangapi serikalini waliowahi kupelekwa jela?! Isitoshe, kutokana na mkakati uliopangwa na wale watu, nina hakika jambo kama hilo haliwezi kutokea.Na hata likitokea, tatizo liko wapi? Kesi itapelekwa mahakamani na hapo inakuwa ndio salama zaidi kwako....!"* Alikumbuka.

*What? Hivi una akili timamu shemeji?! Yaani kesi ikishapelekwa mahakamani ndo inakuwa salama kwangu?!"* Dokta Joselyn Kimario anakumbuka kumshangaa shemeji yake hiyo siku!

*"Ndio maana yake shemeji! Kesi ikishapelekwa mahakamani inakuwa tayari imeshazuia wadau kujadili tuhuma hizo kwenye majukwaa rasmi! Kitakachobaki hapo ni suala la*

*nenda rudi, nenda rudi kwa ajili kufanya uchunguzi zaidi!"* Dokta Joselyn Kimario aliendelea kukumbuka maelezo ya shemeji yake na jinsi walivyojadiliana kwa muda mrefu hadi kufikia muafaka kwamba asingekua tayari kukubali hadi afahamu ni mzigo gani. Baada ya kutoa msimamo wake, Lyimo alirudi kwa hao jamaa na kutoa msimamo aliopewa na shemeji yake. Nao baada ya kujadiliana kwa muda, walikubaliana waseme ni madini ya *uranium* ambayo walidai yanapelekwa Iran. Na ili kuleta picha halisi, hao jamaa walikua na mwenzao mmoja aliyekuwa na hati ya kusafiria ya Iran jambo lililomfanya Dokta Kimario awasadiki! Hata hivyo, kitu ambacho Lyimo na Dokta Kimario hawakukibaini ni kwamba hakukua na uraniam yoyote! Huu ulikua ni mpango uliobuniwa na IBU ili hapo baadae waweze kumtumia Dokta Joselyn Kimario!

"Una uhakika kwamba hawana ushahidi mwingine?" Hatimae Dokta Joselyn Kimario aliuliza baada ya kuibuka toka kwenye kumbukumbu zake!

"Nina uhakika dokta kwavile baada ya kuiba majalada mtaalamu wetu alituma virusi vya kompyuta ambavyo vilishambulia mfumo mzima wa mafaili ya kompyuta kwenye vitengo vyao vyote. Hivyo, usiwe na wasiwasi kwavile tunajua ni nini tunachokifanya."

"Kama ni hivyo sawa, lakini nipeni muda ili nikaongee na wenzangu ili tuangalie ni namna gani tunaweza kufanikisha jambo hili."

"Sawa dokta, lakini kumbuka kwamba usijaribu kuleta ujanja wowote, kwani kufanya hivyo ni kujihatarishia maisha yako mwenyewe. Ninachotaka kusema ni kwamba, tutakuwa tunafuatilia kila hatua unayopiga na hivyo kung'amua ujanja wowote utakaojaribu kuufanya kabla hujaufanya!"

# 14

Dunstan Mkundi, katibu wa Vijana wa DRFA aliamka mapema kama ilivyo desturi yake. Baada ya kutoka kwenye kikao kilichoitishwa na Kamau na kuwaagiza kuitisha maandamano, Mfinanga alikutana kwanza na wenzake usiku uliopita ili kujadili suala hilo. Tatizo ni kwamba, miongoni mwao waligawanyika! Wakati wapo waliokuwa tayari kukubaliana na matakwa ya Kamau, kuna wengine walishachoshwa na shinikizo zinazoletwa kwao kila mara!

Baada ya majadiliano ya usiku uliopita kuchukuwa takribani saa moja bila kufikia muafaka, waliamua kuahirisha kikao chao na kukubaliana kukutana siku ya pili asubuhi. Aidha, walikubaliana kila mmoja aje na pendekezo la namna gani wangeweza kukabiliana na hali hii ya utumwa! Yeye Mkundi alikuwa na pendekezo moja ambalo alishakata shauri kwamba endapo lingekataliwa na wenzake, basi angelitekeleza peke yake! Pendekezo lake lilikuwa ni kwamba yeye na wenzake wakajisalimishe TAKUKURU na waeleze mkasa mzima uliowaingiza kwenye ushirikiano na CDTPE bila kujua nia ya CDTPE! Pamoja na kujisalimisha, alitaka wawaombe msamaha wananchi kwavile walifanya mambo bila kujua kisha watumie nafasi hiyo kueleza maovu yote ya CDTPE! Kwa kifupi, Mkundi alikuwa tayari kufikishwa mahakamani kwa kosa hilo kuliko kuendelea kutekeleza matakwa ya akina Kamau yaliyolenga kuwahujumu Watanzania!

Huku akiwa amejawa na shauku ya kuwasilisha pendekezo lake, alijiandaa kwa haraka lakini kabla hajaondoka, alichungulia nje.

Akashangaa!

Katika hali ambayo hakuitarajia, aliweza kuwaona askari kanzu takribani sita wakiwa wanarandaranda nje ya nyumba yake! Alijaribu kufikiria kwa haraka chanzo cha kuwepo kwa askari kanzu hao lakini alikosa jibu! Baada ya kukosa jibu la maswali yake, alikata shauri la kuwapigia simu Bwana Hassan Muki na Anatory Saibaba! Kama alivyotarajia, habari hii awali ilikuwa ngeni kwao lakini walipotupa macho nje nao waliweza kuwaona askari kanzu kadhaa waliokuwa wakirandaranda nje ya nyumba zao!

Huku akiamini hana hatia yoyote, Dunstan Mkundi alichukuwa mkoba wake na kutoka nje ili aelekee ofisini!

Kabla hajafika kokote alisimamishwa!

"Naitwa OC-CID Ambrose, natokea kituo cha polisi cha Magomeni." Askari kanzu alijitambulisha kwa Dunstan Mkundi kisha akatoa kitambulisho chake na kumpatia, kisha akaendelea, "Bila shaka wewe ndie Bwana Dunstan Mkundi, Katibu wa Umoja wa Vijana wa DRFA, sio?"

"Ndie!" Dunstan Mkundi alijibu kwa mkato.

"Safi kijana, kama ndivyo basi ningependa kukueleza kwamba tangu sasa upo chini ya ulinzi na utakuwa kwenye kizuizi cha nyumbani hadi hapo utakapopatiwa taarifa nyingine. Kwahiyo unaombwa kurudi ndani na huruhusiwi kutoka nje bila ruhusa maalumu!" OC-CID Ambrose aliongea kwa utulivu na ili kuepusha shari, Dunstan Mkundi alitii amri lakini huku akiwa bado hajui ni nini hasa msingi wa sakata hili!

Mpango wa kuwekwa kizuizini Dunstan Mkundi na wenzake uliasisiwa na Bon Mtambo kwa kushirikiana na jeshi la polisi. Baada ya George Kamau kuitisha kile kikao cha siri kilicholenga kuitisha maandamano ya nchi nzima, Layla alizipenyeza taarifa za kikao hicho kwa Bon Mtambo. Kwa kuhofia madhara ambayo yangetokea baada ya maandamano hayo, Bon Mtambo alifanya haraka kuwasiliana na DCI Mwaiswelo ili kutafuta njia za kuzima harakati hizo. Baada ya kujadiliana kwa muda, walifikia muafaka wa kuwaweka chini ya kizuizi cha nyumbani wale wote waliohudhuria kikao hicho ili kuwazuia kukutana!

Kimsingi hii ilikuwa ni siku tulivu kabisa ingawaje iliambatana na hali ya kihoro kwa wengine! Miongoni mwa watu waliokuwa kwenye kihoro ni Dokta Joselyne Kimario aliyekuwa maeneo ya Chanika; shambani kwake alikokusudia kuwe makazi yake pindi atakapostaafu. Aidha, muda mfupi ujao alitarajia kukutana na vigogo wenzake sita ili awaeleze "jambo" muhimu kama alivyoliita mwenyewe!

"Ni hivi Bwana Benson Mnali, hakikisheni mnakuja kwa kutumia gari moja tu badala ya kila mtu na lake. Jambo lingine la kuzingatia ni kwamba, hakikisheni haumtambuliki kirahisi. Bado nasisitiza, kikao hiki ni muhimu sana kwetu kisiasa na kijamii hivyo hamtakiwi kupuuza hata chembe juu ya kile nilichowaeleza! Mkiyapuuza haya ninayowaambia, bila shaka kesho wote tukajikuta Segerea!" Dokta Joselyn Kimario anakumbuka

kutoa maigizo kwa Bwana Mnali, kigogo mwingine wa serikali ambae nae ni mlengwa kwenye kikao hiki.

Robo saa baadae, wageni wake waliwasili huku wakionesha kuwa na shauku ya kujua kulikoni!

“Ndugu zangu, nimewaita kuwaeleza kwamba TanPurity Limited haina budi kufa mapema iwezekanavyo!” Dokta Kimario alieleza na kuwafanya vigogo wenzake wabaki midomo wazi! Ni kweli, walikuwa na kila sababu ya kupigwa na mshangao! TanPurity ni kampuni ya serikali iliyoanzishwa ili kusafisha madini yanayochimbwa nchini. Wazo la uanzishwaji wa kampuni hii lilikuja ili kuondoa utaratibu wa kusafisha dhahabu nje ya nchi na hivyo kukosekana kwa takwimu sahihi za dhahabu inayozalishwa.

“Mbona hatukuelewei Dokta?!”Hatimae Benson Mnali aliuliza baada ya kugundua hata wenzake walikuwa wamegubikwa na mshangao kama yeye!

“Unamaanisha nini Bwana Kimario!?”Bwana Mohamed Mrisho nae aliuliza kwa mshangao!

“Ni nini ambacho hakijaeleweka? Kama sijasikika vizuri ni kwamba lazima tuhakikishe TanPurity Limited inaelekea kaburini! Tutumie madaraka na mamlaka yetu yote kuwashawishi wenzetu juu ya jambo hili!” Dokta Joselyn Kimario alisisitiza kauli yake kwa macho makavu!

“Kwa maslahi ya nani?!”

“Kwa maslahi ya sisi tuliokuwa hapa!” Dokta Kimario alijibu kwa kujiamini!

“Upo sawa Dokta au umechanganyikiwa?!”

“Hapa nina akili timamu na zinazofanya kazi vizuri pengine kuliko wakati mwingine wowote ule!”

“Sikiliza Bwana Kimario, ikiwa lengo la kutuita ni kujadili jambo la kijinga kama hili nasikitika kwamba

kwangu halina nafasi. Siwezi kukaa hapa na kuisaliti nchi yangu kwa manufa...!" Hatimae, Meja mstaafu wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Meja Issa Makame aliyekua kimya kwa muda wote aliongea kwa hasira! Hata hivyo, kabla hajamaliza sentensi yake alikatishwa kwa kicheko kikubwa toka kwa Dokta Kimario! Kicheko hiki kilikuwa kikubwa, kilichomshangaza kila mmoja! Hatimae walianza kupatwa na wasiwasi kwamba huenda Dokta amerukwa akili! Si kwamba kicheko hicho kilikuwa kikubwa tu, bali kilikuwa kirefu pia! Hata hivyo, kama wangekuwa makini wangegundua kwamba hakikuwa kicheko cha furaha; bali ni kicheko kilichoficha huzuni ndani yake!

"Naomba mnisikilize kwa makini sana." Hatimae Dokta Kimario alianza kuongea baada ya kumaliza kicheko chake kirefu, kisha akaendelea "Msizani kwamba nimechanganyikiwa, hapa nilipo nina akili timamu kabisa. Kama ulivyosema Bwana Makame, hata mimi sipendi kuisaliti nchi yangu lakini nasikitika kwamba sifa hiyo mimi na nyinyi tumeshaipoteza kitambo! Nimewaita kwavile nyinyi ni wasaliti wenzangu kwa serikali yetu tukufu. Tumeisaliti serikali na wananchi kwa ujumla! Na kama alivyowahi kusema Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, mtu akishaonja kula nyama ya mtu, basi maisha yake yote yatakuwa ya kula nyama tu! Nasi hatuna budi kuendelea kula nyama, si nyama za ng'ombe bali ni nyama za Watanzania wenzetu; nyama za wapiga kura wetu! Hivyo basi, endapo kuna yeyote miongoni mwenu anayeamini kwamba yeye ni mtu safi, basi kikao hiki hakimuhusu, hivyo anaweza kuondoka. Lakini kama kuna yeyote ambae anajijua yeye si safi kama ambavyo angependa kuonekana, basi kikao hiki kinamuhusu kwa manufaa yake mwenyewe! Binafsi, tayari nimeshachafuka!

Sisemi haya kwa kujisifu au kuonea fahari, bali nayasema kwa huzuni. Huzuni kwa kuisaliti nchi yangu. Huzuni kwa kuwasaliti wapiga kura wangu. Huzuni kwa kumsaliti rais ambae aliniamini na kunipa madaraka kwavile aliamini mimi ni msafi! Hivyo basi, bado nasisitiza kwamba endapo katika sisi kuna yeyote anayejiona ni safi basi aondoke na wale wachafu kama mimi wabaki ili tuendelee na kikao!

"Kama ni mchafu ni wewe peke yako na usiwasingizie na wengine Dokta!"Meja Makame aliongea huku akiwa amefura kwa hasira mithili ya faru aliyekoswakoswa kwa risasi!

"Hata wewe ni mchafu Meja, tena mla rushwa mkubwa! Ni matumaini yangu endapo mheshimiwa rais angefahamu hilo, asingeweza kukupa hata utendaji wa mtaa kwenye nchi hii!" Hatimae Dokta Joselyn Kimario nae alifoka huku ikionesha wazi kwamba amepandwa na jazba!

Pamoja na Dokta Kimario kukanusha suala la yeye kuchanganyikiwa lakini kimsingi hakuwa sawa! Ingawaje ni kweli kwamba bado alikuwa na akili zake timamu, lakini alikosa utulivu wa akili tangu alipoingia mikononi mwa IBU! Hali ambayo kwa namna fulani ilimwondolea busara hata ya namna muafaka ya kuanzisha mazungumzo haya ili apate usikivu mzuri toka kwa wenza wake!

"Nani mla rushwa?!"Meja Makame aliuliza.

"Wewe hapo Meja Makame! Na wala usilete kiburi chako cha jeshini hapa kwani haya ninayokuambia ni kwa manufaa yako mwenyewe!"

"Pumbavu mkubwa!" Meja Makame alifoka na kuinuka kitini kisha akaanza kuondoka! Wakati malumbano kati ya Meja Makame na Dokta Joselyn Kimario yakiendelea, wengine walikuwa wametulia katika

namna iliyoonesha ni kama wameshikwa na bumbuwazi la ghafla!

“Meja Makame!” Dokta Kimario aliita alipoona Meja Makame hatanii katika uamuzi wa kuondoka!

“Unataka nini?” Meja Makame alifoka!

“Niwie radhi Meja, nilitaka tu kupima hisia zako, hivyo badala ya kuondoka ningependa nikuoneshe kitu ambacho bila shaka utakifurahia.” Dokta Joselyn Kimario aliongea kwa utulivu, hali iliyomfanya Meja Makame atulie hapo alipokua lakini akiwa bado anatweta kwa ghadhabu! Bila kupoteza muda, Dokta Kimario aliwasha televisheni iliyokuwa hapo na kisha akaweka santuri ya video!

“Tafadhali Meja, tuangalie hii filamu japo kwa dakika moja!” Dokta Kimario alimweleza Meja Makame.

Akiwa bado amesimama Meja Makame alianza kushuhudia sinema ya ajabu kidogo! Haikuwa ya vita wala mapenzi, bali ni sinema ambayo bila shaka ingeweza kumvutia mtanzania yeyote ambae angepata bahati ya kuiona! Awali ni kama alitaka kuipuuzia lakini alijikuta akiyagandisha macho yake kwenye TV mara baada ya kuona miongoni mwa wahusika wa sinema hii ni yeye Meja Makame!

Matukio yaliyoonekana kwenye sinema hii hayakuwa mageni hata chembe kwenye kifuko cha kumbukumbu cha Meja Makame. Yalikuwa ni matukio yaliyotokea miaka michache iliyopita. Yalikuwa ni matukio ya siku ambayo Meja makame alikutana na watu ambao hadi leo hii hajapata kukutana nao tena na wala hajui walipo! Awali alikutana kwanza na rafiki yake ambae ni mfanyabiashara anayeheshimika sana nchini na kumuomba kwamba kuna wageni wenye shida na yeye. Chanzo cha ugeni huo ni baada ya kuvuja kwa habari kwamba JWTZ

ilitaka kutangaza zabuni ya uagizaji magari. Baada ya maongezi yao ya siri Meja Makame alikiri juu ya jambo hilo na hivyo wakakubaliana lifanyike kila liwezekanalo ili zabuni waipate hao wageni wake. Kwavile walikuwa wameahidi kutoa "ahsante" ya kutosha, Meja Makame akajikuta akivutiwa na maongezi ya rafiki huyo! Hivyo, pasi na kusita, alikula njama na baadhi ya wakubwa wenzake na kuongeza idadi ya magari ya kuagiza mara mbili zaidi ya yale yaliyokusudiwa awali! Si hivyo tu, pia wakala na njama ya kuagiza na vipuri vya magari hayo ingawaje kabla ya hapo hapakuwa na mpango huo!

Majuma machache baadae, zabuni ilitangazwa ambayo kimsingi ilikuwa ni kiini macho tu kwavile mshindi alishapatikana hata kabla ya kutangazwa kwake!

Wakati zabuni hiyo ilipotangazwa Meja Makame alikuwa ndio mwenyekiti wa bodi iliyohusika na kumteua mzabuni mwenye sifa. Kwa kutumia hila na kwa kushirikiana na baadhi ya maofisa wenzake, Meja Makame alifanikiwa kufahamu mzabuni ambae alikuwa ni mwenye gharama nafuu. Baada ya kufahamu gharama za mzabuni huyo, ndipo Meja Makame alipopenyeza taarifa hizi za siri kwa marafiki zake ambao nao walileta zabuni yao yenye gharama za chini kidogo na kuipandikiza!

Baada ya marafiki wa Meja makame kuzawadiwa zabuni hiyo ambayo ilikuwa ni ya mabilioni ya shilingi, hujuma nyingine ikafanyika! Magari na vipuri ambavyo vililetwa havikuwa vipya kama ilivyotakiwa kwenye masharti ya zabuni, lakini hata hivyo likafunikwa kombe! Kwa upande wa Meja Makame nae, zoezi liliisha likiwa limemwacha na utajiri wa kutisha ambao hakuwahi kuuota hapo kabla! Na ili kuhakikisha anakuwa salama kutoka kwenye macho yapendayo kudadisi, akaamua kuutafuta

ukubwa. Hapo ndipo alipopata wazo la kuingia kwenye siasa. Kwa bahati nzuri, aliteuliwa kuwa waziri na hivyo kujijengea ukuta zaidi na kuondoa uwezekano wa kufuatwafuatwa hata na watu wadogo!

"Meja Makame, je bado unahisi kikao hiki hakikuhusu?!" Hatimae Dokta Joselyn Kimario alimzindua toka kwenye shazi zito la kumbukumbu lililokuwa limemea kichwani mwake! Hata hivyo, masikioni mwa Meja Makame sauti hii ilisikika kana kwamba inatoka umbali wa maili kadhaa! Alijitahidi kuvuta kumbukumbu kama angeweza kubaini ni sauti ya nani lakini jitihada zake zilizidi kumwelekeza ndani ya lindi refu lenye kiza totoro! Kitu pekee ambacho kiliweza kuibuka kwenye kumbukumbu zake hizi za sasa ni mdaharo uliofanyika siku chache tu zilizopita! Kwenye mdahalo huo, yeye alikuwa ni mmoja kati ya watoa mada ambae alifanikiwa kuvuta hisia za watu kadhaa waliohudhuria! Kwa kifupi, alikuwa ndie nyota wa mdahalo kutokana na hoja zake!

*Ulikuwa ni mdahalo juu ya rushwa kwenye zabuni za serikali!*

Siku iliyofuatia mdahalo huo, vyombo mbalimbali vya habari vilimwelezea Meja Makame kama jasiri mwenye nia ya dhati ya kupambana na rushwa! Na tangu hapo, akawa anapata mialiko toka sehemu mbalimbali ya kwenda kutoa mada juu ya masuala ya rushwa!

Alipoibuka toka kwenye kumbukumbu za mdahalo huo mara akajihisi kutokewa na ndoto za ajabu! Mchana kweupe; tena akiwa amesimama, aote ndoto! La hasha, akabaini kwamba si ndoto! Kwa namna ya kushangaza kabisa, anga lote karibu yake akalikuta likimezwa kwa giza totoro huku nyota kadhaa zikielekea kupita kwa madaha mbele yake kwa namna ya kumfanyia dhihaka!

Nyota mchana wa jua kali!

Akazipuuza!

Alizipuuza kwa sababu alifahamu fika kwamba nyota hizi hazitambui ya kuwa yeye ni mtu mzito serikalini ambae pia ni meja mstaafu wa jeshi! Zaidi ya hayo, alikuwa kwenye mstari wa mbele wakati wa vita vilivyomng'oa nduli Iddi Amini Dada miaka kadhaa iliyopita!

Hakika, usiposhangaa ya Musa, utashangaa ya Firauni! Hali hii ya kushangaza haikutokea kwa Meja Makame peke yake, bali hata kwa vitu vyenye uwezo usio shaka! Pamoja na uwezo wa kustajaabisha wa ardhi wa kubeba mabilioni kwa mabilioni ya tani juu yake lakini ilielekea kuelemewa na uzito mdogo tu wa Meja Makame! Kama ilivyo kwa viumbe hai wanapoamua kuudondosha mzigo pale wanapohisi kuelemewa nao; ardhi nayo ilifuata silika hii! Bila kutarajia, Meja Makame alikula mwereka na kujibwaga chini, pu!

Patashika, nguo kuchanika; likaibuka pasi shaka!

Vigogo hawa wengine wakajikuta wamepigwa na butwaa! Wakaganda wasijue nini cha kufanya! Ilimchukua sekunde kadhaa Dokta Joselyn Kimario kuweza kuzinduka! Mara moja alizima televisheni na kukurupuka na kwenda kumwangalia Meja Makame hapo alipodondokea.

*Macho yalijipindua, mbonize zikafichama!*
*Kufumba na kufumbua, nako kulishayoyoma!*
*Yasingetishika kwa vidole wala kutiwa mchanga!*
*Ni macho ya kijasiri, yasingeogopa hata simba!*
*Yangemtisha yeyote mwenye thubutu kuyatazama!*

Ilikuwa ni kama sinema! Tangu anaamka, Dokta Joselyn Kimario alikuwa anafuatiliwa kwa ukaribu kwa kila hatua aliyopiga lakini bila ya mwenywe kufahamu! Labda kutokana na kutokuwa na uzoefu kwenye mambo ya kikachero, George Kamau, Glory pamoja na Layla wakiwa kwenye gari waliweza kumfuatilia Dokta Joselyn Kimario tangu alipotoka nyumbani kwake maeneo ya Masaki hadi Makutano ya Barabara ya Mandela na ile ya Kilwa; eneo ilipo Taasisi ya Uhasibu Tanzania! Taa za kuongozea magari zilizopo kwenye makutano hayo ziliweza kumruhusu Dokta Joselyn Kimario kupita lakini bahati hiyo haikuwapo upande wa Geoge Kamau. Walitulia hapo kwenye taa za kuongozea magari na mara simu yake ya mkononi ikaita!

“Ndiyo kijana, lete habari!”

“Amepita hapa sasa hivi na anaendelea na Barabara hii ya Kilwa kuelekea Mbagala!” Mtu aliyekuwa upande wa pili wa simu alijibu. Huyu alikuwa ni mmoja wa vijana wa Kamau aliowaweka kwenye makutano mbalimbali ya barabara kuangalia endapo Dokta Joselyn Kimario angechepuka mahali! Kijana huyu aliwekwa kuchunguza makutano ya Barabara ya Kilwa na ile iendayo Temeke!

“Safi kijana, kaendelee na kazi zako kwavile nishapata uhakika ni wapi anakoelekea kwa sasa.” George Kamau alijibu, na mara taa zikawaruhusu.

Hata pale taa zilipowaruhusu tayari Dokta Kimario alikuwa ameshawaacha umbali mrefu! Aidha, umbali huu ukazidi kuongezeka kadri muda ulivyoenda kutokana na mwendo mdogo wa malori mawili yaliyokuwa mbele yao! Mwendo huu mdogo waliendelea nao hadi Mtoni kwa Azizi Ally pale malori hayo yaliposhika barabara inayoelekea Temeke na hivyo kuwapa nafasi ya kukanyaga

mafuta zaidi. Walipofika Mtoni Mtongani wakashitushwa na gari moja dogo lililokuwa mbele yao!

"Punguza mwendo Layla!" George Kamau alimweleza Layla aliyekuwa kwenye usukani!

"Umehisi nini!?" Layla aliuliza huku akiwa tayari ameshapunguza mwendo.

"Nina mashaka na ile Toyota Mark II nyeusi iliyo mbele yetu. Kuna kila dalili kwamba kuna gari wanaifuatilia hivyo na wewe hivi sasa weka akili zako na kwenye ile gari pia!"

George Kamau alikuwa sahihi! Ingawaje hakuwa na uhakika lakini ukweli ni kwamba gari aliyokuwa anaizungumzia ilikuwa imewabeba askari polisi wawili! Hata hivyo, pamoja na umakini wake wote bado alishindwa kuhisi kuwapo kwa Bon Mtambo aliyekuwa anawafuatilia kila walipopita! Aliyefahamu juu ya uwezekano wa kufuatiliwa na Bon Mtambo ni Layla pekee ambae ndie aliyekuwa amevujisha habari za safari hiyo!

Kufuatia mweleka aliokula Meja Makame, Dokta Kimario alimwendea na kusikilizia mapigo yake ya moyo.

Nayo yalishasimama kitambo!

Akiwa kama aliyechanganyikiwa; Dokta Joselyn Kimario aliwatupia macho wenzake katika namna iliyosema Meja Makame keshafariki! Kafariki kwa mshtuko!

Hapo ndipo akakukumbuka kwamba ni majuma machache tu yaliyopita Meja Makame alirejea toka India kupatiwa matibabu ya moyo!

Kabla hawajafahamu wafanye nini mara vijana wawili waliovalia sare za jeshi la polisi waliingia kikomandoo humo ndani, huku wakiwa wameshikilia bastola mikononi mwao!

Walikuwa ni polisi wa doria waliokuwa wamekurupushana na majambazi huko Temeke!

"Wote mikono juu!" Vijana hawa waliamrisha!

Dokta Joselyn Kimario na wenzake wakabaki wametahayari wasijue nini cha kufanya! Waliamini arobaini yao imeshawadia.

*"Wote turudi sehemu zetu za kazi hadi hapo uchunguzi utakapokamilika!"* Kauli ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa siku iliyopita ilirejea tena masikioni mwa vigogo hawa! Kuibuka kwa askari hawa kwao kulimaanisha kwamba ule uchunguzi aliousema rais ndio umeshakamilika!

"Tafadhalini semeni chochote mtakacho nasi tutawapatia ili msiitoe siri hii!" Hatimae Dokta Kimario alifanikiwa kuongea. Kama ambao hawajasikia, mmoja wa askari hao alienda moja kwa moja ilipo televisheni! Kilichomvuta ni kuona mashine ya VCD ikifanya kazi huku ikionekana kuna CD iliyokuwa inaendelea! Alifika na kuwasha televisheni na kuirudishia CD tangu mwanzo!

Sinema ile ya ajabu ilianza tena! Benson Mnali na wenzake walitumbua macho wakishuhudia sinema hii! Kila mmoja alivuta kumbukumbuku za matukio haya ambayo hapo awali walizani ni matukio ya kwenye harusi tu ndiyo ambayo ingetokea tena wakaja kuyashuhudia kwenye luninga zao! Yalimuonesha kila mmoja kwa wakati wake na mahala pake akifanya yale ambayo wasingependa mwingine ayaone!

"Ni nini hii?!" Hatimae mmoja wa wale askari aliuliza kwa ukali.

"Tafadhali tuzungumze kiutu uzima afande, kama ujuavyo, sisi ni watu wenye nyadhifa zetu kwahiyo.....!"

"Siwezi kuwasikiliza hadi mtuambie nini kinaendelea hapa!" Askari waliweka ngumu.

"Ina maana tukisema ukweli mtatusamehe?" Dokta Joselyn Kimario aliuliza huku akionesha dhahiri kurukwa na akili, kwani haikumchukuwa muda kubaini kwamba swali alilouliza ni la kitoto!

Kusamehewa! Tena mbele ya maiti!

"Hatuwezi kuwasamehe hivihivi, labda tuongee *biashara*!" Askari mwingine aliyekuwa kimya kwa muda wote aliongea!

Kwa mbali, Dokta Joselyn Kimario alihisi mwanga wa matumaini. Aliamini akimalizana na hawa askari, itawapa nafasi ya kuangalia jinsi ya kukabiliana na suala la maiti iliyopo mbele yao!

"Ni hivi vijana, mnajua hii nchi ina.....!" Alishindwa kumalizia! Kila mmoja, miongoni mwa vigogo hawa alibaki ametumbua macho!

Macho ya woga!

Macho ya hofu!

Hawakutarajia jambo hili!

"Ni hivi mzee, naomba fanya kila uwezalo ili ukakutane na Mheshimiwa Rais leo hii kisha umweleze kwamba nahitaji kumpeleka mahali!" Ilikuwa ni simu ya Bon Mtambo alipompigia Mkurugenzi wa Uplelezi nchini, DCI Humphrey Mwaiswelo!

"Mbona sikuelewi kijana!" DCI Mwaiswelo aliuliza.

"Nataka wewe na yeye pamoja na IGP Jaffery Minga niwapeleke sehemu moja nje ya jiji tukajadiliane jambo fulani. Hata hivyo, mweleze mheshimiwa rais asimwambie mtu yeyote juu ya safari hiyo kwavile bado tunalazimika kulifanya jambo hili siri."

"Ina maana unafahamu kuhusu alipo IGP Minga?" DCI Mwaiswelo aliuliza kwa mshangao kwavile bado jeshi la polisi na vyombo vingine vya usalama vilikuwa vinakesha kutafuta ni wapi alipo IGP Jaffery Minga!

"IGP Minga yupo mikononi mwangu lakini usiulize maswali mengi zaidi kuhusu yeye. Jambo la msingi ni kwamba nitamtuma SSP Faraji Zegge kwako ili uwe nae. Ukishakutana na rais na kumwambia juu ya wito huu, ndipo mtaungana na SSP Faraji ambae atawapeleka alipo IGP Jaffery Minga kisha atawaleta huko ninakotaka tukutane!" Bon Mtambo alieleza.

"Sawa kijana, labda kama kuna lingine!"

"Ni hayo tu mzee lakini hivyo sasa hivi! Kamtake radhi rais kwa niaba yangu kwa kumvurugia ratiba yake ya ofisi!" Bon Mtambo alimalizia.

Wakati kiwiliwili cha Meja Makame kikiwa bado hapo chini, wale askari waliokuwa wameingia hivi punde nao walipaa hewani ghafla na kujibwaga chini! Miili yao ambayo sekunde chache zilizopita ilikuwa ikipumua kuashiria afya njema kwao, hivi sasa ilikuwa imelalia dimbwi la damu, kila mmoja ya yake mwenyewe!

Wameuawa, pengine ili wasisikie hicho kilichotaka kutamkwa na Dokta Joselyn Kimario!

Wakiwa bado wamehamanika huku wasijuwe la kufanya mara watu wawili waliaficha sura zao kwa soksi waliingia mithili ya *maninja*!

“Endeleeni na kilichowaleta hadi mnafikia muafaka nasi tutashughulika na hizi maiti! Msiwe na hofu, kila kitu kitaenda sawa!” Mmoja wa maninja hawa aliwaambia akina Dokta Kimario kisha akaziendea zile maiti za askari na kuanza kuzipekuwa.

“Mwisho wako umefika Kamau!” Sauti kali ilisikika toka nyuma yao! Huku wakiwa bado hawajui nini kinatokea, mara mtu mmoja aliyekuwa nae kaficha uso wake aliingia kijeshi huku akijiviringisha! Jamaa aliyekuwa akianza kuzipekuwa maiti alianza kuvurumisha risasi kadhaa lakini ilikuwa ni kama mtu asiye ni mafunzo ya kulenga shabaha! Risasi zote zilimkosakosa kutokana na vile alivyokuwa akijiviringisha hewani!

Kati ya wale *maninja* wawili walioingia awali, mmoja wao ilikuwa ni kama aliyepigwa na butwaa! Alikuwa akijaribu kukumbuka ni wapi alipata kuisikia sauti hii iliyoashiria mwisho wa Kamau! Butwaa hili likahamia kwa mwenzake aliyekuwa ameshikwa na bumbuwazi la sekunde chache likitokana na kushitushwa na umahiri wa adui yake katika kukwepa risasi! Yeye alikuwa ni mtaalamu sana katika kulenga shabaha, lakini hapa alionekana ni kama mtu asiye na uzoefu wowote katika matumizi ya bastola! Mzubao wake ambao haukudumu hata kwa sekunde tano ulikuwa ni kosa kubwa sana la kiufundi hususani ndani ya uwanja wa mapambano! Kabla hajajuwa achukue hatua gani nyingine, adui yake alikuwa ametua sentimeta chache tu mbele yake na ghafla alishtukia mkono wake ulioshika bastola ukipigwa teke zito na kuifanya bastola yake ipae hewani! Kabla bastola haijafika

chini, yalifuata mapigo matatu ya nguvu yaliyomtupa huyo mtu hadi chini huku akigumia kwa maumivu!

Pigo kali lililomkuta mwenzake likamfanya yule aliyekuwa akijaribu kuikumbuka sauti ya mbabe huyu, nae kuzinduka na kuchomoa bastola! Hata hivyo, kabla hajafanya chochote nae alijikuta akipigwa teke kali lililomtupa chini na bastola yake mkononi! Akiwa hapohapo chini alikoki tena bastola yake lakini kabla haijanyesha mvua ya risasi mbabe wao alijirusha hewani na kutua katikati ya kifua chake kwa kishindo kizito!

"Mamaa......!" Pigo zito la kifuani ambalo bila shaka halikuendana na uwezo wake lilimfanya atoe sauti kali ya kike iliyoashiria maumivu makali! Bila kutarajia alijikuta akiiachia bastola yake bila kutaka! Sauti hii kali ya kike ndio iliyowazinduwa hata wale waheshimiwa ambao bado nao walikuwa wamekumbwa na bumbuwazi wakiwa hawajui ni nini hasa kinachotokea mbele yao! Kama walioambizana, walianza kukurupuka na kutaka kukimbia! Hata hivyo, kwa kasi ya kufumba na kufumbua, huyu mtu aliyekuwa anagawa vipigo alitoa bastola yake na kuachia risasi tatu hewani kama onyo!

"Tulieni hivyohivyo, la sivyo nitazitawanya bongo zenu sakafuni sasa hivi!" Mr. Mbabe aliongea kwa sauti kali na kumfanya yule aliyetoa sauti ya kike kuzinduka kwenye kipigo na kuanza tena kuikumbuka sauti hii! Wakati huyu akijaribu tena kuikumbuka sauti hii, mwenzake aliinuka na kwenda kumkumba adui yake na wote wakaenda chini. Mapigano makali yalizuka kati yao huku wakiwa wanabiringishana hapo chini hadi yule mtoa vipigo alipofanikiwa kusimama na kumwashiria mwenzake nae asimame ili waoneshane vizuri kinaume!

Kufuatia ishara hiyo nae akainuka na kuanza kuchapana makonde na mateke!

Mapigano makali yalidumu kwa takribani dakika mbili hadi yule aliyetoa sauti ya kike alipokuja kutaka kumsaidia mwenzake baada ya kuona anaelemewa! Hata hivyo, ni kama alipiga hesabu zake vibaya, kwani bila kutarajia alijikuta kipigo kikianza kumrudia yeye na kutoa nafasi kwa mwenzake kuanza kutimua mbio!

Kuona mwenzake anaanza kutimua mbio nae alitaka kufuata nyayo lakini kabla hajafika popote alipigwa teke zito la shingoni lililomzoazoa na kwenda kumbwaga chini mithili ya gunia la pumba! Alitaka kuinuka lakini akarudishwa tena chini na teke kali la tumboni kisha huyu mtoa vipigo akamgeukia yule mtu aliyekuwa anakimbia huku akichechemea kwa kipigo!

Alijaribu kumkimbiza lakini alichelewa, kwani alikuwa ameshafika mlangoni na kuanza kutoweka kwenye upeo wa macho yake!

“Simama Kamau, la sivyo nitakuua kwa risasi!”Mr. Mbabe alipiga kelele lakini hata hivyo alishachelewa kwani huyo mtu aliyekuwa amemtaja kwa jina la Kamau alikuwa keshatoka nje tayari kwa kwenda kupanda gari iliyokuwa inamsubiri hapo nje!

“Tulia hapo hapo George, na leo ndio mwisho wa ufedhuli wako!” Dereva aliyekuwa garini akimsubiria George na mwenzake aliongea huku akiwa ameelekeza bastola yake kwa George Kamau! Dereva huyo alitoa amri hiyo wakati Kamau alipokuwa anajiandaa kuingia garini ili watoweke eneo hilo!

“*What*!?(Nini!?)” George Kamau aliuliza huku akiwa ametumbua macho ya uoga yaliyokuwa yanachungulia mdomo wa bastola!

"Ni nini hujasikia George? Nimesema leo ndio mwisho wa ufedhuli wako!"

*"Are you serious Layla?! Are you betraying me, enh?!"* Kamau aliendelea kuuliza kwa mshangao huku akimaanisha endapo kweli Layla ameamua kumsaliti!

*"I am serious George, but I am not betraying you! What i was doing is betraying my fellow Tanzanians whom welcomed me in their country and made me feel at home!"* (Ni kweli George, hata hivyo sikusaliti wewe, bali nilichokuwa nafanya ni kuwasiliti Watanzania walionikaribisha nchini mwao na kunifanya nijisikie kama nipo nyumbani!") Layla aliendelea kuongea kwa sauti ya upole na kumwamrisha Kamau ainue mikono juu na kumwongoza alikotokea!

Huko ndani, ile sauti ya kumwamrisha Kamau asimame la sivyo angeuawa kwa risasi ilijipenyeza barabara masikioni mwa yule mtu aliyekuwa akitoa sauti ya kike! Sauti hii sasa aliitambua vyema kwamba ni sauti ya Bon Mtambo! Kufuatia kuitambua sauti hii, alijikuta akikumbwa na mchecheto kupita kiasi! Mithili ya mtu aliyechanganyikiwa, alianza kukimbia akiuelekea ukuta ili aruke na kupotea maeneo hayo. Hiki kilikuwa ni kipindi kile wakati Bon Mtambo alipoenda kujaribu kumkamata Kamau! Wakati Bon Mtambo alipokuwa anarudi ili amkabili huyu aliyebaki, alikuta anajiandaa kushika ukuta ili arukie nje!

"Simama hapo hapo Glory, la sivyo nitakuua!" Bon Mtambo alipiga kelele na kuachia risasi kadhaa za tahadhari! Mchecheto uliongezeka maradufu pale alipojuwa ameshatambulika! Aliwahi kuushika ukuta, lakini alishindwa kuupanda kutokana na mchecheto! Bila kutarajia, aliuachia na kujibwaga chini na kukaa huku akiwa amejikunyata mithili ya kinda la ndege

lililonyeshewa mvua ya mawe! Hapo hapo alianza kulia kwa kwikwi na kuomba asamehewe!

"Hakuna msamaha Glory, ulijiona mwerevu sana pale uliponinunulia simu yako ya kijasusi kule Marekani! Ulizidi kujiona mwerevu zaidi pale ulipozani unanihadaa ili nikununulie mkufu uliokusudia uwe unanasa maongezi yangu na kumpelekea bwana wako Kamau! Lazima ulipe kwa uovu wako!" Bon Mtambo alimweleza Glory kwa sauti ya upole na kumwamuru asimame!

Hata hivyo, Glory alibisha kusimama hadi Bon Mtambo alipopiga risasi mbili karibu na miguu yake ndipo akasimama huku akipiga ukelele wa hofu!

"Kipokee kipusa chako Bon!" Ghafla sauti laini ilisikika kutoka mlangoni. Bon Mtambo alipogeuka, alipigwa na butwaa baada ya macho yake kugongana na ya Layla aliyekuwa amemwongoza mbele yake George Kamau ambae mikono yake ilikuwa imefungwa nyuma kwa pingu!

"Safi sana Layla, nazani huu ni wakati wao wa kufahamu kwamba Afrika Mashariki ni eneo huru dhidi ya vitendo vya kihalifu!" Bon Mtambo aliongea kwa bashasha, huku akiwa haamini kile anachokiona mbele yake. Kabla mshangao wake haujayeyuka, ghafla Insepkta Cecy, Inspekta Mussa Ndimbu na IGP  Minga waliingia kiaskari humo ndani huku wote wakiwa wameshika bastola mikononi mwao! Hapo ndipo Bon Mtambo akagundua kwamba tayari dakika tano zilikuwa zimeshapita. Wakati anawaacha kwenye gari, aliwaambia wasubiri kwa dakika tano na wakiona kimya wamfuate!

Waheshimiwa waliokuwa bado wakitweta kwa hofu, walimuona IGP  Minga akiwa amewatupia jicho kali kisha akaanza kuongea na simu! Ilipita kama dakika moja

tangu IGP Minga aongee kwenye simu kabla ugeni mwingine mzito haujawasili! Bila kutarajia, mheshimiwa mmoja alijikuta anakaa chini bila kuamriwa! Katika hali ya kawaida, jambo hili ni kinyume kabisa cha maadili! Kawaida ni kwamba anapoingia mtu kama huyu watu wote husimama badala ya kukaa kama alivyofanya Mheshimiwa Benson Mnali!

Hata hivyo, hii haikuwa hali ya kawaida!

Kituko kingine kikatokea! Wakati Mheshimiwa Mnali akikaa chini kwa mchecheto, mheshimiwa mwingine aligeukia upande huku akionekana kushusha shati alilokuwa amechomekea hapo awali! Ni hofu! Hofu! Hofu! Ni hofu hii ndio iliyomfanya Mheshimiwa Mrisho atokwe na haja ndogo bila kutarajia!

Kwa hakika, mgeni aliyeingia alikuwa ni kama amekuja kutapakanya hofu kwa waheshimiwa! Ilikuwa ni mithili malaika mtoa roho aliyekata shauri la kujionesha waziwazi mbele ya wagonjwa mahututi!

Mgeni huyu alitupa macho yake huku na huko kisha akashitushwa na mwili wa Meja Makame uliokuwa umelala chini huku ukionesha dalili zote za kukosa uhai! Upande mwingine, alishuhudia miili mingine miwili ya wanaume waliovalia sare za jeshi la polisi! Baada ya hapo, macho ya mgeni yakatua kwenye miili iliyoonesha uhai na afya tele licha ya kuonesha dalili zote kwamba imelowana kwa hofu! Aidha, macho yake yalitembea tena kwa haraka haraka na kutua kwa wasichana warembo wawili waliokuwa na sifa zote za kuitwa wasichana warembo! Hata hivyo, wakati uso wa mmoja wao ukionekana kusawajika, bila shaka kutokana na kipigo, uso mwingine ulionesha nuru halisi ya mwanamke mrembo, anayevutia,

na mwenye uwezo wa kumteka mwanaume yeyote yule hata aliye na hisia mfu! Hisia kuwa mfu sawa; macho je?!

Mgeni akameza mate!

Umezaji mate wa aina hii unaleta tafsiri fulani ambayo hata hivyo nisingependa kuielezea hapa kutokana na uzito wa mgeni mwenyewe!

Macho ya mgeni huyu yakahamia kwa mwanaume mmoja ambae uso wake ulikuwa unavuja damu kutokana na kipigo! Alimwangalia kwa makini kwa sekunde kadhaa, kisha akamkumbuka kama ni mmoja wa wafanyabiashara maarufu hapa jijini! Hata hivyo, hakuweza kulikumbuka jina lake, ambalo ni George Kamau!

Kutoka kwa George Kamau, macho ya mgeni aliyarudisha kwa waheshimiwa waliokuwa wameshitushwa kupita kiasi kutokana na ujio wake ambao hawakuhutarajia! Mara nyingi mgeni huyu uso wake huwa unaundwa na tabasamu murua! Hata hivyo, leo ilikuwa ni tofauti kabisa! Na ilikuwa ni tofauti maradufu alipoyatupa macho yake kwa akina Mheshimiwa Benson Mnali!

Hasira za wazi zilidhihirika machoni mwake!

Kuna wakati, ungehisi labda alitamani kuwafanya asusa wakiwa bado wabichi! Hata hivyo, mgeni huyu hakuwa mla nyama za watu!

Kuna wakati, ungehisi labda alitamani kuwarukia na kuwatandika makonde kadhaa ya uso yatakayowang’oa hata meno yao ya mbele, na ikibidi hata magego! Lakini kwa mtu anayeongozwa na maadili nalo ni kinyume!

Inasemekana mgeni huyu nae alikuwa ni miongoni mwa vijana shupavu wa Tanzania walioenda kumshikisha adabu Nduli Iddi Amini Dada enzi hizo! Hata hivyo, sina hakika kuhusu ukweli wa hilo na kama ni kweli basi bila shaka huenda alitamani waheshimiwa waliopo mbele yake

wageuke Iddi Amin ili apate sababu ya kuwararua hapahapa!

Mnh! Amiri Jeshi Mkuu aingie mwenyewe vitani!

Yote hayo, yangehisiwa kutokana na kuonesha dhahiri kuchukizwa na haya anayoyaona mbele yake!

Mithili ya mtu anayetafuta faraja baada ya kukinaishwa kwa kuyaona yasiyovutia, mgeni aliyarudisha macho yake kwa Bon Mtambo! Sura ya mgeni ikachanua kidogo kiasi cha kuanza kuonekana kwa lile tabasamu lake lililozoeleka! Bon Mtambo kwa upande wake, aliyaona macho haya ni kama yanayotaka kuuliza jambo fulani kutoka kwake, hivyo bila kuchelewa alianza kueleza:

"Mheshimiwa rais, mbele yako ni baadhi tu ya wahujumu wa nchi hii ambao uliwaamini na kuwapatia madaraka na mamlaka ya kulinda mali na maslahi ya Watanzania! Badala yake, wamekugeuka wewe, wapiga kura wao na Watanzania kwa ujumla! Ni wahujumu hawa ambao walipanga njama za kunifanya nionekane gaidi na mhalifu wa kimataifa pindi walipogunduwa kwamba nipo mbioni kuwaumbua! Yaliyosalia mheshimiwa rais ni mambo ya kisheria, mimi bado nipo kwenye harakati za kufunga kazi dhidi ya wahujumu wengine waliosalia! Vita bado ni tete, ingawaje inaelekea ukingoni na lazima nihakikishe nakusanya ushahidi wote muhimu utaowakilishwa mahakamani! Hata hivyo, kwa sasa habari hizi zisitangazwe ili kutotoa ruhusa kwa wengine kutoroka." Bon Mtambo aliongea kwa sauti ya upole iliyomgusa hata mheshimiwa rais mwenyewe!

Punde si punde, gari aina ya Land Rover 110 ya polisi iliingia na kutoa nafasi kwa Bon Mtambo na vijana wake kuondoka eneo hilo na kuelekea ilipo kambi ya ISLIB!

# 15

Ilikuwa inakaribia saa nane usiku! Sehemu kubwa ya jiji la Dar es salaam ilikuwa kimya mithili ya eneo la makaburi! Aidha, ukimya huu ulikuwa mara dufu kusini mwa jiji hili, hususani kwenye barabara kuu itokayo Dar es salaam kuelekea mikoa ya Lindi na Mtwara. Lori moja, katika barabara hii, liliongozwa na gari nyingine mbili aina ya Land Cruiser VX. Gari iliyokuwa mbele kabisa iliwabeba Bon Mtambo, Njoroge, Okello, pamoja na vijana wao kutoka jeshi la polisi. Aidha, gari iliyofuata ni ya huduma ya kwanza iliyowabeba wataalamu wa utabibu kutoka Jeshi la Wananchi Tanzania. Lori lililokuwa nyuma ni mali ya JWTZ na ilikuwa imebeba kikosi maalumu cha wanajeshi takribani hamsini kutoka kambi ya jeshi ya Twalipo! Wote hawa, walikuwa na lengo moja tu; kuvunjilia mbali mtandao haramu wa kihalifu unaondesha hujuma mbalimbali nchini Tanzania!

Baada ya kupenyezewa taarifa na Layla kuhusu hali ya kambi ya ISLIB, Bon Mtambo alikata shauri la kuwashirikisha JWTZ! Aidha, JWTZ nao walimteua Luteni Francis Mwaka kuongoza kikosi hicho maalumu. Baada ya Luteni Mwaka kupewa jukumu hilo, alikutana na Bon Mtambo akiwa na wanajeshi wenzake watano wakapanga namna watakavyoingia na kuanzisha mashambulizi kwenye kambi ya ISLIB.

Jemedari wa kwanza kuwapanga vijana wake alikuwa ni Luteni Francis Mwaka kutoka JWTZ.

Aliwapanga askari wake kwa kuizunguka kambi ya ISLIB isipokuwa upande wa barabara Kuu ya Kilwa ambako ndiko kwenye lango kuu la kuingilia kwenye kambi. Wote walikuwa na bunduki aina ya AK 47 mikononi mwao tayari kabisa kwa kufanya mashambulizi pindi watakapopewa amri ya kufanya hivyo! Aidha, vijana wengine wa Bon Mtambo wakiongozwa na SSP Faraji Zegge walikuwa pamoja na vijana wengine kiasi cha kumi kutoka JWTZ. Hawa walikuwa wamejificha umbali wa karibu meta hamsini kutoka lango kuu!

Kwa upande wa Bon Mtambo, yeye aliongoza kikosi kidogo cha watu watano ambapo yeye mwenyewe, Daniel Chacha pamoja na Layla wakiwa upande wa kushoto wa barabara inayoelekea lango kuu la kambi ya ISLIB; na upande wa pili wa barabara alikuwepo William Okello, Inspekta Fareed Mwinyimkuu pamoja na Inspekta Cecy! Wote hawa walinyata na kuwa karibu kabisa na lango kuu huku wakiwa wameshikilia bastola zao zenye viwambo vya kuzuia sauti huku migongo yao ikining'iniza bunduki! Hapo langoni, na maeneo ya jirani, kulikuwa na takribani askari kumi wa ISLIB wakilinda kambi!

Jonathan Njoroge alikuwa na Inspekta Mussa Ndimbu pamoja na Sajenti Marwa kutoka JWTZ. Wakati Sajenti Marwa alikuwa nyuma ya usukani wa gari, Njoroge na Inspekta Mussa Ndimbu walikuwa sehemu ya nyuma kabisa ya gari huku mlango wa gari wakiwa wameuegesha tu. Kwa kawaida, sehemu hii huwa haina viti, hivyo walikuwa wamechuchumaa huku wakiwa na bastola zao mkononi tayari kwa lolote!

Sajenti Marwa aliiacha Barabara kuu iendayo mikoa ya kusini na kushika barabara ya vumbi inayoelekea kambini! Huku akiwa amewasha taa zenye mwanga hafifu,

aliendelea kukanyaga mafuta na alipofika umbali wa takribani meta hamsini kutoka lango kuu, mara gari yake ikazima! Huku akiwa tayari kwa lolote, aliteremka na kwenda kufunua boneti la gari na kutupa jicho pembe kuzunguka eneo hilo! Wakati huo huo, Jonathan Njoroge na Inspekta Mussa Ndimbu wakafungua mlango na kuushikilia na kuufanya kama bado umefungwa!

Kama walivyotarajia, askari watano wa ISLIB walilijia gari la akina Njoroge kwa mwendo wa kasi huku wakiwa na bunduki mikononi mwao! Kama vile hajawaona, Sajenti Marwa aliendelea kukagua boneti na walipomkaribia tu, Njoroge na Inspekta Mussa Ndimbu waliruka toka garini na kuachia risasi kadhaa na kuwaua askari wote ambao walishamkaribia Sajent Marwa! Kitendo hiki cha akina Njoroge kiliwaibua askari wengine takribani watano wa ISLIB waliokuwa wamejificha ng'ambo ya barabara na kuanza kufyatua risasi hovyo ambazo hata hivyo hazikuleta madhara kwa akina Njoroge! Wakati haya yanatokea, tayari Sajent Marwa alikuwa amesharuka kutoka kwenye boneti na kuwafyatulia risasi kadhaa!

Milio ya risasi iliwafanya walinzi waliokuwa kwenye lango kuu kutaharuki na kuanza kukimbilia eneo la tukio! Hata hivyo, kabla hawajafika kokote, walijikuta wakishambuliwa kutoka pande zote za barabara; mashambulizi yaliyofanywa na kikosi cha Bon Mtambo kilichokuwa jirani na lango kuu!

Baada ya mashambulizi haya, kikosi cha Bon Mtambo kilijitoa mafichoni na kwenda kulikabili lango kuu ambapo waliiachia risasi kadhaa kwenye makufuli ya lango hilo. Bila ajizi wala ubishi, lango hilooo, likafunguka! Kufunguka kwa lango kulimpa nafasi Sajent Marwa aliyekuwa anakuja kasi kwa gari kisha akapitiliza moja kwa

moja hadi ndani! Kabla gari haijasimama vizuri, aliruka na kujiviringisha huku akikoswakoswa na risasi! Ndani ya robo dakika tangu Sajenti Marwa aruke toka garini, Bon Mtambo alifyatua bomu walilokuwa wametega humo garini na kusababisha mlipuko mkubwa ulioleta kizaazaa na taharuki kwa walinzi waliokuwa ndani ya kambi!

Wakati hali ya taharuki ikiwa imeshatawala, kikosi cha Njoroge kiliungana na kikosi cha Bon Mtambo na kufanya mashambulizi zaidi wakielekea kwenye jengo moja. Muda huohuo, kikosi cha SSP Faraji Zegge nacho kilikuwa kimeshatoka mafichoni na kuielekea kambi huku wakiwashambulia askari waliofanikiwa kutoroka kambini!

Kikosi cha Bon Mtambo, Okello na Njoroge viliungana pamoja na kuongozwa na Bon Mtambo hadi vilipofika kwenye jengo walilolikusudia! Kabla hawajafanya chochote, mara mlango wa jengo hilo ulifunguka na hapo hapo mashambulizi ya risasi yakaanza kutokea kwa ndani. Mapambano ya silaha yalipamba moto kati ya kikosi cha Mtambo na kile kilichokuwa ndani ya jengo! Mapambano haya yaliendelea kwa takribani dakika moja hadi kilipofika kikosi cha SSP Faraji Zegge akiwa na kiasi cha vijana kumi wa JWTZ! Kuingia kwa kikosi hiki kuliongeza kasi ya mapambano toka pande zote mbili!

Katikati ya ufyatulianaji wa risasi, Bon Mtambo, Okello, pamoja na Inspekta Fareed walifanikiwa kujipenyeza ndani ya jengo. Walipoingia tu, Bon Mtambo alipiga risasi swichi kubwa ya umeme na kusababisha jengo zima kuwa gizani! Kizaazaa kikazuka humo ndani na kusababisha tafrani ya mwaka! Bon Mtambo na wenzake walibana sehemu moja na hivyo kuanza kupeleka mashambulizi kuelekea kwenye kundi la askari waliokuwa wameshataharuki. Kiasi cha dakika moja baadae, ulisikika

mlipuko mwingine mkubwa sana wa bomu kutokea nje na hivyo kuchochea moto kwenye mtafaruku uliokuwapo! Mlipuko wa bomu ulikuja baada ya Bon Mtambo kupiga filimbi ya ishara ya kufanya hivyo! Baada ya mlipuko huo, kikosi cha Luteni Francis Mwaka kikasonga mbele na kuizunguka kambi huku wakimpiga risasi za mguu kila askari wa ISLIB aliyejaribu kutoroka!

Baada ya mapambano ya karibu dakika kumi, eneo lote likawa kimyaaa! Hii ilikuja baada ya kikosi cha Luteni Mwaka na kile cha SSP Faraji Zegge kufanikiwa kuiteka ngome ya ISLIB na askari waliosalia wote kuwekwa chini ya ulinzi! Hata hivyo, mapambano yaliacha maafa makubwa kwa pande zote mbili. Kiasi cha askari watano wa JWTZ waliuawa na takribani kumi kujeruhiwa! Aidha, Inspekta Cecy pamoja na Inspekta Daniel Chacha walijeruhiwa huku Jonathan Njoroge akiwa amejeruhiwa vibaya! Kwa upande wa vibaraka wa ISLIB nako kulikuwa na vifo na majeruhi kadhaa huku wengine wakiwa wamejeruhiwa vibaya, na wapo pia waliokuwa wamebakiza dakika chache tu za kuishi hapa duniani!

Hata hivyo, Bon Mtambo alikuwa hajamaliza kazi!

Kwa kutumia msaada wa ramani huku pia akiongozwa na Layla, Bon Mtambo na kikosi chake walianza kupekuwa sehemu mbalimbali humo ndani! Walizunguka kutoka chumba kimoja hadi kingine hadi walipofika kwenye ofisi moja iliyokuwa na mlango mnene! Aligeuka nyuma na kujadiliana na wenzake namna ya kuingia kisha wote wakakubaliana waulipue kwa bomu dogo!

“Tulindeni wakati mimi na Layla tukifanya upekuzi humu ndani!” Bon Mtambo alimwagiza Okello na vijana wengine wa JWTZ aliokua ameongozana nao. Baada ya

kupekuwa kila mahali, hatimae macho ya Bon Mtambo yalitua kwenye kitini (*handout*) chenye ukubwa wa wastani.

Ni kama alipigwa na shoti ya umeme! Alitulia kwa muda huku akihisi akili yake kutaka kufa ganzi! Kwa mara nyingine aliyatuliza macho yake kwenye kitini ili athibitishe kile alichokisoma! Alipoangalia tena, akakuta kumbe alikuwa sahihi!

ISLIB/IBU STRATEGIC PLANNING!

Ni kama alipatwa hofu kuangalia nini kiliandikwa! Hivi ndivyo binadamu alivyo! Sio jambo la kawaida kumkuta mtu akiwa amejawa na furaha mara baada ya kukoswakoswa kugongwa na gari. Ingawaje amesalimika, mtu huyu aghalabu utamkuta akiwa anatweta kwa hofu na taharuki!

Ndivyo ilivyokuwa kwa Bon Mtambo!

Baada ya kurejewa na ufahamu, alichukua hicho kitini ambacho chini yake alikuta kingine! Ni taharuki iliyokuwa imemtawala ndio ambayo bila shaka ilimfanya ashindwe kukiona kabla!

Akaogopa zaidi, pengine kuliko awali!

Majina!

Alihofia kuona majina yaliyomo kwenye kitini hicho! Alifikicha macho yake na kujaribu kusoma vizuri kilichoandikwa juu yake!

ISLIB/IBU MINUTES!

Hii ilimaanisha kwamba humo ndimo kuna muhtasari wa vikao vyote vilivyofanyika na majahili hawa! Wahujumu wakubwa wa nchi yetu! Aghalabu, kwenye muhtasari wa vikao hivi ndimo mnakuwa na majina ya wajumbe waliohudhuria kwenye kikao husika!

"Tufanye haraka Bon!" Layla alimgutua toka kwenye bumbuwazi! Alichukua vitini hivyo kisha

akavipekuwa kwa harakaharaka ambapo alikuta taarifa zote muhimu ambazo mpelelezi yeyote angezihitaji!

“Twendeni, tutawaagiza polisi waje kuendelea na ulinzi wa hapa na sisi hatuna budi kwenda kuwakamata usiku huu huu wote waliohorodheshwa humu!” Bon Mtambo aliwaeleza wenzake kisha akaanza kumpangia kila mmoja wapi kwa kwenda huku yeye, Layla na Inspekta Faraji Zegge wakienda kwa Fredrick De Souza!

“Bon, amka usikilize taarifa ya habari na uniambie endapo nimepeleka taarifa sawa na ulivyotaka!” Alikuwa ni Layla akimwamsha Bon Mtambo ambae kutokana na hekaheka za usiku uliopita, alikuwa bado kwenye usingizi mzito!

Bila kupoteza muda, aliamka na kukaa kitako ambapo mtangazaji wa televisheni moja nchini alikuwa ndo anaanza kusoma habari!

*“…..Ile sintofahamu kuhusiana na Mtanzania aitwae Bon Mtambo Naseer hatimae imefikia tamati baada ya kuvunjwa kwa mtandao mkubwa wa hujuma nchini. Kwa karibu majuma mawili hivi sasa, Bon Mtambo amekuwa akiripotiwa na vyombo mbalimbali vya habari kwamba anahusika na biashara haramu ya madawa ya kulevya pamoja na ugaidi. Hata hivyo, habari tulizozipata asubuhi hii zinasema kwamba Bon Mtambo si gaidi na wala hajiusishi na biashara haramu. Habari kwamba Bon Mtambo anahusika na tuhuma hizo zilipikwa na wanamtandao waliokuwa wanaendesha hujuma zao nchini baada ya kugundua kwamba Bon Mtambo amepewa jukumu la kuuvunjilia mbali mtandao huo wa kifedhuli. Aidha, habari hizo zinaendelea kueleza kwamba lengo la kupikwa kwa tuhuma hizo ilikuwa ni kumchafua*

*Mtanzania huyo machoni mwa jamii ili ashindwe kuendesha vita hivyo. Habari ambazo zimethibitishwa na DCI Humphrey Mwaiswelo zinaendelea kusema kwamba mtandao huo ulikuwa unaendeshwa na wawekezaji wakubwa waliokuwa wanaongozwa na George Kamau pamoja Fredrick De Souza. George Kamau ni mfanyabiashara kutoka Kenya na Fredrick De Souza ni mwekezaji kutoka Afrika ya Kusini. Fredrick De Souza pamoja na wenzake walikuwa wanaendesha hujuma hizo chini ya mwamvuli wa kampuni ya ISLIB pamoja na taasisi ya CDTPE! Aidha, walikuwa pia wanaitumia kampuni ya TanEuro Energy katika kufanikisha malengo yao. Habari zaidi zinaendelea kusema kwamba, taasisi ya CDTPE ilikuwa inatumika kuwahonga viongozi wa taasisi mbalimbali kama vile vyama vya siasa, asasi za kiraia pamoja na vyama vya wafanyakazi wakati TanEuro Energy ilikuwa inatumika kwa kuwahonga viongozi na watendaji wa serikali nchini. Aidha, IBU, kitengo cha siri cha ISLIB ilikuwa inatumika kuwashinikiza viongozi waliohongwa na CDTPE pamoja TanEuro Energy ili wafanye mambo yaliyo na maslahi kwa wahujumu hao. Hata hivyo, pamoja na yote hayo, Mtanzania Bon Mtambo amefanikiwa kuuvunja mtandao huo akishirikiana na Jonathan Njoroge kutoka Kenya, pamoja na William Okello kutoka Uganda. Vilevile, vijana hao shupavu walipata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa baadhi ya vijana wa jeshi la polisi wakiongozwa na SSP Faraji Zegge Omar pamoja na vijana wa Jeshi la Wananchi wakiongozwa na Kapteni Francis Mwaka! Habari zinaendelea kusema kwamba, hadi sasa Kamau, De Souza pamoja na wenzao wote wamekamatwa na wanashikiliwa kituo kikuu cha polisi. Aidha, viongozi wa DRFA pamoja na wale kutoka baadhi ya asasi zisizo za kiserikali, vyama vya wafanyakazi na NGO, nao wamekamatwa na baadhi yao wanahojiwa kabla ya kufikishwa mahakamani. DCI Mwaiswelo vilevile amethibitisha kwamba, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Jaffery Minga yupo salama mikononi mwa Bon Mtambo.*

*Kutoweka kwa IGP Minga kulikuja baada ya Bon Mtambo kugundua kwamba wahujumu, kupitia waziri wa mambo ya ndani ya nchi, Bwana Elisante Josephat walikuwa na mpango wa kumchezea akili Bwana Minga ili afanye mambo yenye manufaa kwao.Hata hivyo, kamatakamata bado inaendelea kwa baadhi ya watendaji wa serikali ambao nao walikuwa wanashirikiana na wahujumu hao wa nguvu za watanzania!"*

"Safi sana Layla, hiyo habari ni kama ulii-*copy* toka kichwani mwangu na kui-*paste* kichwani mwako ndipo ukaiandika!" Bon Mtambo alimweleza Layla kisha wote wakakumbatiana na kuruhusu hali ya kelele zisizo za kawaida itawale kati yao!